6 FEBRUARI, 2015

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 6 Februari, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (Mapitio ya Nusu Mwaka), Februari, 2015. *[The Monetary Policy Statement (The Mid-Year Review), February, 2015]*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Bunge au Mwakilishi wake. Mwakilishi wake Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya.

**MHE. MAGDALENA HAMIS SAKAYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI TEULE YA BUNGE):**

Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge Iliyoundwa Kuchunguza na Kuchambua Sera Mbalimbali Zinazohusu Masuala ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji na Uwekezaji, ili Kubaini Kasoro Zilizomo Katika Matumizi ya Ardhi.

**SPIKA.** Ahsante sana, Katibu tuendelee!

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 107

### Wafungwa na Mahabusu Kutoruhusiwa Kupiga Kura

**MHE. EZEKIA D. WENJE** aliuliza:-

Mtu anapokuwa mfungwa/mahabusu hakumwondolei haki zake za msingi kama vile haki ya kuishi na haki ya uraia; na kwa kuwa moja ya sifa ya mtu kupiga kura ni uraia:-

Je, ni kwa nini wafungwa na mahabusu wa nchi hii hawaruhusiwi kupiga kura?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Dibogo Wenje, kama ifuatavyo:-

Ibara ya 1(5)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inafafanua kuwa kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ibara ya 5(2) ya Katiba hiyo na sheria za Uchaguzi, wafungwa wenye vifungo kuanzia miezi sita na kuendelea hawaruhusiwi kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi, imeshaaza kufanya utafiti na mazungumzo na taasisi zinazohusika na kundi la wafungwa chini ya miezi sita na mahabusu ili kuweka utaratibu mzuri wa kuwawezesha kushiriki katika mchakato wa Uchaguzi kuanzia kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kushiriki kwenye zoezi zima la uchaguzi.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, baada ya kusoma majibu niliyopewa, ilibidi nichukue Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katiba yetu, siyo kweli kwamba katika Ibara yake ya 5(2), inasema kwamba wafungwa waliofungwa kifungo cha zaidi ya miezi sita, wasiwe na uwezo wa kupiga kura. Ukisoma Katiba hiyo, Ibara ya 5(2) (c) inasema:

Watu waliotiwa hatiani kwa makosa fulani ya jinai, siyo hata makosa yote ya jinai, lakini pia haijaweka *limit* ya kifungo.

Mheshimiwa Spika, sasa maswali yangu ni kama ifuatavyo:-

(1), Serikali imesema kwamba wameanza mazungumzo na wanaohusika, Tume ya Uchaguzi ya Taifa kuweka utaratibu wa hawa wafungwa kupiga kura.

Je, Serikali inatupa *commitment*, kwamba katika huu uchaguzi unaokuja, mwaka huu na katika hata *referendum*, watakuwa wamemaliza huo mchakato, ili hao watu ambao wako gerezani pamoja na mahabusu, wapate hiyo haki yao ya msingi ya Kupiga Kura. *(Makofi)*

(2), Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Katiba haisemi, haikatazi hawa watu Kupiga Kura, hata hawa watu waliofungwa zaidi ya labda miaka miwili, mwaka mmoja ambao hawajaua mtu, yaani ni makosa tu fulani fulani ya jinai, wengine wamefungwa labda kwa makosa ya madai, sasa hawa pia watawekewa utaratibu lini wa kupata haki yao ya msingi ya kupiga kura?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Wenje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, unapopitia vifungu vile unavyosema Mheshimiwa Wenje, kifungu cha 5(1)(2), unapata yale makosa ambayo yanaweza kumfanya raia wa Tanzania asiweze kupiga kura, na wakati wa jibu langu la msingi nimesema, ukichukua Katiba, ukafuatilia pia na Sheria za Uchaguzi, zinatufikisha mahali ambapo ilikuwa si ruhusa kwa wafungwa kupata hiyo nafasi ya kuweza Kupiga Kura.

Kwa hiyo, kwa swali lake la kwanza, *commitment* ya Serikali kama nilivyosema, kwa wafungwa wale ambao wamefungwa kifungo chini ya miezi sita, tayari mchakato umeshaanza wa kuangalia ni namna gani mwaka huu wanaweza wakasaidiwa na kuona wanapatiwa haki yao ya Kupiga Kura. Lakini baada ya kutathimini sheria na mambo yote ambayo yanawapelekea wao kupata haki hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ametaka pia kujua na wale wengine ambao hawakuhukumiwa kwa makosa ya jinai, Serikali inasema nini kuhusu juu yao! Serikali itaendelea kuangalia Katiba na sheria mbalimbali na kama zitatufikisha katika hatua ya kuona kwamba wanastahili kupata haki hiyo ya kupiga kura, basi Serikali itafanya hivyo.

Kama itaona kwamba, kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa sheria mbalimbali, suala hilo litakuwa gumu, basi tutaendelea kuwa na mfumo utaratibu tulionao sasa. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nimwulize Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa ndani ya mahabusu kuna wafungwa wengi wamo mle wengine wanasoma mpaka wanafika kuhitimu shahada ya sheria na wakirudi uraiani mnawatambuaje nao angalau wapate kazi za kuajiri kama wananchi wengine ambao wako uraiani?

**SPIKA:** Kazi za kuajiriwa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE**: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Maryam Msabaha, kwa swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, haki ya kujiajiri ama kuajiriwa katika nchi yetu ya Tanzania haimfungi mtu yeyote mahali popote na wakati wowote. Kama wako wafungwa, ambao katika kipindi chao cha kutumikia kifungo, wameweza kusoma na kupata taaluma mbalimbali, na mara wanapomaliza kifungo chao na kuwa raia huru nje ya magereza, tunawaomba tu, wafuate utaratibu wa kisheria wa nchi yetu, matangazo ya ajira za kuajiriwa yanatolewa kwa taratibu na Watanzania wote wanaruhusiwa kuomba na wote wataajiriwa kama wanazo sifa za kupatiwa ajira.

Vile vile nichukue nafasi hi kuwahimiza wafungwa wanapotoka ndani ya kifungo chao, na kama wameweza kupata ujuzi na elimu zaidi ya ile walioyokuwa nayo, iko nafasi pia ya kupatiwa ushauri na wakaweza pia kujiajiri kutokana na taaluma walizonazo. *(Makofi)*

Na. 108

**Kuwawezesha Wajasiriamali**

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Suala la la kuwawezesha wajasiriamali na vikundi mbalimbali vya wananchi wanaohitaji kupambana na umasikini ni jambo muhimu sana:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa dhati wa kuwawezesha wajasiriamali na vikundi mbalimbali vinavyohitaji msaada?

(b) Je, kwa nini Serikali isianzishe chombo au benki ya wajasiriamali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Dafa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inawawezesha wajasiriamali na vikundi mbalimbali vinavyohitaji msaada kupitia sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ya mwaka 2004 na sheria ya uwezeshaji wananchi kiuchumi namba sita ya mwaka 2004.

Sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, imeainisha nia ya Serikali ya kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji kwa kuboresha vyanzo vya akiba na kuchukua hatua za kuondoa vikwazo mbalimbali ili kuwezesha mabenki kukopesha kikamilifu amana zilizopo na kwa gharama nafuu. Kutokana na sera hii, mipango ya miradi na mifuko mbalimbali imeanzishwa ili kuwawezesha wananchi kukopa kwa urahisi.

Mifano ya mipango na mifuko hiyo ni pamoja na Mpango wa Kuwadhamini Wajasiriamali Wadogo na wa kati unaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania, Mpango wa Kuwawezesha Wananchi na kuongeza ajira.

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo au *Self,* Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Mfuko wa Maendeleo ya Wananwake, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo MKURABITA, Mradi wa Kukuza Ushindani wa Sekta Binafsi na kadhalika.

Aidha, umeanzishwa Mpango Kazi wa Serikali wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini kwa lengo la kuwapunguzia wajasiriamali muda na gharama za kuwekeza na kufanya biashara.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mikopo kwa wajasiriamali, Mwaka 2007 Serikali ilianzisha Benki ya Wanawake kwa lengo la kutoa mikopo kwa wajasiriamali. Kwa sasa Serikali inaendelea na mchakato wa kuanzisha Benki ya Majasiliamli katika sekta ya Kilimo pamoja na Biashara.

Hata hivyo, utaratibu ulipo sasa, unaweshesha wakulima kuwapatia mikopo kupitia Benki ya Maendeleo ya Rasilimali, ambapo kumetengwa dirisha maalum kwa ajili ya mikopo ya pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto wanayokumbana nayo wajasiriamali wadogo wanapotaka kukopa kutoka katika taasisi za fedha, hasa zile za kibiashara.

Hatua ya Serikali kuanzisha Benki ya Kilimo, Benki ya Wanawake na Dirisha la Kilimo katika Benki ya *TIB* ni kuwawezesha wajasiriamali wadogo kupata mikopo kwa urahisi.

Aidha Serikali kupitia Benki Kuu, inaendelea kufanya mazungumzo na wenye taasisi nyingine binafsi zinazotoa huduma za kifedha na mikopo ili kulegeza masharti ya kukopesha, likiwemo suala la riba za mikopo kuwa juu sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri kiasi ya Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza, ni ukweli usiopingika kwamba asilimia zaidi ya 60, ya wananchi wa nchi yetu ni vijana, na wao ndiyo wanahangaika kutafuta ajira, kutafuta mitaji. Waziri ameeleza vizuri kwamba iko sera.

Je iliwahi kufanyika tathimini ya sera hii, imesaidia vijana wangapi, wajasiriamali wangapi na kama tathimini hiyo imefanyika, inaweza kuletwa hapa Bungeni, na kama haijafanyika, Serikali inatamka nini, inaliahidi Bunge italeta tathimini hiyo ili tujue, vijana na wajasiriamali wamenufaika kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Waziri amezungumzia kuhusu taasisi za fedha kusaidia wajasiriamali na wananchi kwa ujumla. Ni ukweli usiopingika na yeye mwenyewe amekubali kwamba, liko tatizo la riba, na suala hili la riba ni la muda mrefu, vijana hawawezi kwenda kukopa kwa sababu riba ziko ju sana.

Serikali inatamka nini na ni lini italeta ratiba kamili ya kupunguza riba na kuwasaidia vijana waweze kukopa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU**: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Shekifu kwa kuonyesha jinsi anavyojali vijana wa Tanzania.

Sasa nikijibu swali lake la kwanza, ni asilimia zaidi ya 60 ambao ni vijana katika nchi hii na kwamba tuna Sera ya Uwezeshaji, tuna Sheria ya Uwezeshaji, tuna mikakati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda Bunge lako Tukufu lijue, kwamba siyo Wizara ile ambayo iko chini ya Waziri Mkuu na Baraza la Uwezeshaji peke yake inayowezesha. Tunataka sekta zote ndani ya Serikali hata sekta binafsi na *NGOs* ziwezeshe vijana ili tuweze kuwawezesha wengi kwa mara moja.

Kuna mkakati ambao tumeweka ambao tulikuwa tunapenda tuuzindue katika Bunge hili na mimi nafikiri itawezekana kuuzindua katika Bunge hili ili mkakati ujulikane na kila mmoja awezeshe na aone fahari ya kuwawezesha vijana wa Watanzania kwa sababu ndiyo namna pekee ya kujenga uchumi wa nchi yetu.

Sasa Mheshimiwa Shekifu ametaka kwamba kama tumerejea sera hiyo, tumerejea na Serikali inategemea kuleta mabadiliko kidogo au marekebisho kidogo kwenye sheria ya uwezeshaji kusudi iwe ni lazima, isiwe ni hiari tena.

Sasa kuhusu suala la riba, ambalo ndilo swali lake la pili. Kwa kweli riba ni suala la soko la fedha. Huwezi ukakuta Serikali inasema kwamba, riba itakuwa kiasi fulani, kwa sababu huu ni uchumi wa soko huru. Kwa hiyo, Serikali haiwezi ikasema, ila Serikali inaweza ikachukua mikakati mbalimbali.

Kwa mfano, kulikuwa na suala la kuongelea riba inayotozwa kwenye *treasury bills* ya Serikali, ile inafanya mabenki yasitake kukopesha sekta binafsi kwa sababu ni mahali ambapo ni rahisi, ni salama kuliko sekta binafsi.

Kwa hivyo, kupitia mikakati kama hiyo ya kupunguza riba kwenye *treasury bills* na mwengine ambayo yanaweza yakafanywa na Serikali, ikaweza kuifanya ribai kashuka chini. *(Makofi)*

Hata hivyo nataka kurudia, suala la riba ya mikopo kutoka mabenki na taasisi za fedha, ni suala la uchumi huru na hakuna Serikali ambayo inaweza ikasema leo riba iwe namna hiyo, ama sivyo tutaua soko la fedha.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia hii nafasi. Kwa kuwa suala la wajasiriamali, moja ya lengo lake ni kupunguza umasikini, na kwa kuwa katika mkakati wa *TASAF III* ni kuwapatia kaya masikini ruzuku ya fedha karibu bilioni 80 kwa ajili ya kupunguza, kwa malengo makubwa matatu, njaa, elimu na afya.

Je, ni kwa nini sasa Serikali isitumiefedha hizo zaidi ya bilioni 80 kwa ajili ya kuwapatia mikopo wajasiriamali au kaya hizo masikini ili waweze kuondokana na kipindi hicho kifupi cha miezi minne ambacho mnataka kuwapatia chakula, afya na maji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU**: Mheshimiwa Spika, na mimi nafarijika kwamba Bunge lako Tukufu, limehamasika kuona kwamba ujasiriamali unashika hatamu ndani ya nchi hii ili kuweza kuinua uchumi wa Watanzania na wao washike hatamu ya uchumi wao. Sasa kuhusu shilingi bilioni 80 za *TASAF*, kwamba badala ya kutoa kwenye kaya masikini tutoe kwa vijana wajasiriamali, katika kaya hizi masikini na vina nao wapo.

Vijana nao wapo kwa sababu unapokuwa masikini huwezi ukafanya jambo lolote, madhumuni ya *TASAF* ni kuwanyanyua watu katika umasikni uliokithiri ili haimaye hata wawe na uwezo wa kufikiria watafanya miradi gani na waondokane na umasikini badala yake wawe na maisha bora zaidi.

Kwa hiyo, suala la vinaja litatiliwa mkazo na kwa sababu suala la *TASAF* liko chini ya Ofisi ya Rais na liko chini ya *portfolio* yangu, basi nitaliona hilo la Mheshimiwa Silinde linaweza kufanywa kwa namna gani, lakini kupitia kaya masikini. *(Makofi)*

Na. 109

**Kujenga Hospitali ya Wilaya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro**

**MHE. DKT. LUCY SAWERE NKYA** aliuliza:-

Halmashauri ya Morogoro haina hospitali ya wilaya hivyo kulazimu wagonjwa kusafiri umbali mkubwa kufuata huduma hiyo mjini Morogoro:-

Je, ni lini Serikali itajenga hospitali ya wilaya katika Halmashauri hiyo ili kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kufuata huduma za kitaalam Morogoro Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ina vituo sitini na nane vya tiba, kati ya hivyo vituo vinane ni vya serikali na sita ni vya Mashirika ya Dini na kimoja ni kile cha Magereza.

Zahanati sitini, kati ya hizo arobaini na nne ni za Serikali, nane ni za madhehebu ya dini, nne za watu binafsi na nne ni za taasisi nyinginezo.

Kati ya vituo vinane vya Afya vilivyopo vituo viwili vya Tawa na Dutumi vinatoa huduma za upasuaji, hali ambayo imesaidia kupunguza rufaa za wagonjwa wa kutoka vituo vya afya kwenda kwenye hospitali ya mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imefanya jitihada mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya katika Halmashauri. Mwaka wa fedha wa 2013/2014 Halmashauri imejenga wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya cha Dutumi ili kitumike kama hospitali ya Wilaya kwa muda. Ujenzi wa wodi hiyo uligharimu Shilingi milioni mia moja ambazo zilitoka katika bajeti ya Halmashauri. Ujenzi wa wodi hii upo katika hatua ya upauaji.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali ya Wilaya upo katika hatua za awali ambapo mwaka 2012/2013 Halmashauri ilitenga eneo lenye ukubwa wa hekta 6.65 katika Tarafa ya Mvuha kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Wilaya. Mwaka wa fedha 2014/2015 Halmashauri imeomba kiasi cha Shilingi milioni hamsini na saba katika maombi maalum kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imeomba tena Shilingi milioni mia saba katika Bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za Wilaya. Ujenzi utaanza mara baada ya fedha hizo kupatikana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt.a Lucy Nkya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijijini inakuwa ni vigumu sana kusema kwamba unakwenda kuboresha kituo cha afya kimoja ambacho kiko mbali sana na maeneo mengine, kufuatana na milima, barabara na umbali.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuangalia basi kwenye kila tarafa tuweze kupata kituo cha afya karibu na wananchi ambacho kitatoa huduma za upasuaji ili tuweze kupunguza vifo vya akina mama.

Maana yake ni kwamba tupate *theatre* moja pale Mkuyuni ambayo tunajenga hatujapata hela za kumalizia? Tunajenga tena Ngerengere, tunasaidiwa na *Lions Club,* hatujaweza kumaliza. Lakini tunachoomba sasa tupewe vifaa pamoja na wahudumu kwenye hizi mbili, kwa sababu kule kusini kuna…

**SPIKA:** *Nina*wasi wasi, kama siyo swali, kama hotuba hivi, sasa si…

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, kule Kusini ziko mbili. Sasa mimi ninachoomba ni kwamba, je, TAMISEMI haioni kwamba kuna umuhimu wa kusaidia ku-*upgrade* na kuwapa vyombo kituo cha afya cha Ngerengere na kituo kimojawapo katika Tarafa ya Mkuyuni ambapo akina mama wanakufa sana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Nafikiri hili suala la ujenzi wa hospitali lilianza muda mrefu. Mara ya kwanza wakaleta Shilingi milioni mia moja ambazo hatukujua zilikwenda wapi, na sasa hivi tunaahidiwa kila wakati.

Mimi ningeomba kwamba, sambamba na ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri basi TAMISEMI waone umuhimu wa kutusaidia kusudi tuweze kuwa na hospitali ambayo ita-*integrate* wananchi wote kwa pamoja, tutoe huduma ambazo ni kamili. Kuna matatizo makubwa….

**SPIKA:** Mheshimiwa Naomba, umetumia dakika tano peke yako. Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *concerns* za Mbunge tunaziona. Mimi nimekwenda Morogoro, nimekwenda mpaka katika hili eneo tunalolizungumza. Dutumi pale iko Matombo. Kutoka pale Morogoro kwenda Matombo ni Kilometa mia moja, kwa hiyo unaweza ukaona jinsi anavyozungumza pale. *(Makofi)*

Kilichofanyika pale, na wanatumia hospitali ya mkoa ndiyo inatumika kama Hospitali ya Wilaya hiyo hiyo inatumika kama Mkoa, na *congestion* ya Morogoro pale manispaa tunaifahamu, ni kubwa sana. Kwa hiyo, anachosema Mheshimiwa Mbunge mimi ninakielewa, anasema kitu ambacho ni kikubwa sana ambacho na sisi tuko *concerned*.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika ni nini. Wakaamua kwamba wachukue kituo cha Afya cha Dutumi kitumike hicho kwa muda kama Hospitali ya Wilaya. Hizi Milioni mia moja anazozungumza hapa nime-*check* mimi na Mganga Mkuu nikamwuliza zimekwenda wapi, ndizo hizo zinazotumika.

Hicho kinachojengwa pale inaonekana ni *maternity ward* lakini *maternityward* hiyo ndiyo wanataka wai tumie kama Hospitali ya Wilaya, ni ili kujibu swali hili swali analoliuliza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya kuijenga ni Shilingi bilioni nne. Hawa wamepeka *special request*, ukiangalia maelekezo ya Bajeti yaliyotolewa sasa hivi hata *special request* yenyewe sasa imeshakataliwa, haipo tena, nilikuwa nasoma nikaangalia haipo tena. Kwa hiyo *there is a big problem* hapa.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali hili, kitu mbacho kinafanyika hapa kwa sababu lilikuwa refu, nijibu kwa kifupi tu. Ni kwamba, cha kwanza wanachotakiwa kufanya, haya yote aliyoyasema hapa, ni wanatakiwa watafute, anaweza akaenda kwenye hospitali ya BAKWATA au ya Kanisa pale wakasema hapa sisi tunataka huduma hii ipatikane hapa, wanaita *Designated Hospital* (Hospitali Teule). Wakipeleka pale wakishaitamka hivyo ikakubalika pale ikapita katika *RCC* maana yake sisi kama Serikali tutaheshimu mpango huo…

**SPIKA:** Naomba Waheshimiwa Wabunge, tukiwa ndani ya Bunge mjue tuko ndani ya Bunge, naona mazungumzo yanaendelea. Tuendelee tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, niendelee. Tutaheshimu mpango huo. Wengi tuwamefanya, Wabunge walioko hapa wengi hapa hawana hospitali ya Wilaya kwa maana ya Hospitali ya kwao wao.

Wameamua tu kwamba mimi nimekwenda pale BAKWATA wametukubalia kwamba pale tutapageuza patakuwa hospitali ya Wilaya. Ukienda Hai pale kwetu *Machame Hospital* pale ni *Designate Hospital*. Pale patapelekwa heshima zote na sifa zote pamoja na huduma zote zinazohusu hospitali ya Wilaya, zitapelekwa pale. *(Makofi)*

Anachosema Dkt. Nkya ni cha msingi. mimi nashauri, na tutasaidiana na wao, kuona kwamba *at least* wanapata mahali. Lakini kwa sasa hivi Dutumi ndio wameamua katika Halmashauri kwamba itumike kwa ajili ya matumizi hayo. Hizo milioni mia moja zilitumika kwa ajili ya kujenga hiyo wodi.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo lililoko Morogoro Vijijini ni karibu sawa na tatizo lililoko Wilaya ya Njombe, ambako Hospitali ya Wilaya imechukuliwa kufanywa Hospitali ya Mkoa na kufanya wananchi kupata adha kubwa.

Je, ni lini Hospitali ya Mkoa itajengwa, itakamilika kujengwa lini ili wananchi wa Njombe warudishiwe hospitali yao ya Wilaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, siyo, au hukujiandaa. Kama hukujiandaa basi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Leniana Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ni kweli Sera ya nchi yetu sasa hivi, tangu 2007 ni kuhakikisha kwamba kila mkoa uweze kuwa na hospitali ya rufaa ya mkoa. Juhudi hizo tumeziona katika Mkoa wa Singida wanakwenda vizuri, Manyara wanakwenda vizuri, pale Mara wanakwenda vizuri, hospitali ya kwangu nayo wanakwenda vizuri.

Kwa hiyo, natoa maelekezo kwa nchi nzima, Mkoa wa Njombe wajiandae, michoro ipo na ushauri upo Wizara ya Afya, ili kusudi juhudi zile zitokane na Mkoa kwa sababu siyo mradi ambao labda ni *centralized* katika ngazi ya kitaifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, juhudi hizi ambazo zimeanza na mikoa mingine, sisi Serikali bado tunaangalia kwa sababu ni mzigo mkubwa wa mikoa husika na nchi kwa ujumla kutafuta wadau wengine chini ya *PPP* tuweze kuona uwezekano wa kuanza kujenga hospitali hizi za Rufaa za mikoa kwa kushirikiana na sekta Binafsi na sekta ya Umma.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kupitia nafasi hii naomba nitoe maelekezo kwa wamiliki wote wa hospitali na vituo vya huduma ya afya vya wadau mbalimbali. Katika ufuatiliaji ambao Wizara ya Afya tumefanya tumebaini hospitali za wenzetu hususan ambazo zinamilikiwa na Mashirika ya Dini wana watumishi ambao ni hewa.

Katika miezi sita iliyopita tumebaini watumishi mia nne sitini na wawili (462). Natoa maagizo pesa zile zote zilizokuwa zinakwenda katika hospitali hizi zirudi mara moja Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zoezi hili ni endelevu. Katika hatua hii ya awali hata hospitali ambazo huko nyuma zilikuwa zinakuwa na watumishi hewa si kama ilivyo kwenye hospitali hizi za Mashirika ya Dini. Hospitali moja unakuta kuna watumishi zaidi ya sitini, hamsini na, arobaini na, thelathini na.

Ni suala ambalo halikubaliki kwa sababu makubaliano ambayo yapo kati ya Serikali na mashirika ya dini ni ya heshima na kwa makubaliano. Wajengewe uwezo wale watumishi ambao ni watumishi wanaosimamia utumishi pamoja na suala zima la *manpower management* kwenye hospitali hizo. Uhalifu mkubwa uko hapo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Halmashuri husika na mikoa husika ifanye kazi kwa karibu na hospitali hizi. Wafanye kazi kwa karibu na kuwajengea uwezo. Suala hili liendane na kusaini mikataba ile ya makubaliano, yaani *service agreement* ili kusudi ufuatiliaji uwe karibu katika hospitali ambazo ziko kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea, tunaomba Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha Mheshimiwa Assumpter Mshama, anauliza swali hilo.

Na. 110

**Kuhusu Muswada wa Kufanya VICOBA Kutambuliwa Kama SACCOS**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA** aliuliza:-

VICOBA vimekuwa Mkombozi na msaada mkubwa katika kuondoa umasikini hasa kwa watu wenye kipato kidogo na wanaokaa pamoja.

Je, ni lini Serikali italeta Sera au Muswada ili VICOBA Vidhaminiwe na Kutambuliwa kama *SACCOS*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika katika mkutano wa kumi na tano wakati nikijibu swali Namba 209 tarehe 9 Juni, 2014 lililoulizwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama nilisema:-

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo Serikali ilimwajiri Mshauri Mwelekezo kutoka *Economic and Social Research Foundation (ESRF)* mwaka 2013 kufanya utafiti wa mapitio ya sera ambayo itazingatia mabadiliko yaliyopo katika sekta hii muhimu.

Aidha ripoti ya awali kuhusu utafiti wa mapitio ya sera ya taifa ya sekta ya huduma ndogo ndogo za fedha imekamilika. Imebainisha maeneo muhimu ya kufanyia kazi kama vile mafanikio, wigo, mapungufu pamoja na changamoto zake.

Baada ya zoezi la mapitio ya sera ya taifa ya huduma ndogo ndogo za kifedha kukamilika Serikali itaandaa Muswada wa sheria za kusimamia taasisi ndogo ndogo za huduma za fedha *(Microfinance Act)* zikiwemo *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Fedha tarehe 16 Januari, 2015 imepokea rasimu ya sera tajwa hapo juu. Hatua itakayofuata itakuwa ni kuwashirikisha wadau na baada ya kuwashirikisha wadau na kuridhia itapelekwa Serikalini, yaani kwenye Baraza La Mawaziri kupata idhini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata idhini na maelekezo ya Serikali utaandaliwa Muswada ambao utafikishwa Bungeni.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mshama swali la nyongeza.

**MHE. ASSUPMTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipatia nafasi kwa ajili ya maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza ninaishukuru Serikali kwa kuonesha kulishughulikia suala hili la *VICOBA*, ambalo Naibu Waziri anakiri mwenyewe kwamba nililiuliza kipindi kilichopita, takriban sasa ni miezi minane, na inaonesha kuna kitu kinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yetu ya Misenyi tuna VICOBA zaidi ya mia tatu na kila kikoba kinabeba watu thelathini. Lakini tunasuasua kwa sababu hatuna wezesho. Swali ni kwamba Kama ulivyosema Naibu Waziri. Je, huu Muswada utachukua tena miezi minane na kama itakuwa miezi minane Wabunge tutakuwa tumeshaondoka Bungeni, ambao tumeanzisha mchakato huu. Lini utaletwa rasmi katika Bunge hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wanawake wameonesha ni wa mstari wa mbele katika masuala ya ujasiriamali.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wanawake wanawezeshwa, ukizingatia kuwa ukimwezesha mwanamke umewezesha jamii nzima.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mshama kwa jinsi anavyowajali wanawake wa Nkenge na wanawake wa Tanzania, kwa sababu sera hii itatumika kwa nchi nzima. Nikiri tu mimi nilifika Nkenge na niliwaona wanawake wa Nkenge wakiwa na mwamko na jinsi ambavyo walitoa ushuhuda jinsi *VICOBA* vilivyoweza kuwasaidia katika maisha yao na kuwaendeleza watoto wao.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, niseme tu kwa niaba ya Waziri wa fedha kuwa sisi kama Wizara, kwa kuwa hii ripoti tumeipokea Januari hii tutahakikisha tunaharakisha hatua zilizosalia nilizozisema. Moja ikiwa ya wadau na ya pili ikiwa ya kupeleka kwenye *cabinet* ili iweze kupata idhini na baada ya hapo jukumu litakuwa liko kwenye kiti chako Mheshimiwa Spika kwa ajili ya kupangia Muswada kama utaratibu ambavyo zinataka.

Serikali inatambua umuhimu wa akina mama katika kuondokana na umasikini. Moja, akina mama ni waaminifu na ni wachapa kazi. Mkopo ukipokelewa na akina mama una uhakika wa kurejeshwa na hata kwenye familia mkopo ukichukuliwa na mama akawa anajua una uhakika wa kutumika katika kusudi lililokuwa limekusudiwa.

**SPIKA:** Mama *VICOBA*…

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, hiyo ni dhahiri, na kwa kuwa si siku ya wanawake nisingesema sana lakini nimeona ukweli. La pili…

**SPIKA:** Jibu kwa kifupi maana mpaka nimesahau kama mpo hapa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.M. NCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, nilikuwa namalizia hilo la pili.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Waziri kwa majibu mazuri kuhusiana na habari ya kuwawezesha wanawake kupitia mfumo wa *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Benki ya Posta imeanza mchakato wa kutengeneza *products* ya kukopesha wana-*VICOBA*.

Je, Serikali iko tayari kuwaharakisha Benki ya Posta ili wana-*VICOBA* wote waweze kukopa kwa haraka na ukizingatia saa hizi wanawake wanahitaji sana mitaji?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.M. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba nijibu swali la Mheshimiwa Devotha Likokola, kama ifuatavyo:-

Serikali haina pingamizi na ushauri alioutoa, tutaongea na wenzetu wa Benki ya Posta, waangalie *capacity* yao ya kuweza kukamilisha hiyo shughuli ya kuwafikia akina mama. Bahati nzuri Benki ya Posta na yenyewe ina mtandao mkubwa. Kwa hiyo, ni *capacity* tu ya utumishi na mahitaji ya namna ya kuwaelimisha ili waweze kutimiza matakwa yao waliyoyaweka katika malengo yao bila kuathiri mtaji wa benki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwani V*ICOBA* ni wanawake tu. Tunaendelena swali linalofuata, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swali langu zuri kwa siku hii ya leo naomba uniruhusu dakika moja tu kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha Ndugu yangu Mheshimiwa Saada Mkuya kwa jitihada anazozifanya katika Wizara yake.

Vile vile nitakuwa sijamfanyia haki kuishikiri mikono yake miwili jinsi inavyofanya kazi, Mungu saidia akiwemo Mheshimiwa Adam Malima na Mheshimiwa…

**SPIKA:** Haloo! Mheshimiwa Ayoub, hatufanyi hivyo kwenye kipindi cha Maswali. Niulizie Namba tu. Uliza swali, habari nyingine achana nazo.

Na. 111

**Kuhusu Maamuzi ya Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar Kutotambiliwa Bara**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Kwa kuwa maamuzi ya Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ambaye yuko Zanzibar hayana uzito kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Zanzibar ambapo ushuru wa biadhaa hizo hukadiriwa upya mara zinapofika Tanzania Bara:-

Je, kuna ulazima gani kwa *TRA* kuwa na Afisa Mwandamizi wa cheo cha Naibu Kamishna kwa upande wa Zanzibar mwenye watumishi wengi chini yake wakati kazi wanazofanya za kukagua na kuzifanyia tathmini bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Zanzibar haitambiliwi na Mamlaka husika Tanzania Bara?

Je, Serikali haioni kuwa utaratibu wa kuichukulia Zanzibar kama nchi ya kigeni unakiuka Katiba ya Nchi na makubaliano katika Hati ya Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayub, Namba 111, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kuwa na Afisa Mwandamizi wa cheo cha Naibu Kamishna, Zanzibar kutokana na majukumu yake muhimu aliyo nayo katika kusimamia ukusanyaji wa kodi zote za Muungano kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, bidhaa zinazoingia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia vituo vyote vya forodha Tanzania Bara kama vile uwanja wa Mwalimu Julius Nyerere,mipaka ya Namanga, Sirari, Bandari zote kwa upande wa Tanzania Bara na vinginevyo vinatumia mfumo wa pamoja unaoitwa *Central Evaluation System*.

Mfumo huu umeweka usawa katika ukadiriaji wa ushuru wa forodha na kuondoa tofauti zinazotokana na uthamini katika kituo na kituo sipokuwa kwa vituo vya forodha kwa upande wa Zanzibar.

Mpaka sasa, vituo vya Forodha Zanzibar bado havijajiunga katika mfumo huo, hivyo kupelekea kuendelea kuwepo kwa utofauti ya uthamini ya bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia vituo vya forodha vya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, uthaminishaji wa mizigo inayoingia Tanzania Bara kupitia Zanzibar unafanyika kwa lengo la kuweka uwiano wa kibiashara, yaani *fair competition.*

Mpaka sasa Vituo vya Forodha Zanzibar bado havijajiunga katika mfumo huo, hivyo kupelekea kuendelea kuwepo kwa utofauti ya uthamini kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia vituo vya Forodha vya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Uthaminishaji wa mizigo inayoingia Tanzania Bara, kupitia Zanzibar, unafanyika kwa lengo la kuweka uwiano wa kibiashara yaani (*Fair Competition*) hasa kwa kuwa bidhaa nyingi zinazoingia nchini zinalenga soko moja la Tanzania Bara.

Baada ya kufanyiwa uthamini bidhaa zinazotakiwa kulipiwa kodi ya ziada ni zile tu ambazo zitabainika kuwa udhamini wake ni wa chini ikilinganishwa na uthamini wa bidhaa hizo kwa kutumia mfumo wa pamoja yaani wa *Central Valuation System.*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uthamini unaofanywa na Naibu Kamishana wa Mamlaka ya Mapato Tanzania aliyepo Zanzibar na kamwe haichukulii Zanzibar kuwa ni nchi ya Kigeni bali kama upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao unatumia mfumo wa uthamini wa bidhaa ambao ni tofauti na ule unaotumika Tanzania Bara.

Kutokana na kuwepo kwa mifumo tofauti ya uhaminisha wa bidhaa kutoka nje kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, bidhaa zote zinazoingizwa Tanzania Bara kupitia Zanzibar hulazimika kulipia sehemu tu ya kodi ambayo haikulipwa Zanzibar na siyo kodi yote kwa bidhaa husika.

Aidha pande zote za Muungano yaani, Tanzania Bara na Zanzibar zipo katika himaya moja ya forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na hivyo hutoza viwango vya ushuru wa Forodha vinavyofanana.

Mpaka sasa Vituo vya Forodha Zanzibar bado havijajiunga katika mfumo huo, hivyo kupelekea kuendelea kuwepo kwa utofauti wa uthamini kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia vituo vya Forodha vya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Uthaminishaji wa mizigo inayoingia Tanzania Bara, kupitia Zanzibar, unafanyika kwa lengo la kuweka uwiano wa kibiashara yaani (*Fair Competition*) hasa kwa kuwa bidha nyingi zinazoingia nchini zinalenga soko moja la Tanzania Bara.

Baada ya kufanyiwa uthamini bidhaa zinazotakiwa kulipiwa kodi ya ziada ni zile tu ambazo zitabainika kuwa udhamini wake ni wa chini ikilinganishwa na uthamini wa bidaa hizo kwa kutumia mfumo wa pamoja yaani wa *Central Valuation System.*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uthamini unaofanywa na Naibu Kamishana wa Mamlaka ya Mapato Tanzania aliyepo Zanzibar na kamwe haichukulii Zanzibar kuwa ni nchi ya Kigeni bali kuwa upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao unatumia mfumo wa uthamini wa bidhaa ambao ni tofauti na ule unaotumika Tanzania Bara.

Kutokana na kuwepo kwa mifumo tofauti ya udhaminishaji wa Bidhaa kutoka nje kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, bidhaa zote zinazoingizwa Tanzania Bara kupitia Zanzibar hulazimika kulipia sehemu tu ya kodi ambayo haikulipwa Zanzibar na siyo kodi yote kwa bidhaa husika.

Aidha pande zote za Muungano yaani, Tanzania Bara na Zanzibar zipo katika himaya moja ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na hivyo hutoza viwango vya ushuru wa Forodha vinavyofanana.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye si muda mrefu huenda akashika nafasi kubwa kuliko aliyo nayo. Na ni ndoto hizo. Ninaomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Katika swali la msingi umesema Zanzibar hulazimia kulipa sehemu ya kodi ambayo haikulipwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi nina kilio na mimi vile vile uteuzi wangu umetoka kwa wananchi. Wapiga Kura wangu wanao mzigo wao umekaa muda mrefu juu ya meza yao. Hivi sasa vigezo vinavyotumiwa havikidhi suala hili.

(a) Je, ni lini utakaa na wafanya biashara hao ili kumaliza tatizo hilo kwa umakini kabisa ili *Hansard* zikae sawa?

(b)
Katika kujibu swali la msingi umesema kwamba kuna mifumo miwili tofauti.

Je, ni sababu gani zilizopelekea kuwa na mifumo miwili tofauti na kama ni halali kwa mfumo huo tofauti.

Je, bidhaa zinazotoka nje kupitia Tanzania Bara na baadaye zikapelekwa Zanzibar, ni halali kulipishwa kodi ile na kubakia Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA)**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza nimpiongeze kwa kuwa mfuatiliaji makini wa mambo yanaowahusu Wapiga Kura wake na wananchi wa Zanzibar.

(a) Kuhusu swali la kwanza alilosema kama nitakuwa tayari na ni lini kulimaliza suala lile ambalo ni kesi moja. Niseme tu awaarifu, wafike ofisini siku ya Jumatatu, kwani tutakuwa tumeisha rudi Dar es Salaam, ili niweze kulipitia jambo lao na niweze kuongea na watumishi wa Mamlaka kuhakikisha kwamba linapata majawabu.

Wengine wote ambao wanapata tatizo ambalo ni *case by case*. Yaani tatizo maalum, tufanye tu mawasiliano ambayo ni ya kiutawala. Mawasiliano ya kiutendaji ili yaweze kushughulikiwa.

Kuhusu swali la pili alilosema kama ni muafaka kwa kuwa na uthamini tofauti. Niweke tu wazi kwamba, ni dhahiri uchumi wa Zanzibar na wa Tanzania Bara, kuna tofauti. Tofauti hiyo ndiyo iliyoko katika mazingira ya kindugu ambao umewezesha kwamba vile vitu ambavyo vinatumika Zanzibar, vinaweza vikafanyika *valuation,* uthamini kwa namna ya matumizi ya Zanzibar.

Kwa vile ambavyo vinatakiwa kwenda Tanzania Bara hawalipi kodi mpya. Badala yake wanalipia ile tofauti ambayo inatokana na kama bidhaa ile ingelidhaminishwa kwa mfumo wa pamoja ambao nimetoka kuutaja hapa ambao bei yake ingelikuwa sawasawa na ungelikuwa umeingilia katika sehemu nyingine ile, ili kuweka usawa katika bidhaa zile zinazokwenda kwa ajili ya matumizi ya kibiashara.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninalo swali moja la nyongeza.

Kutokana na Muungano uliopo, huoni kwamba Mheshimiwa Waziri, kuwa na *TRA* moja inayosimamiwa na Wizara ya Fedha Zanzibar na Wizaraya Fedha Tanganyika kwamba huu ni mpango wa makusudi wa kuiuwa Zanzibar kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza Muungano wa Zanzibar na Tanzania Bara siyo tu ni Muungano wa vitabu. Ni Muungano wa watu. Ikiwa ni Muungano wa Watu hivi vitu tunavyofanya ni kwa ajili ya manufaa ya watu.

Kwa hiyo siyo tu ni mambo ya kisera peke yake. Ningelikuomba umwulize Mheshimiwa Muhamed Seif Khatib, akuambie kwamba Bibi zangu wako kule Konde. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapotengeneza vitu, hatuna maana ya kuathiri uchumi wa Zanzibar. *Zanzibar Revenue Authority* ya Zanzibar, na *TRA* wanafanya kazi kufuatana na mujibu wa sheria na hii haina uhusiano na kuathiri uchumi wa Zanzibar. Kwa sababu kile ambacho kinahusu Zanzibar ambayo ina Serikali inayofanya kazi.

Serikali ya Zanzibar huwezi ukainyofolea vitendea kazi vyake vyote ikiwapo hiyo ya kukusanya kodi ambazo zinatakiwa zipatikane kwa kule Zanzibar. Lakini linapohusu jambo la kodi zile za Muungano, vile vyote ambavyo Zanzibar inastahili kupata inavipta.

Mimi nikuambie kwa muda huu malalamiko yaliyokuwa yanakuja mengi sana ya kiutendaji yameishatekelezwa na yale yaliyokuwa ya Kikatiba yameishatekelezwa kwenye Katiba Inayopendekezwa. Hakutakuwepo tena na malalamiko na Taifa hili litaendelea kusonga mbele. *(Makofi)*

Na. 112

**Kumuua Mtuhumiwa**

**MHE. MUSTAPHA BOAY AKUNAAY** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Kifungu cha 11 na 12 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 R.E. 2012 hairuhusu Askari Polisi au mtu yeyote anayemkamata mtuhumiwa kumwua:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Askari wa Jeshi la Polisi wanaowaua watuhumiwa walio chini ya Ulinzi wakidaiwa kuwa wanatoroka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Kifungu cha 11 na 12 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 zinazuia matumizi ya silaha isivyo halali. Hata hivyo Kifungu cha 29 (1) (a), (b), )i) na (ii) cha sheria hiyo kinampa Askari Polisi Mamlaka ya kutumia silaha dhidi ya mtuhumiwa anayetaka kutoroka chini ya Ulinzi halali wa Polisi.

Mheshimiwa Spika, endapo Askari Polisi atakiuka masharti ya Sheria na kufanya kitendo kilicho kinyume na maadili ya kazi yake, kinachoweza kupelekea kujeruhi au kifo kwa mtuhumiwa hatua za kisheria huchukuliwa dhidi yake ikiwemo kufikishwa Mahakamani au na kufukuzwa kazi.

**MHE. MUSTAPHA BOAY AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, ni wazi kutokana na majibu Serikali, kwamba matumizi ya silaha dhidi ya raia ni makosa ya jinai.

Je, Serikali imechukua hatua gani kwa askari wa Polisi waliokuwa wamepiga raia wanaoandamana mpaka na wanafunzi na kuwaumiza na kuwaua?

Je, kutokana na kwamba Askari hao wamevunja sheria kwa kuwaumiza raia na kuwauwa. Serikali iko tayari sasa kuwafidia watu hao au familia yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la msingi nilijibu kuhusu kuumiza lakini pia muhimu kuliko yote ni kupoteza maisha. Askari anapochukua hatua za kisheria ambazo zitasababisha maumivu au kifo zikiwa halali, atakua hawezi kufikishwa Mahakamani. Kama yule ambaye anahusika anaweza kujaribu kumfikisha Mahakamani basi kwa sababu ya sheria basi haki inaonekana iko upande gani na inakuwa hakuna tatizo.

Kuhusu kufidia ni kwamba, iwapo kumetokea kuumizwa mtu na akaenda Mahakamani. Mahakama ikishatizama mazingira ya kuumizwa au kupoteza maisha kwa kifo ndiyo inayoweza kuamua kufanywe nini.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kama hivi ifutavyo:-

Kwa kuwa vitendo vingi vya uhalifu, hulindwa na huzuiwa visitokee kutokana na taarifa za kiintelijensia. Na kwa kuwa taarifa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kutoka kwa mwuliza swali, inaelekea kwamba wako baadhi ya raia ambao wamekufa wakiwa mikononi mwa Polisi.

Hivi karibuni kuna Polisi ambaye aliuawa hapa Dodoma wakati akimwokoa mtoto mdogo ili asiuliwe.

Je, Mheshimiwa Waziri, nini mkakati wa ziada wa taarifa za Kiintelijensia kuzuia mauaji haya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANIYA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, kama hivi iuftavyo.

Taarifa za Kiintelijensia ni muhimu katika kulifanya taifa lolote liwe imara na lipate utulivu unaohitajika. Kwetu na kwa wenzetu taarifa hizi zinatumika sana na bila ya taarifa hizi kwa kweli taifa linaweza likayumba au likayumbishwa na wale ambao wanataka wafanye kile wanachokita.

Sasa taarifa hizi zinasaidia kuweza kuepusha matukio mabaya au vifo au jambo lingine, ingawa kuna baadhi wakiambiwa kuna taarifa za intelijensia wanafanya masihara. Mimi ninawaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi ambao wanatusikiliza kwamba hizi taarifa zinakuwa ni taarifa za kweli na iko haja ya kusikiliza na ushauri unaotakiwa ufuatailiwe. *(Makofi)*

Na. 113

**Utaratibu wa Kubadilishana Wafungwa**

**MHE. RITAA E. KABATI** aliuliza:-

(a) Je ni nchi ngapi ambazo Tanzania tuna utaratibu wa kubadilishana wafugnwa?

(b) Kama zipo ni nchi zipi hizo na ni wafungwa wangapi ambao tumeshafanya nazo zoezi hilo la kubadilishana wafungwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda nijibu swali la Mhehsimiwa Ritta E. Kabati, lenye sehemu (a) na (b), kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini Mkataba wa kubadilishana wafungwa na nchi mbili tu. Ambazo ni Thailand na Mauritius.

(b) Nchi tulizoingia nazo Mkataba ni hizo mbili na mpaka sasa tumeishafanikiwa kupokea wafungwa 10 kutoka nchini Mauritius na kati ya hao tisa (9) walikuwa ni wanaume na mmoja (1) ni mwanamke. Wafungwa tisa hao waliopokelewa wameishamaliza adhabu zao, na amebakia mfungwa mmoja ambaye atamaliza mwaka 2021.

**MHE. RITAA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Ninakushukuru Mheshimiwa kwa majibu uliyonipatia lakini ninaomba nikulieze maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa nchi za China na India, tumekuwa nao mahusiano mazuri sana ya kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia na kwa kuwa kuna baadhi ya Watanzania wenzetu wamefungwa huko kutokana na makosa mbalimbali.

Hata tulipokwenda China tulipata taarifa kwamba Watanzania wengi sana wamefungwa China.

Je, kwa nini Tanzania isijenge mahusiano ya kubadilishana Wafungwa kati ya Tanzania na nchi hizo?

Swali la pili, kwa kuwa kuna baadhi ya Watanzania waliofungwa katika nchi mbalimbali kutokana na makosa yakiwemo ambayo yamesababishwa kupatiwa adhabu ya kifo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia msaada wa kisheria wafungwa ambao wamefungwa katika nchi hizo nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, uhusiano wetu na China na India ni mzuri sana. Hata hivyo katika mataifa ambayo raia wetu wengi wamefanya makosa huko basi ni hizo nchi mbili ambazo umezitaja. China, Kenya na India ndiko kuliko na Watanzania wengi ambao wana migogoro na sheria za huko.

Kama nchi taratibu tunazichukua kuhakikisha kwamba kupitia Diplomasia tunaweza tukaingia mkataba kama tulioingia na nchi nyingine ili hawa watu ambao wako kwenye maeneo yale waweze kuja kutumikia vifungo vyao vilivyobakia baada ya Mikataba kufungwa hapa nchini.

Watu ambao wako nchi mbalimbali wana *access* ya huduma za kisheria kama watawasiliana na Balozi zetu ambazo ziko kule. Hatuwezi tukawatelekeza, isipokuwa jambo moja kubwa ambalo ningelisema hapa ni kwamba kwa wananchi wetu wanapotaka kwenda nchi yoyote ile, jambo la kwanza wajue sheria za kule.

Wajue Sheria za kiuhamiaji na nyingine, ili wasiwe wanafanya makosa pengine wakiwa hawajui au kwa makusudi. Basi wajaribu kuepuka kufanya makosa wanaposafiri huko.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, zipo habari kwamba Wafugnwa waliofungwa katika nchi hii ya Mauritius ni wale wanaojishughulisha na Madawa ya Kulevya. Ndiyo maana nchi iliingia makataba wa kubadilishana wafungwa.

Je, ni kwa nini Serikali ikawa imeingia na nchi mbili hizi kubadilishana wafugnwa na si zaidi na kwa sababu zipi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda nijibu swali moja la Mheshimiwa Haroub Muhamed Shamis, kama hivi ifutavyo:-

Mikataba ambayo mpaka sasa hivi iko hai, ni ya Shelisheli na Mauritius na hata huko ambako hatuna mikataba makosa makubwa waliyoyafanya Watanzania ni ya Madawa ya Kulevya. Pengine kuendelea kufanya mikataba kunaweza kukawanufaisha.

Lakini ninafikiri jambo la kwanza ni kujaribu kuwasihi vijana wetu kuachana na mambo hayo. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba bado tuna nchi ambazo tunaendelea kujadiliana nazo na pengine hatima yake itakuwa ni mikataba mingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuendelee na Wizara ya Maji, muda wetu unakwisha. Ninamwita sasa Mheshimiwa Dkt. Agustine Lyaonga Mrema, atakayeuliza swali kwa niaba yake ni Mheshimiwa Betty Machangu. *(Makofi)*

Na. 114

**Kusambaza Maji ya Kutosha Njia Panda – Himo**

**MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya wananchi katika kijiji cha Kilototoni, Njia Panda Himo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kilototoni Njia Panda-Himo ni kati ya vijiji vinavyopata huduma ya maji kutoka kwenye mradi wa maji Kiria-Kahe uliofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani, ambao ulikamilika mwezi Desemba, 2012. Asilimia 45 ya wananchi wa kijiji hicho wanapata huduma ya maji kutoka kwenye mradi huo.

Aidha, Halmashauri kwa kushirikiana na Shirika la Ujerumani liitwalo *AKO (Aktionskreis Ostafrika e.v.)* ina mpango wa kuboresha mradi wa maji wa Kilema-Mandaka ili uweze kutoa huduma ya maji kwa asilimia 100 kwa wananchi wa kijiji cha Kilototoni, Njia Panda-Himo.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kujenga chanzo cha chemchem cha Manga, ambacho kitaongeza maji kwenye mradi wa Kilema-Mandaka na kujenga miundombinu ya maji itakayotoa huduma ya maji eneo lililobakia la Kijiji cha Kilototoni Njiapanda-Himo. Shirika la *AKO* limetenga jumla ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya kazi hiyo ambapo utekelezaji wa mradi huo umeanza mwaka huu 2014/2015.

Kazi ya ujenzi wa tanki la mita za ujazo 100 umekamilika, ujenzi wa chanzo umefikia asilimia 20 na ununuzi wa mabomba unaendelea kufanyika. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2015.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali la nyongeza. Ni hivi karibuni nilimwuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba kumekuwa na mradi wa vijiji 10 kwenye kila Wilaya.

Lakini kwa zaidi ya miaka 10 sasa huo mradi haujatekelezeka na mimi nikasema katika Jimbo la Vunjo kuna vijiji vinaitwa Mawanjeni, Matala kwa miaka 52 sasa yaani tangu wakati wa uhuru mpaka leo hawajapata maji na nikasisitiza nikasema hivi ni vijiji ambavyo viko chini ya Mlima Kilimanjaro ambao ndio unatiririsha maji.

Sasa nikamwuliza Mheshimiwa Waziri ni lini Serikali itatoa maji katika vijiji hivi?

Mheshimiwa Spika, kuna wanasiasa wanapenda umaarufu kwa kuwaambia wananchi kwamba wasichimbe mitaro wakati *contractor* wa maji anapotaka kuweka maji. Nataka Serikali ifafanue.

Je, ni nani ana jukumu la kuchimba ile mitaro au wananchi wanashirikishwaje katika hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nilikiri kwamba vijiji anavyovitaja vipo katika mpango wa Vijiji 10 ambao tutautekeleza na katika bajeti yetu ya milioni 900 tayari tumeshapeleka shilingi milioni 295. Kwa hiyo, awe na subira na nimefika maeneo hayo, tutaendelea kutekeleza.

Swali la pili, ni kuhusu wananchi kuchangia, katika Miradi hii ya Vijiji Kumi kila kijiji kinatakiwa kuchangia kati ya 4% hadi 5%. Kwa hiyo, wakati mwingine wananchi wenyewe wanaamua kwamba tutashiriki katika kazi kama hizo au kwa maana ya kuchangia pesa.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said!

Na. 115

**Ahadi ya Kuajiri Vijana 15 Kutoka Zanzibar Waliosomea Masuala ya Mambo ya Nje**

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID** aliuliza:-

Wapo vijana 15 waliosomea masuala ya Mambo ya Nje walioahidiwa kuwa wataajiriwa pindi watakapomaliza mafunzo hayo lakini hadi sasa hawajaajiriwa;

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, kwa nini mpaka sasa hivi vijana hao hawajaajiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Mwanakhamisi Kassim said, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuleta uwiano wa watumishi wanaofanya kazi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara iliahidi kuajiri vijana 15 kutoka Zanzibar. Kufuatia ahadi hiyo, ni kweli kwamba vijana 18 walianza mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Masuala ya Mambo ya Nje *(Postgraduate Diploma in International Relations)* katika Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Jijini Dar es Salaam mwezi Novemba, 2011. Kati ya hao, vijana 17 ndiyo waliokamilisha tafiti zao na kuziwasilisha Februari, 2013 na kuhitimu mafunzo yao Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu wa watumishi na kuleta uwiano kati ya pande mbili za Muungano, Wizara imechukua hatua ya kuomba kibali Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumisni wa Umma, cha kuajiri Watumishi wapya 34 wa kada mbalimbali ikiwemo kada ya Maafisa Mambo ya Nje katika mwaka wa fedha 2013/2014. Baada ya maombi hayo, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitoa kibali cha nafasi 19 tu.

Mheshimiwa Spika, kati ya nafasi hizo 19 za ajira mpya zilizoidhinishwa na Utumishi, Wizara ilitakiwa kutenga nafasi nne kwa upande wa Zanzibar. Hata hivyo, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza idadi, Wizara yangu ilipeleka mapendekezo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili nafasi saba badala ya nne zitengwe kwa watumishi waliohudhuria mafunzo ya kidiplomasia katika Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwahamisha watumishi hao kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuja Serikali ya Muungano wa Tanzania, kujaza nafasi hizo saba zilizoidhinishwa unafanywa kwa mujibu wa taratibu za miongozo iliyopo na tunaamini kuwa katika muda mfupi ujao watumishi hao wataweza kujiunga na Wizara. Nafasi nyingine

nane kati ya 15 zilizotolewa na Wizara kwa upande wa Zanzibar zitaendelea kushughulikiwa kulingana na ikama ya Wizara.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said swali la nyongeza.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nasikitika kwa Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyonijibu, lakini wanafunzi niliouliza mimi siyo hao anaosema yeye, ni wanafunzi kutoka Zanzibar. Je, ni lini wanafunzi hao niliouliza wataajiriwa katika Wizara yako?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Ni kwamba utaratibu uliopo sasa hivi kwa ajira ambazo ni za Muungano ni 79% kwa 21%, lakini *the bottom line* ni *qualifications*. Kwa hiyo, wanafunzi wa Zanzibar au watu wa Zanzibar au vijana wa Zanzibar wakitaka kuajiriwa zile nafasi huwa zinatangazwa pande zote mbili, nafasi hizo za Muungano. Kwa hiyo, kama zimetoka hizo 19 lazima wao watapata 21%. Hiyo tumeshakubaliana na Waziri mwenzangu na kwa upande wa Serikali nzima hilo wanalijua na tutatekeleza hivyo kwa nafasi zote ambazo ni za Muungano.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kwamba labda kutakuwa na upendeleo wa aina fulani, hapana! Kama wata-*apply* sisi tutawachukua, lakini wakati mwingine hawaombi kabisa, hivyo huwezi ukalazimisha kwamba lazima waajiriwe.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Magdalena Khamis Sakaya atauliza swali hilo!

**Masoko ya Uhakika kwa Mazao ya Wakulima**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:

Mwaka 2014/2015 Serikali ilianzisha utaratibu mpya wa kuwapatia wakulima pembejeo za kilimo na Vyama vya Ushirika kupata mkopo kutoka katika Taasisi za Fedha ili kuongeza uzalishaji:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha mazao ya wakulima yanapata masoko ya uhakika ili waweze kulipa mikopo kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuhimiza na kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula ikiwemo utaratibu kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na chakula cha kutosha.

Kutokana na mikakati hiyo katika msimu wa 2013/2014 uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia jumla ya tani 16,015,238 ambapo tani 6,734,437 ni mahindi na tani 1,681,125 ni mchele na hivyo taifa kujitosheleza kwa chakula kwa 125%. Aidha, makadirio ya mahitaji ya mazao ya chakula kwa Taifa ni tani 12,767,879 na hivyo kuwepo na ziada ya tani 3,247,359 za mazao yote ya chakula ambapo ziada ya mahindi ni tani 1,547,568 na mchele ni tani 794,161.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba, mazao ya wakulima yanapata masoko ya uhakika na

endelevu, Serikali kwa kushirikiana na wadau inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuongeza uwezo wa *NFRA* na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko wa kuhifadhi nafaka ghalani…..

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sana tupunguze kuzungumza kwa sababu anayejibu wala hasikiki.

Naomba uendelee kujibu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze hiyo *para* upya.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha mazao ya wakulima yanapata masoko ya uhakika na endelevu, Serikali kwa kushirikiana na wadau inatekeleza mikakati ikiwemo kuongeza uwezo wa *NFRA* na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko wa kuhifadhi nafaka ghalani kwa takribani tani 740,000 ifikapo mwaka 2016/2017; kuimarisha mfumo wa masoko ikiwemo Stakabadhi Ghalani na Soko la Bidhaa (*Commodity Exchange*); Kuboresha mifumo ya taarifa za mawasiliano za uzalishaji na masoko; kujenga masoko katika vituo vya mpakani ili kurahisisha uuzaji wa mazao nje na kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kwa kusambaza taarifa za hali ya chakula na taarifa kuhusu masoko ya nje ya nchi ili iweze kushiriki katika biashara ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, mikakati mingine ni pamoja na kuruhusu uuzwaji wa mazao nje ya nchi bila vikwazo na kurahisisha taratibu za utoaji wa vibali ambapo Wizara imekasimisha madaraka ya utoaji wa vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ambapo wale wote wenye kuhitaji watapata huko karibu na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko itaendelea kutafuta masoko ya mazao katika nchi za nje ambapo ziara za kutafuta masoko zimefanyika katika nchi za Kenya, Sudani ya Kusini, Comoro na Afrika Kusini.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutafuta masoko zaidi nchi za Congo DRC, Comoro, Burundi, Oman na Gulf States.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika kukabiliana na tatizo la miundombinu ya uhifadhi wa nafaka Serikali imepanga kujenga maghala mapya na vihenge *(silos)* kwenye maeneo ya kimkakati pamoja na kukarabati maghala 275 ya vijiji kupitia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)* ambapo katika mwaka 2013/2014 maghala 30 yamekarabatiwa na katika mwaka wa fedha 2015/2016 maghala 207 yatakarabatiwa. Maghala hayo yatatumika kuhifadhi mazao ya ziada na yataunganishwa na mfumo wa Stakabadhi Ghalani na soko la bidhaa (*Commodity Exchange*).

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sakaya swali la nyongeza!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize maswali mawili madogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati mingi iliyoelezwa na Naibu Waziri kwenye swali langu la msingi, bado mazao ya wakulima ya mwaka jana mengi hayajapata masoko na wengi wameshindwa hata kulima msimu huu na wengi wameshindwa hata kulipa ada za watoto wao kwa sababu bado mazao yapo ndani na mengine pia yameharibika.

Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Waziri anasema wamefanya ziara maeneo mbalimbali ikiwemo Kenya, Sudan, Comoro na Afrika Kusini. Soko la ndani la mazao ni dogo sana. Ni nini mafanikio ya ziara hizi kwanza badala ya kuendelea na ziara nyingine anazosema sijui kwenda Gulf State, Burundi, Oman, Congo na Comoro. Ni nini mafanikio kwanza ya ziara hizi za nchi hizi ambazo hakuna majibu ya nini kimetokea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, mikopo ya benki ina muda wa kurudisha na pia ina riba na Serikali imeanzisha mfumo mpya wa wakulima kwenda kukopa kabla ya kuandaa mfumo wa masoko. Serikali haioni hatari ya wakulima kuja kufungwa na kufilisiwa kwa kushindwa kulipa mikopo ya benki kwa wakati? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, anauliza kwamba nini mafanikio, naweza kusema kwamba mafanikio ni makubwa sana ila muda ni mfupi na kwamba hatuwezi kuandika kila kitu kwenye majibu tunayojibu hapa mbele.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Mahindi ziada tani 1,500,000, hivi ninavyozungumza Wizara yetu kupitia Kitengo chake cha Usalama wa Chakula kimefanya tathmini ya mazao yaliyopo nchini kwa wakulima. Sasa kutoka ziada ile 1,500,000 sasa hivi kwenye soko kuna mahindi ambayo hayazidi tani 700,000 kwa wananchi. Kwa maana nyingine ni kwamba taratibu hizo tulizozitoa, masoko ambayo tumeyatafuta, zaidi ya tani 800,000 tayari zimeshauzwa nje ya nchi, lakini pia wapo na wananchi ambao wananunua humu humu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Shirika la Umoja wa Mataifa *(World Food Program – WFP)* tumeshaingia nao mkataba wa kuwauzia zaidi ya tani 50,000 na wameshachukua kati ya hizo zaidi ya tani 20,000 na wanaendelea. Watu binafsi pia wamechukua mahindi hayo, taasisi zetu kama vile Magereza, shule na maeneo mengine wameshachukua mahindi zaidi ya tani 10,000 na tunaendelea hivyo. Kwa hiyo, kuna soko la nje na soko la ndani bado mahindi haya yanaendelea kwenda na hivyo hivyo pia kwenye suala la mpunga au mchele.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anasema kwamba wakulima wanakopa benki na kwa maana hiyo wanaweza kushindwa kulipa. Kwanza naomba niseme mahindi tunayonunua tunaomba yawe ya wakulima na hatufikiri mtu anakwenda kukopa benki halafu anakuja kununua mahindi

anaiuzia *NFRA* sasa yanapotokea matatizo ya kibajeti kama ilivyotokea mwaka huu Serikali ikashindwa kulipa mapema watu wanaanza kupigwa riba za kibenki.

Mheshimiwa Spika, naomba nilifahamishe Taifa na wakulima kwamba mwaka unaokuja tutanunua mahindi kwa wakulima na hatutanunua mahindi kwa wafanyabiashara kwa sababu wafanyabiashara hawa wamekuwa wanawalalia sana wakulima. Kwa hiyo, tunataka tuhakikishe kwamba mahindi tunayonunua au mchele au mtama ni wa wakulima wenyewe na siyo wafanyabiashara. Kwa hiyo, wasiende kukopa benki halafu baadaye wakicheleweshewa wanaanza kusema tunapata hasara kwa sababu riba za benki zinakuwa kubwa sana.

**SPIKA:** Naomba tuendelee, nina maswali sita kwa muda wa dakika kumi, haiwezekani! Kwa hiyo, nakwenda Wizara ya Kazi na Ajira Mheshimiwa Sylvester Mabumba atauliza swali hilo.

Na. 117

**Tatizo la Ajira Nchini**

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA** aliuliza:-

Suala la ajira hapa nchini limekuwa ni tatizo kubwa sana:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulipatia ufumbuzi tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ukuzaji ajira nchini linahusisha wadau wote ikiwemo Serikali, Sekta Binafsi,

Mashirika ya Kijamii na ya Kidini, pamoja na vijana wenyewe wasio na ajira. Jukumu kubwa la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ya kisera, kisheria na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mikakati mbalimbali ya namna ya kutatua tatizo la ukosefu wa ajira nchini kama ifuatavyo:-

(i) Serikali imekuwa ikitoa mafunzo na miongozo ya namna ya kuingiza masuala ya ukuzaji wa ajira katika bajeti na program za Wizara, Idara za Serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo la mafunzo haya ni kuwezesha taasisi hizi kubainisha fursa za ajira zitakazozalishwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

(ii) Wizara ya Kazi na Ajira imeandaa Program ya Kukuza Ajira kwa vijana ambayo imejikita katika kuwapatia vijana mafunzo ya ujasiriamali, mikopo ya masharti nafuu na maeneo ya uzalishaji na biashara.

(iii) Serikali imeendelea kuboresha sekta ya elimu na mafunzo ili iweze kutoa wahitimu wenye taaluma zinazoendana na mahitaji ya soko la ajira na hivyo kufanya wahitimu wengi kuwa na ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira.

(iv) Serikali imeendelea kuboresha mitaala kwa kuhitimiza vyuo kuingiza masomo ya ujasiriamali.

(v) Serikali pia imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwenye sekta zenye uwezo wa kutoa ajira zaidi ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye sekta mbalimbali na hivyo kufanya vijana wengi waweze kuajiriwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabumba maswali ya nyongeza!

**MHE. SYLSVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali

madogo ya nyongeza. Kwanza, kutokana na mikakati na program ambazo yeye kaelezea hapa, nataka kujua ni tathmini ipi ya kina ambayo Serikali imefanya kubaini kama mikakati hii imekuwa na tija katika suala zima la ajira kwa vijana?

Pili, kama tutakumbuka vizuri, wakati wa mdororo wa uchumi Serikali ilikuwa ina mpango wa dharura kunusuru wafanyabiashara nchini. Je, haioni sasa ni wakati muhimu au muafaka kuja na mpango wa dharura kuhakikisha kwamba vijana na akinamama wanapata ajira kwa sababu wengi wanateseka sana mitaani na katika nchi yao hii wakiwa wengine wamesoma vizuri, je, tatizo hili litakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, mikakati hii imeanza na imeanza kuzaa matunda na tumekuwa tukitoa taarifa za ajira ambazo zinapatikana kwenye maeneo mbalimbali ya Serikali pamoja na yale ya uzalishaji ikiwa ni pamoja na kilimo. Nina hakika kwamba mikakati hii tukiendelea kuifanyia kazi tutaweza kufanikiwa, lakini ni mpango wa ajira wa dharura.

Mheshimiwa Spika, nadhani tukiendelea na mikakati hii ambayo nimeieleza, tutafanikiwa na napenda niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yenu ninyi ni wadau wakubwa sana. Hetu tusaidieni katika suala la kukuza ajira kwenye Majimbo yetu kwanza kwa kuainisha na kutambua vijana wanaohitaji ajira na baada ya hapo ndipo tuweze kuwaona wadau mbalimbali waweze kusaidia.

Mheshimiwa Spika, ningewaalika katika Jimbo la Segerea, mje muone jinsi ambavyo tumeweza kutambua vijana wako wapi, vikundi na vijiwe karibu 500 vya bodaboda, wajasiriamali, Mamantilie na *VICOBA* na baada ya hapo sasa tunakwenda kwenye hatua nyingine ya kuona tunaweza tukawasaidia vipi na hii mitaji na mikopo haipatikani Serikalini tu, lakini hata kwenye sekta binafsi inawezekana.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Mendrard Lutengano Kigola!

Na. 118

**Kuongeza Nafasi za Ajira kwa Vijana**

**MHE. MENDRARD L. KIGOLA** aliuliza:-

Taifa linakabiliwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa vijana wote wanaomaliza Vyuo Vikuu wanatafutiwa kazi?

(b) Je, kwa nini Serikali isiandae mikakati maalum ya kuwapa vijana mitaji kwa njia ya mikopo ili waweze kujiajiri.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mendrard Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa takwimu zinaonesha kwamba, takribani Vijana 150,000 wanahitimu kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu nchini kila mwaka, lakini nafasi za kazi za kuajiriwa vijana hawa wanaomaliza Vyuo Vikuu na Elimu ya Juu, Serikalini, Sekta nyingine ya Umma na Sekta binafsi ni takribani 50,000 tu. Kwa maana hiyo, kwa hali ya sasa ya uchumi na maendeleo nchini ikiwemo na hali yetu ya maendeleo ya viwanda, vijana wote wanaomaliza masomo vyuo vya elimu ya juu hawawezi kupata ajira ya kuajiriwa. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili vijana wanaomaliza elimu ya juu na kukosa ajira ya kuajiriwa na pia vijana wengine,

waweze kujiajiri kwenye sekta ya ujasiriamali, kilimo na biashara. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kushirikiana na taasisi za elimu, programu za ujasiriamali zinahamasishwa katika ngazi mbalimbali za elimu ili kufundisha stadi za ujasiriamali na kuhimiza tabia za kujiajiri hasa kwa vijana wanaomaliza ngazi mbalimbali za masomo ndani.

(ii) Wizara ya Kazi na Ajira imeandaa programu ya Kitaifa ya muda mrefu ya kukuza ajira ambayo nimeielezea katika jibu langu kwenye swali lililopita. Programu hii itawezesha makundi ya vijana wa kike na kiume wajasiriamali kuwezeshwa kwa kupata mafunzo na mitaji ya uzalishaji ili kuwawezesha kuendeleza miradi ya kiuchumi, kujiajiri na hata kuajiri wengine. Mpango wa muda mfupi utakuwa mwanzo wa kigezo cha kutekeleza kwa ufanisi mpango wa muda mrefu.

(iii) Kwa kushirikiana na taasisi za mafunzo, utafiti, Vyama vya Waajiri na Wafanyakazi, Wizara itaanzisha na kutekeleza programu rasmi na zisizo rasmi za mafunzo ili kuongeza uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa kwa nguvu kazi hii ya Taifa katika ajira rasmi na ya kujiajiri.

(iv) Wizara imekuwa pia ikishiriki maonesho na programu zingine kama vile maonesho ya Ujasiriamali ya Nguvukazi/Juakali ambayo huandaliwa kwa mzunguko na nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile kuna programu nyingine na mfano ni ile ya kukuza ajira ijulikanayo kama "Kazi Nje Nje."

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Mifuko kadhaa ya mitaji ya kuwakopesha vijana na wajasiriamali. Mifuko hii imeanzishwa katika Wizara mbalimbali kama Wizara ya Kazi na Ajira, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Uwekezaji na Uwezeshaji, TAMISEMI na Wizara ya Fedha ikiwemo

na Benki Kuu. Pia Serikali inahamasisha sekta binafsi na benki za biashara kuwakopesha vijana kwa riba nafuu ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine.

Mheshimiwa Spika, toka asubuhi masuala haya yamekuwa yakizungumzwa na wenzangu kutoka Serikalini, kwa hiyo, nadhani imeeleweka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigola swali la nyongeza!

**MHE. MENDRARD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu ya Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, Serikali ilikuwa imetangaza kwamba, itashusha ajira kwenye Halmashauri zetu, lakini cha ajabu Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi mpaka leo haijapewa kibali kwa ajili ya kuajiri wafanyakazi pale na tuna *shortage* kubwa ya wafanyakazi katika sekta zote; afya kule hatuna wafanyakazi, hata Watendaji wa Vijiji hatuna wengine tuna matatizo hayo. Je, Serikali itatoa kibali lini kwa Wilaya ya Mufindi ili iweze kuanza kutoa ajira? (*Makofi*)

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri ametaja kwamba, kuna Mifuko katika Wizara kwa ajili ya kusaidia vijana, lakini sijawahi kuona Wizara yoyote hata Wizara yake ya Kazi na Ajira, huo Mfuko ukitoa fedha kwenye Wilaya zetu. Je, yuko tayari kuniandikia barua niweze kufuatilia hiyo Mifuko ili vijana wangu wa Wilaya ya Mufindi waweze kupewa hiyo mitaji kwa lengo la kuwawezesha kuendesha shughuli zao?

**SPIKA:** Naomba ujibu sehemu ya pili, sehemu ya kwanza atajibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, Mifuko hii niliyoitaja ipo na toka asubuhi imekuwa ikitajwa na Waziri wa Uwezeshaji na Uwekezaji pamoja na Wizara ya Fedha. Ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge kwenye Jimbo lake ni kufanya maandalizi haya ya kutambua vijana ambao wako kwenye vikundi vya ujasiriamali na kama vigezo

vitakuwa vinawezekana, basi yeye aje kwenye Wizara hizi ambazo nimezitaja kulingana na mahitaji wanaweza wakapata hiyo mitaji na mikopo.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejementi ya Utumishi wa Umma)!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa zile nafasi mbadala huwa hazina matatizo ya kibali kwa sababu bajeti yake inakuwepo, lakini kwa nafasi mpya inabidi Wakurugenzi au Maafisa Utumishi waingize bajeti kwenye mfumo wetu wa kielektroniki ambao ni taarifa za wafanyakazi pamoja na mishahara. Wasipoingiza kwenye mfumo hawawezi wakapata kibali kwa sababu bajeti yao haipo, lakini kama bajeti yao ipo na wameweka kwenye mfumo kwa mwaka husika kibali kinatolewa wakati wowote. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge alete barua tu, kama ziko kwenye mfumo tutampa kibali wakati wowote.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Suleiman Nchambi. Hayupo! Kwa niaba yake Mheshimiwa Jafo!

Na. 119

**Kusitisha Uwindaji wa Kitalii na Kiraia**

**MHE. SELEMAN S. JAFO (K.n.y. MHE. SULEIMAN N. SULEIMAN)** aliuliza:-

Ujangili umekithiri sana nchini:-

Je, kwa nini Serikali isisitishe uwindaji wa kitalii na wa kiraia kwa kipindi cha miaka kumi (10) kama ilivyowahi kufanya huko nyuma?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.N. MADELU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Nchambi, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Uwindaji wa kitalii ni moja ya matumizi endelevu ya raslimali ya wanyamapori. Kazi ya uwindaji wa kitalii huongozwa na matokeo ya utafiti unaotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori hapa Tanzania. Kupitia tafiti hizo Wizara hukusanya takwimu kuhusu idadi ya wanyamapori na wanyamapori wanaoweza kuwindwa bila kuathiri ongezeko la idadi ya wanyamapori. Kwa mfano, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti, uwindaji unalenga kupunguza wanyamapori madume yaliyofikia ukomo wa kuzaa (yaani wanyamapori wazee).

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utafiti kutoka *TAWIRI* hutumiwa na Wizara kutoa migao ya wanyamapori wanaopaswa kuwindwa na uwindaji husimamiwa na Idara ya Wanyamapori kwa kuzingatia Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwindaji huu, Serikali pia hupata fedha za kigeni. Kwa mfano, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2013/2014, Serikali ilipata wastani wa USD 17.9 na Sambamba na mapato haya, pia uwindaji wa kitalii hutoa ajira kwa Watanzania takribani 3,700. Aidha, shughuli za uwindaji wa kitalii hufanyika kwa uadilifu mkubwa ambapo wawindaji huzingatia migawo ya wanyamapori inayotolewa kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, uwindaji wa kitalii na kiraia huchangia katika kuimarisha ulinzi wa maeneo ambayo zoezi hilo hufanyika. Uwepo wa wawindaji hao siyo tu hupunguza wawindaji haramu, bali pia huimarisha miundombinu kama vile barabara, nyumba za kulala wageni na mifumo ya maji

safi kwa watumishi. Makampuni ya uwindaji wa kitalii husaidia katika kuimarisha ulinzi wa vitalu, hivyo kufunga shughuli za uwindaji wa kitalii kutapunguza ulinzi katika vitalu husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada za makusudi katika kupambana na ujangili hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya watumishi hususan askari, kufanya doria za mara kwa mara na doria maalum.

Mfano katika Pori la Akiba la Selousy idadi ya askari imeongezeka kutoka 250 kwa mwaka 2012 hadi kufikia 680 mwaka 2014 ambapo pia siku za doria zimeongezeka kutoka 30,000 mwaka 2012 hadi 163,000 kwa mwaka 2014, kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uhifadhi ya Wanyamapori, kuzinduliwa kwa Mkakati wa Kupambana na Ujangili, kufanya uelimishaji wa wananchi na Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau imefanya makubaliano ya Kimataifa ya uhifadhi ambapo imefanya makubaliano ya Kimataifa ya uhifadhi ambapo imeazimia masuala mbalimbali. Moja ya maazimio yaliyosainiwa ni Makubaliano ya Arusha yanayohusu uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, Makubaliano ya Arusha yanalenga kukuza ushirikiano baina ya Tanzania, Uganda, Kenya, Msumbiji, Malawi, Sudani ya Kusini, Zambia na Burundi katika kutokomeza ujangili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafo swali la nyongeza!

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana tena yaliyotosheleza, nataka kuuliza swali moja tu la nyongeza. Uwindaji wa Kitalii kama tulivyosema unaleta sana pato la uchumi na tukizungumzia nchi yetu kwa sasa hivi tunakabiliana na changamoto kubwa sana ya kibajeti, lakini Wizara hii tunapozungumza suala zima la uwindaji wa kitalii juzi juzi tu tulitoa maazimio kwamba, Serikali itoe tangazo lakini mpaka hivi sasa tangazo halijatoka.

Nini kauli ya Serikali kwa ujumla kwa sababu tunataka mapato katika sekta ya utalii, lakini tunaona badala ya tangazo kutolewa Bungeni linakwenda kutolewa kwenye vyombo vya habari. Serikali inazungumza nini kuhusu hilo?

**SPIKA:** Lile tangazo mbona walisema tarehe 15 Februari! Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi kwa sababu majibu yalikuwa marefu. Ile ahadi ilisema tarehe 15 Februari.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.N. MADELU):** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, Maazimio ya Bunge ambayo Serikali imeyapokea itayafanyia kazi kwa sababu ni maazimio na kama Bunge limeshayapitisha na Serikali imepokea, basi itayafanyia kazi.

**SPIKA:** Lile jibu lake refu mno limekwenda nje ya pale alipouliza. Swali linalofuata Mheshimiwa Clara Mwatuka!

Na. 120

**Kuwaondoa Boko katika Bonde la Mto Lukuledi**

**MHE. CLARA D. MWATUKA** aliuliza:-

Bonde la Mto Lukuledi katika Vijiji vya Nanganga ya Masasi na Nanganga ya Ruangwa lina ardhi nzuri na yenye rutuba na mto huo ni makazi ya viboko ambao huharibu sana mazao katika mashamba ya wakazi wa eneo hilo na Uongozi wa Wilaya unafahamu tatizo hilo:-

Je, ni kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kuleta *Game Scout* ili kuwaondoa viboko hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.N. MADELU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna tatizo la viboko wanaoharibu mazao katika mashamba ya wakazi wa eneo la Bonde la Mto Lukuledi, Vijiji vya Nanganga Wilaya ya Masasi na Ruangwa. Viboko hao huonekana zaidi kipindi cha masika (Disemba – Machi). Sababu za kuongezeka kwa matukio haya ya viboko kuharibu mazao ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kibinadamu, mfano; kilimo na ukataji miti unaopelekea viboko kuharibu mashamba ndai ya mita 60 kutoka kwenye kingo za mto ambapo kisheria hairuhusiwi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya za Ruangwa na Masasi, imechukua hatua mbalimbali za muda mfupi na mrefu katika kutatua tatizo la Viboko. Hatua za muda mfupi zilizochukuliwa ni kuwafukuza na pengine kuwaua viboko panapokuwepo mapambano wanaosababisha uharibifu pindi wanapojitokeza. Hatua za muda mrefu zilizochukuliwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kuajiri Watumishi watatu wa Wanyamapori wanaoshirikiana na Askari wa Wanyamapori wa Vijiji.

Pia Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imeajiri Askari Wanyamapori mmoja ambaye hushirikiana na Askari Wanyamapori wa Pori la Akiba la Lukwika – Lumesule/ Msanjesi. Kwa pamoja wamekuwa wakifuatilia matukio ya wanyamapori Wilayani na kuchukua hatua ipasavyo. Pia katika bajeti ya mwaka 2014/2015 Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imepanga kuajiri mtumishi mmoja wa kada ya Mhifadhi Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Desemba 2013 hadi Machi, 2014 matukio saba ya viboko waharibifu yaliripotiwa ambapo viboko wawili waliuawa katika Vijiji vya Nanganga na Nangookata na viboko watano walirudishwa kwenye maeneo yao kutoka katika Vijiji vya Chikwale, Maparagwe, Chikundi, Namihungo na Nasindi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa wananchi wanaoishi kandokando ya mito na maziwa,

kuweka makazi au shughuli za kiuchumi kwenye umbali usiopungua mita 60 kutoka ukingo wa mto au ziwa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili watambue athari za uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, elimu itaendelea kutolewa juu ya haja ya kuwalinda wanyamapori kupitia *WMAs (Wildlife Management Areas)* hatua ambayo itawanufaisha wananchi kiuchumi kupitia utalii.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa bonde hili la Mto Lukuledi limebanwa kiasi kwamba, upana wake hautoshi kwa kilimo na wakazi wa vijiji hivi viwili wanategemea sana bonde lile kwa mazao mchanganyiko ya chakula na kilimo cha umwagiliaji. Sasa hatua ya kusema kwamba, wachukue tahadhari kwa kukaa mbali na mto kwa mita 60 haiwezekani kwa sababu kilimo hicho cha umwagiliaji kinahitaji maji yatoke mtoni na kilimo cha mazao mchanganyiko kinategemea bonde hilo hilo ambapo hivi sasa wakulima wanakimbia mashamba yao na kwenda kutanga tanga majangwani. Je, Serikali inasemaje juu ya kunusuru mashamba haya ili yamilikiwe na wenyewe? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa, Serikali inaona ugumu kuwaua wanyama hawa ingawa imesemwa hapa kwamba kuwaua na kuwafukuza, lakini san asana tunaambiwa tusiwaue labda kama wameharibu mazao, lakini zaidi ni kuwatunza. Je, ili kunusuru mashamba ya watu hawa, Serikali haioni haja ya kuwafukuza hawa wanyama ili wenye mashamba wamiliki vyema mashamba yao?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L.N. MADELU):** Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko la wananchi

na ongezeko la shughuli za kilimo hata kama zile mita zisingetengwa bado ongezeko la wananchi lingehitaji ardhi kubwa zaidi kuliko hiyo. Kwa hiyo, la msingi kwa sababu kisheria na kwa afya ya wananchi hawa kukwepa kushambuliwa na viboko, nadhani bado kuna umuhimu wa kuwa na njia mbadala ya Halmashauri kuwa na mpango mzuri wa ardhi kuliko kutegemea ile ambayo itakuwa na mgogoro kwa namna ya kuhatarisha maisha ya wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, hili la pili na lenyewe kwa sababu ni mambo ya kisheria, nimwombe Mheshimiwa Mbunge aridhie kwamba, Serikali imepokea kwa sababu mambo yanayohusu migogoro ya ardhi yanatakiwa yashughulikiwe kisheria ili kupata suluhisho la kudumu ambalo si jambo la kulitolea kauli hapa kabla ya kufuatilia taratibu za kisheria.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale atauliza swali hili!

Na. 121

**Uwepo kwa Madini ya Urani Mlima Mbalizi**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Kumekuwepo na uvumi kwamba, Mlima Mbalizi – Mbeya Vijijini una madini ya Urani na mengine kutokana na utafiti uliofanywa na makampuni kadhaa katika mlima huo.

(a) Je, habari hizi ni za kweli?

(b) Kama habari hizo ni za kweli, je, ni lini kazi ya uchimbaji madini hayo itaanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji

Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika maeneo yanayozunguka Mlima Mbalizi ni kweli kuwa makampuni ya utafutaji wa madini yalipewa leseni ya kutafuta madini na yanaendelea na kazi hiyo. Hata hivyo, taarifa rasmi tulizonazo hivi sasa zinabainisha kwamba, kwenye eneo hilo kuna madini ya *niobium* eneo la Panda Hill na sio madini ya Urani. Kimsingi madini ya Urani hupatikana zaidi kwenye miamba aina ya *granite*, *pegmatite* na *sandstone* ambayo haipo kwenye eneo la Mlima Mbalizi. Aina ya miamba iliyopo kwa wingi katika Mlima Mbalizi ni *volcanic*, *travertine* na *carbonatite* ambayo hata kama ikitokea ikatunza madini ya Urani, itakuwa ni kwa kiasi kidogo sana ambacho hakiwezi kuchimbwa kwa faida.

(b) Mheshimiwa Spika, hatutarajii uchimbaji wa Urani kuwepo kwenye Mlima Mbalizi kwa kuwa hakuna ugunduzi wa madini hayo uliofanyika. Uchimbaji pekee tunaoutarajia kuanza mwaka 2016 ni ule wa madini ya *niobium* huko Songwe, Mbeya chini ya Kampuni ya Panda *Hill Limited* wakati kazi ya kuhamisha Gereza la Songwe itakapokamilika.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Waziri, hata hivyo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, hii kazi ya kutafiti madini katika Mlima Mbalizi imechukua muda mrefu na imekwenda kwa karibu miaka sita au saba iliyopita. Je, kazi hiyo itakwisha lini sasa?

Swali la pili, Mlima Mbalizi umezungukwa na watu wengi, hasa Mji mdogo wa Mbalizi, watu wamelima, wamejenga, Serikali inawaambia nini wananchi wale ili kutowakatisha tamaa maana wasije wakafikiri kwamba, watahamishwa au watafanywa nini. Naomba Serikali iwe na kauli yake hapa. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ni kwamba kazi ya utafutaji na uchimbaji wa madini huchukua muda mrefu kwa sababu unaanza na *initial survey,* unakwenda ukishapata dalili unaanza kuchoronga kutafuta, ukishafikia hatua hiyo unaanza kutafuta pesa na ukishapata pesa ndipo unaanza kuomba madini ili upate *MDA* kwa ajili ya uendelezaji. Kazi hii inaendelea na itakapokamilika Serikali itaingia mkataba na wawekezaji na madini yataanza kuchimbwa kwa kadri itakavyokuwa imegundulika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili, kwamba kuna wananchi ambao wamezunguka, niombe tu wananchi watoe ushirikiano na hawa watafutaji wa madini na pale itakapopatikana sheria yetu ya madini itatumika kuwa-*compensate* na kama madini yameshapatikana basi watakuwa *compensated* na watahamishwa kulingana na sheria ilivyo.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na Wizaraya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba atauliza swali hilo!

Na. 122

**Mawasiliano Hafifu Vijiji vya Kinazi na Kajawa**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Katika Jimbo la Manyovu maeneo ya Vijiji vya Kinazi na Kajawa bado mawasiliano ni hafifu sana:-

Je, ni lini minara itawekwa katika vijiji hivyo ili kurahisisha mawasiliano?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilifanya tathmini ya Vijiji vya Kata za Kajana na Kinazi na kuviingiza katika awamu ya kwanza ya mradi unaotekelezwa na Kampuni ya Simu VIETTEL,, ambapo mradi huo unatarajiwa kufikisha mawasiliano katika vijiji 1,500 nchini na kutarajia kukamilika ifikapo Julai, 2015.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpa taarifa Mbunge kwamba Jimbo la Manyovu, Wilaya ya Buhigwe limepata minara katika Kata ya Biharu, Kilelema na Muyama kupitia Mradi wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Obama, swali la nyongeza!

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa majibu yao, lakini maswali yangu mawili yako kama ifuatavyo:-

Wizara ya Mheshimiwa Waziri ilishatoa barua ambayo alikuwa amesema atajenga minara katika Kata ya Biharu ambayo mpaka sasa bado hajajenga, lakini ameahidi tena atakamilisha kupeleka minara ya Kinazi na Kajana. Sijajua atafanyaje na juhudi zake yeye mwenyewe binafsi kuhakikisha kwamba hii minara inajengwa kabla ya muda huu, yeye binafsi ana mikakati gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa niliandika barua kuwapelekea Wabunge kueleza hatua ya utekelezaji, lakini bahati mbaya sana kulitokea matatizo ya ucheleweshaji wa

kufika vifaa na jana tena nimeandika barua kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge hatua tuliyofikia mpaka hivi sasa. Kwa hiyo, naamini karibuni minara hiyo kwenye Kampuni za *VODACOM, AIRTEL* na *TIGO* itaweza kujengwa.

Kuhusu hii awamu ya minara inayojengwa na Kampuni ya *VIETTEL, VIETTEL* ni tofauti na Kampuni nyingine. Hivi sasa *VIETTEL* imefungua Ofisi kila mkoa na kazi ya ujenzi imeanza. Suala tunalolihangaikia sasa hivi ni utoaji vifaa pale bandarini ambapo tunaamini ifikapo wiki inayokuja vifaa vitakuwa vimekamilika na kazi ya kujenga minara hiyo itakuwa imekamilika ifikapo mwezi wa Juni, 2015 kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge mnaona pale mwishoni maswali karibu sita hayajakuwa na maswali ya nyongeza kwa watu wengine, lakini ukiangalia Waheshimiwa Mawaziri majibu yenu ni marefu mno. Kwa hiyo, tutatoa sisi *circular* ya Spika namna mtakavyojibu maswali yatakuwa marefu ya kiasi gani, kwa sababu unakuta mwingine anajibu kitu kingine huko, swali aliloulizwa anazunguka bila sababu.

Kwa hiyo nitatoa *circular* kusudi muwe na *limit* ya majibu. Kwa sababu yakiwa marefu hata wenzenu wanaosikiliza yanakuwa *bored,* kwa maana kwamba inaleta kama usingizi singizi, kwa kuwa inakuwa kama hotuba nyingine. Kwa hiyo yakiwa mafupi yanakuwa *focused* yanatoa nafasi nyingi ya maswali ya nyongeza. Kwa hiyo na hiyo inakuwa *live.*

Kipindi cha maswali kinatakiwa kiwe *live* siyo tena wakati wa hotuba zingine. Ahaa! Siyo wakati huo. Kwa hiyo tutatoa *circular* hiyo kuanzia Bunge lijalo mtakuwa mnaambiwa ni maswali *page* za namna gani na *font* za namna gani. Maana wengine wanafanya *page* moja lakini zile *font* ndogo ndogo kwa hiyo inakuwa kama *page* tatu. Kwa hiyo, hilo mlizingatie tutaitoa hiyo. Nilitaka kutaja Wizara fulani zilizoandika hovyo leo lakini nimewasamehe. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge niwatambue wageni waliopo hapa. Katika jukwaa la Spika pale kuna wageni wafuatao:-

Mheshimiwa Balozi wa Ireland nchini Mheshimiwa Flonnuala Gisenan ameambatana na Ndugu Aran Gorrigan – *Senior Government Advisor* kutoka Ubalozi wa Ireland. Ni wageni wa kwangu leo tutakuwa nao baada ya kipindi cha asubuhi. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani ambao ni Wanamazingira kutoka Mtandao wa Mazingira Dodoma *(DONET)* wakiongozwa na Ndugu Josiah Mshuda – Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao huo. Huyo Mkurugenzi yuko wapi, yuko pale na wenzako wasimame kama wapo. Ahsante sana tumefurahi kuwaoneni. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Highness Kiwia ambao ni Umoja wa Wamiliki wa Maduka ya Dawa kutoka Jijini Mwanza ambao ni Ndugu Bosco Clemence, Ndugu Hussein Ally, Ndugu Gaspar Minja, Ndugu Imelda Ngassa, Ndugu Stella Steward na Ndugu George William.

Wako wapi hao wote niliowataja? Ahsante sana nadhani Waziri atawapeni *appointment,* tumeshazungumza na Mheshimiwa Kiwia atawapangia muda ambao ni muafaka mkae nao, tumeshaongea nao.

Kuna wageni 40 wa Mheshimiwa Gregory Teu (Mb). ambao ni Wenyeviti wa Kata, Mabalozi wa Nyumba Kumi na Viongozi Mbalimbali kutoka Jimbo la Mpwapwa, Dodoma, naomba hawa wageni 40 wasimame walipo, sijui wako wapi naona hata nyumba haikutosha baadaye wataingia.

Tuna wageni 30 wa Mheshimiwa Aliko Kibona ambao ni Wajasiriamali kutoka Jimboni kwake wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje Ndugu Reward Songa, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Ndugu Musa Otieno na Katibu wa CCM Wilaya, Mama

Hamida Mbogo. Naomba wote hao wasimame walipo, ahaa!! ndio nyinyi hapa. Ahsante sana karibu sana. Naona leo mazungumzo yalikuwa ya wajasiriamali nafikiri mmefaidika hapa na hiyo Mifuko waliyosema. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya ambaye ni Ndugu Sylivia Ulanga. Sijui Ulanga huyo yupo wapi. Sylivia yuko pale amekaa. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Abdulla Juma Abdallah Sadala, Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni vijana wahamasishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kuwawezesha walemavu kiuchumi (*Arusha Move Unity*) ambao ni yupo Ndugu Hussein Sechonge – Mwenyekiti; Ndugu Isack Chalo, Ndugu Mary Msuya, Ndugu Timoth Mzava, Ndugu Anneth Peter, Ndugu Disma Kibua. Hawa wako wapi. Ahaa!!! karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 99 wa Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Naibu Waziri wa Uchukuzi ambao ni Makatibu Kata na Makatibu wa Matawi ya CCM kutoka Jimbo la Buchosa, Sengerema wakiongozwa na Ndugu Hassan Moshi Ntalika, naomba wasimame hao wote walipo. Haya karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kikundi cha Wabunge kuhusu masuala ya Lishe, Uhakika wa Chakula na Haki za Watoto ambao ni Ndugu Tumaini Mikindo – Mkurugenzi Mtendaji – PANITA; Ndugu Magreth Paul – Afisa Mradi – PANITA na Ndugu Dkt. Dolf Lintelo – Kutoka Chuo Kikuu cha Sussex Uingereza. Hao wako wapi, *okay* karibuni sana na nyinyi wageni mliotoka mbali karibuni sana. (*Makofi)*

Tuna wageni 52 wa Mheshimiwa Rose Kamili, ambao ni Wajumbe wa Chama cha Wafugaji Tanzania. Naomba hawa wageni 52 wasimame pale walipo. Ahsanteni sana karibuni. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Maru Nagu, ambao ni Wafugaji 70 kutoka Chama cha Wafugaji Tanzania wakiongozwa na Ndugu George Giniuas Bajura – Mwenyekiti wa Chama na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hanang Ndugu Ester Laban. Hawa nao wako wapi sijui naamini kama wameingia. Ni hao hao kwa hiyo walikuwa wageni hao basi. Ahsante karibuni sana. Wameandika vibaya kwa hiyo wageni wa Dkt. Mary Nagu na Mheshimiwa Rose Kamili. *(Makofi)*

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa John Shibuda (Mb.) ambao ni Viongozi wa Chama cha Wafugaji kutoka Kanda ya Ziwa wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Juvenar Mrashan na Katibu wa Chama Ndugu Kusundwa Wamarwa. Hawa saba wako wapi, wote wafugaji wako hapo. Ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni 10 wa Mheshimiwa Martha Mlata (Mb) ambao ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Kata ya Ntyuka wakiongozwa na Mchungaji Gabuleni Mnyikondo wa Kanisa la Sabato Ntyuka na hao wasimame wako wapi? Ahaa ahsanteni sana. (Makofi)

Tuna wageni wa Mhe. Stephen Masele, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni. Yuko Ndugu Jumanne Maziku, Ndugu Juma Derefa, Ndugu Jackson Mhandi na Ndugu Joseph Mpinginya. Naomba wasimame hawa kama wapi. Nafasi nafikiri imetosha watu wengi hawakuenea.

Tuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni, haiwezekani kuweko hapa, Wanachuo wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Kilimo na Mifugo *(TRACD)* – Dodoma. Kama wapo wasimame, *I don't think* nafasi haiwezi kutosha. Basi wataingia baadaye karibuni sana.

Kuna matangazo ya kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa

Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa "C".

Waheshimiwa Wabunge, leo tutakuwa na tafrija ndogo pale viwanja vya wapi? Naomba niwatangazie Wabunge kwamba leo tarehe 6 Februari, kutakuwa na tafrija ya Wabunge kujipongeza kwa kuupokea mwaka mpya wa 2015 na pia kupokea vikombe vya wale Wabunge *Sports Club* walivyopata Arusha mara baada ya kuahirisha Bunge jioni. Tafrija hiyo itafanyika katika viwanja vya Bunge nyuma ya jengo la Utawala sio kwenye viwanja vya maegesho ya gari kama ilivyotangazwa. Kwa hiyo, ni hapa mahali pa kawaida tunapofanya tafrija. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa, mkatoe na uchovu mlionao kwa muda wote mliokaa hapa.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati Teule Iliyoundwa Kuchunguza na Kuchambua Sera Mbalimbali Zinazohusu Masuala ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji na Uwekezaji ili Kubaini Kasoro Zilizomo Katika Matumizi ya Ardhi kama ilivyosomwa Bungeni

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati Teule, Mheshimiwa Ole-Sendeka, kwa sababu hili ni suala la Kisera, halafu ni suala ambalo lina matatizo mengi, nitamruhusu amalize kusoma hiyo hotuba bila ya kujali muda kusudi isomeke yote. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA – MWENYEKITI WA KAMATI TEULE:** Mheshimiwa Spika**,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 122 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, bila ya kuathiri Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayohusu muundo wa Taarifa

ya Kamati Teule, Taarifa hii inasomwa pamoja na Juzuu mbili za maelezo ya matokeo ya uchunguzi uliofanywa na Kamati Teule zikiwa na viambatisho vyake. Viambatisho hivyo, ni:

(i) Randama ya yaliyojitokeza wakati Kamati ilipofanya ziara ya kiuchunguzi;

(ii) Orodha ya Mashamba yaliyotelekezwa kwa muda mrefu bila kuendelezwa; na

(iii) Nakala za Taarifa Rasmi za Bunge zinazohusu majadiliano ya Kamati wakati wa uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha Kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge, chanzo cha kuundwa kwa Kamati hii ni Hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, mnamo tarehe 1 Novemba, 2013.

Hoja hii ilifuatiwa na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kero na madhara yanayotokana na migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Miongoni mwa Wabunge waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mheshimwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani na Mheshimiwa Saidi Amour Arfi waliozungumzia migogoro iliyopo baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, mtoa hoja, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, alipewa nafasi ya kuhitimisha hoja yake na kueleza kama ifuatavyo naomba kunukuu:

"Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa niliyoitoa leo asubuhi wakati wa kuchangia hoja ya kuahirisha shughuli, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, likubali kuunda Kamati Teule ya kuchunguza na kuchambua Sera

mbalimbali zinazohusu masuala ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji, Wanyamapori na uwekezaji ili kubaini kasoro zilizomo katika matumizi ya ardhi na hatimaye kuleta mapendekezo Bungeni ambayo yakitekelezwa na Serikali yatapunguza na kuondoa migogoro ya muda mrefu inayoendelea kati ya Wafugaji na Wakulima, na Hifadhi, Wawekezaji na Watumiaji wengine wa ardhi." Mwisho wa kunukuu.

Maelezo ya Mheshimiwa Profesa Peter Msolla yalitaka kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge kwa ajili ya kuchunguza migogoro miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi na kutoa mapendekezo Bungeni. Baada ya maelezo hayo, hoja iliungwa mkono na kuafikiwa na Bunge.

Kamati Teule ya Bunge iliundwa na Wajumbe wake kutangazwa tarehe 9 Novemba, 2013, chini ya Kanuni ya 120(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 kwa ajili ya kuchunguza sababu za kuwepo kwa migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Wajumbe walioteuliwa na kutangazwa siku hiyo ni: Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Christopher Olenyokie Ole-Sendeka.

Mheshimiwa Spika, baada ya uteuzi huo, katika kikao chetu cha kwanza, Wajumbe walimchagua Mheshimiwa Christopher Olenyokie Ole-Sendeka, kuwa Mwenyekiti wa Kamati, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 19 Januari, 2014 Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliteuliwa kuwa

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kutokana na uteuzi huo, Mheshimiwa Spika alimteua Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, kujaza nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ya Bunge ilipewa Hadidu za Rejea zifuatazo:-

(i) Kuchambua Sera mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi ili kubainisha kasoro zilizomo na kuchunguza mikakati ya utekelezaji wa Sera hizo iliyowekwa na Serikali;

(ii) Kufanya mapitio ya taarifa nyingine za Kamati na Tume zilizoundwa huko nyuma kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji;

(iii) Kuchambua mikakati yote ya Serikali ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji;

(iv) Kuchambua mikakati ya kulinda vyanzo vya maji pamoja na uharibifu wa mazingira;

(v) Kutoa mapendekezo yatakayoondoa migogoro iliyopo na kudumisha uhusiano mzuri na utangamano kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi;

(vi) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na utendaji;

(vii) Mambo mengine yoyote ambayo Kamati itakayoona yanafaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ya Bunge ilipewa Hadidu za Rejea zifuatazo:-

(i) Kuchambua Sera mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi ili kubainisha kasoro zilizomo na kuchunguza mikakati ya utekelezaji wa Sera hizo iliyowekwa na Serikali;

(ii) Kufanya mapitio ya taarifa nyingine za Kamati na Tume zilizoundwa huko nyuma kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji;

(iii) Kuchambua mikakati yote ya Serikali ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji;

(iv) Kuchambua mikakati ya kulinda vyanzo vya maji pamoja na uharibifu wa mazingira;

(v) Kutoa mapendekezo yatakayoondoa migogoro iliyopo na kudumisha uhusiano mzuri na utangamano kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi;

(vi) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na utendaji; na

(vii) Mambo mengine yoyote ambayo Kamati itakayoona yanafaa.

Mheshimiwa Spika, namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake: Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni pamoja na:-

(i) Kupitia machapisho mbalimbali kuhusiana na migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi;

(ii) Kukutana na kujadiliana na wadau mbalimbali wakiwemo wanataaluma na Asasi Zisizo za

Kiserikali (AZISE) na marafiki wengine wa Kamati kama vile Waheshimiwa Wabunge na vyama vya wakulima na wafugaji;

(iii) Kuwahoji mashahidi kutoka taasisi za Serikali;
(iv) Kuchambua nyaraka mbalimbali zilizowasilishwa na mashahidi na marafiki wa Kamati wakati wa majadiliano na mahojiano;

(v) Kutembelea baadhi ya sehemu zilizoathirika na migogoro na kuchaguliwa kama sampuli *(Sample)* katika uchunguzi.

Kamati ilitembelea wilaya kumi na tisa (19) za mikoa kumi na moja (11) ambayo ni: Pwani, Morogoro, Dodoma, Manyara, Arusha, Kigoma, Tabora, Kagera, Rukwa, Katavi, na Mbeya.

Kufanya mikutano ya hadhara katika vijiji 53 vya wilaya za mikoa hiyo kwa lengo la kupata taarifa na maelezo kutoka kwa wananchi wanaoishi kwenye baadhi ya maeneo yenye migogoro ya ardhi. Orodha ya vijiji hivyo ni Kielelezo Na. 01.

Orodha ya Mashahidi waliohojiwa na Kamati pamoja na Marafiki wakiwemo Wabunge waliojadiliana na Kamati kuanzia tarehe 28 Novemba, 2013 hadi tarehe 4 Februari, 2014 ni Kielelezo Na. 02.

Mheshimiwa Spika, hali ya migogoro; baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi imeelezwa katika Juzuu ya Kwanza ya Maelezo kuhusu hali ya migogoro na mapitio ya sera, mikakati na sheria.

Kwa muhtasari, mapitio ya nyaraka zilizofanyiwa kazi na Kamati yameonesha kuwa hali hiyo imedumu kwa muda mrefu sasa licha ya kuwepo kwa Sera, Mikakati na Sheria madhubuti kwa ajili ya kusimamia masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Migogoro baina ya wakulima na wafugaji itaendelea kudumu kwa muda mrefu zaidi endapo haitapatiwa ufumbuzi, ikiwamo jitihada za viongozi kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

Hali ya sasa ya migogoro hiyo ni mbaya zaidi na inatishia kutoweka kwa amani, umoja na utangamano wa wananchi katika maeneo yenye migogoro na taifa kwa ujumla.

Hivi sasa katika maeneo yenye migogoro, uhasama baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi umefikia kiwango cha juu; ambapo imekuwa vigumu kwa jamii hizo kukaa pamoja katika mikutano, kushirikiana katika shughuli za ujenzi wa taifa au za kijamii, kutumika kwa lugha za kibaguzi na ukabila na hivyo kusababisha mapigano ya mara kwa mara na hata mauaji miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, katika kudhihirisha kuwa tatizo hili lilifahamika Serikalini, barua ya tarehe 19 Februari, 1986 yenye Kumb. Na. PMO/DSM/A.40/01/01, kutoka kwa Msaidizi wa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenda kwa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Vijijini, inathibitisha zaidi.

Kwa mujibu wa barua hiyo, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Joseph S. Warioba) alitaka kuona mgogoro baina ya wakulima na wafugaji wa kijiji cha Kambala kilichopo katika wilaya ya Mvomero Mkoa wa Morogoro, unapatiwa ufumbuzi wa kudumu ifikapo tarehe 01 Machi, 1986, kama inavyodhihirika katika nukuu ya barua hiyo, migogoro hiyo bado inaendelea hadi leo ninanukuu:-

"...*pamoja na barua hii, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais atapenda kuona suala hilo linapatiwa ufumbuzi wa kudumu na hatua za haraka zinachukuliwa mara moja kumaliza uhasama uliopo kati ya wafugaji na wakulima*."

Mheshimiwa Spika, Kwa barua hiyo, bila shaka, Mkuu wa Wilaya alitakiwa kuhakikisha kuwa mgogoro unakwisha kabisa ili kuondoa uhasama uliokuwepo baina ya makundi hayo ya watumiaji wa ardhi katika Kijiji cha Kambala. Nakala ya barua hiyo ni Kielelezo Na. 01 kwenye Juzuu ya I.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa ni takriban miaka 28, mgogoro kati ya wakulima na wafugaji wa Kijiji cha Kambala umeendelea kukua na kusababisha vifo, uharibifu wa mali, uvunjifu wa amani na kuathiri shughuli za maendeleo ya wananchi.

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu migogoro hiyo kwa lengo la kubaini kiini, sababu na namna ya kutatua tatizo la msingi. Maelezo ya kina kuhusu matokeo ya baadhi ya tafiti hizo yameelezwa katika Juzuu ya II.

Mheshimiwa Spika, Kwa hali halisi ya migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini, Serikali na wananchi kwa ujumla hawana budi kujitathmini wajibu wao katika kudumisha amani, usalama na maendeleo ya Taifa.

Endapo migogoro hii itaendelea, Taifa lisitarajie kufanikisha Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)* katika shughuli za kiuchumi na kijamii na kukua kwa uzalendo na mshikamano miongoni mwa wananchi. Ni vema hatua madhubuti zikachukuliwa sasa kama ilivyo katika mapendekezo ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, aina na sababu za migogoro; Ili kuchambua vema kiini halisi cha migogoro ya ardhi miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi, uchambuzi wa Kamati umeainisha migogoro hiyo katika aina tano zifuatazo:-

(i) Migogoro baina ya wakulima na wawekezaji.
(ii) Migogoro baina ya wafugaji na wawekezaji.
(iii) Migogoro baina ya wakulima/wafugaji dhidi ya maeneo ya Hifadhi.
(iv) Migogoro baina ya wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, chanzo cha migogoro ya aina zilizotajwa hutofautiana kutoka aina moja na nyingine na sehemu moja na nyingine. Aidha, aina moja ya mgogoro inaweza kusababisha kuibuka kwa aina nyingine ya mgogoro.

Mheshimiwa Spika, Sababu za Migogoro baina ya Wakulima, Wafugaji, Wawekezaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi: Kamati ilibaini kuwepo kwa sababu mbalimbali za kuibuka, kukua na kuendelea kuwepo kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Sababu hizo zimeelezwa katika Juzuu ya I, ambazo baadhi yake ni:-

(a) Vijiji kutokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi.

(b) Kutokutengwa kwa maeneo mahsusi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

(c) Kutotengwa kwa maeneo mahsusi kwa ajili ya malisho.

(d) Kilimo na ufugaji wa kuhamahama.

(e) Kutambua umuhimu na thamani ya ardhi na kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kunakosababishwa na:

(i) Ongezeko kubwa la idadi ya watu na idadi ya mifugo;

(ii) Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya shughuli za ufugaji;

(iii) Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya kilimo;

(iv) Upanuzi wa maeneo ya Hifadhi za Taifa;

(v) kupanuka na kuanzishwa kwa miji mipya;

(vi) Ongezeko la vitalu vya uchimbaji madini na uwindaji;

(vii) Kupungua kwa ardhi inayofaa kwa uzalishaji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa mazingira.

(f) Kutokupimwa na kubainishwa kwa mipaka kati ya vijiji.

(g) Watu wachache kumilikishwa maeneo makubwa ya ardhi.

(h) Kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa sera na sheria.

Mheshimiwa Spika, mfano wa maeneo yasiyosimamiwa vizuri kwa mujibu wa maelezo ya wadau mbalimbali ni:-

(i) Tamko la Sheria ya Ardhi za Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 kuhusu kutengwa maeneo mahsusi kwa ajili ya shughuli za ufugaji;

(ii) Utaratibu wa kupunguza mifugo uliowekwa na Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo, Na. 13 (2010);

(iii) Utaratibu wa vibali maalumu wakati wa kuhamisha mifugo kutoka sehemu moja kwenda nyingine uliowekwa na Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, Na.12 ya mwaka 2010; na

(iv) Maelezo ya Sera ya Maji kuhusu uvunaji, uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa ajili ya matumizi ya mifugo na kilimo.

(i) Kutokuwepo kwa chombo cha kuratibu matumizi ya Ardhi.

(j) Upungufu na ukosefu wa Maji.

(k) Dosari za Maudhui ya Sera na Sheria.

(l) Uwekezaji Usiofuata Sheria na Taratibu ambapo baadhi ya wawekezaji:-

(i) Wamepewa au kumilikishwa maeneo ya ardhi bila wananchi wa maeneo husika kushirikishwa na bila ya kufuata taratibu zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria.

(ii) Wameyatelekeza mashamba jambo linalosababisha wakulima/wafugaji kuvutiwa kufanya shughuli zao katika mashamba hayo wakiamini kuwa ni ardhi isiyo na mmiliki.

(iii) Wawekezaji wanakodisha maeneo yao kwa wakulima au wafugaji badala ya kuyaendeleza kama ilivyokusudiwa. Katika utaratibu huu, wawekezaji

huyakodisha mashamba hayo kwa gharama kubwa ambazo wakulima wadogo au wafugaji hushindwa kuzimudu. Utaratibu huu unachangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro baina yao na wawekezaji.

(iv) Wamepewa mashamba pasipo kufuata taratibu za kisheria. Kwa mujibu wa *Sheria ya Uwekezaji* ya mwaka 1997, wawekezaji wanatakiwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kabla ya kupewa ardhi kwa ajili ya mashamba. Utaratibu uliopo kwa sasa, unamwezesha mwekezaji kupata ardhi kupitia mojawapo kati ya Wizara ya Ardhi au *TIC*.

(m) Kutozingatiwa kwa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi.

(n) Kauli za baadhi ya viongozi wa serikali na viongozi wa kisiasa kusigana na kukinzana kuhusiana na migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

(o) Rushwa kwa baadhi ya Watendaji wa Serikali katika ngazi mbalimbali.

(p) Mila na Desturi za Wakulima/Wafugaji zinazochochea Migogoro ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchunguzi wa Kamati Teule kuhusu migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi yamefafanuliwa kwa kina katika juzuu ya II kwa kufuata mtiririko wa Hadidu za Rejea. Aidha, uchambuzi na matokeo hayo unaainishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya Rejea ya kwanza: Uchambuzi wa Sera na mikakati ya utekelezaji; Kamati ilifanya uchambuzi wa sera mbalimbali ili kubaini na kuainisha namna sera hizo zinavyohusiana na migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Kamati ilibaini kuwa, sera hizo zinatoa mwongozo wa masuala mbalimbali yakiwemo, matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji, uhamasishaji katika uwekezaji na uboreshaji wa sekta za kilimo na mifugo.

Katika hatua hii ya uchunguzi, Kamati ilichambua sera zifuatazo:-

(i) Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997;
(ii) Sera ya Taifa ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997;
(iii) Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013;
(iv) Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006,
(v) Sera ya Maji ya Mwaka 2002,
(vi) Sera ya Uhamasishaji wa Uwekezaji ya mwaka 1996, na
(vii) Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997, Kamati imebaini kuwa Sera ya Taifa ya Ardhi imedumu kwa zaidi ya miaka 18, lakini migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuwepo na kuongezeka licha ya sera hiyo kuwa na maudhui yanayodhibiti kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro.

Maudhui ya Sera ya Taifa ya Ardhi pamoja na mambo mengine, yanatambua uwepo wa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi kama inavyotamkwa na Sera ya Taifa ya Ardhi katika Aya namba 7.3:- Naomba kunukuu.

*"Kumekuwa na ongezeko la migogoro ya kijamii, hofu ya uharibifu wa mazingira na migongano ya matumizi ya ardhi kutokana na ugawaji hovyo wa maeneo ya wafugaji kwa wakulima wa mashamba makubwa. Hali hii imepunguza maeneo ya malisho…"*

*"Uhamaji holela wa Wafugaji na mifugo yao husababisha migogoro ya umilikaji ardhi na migongano ya*

*matumizi ya ardhi katika maeneo yenye jamii za makazi ya kudumu...*" Mwisho wa kunukuu.

Aidha, maudhui ya jumla ya sera yanabainisha vichocheo mbalimbali vinavyoibua migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Vichocheo hivyo ni vifuatavyo:-

(i) Ongezeko kubwa la watu,
(ii) Ongezeko la mifugo,
(iii) Kupungua kwa maeneo ya malisho,
(iv) Uhamishaji wa mifugo kutoka kwenye maeneo yasiyo na malisho na maji ya kutosha kwenda kwenye maeneo yenye mahitaji hayo,
(v) Ukuaji wa miji,
(vi) Utekelezaji wa Sera ya uwekezaji,
(vii) Uanzishaji, upangaji upya na upanuzi wa vijiji na miji,
(viii) Kuwepo kwa ongezeko la mahitaji makubwa ya ardhi,
(ix) Kubadilika kwa aina ya umiliki wa ardhi kimila kuwa wa aina ya umiliki binafsi wa ardhi, na
(x) Baadhi ya hukumu za Mahakama kuhusu uhalali wa miliki za kimila za ardhi.

Maudhui ya Sera hizo yanaonesha nia ya kuendeleza sekta ya ardhi na kuepusha migongano miongoni mwa wamiliki na watumiaji mbalimbali wa ardhi. Kwa kuzingatia maudhui hayo, Serikali inaweza kulinda rasilimali za ardhi na kuwawezesha watumiaji mbalimbali kuwa na haki sawa katika kupata na kutumia ardhi.

Mheshimiwa Spika**,** pamoja na ubora wa Sera ya Taifa ya Ardhi, kuna kasoro mbalimbali za kiutekelezaji zinazotokana na kutozingatiwa kwa matamko ya sera katika masuala mbalimbali yanayohusu umiliki na utumiaji wa ardhi. Kasoro hizo zimefafanuliwa kwenye Juzuu ya II sehemu ya maelezo ya matokeo ya uchambuzi na uchunguzi wa Kamati. Miongoni mwa kasoro hizo ni pamoja na:-

(i) Kutokulipa fidia kwa wananchi ambao ardhi yao imetwaliwa na Serikali. Pia kutolipwa kwa kiwango wanachostahili na kwa wakati kulingana na thamani ya ardhi;

(ii) Uangalizi na usimamizi duni wa matumizi ya ardhi;

(iii) Kutozingatiwa kwa uamuzi wa Serikali za vijiji katika masuala ya ardhi;

(iv) Ugumu katika kupata, kumiliki na kutumia ardhi;

(v) Matumizi ya ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji;

(vi) Udhaifu katika usimamizi wa sheria za ardhi

(vii) Wananchi kutoshirikishwa ipasavyo katika utoaji wa ardhi kwa wawekezaji;

(viii) Kutozingatiwa kwa utunzaji wa maeneo ya hifadhi;

(ix) Kutokuwa na chombo madhubuti cha utatuzi wa migogoro ya ardhi;

(x) Kutokuwepo kwa ramani ya maeneo yaliyopimwa;

(xi) Kutoainishwa kwa mipaka halisi ya vijiji; na

(xii) Kutokuwepo kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi na mifano halisi ya kasoro hizo umeainishwa na Kamati kwenye Juzuu ya II. Aidha, uchambuzi wa baadhi ya sheria zinazohusika na matumizi ya ardhi umewekwa kwenye Juzuu hiyo. Sheria hizo ni:-

(i) Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999;

(ii) Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999;

(iii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982;

(iv) Sheria ya Utwaaji Ardhi Na. 47 ya mwaka 1967; na

(v) Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007.

Aidha, zipo kasoro katika utekelezaji wa sheria hizo pamoja na mkakati wake wa utekelezaji umebainika kuwa na kasoro hizo zinazochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi miongoni mwa wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mkakati wa utekelezaji wake:

Matamko ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006, na kuweka mazingira mazuri yatakayotoa fursa ya kuboresha sekta ya mifugo kwa kuongeza uzalishaji na kubadilisha ufugaji kuwa wa kisasa na kibiashara hivyo kukuza ajira.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa utekelezaji umefafanua namna ya kutekeleza matamko ya sera. Katika uchambuzi, Kamati imebaini kuwa licha ya kuwepo matamko hayo na mkakati uliowekwa, zipo kasoro katika maeneo mbalimbali ya kiutekelezaji kama zilivyofafanuliwa katika Juzuu ya II. Baadhi ya kasoro hizo ni:-

(i) Kushindwa kuugeuza ufugaji wa asili kuwa wa kisasa na wa kibiashara,

(ii) Kutokutengwa kwa maeneo mahsusi kwa ajili ya shughuli za ufugaji,

(iii) Kutokuzingatiwa kwa uwiano wa mifugo na malisho,

(iv) Kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo; na

(v) Kutokuwepo kwa huduma madhubuti kwa ajili ya tiba na kinga za magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Ili kufahamu mfumo wa kisheria wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo, Kamati ilichambua sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula, Na. 11 ya Mwaka 2010;

(ii) Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya Mwaka 2010;

(iii) Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003; na

(iv) Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008.

Uchambuzi wa Sheria hizo ulionesha kuwa, kama ilivyo kwa Sera, zipo kasoro pia katika utekelezaji na usimamiaji wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Sera na Sheria za Maji na Mazingira. Kamati ilichambua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002. Vile vile Kamati ilifanya uchambuzi wa sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009 *(The Water Supply and Sanitation Act, No. 12, 2009);*

(ii) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 *(The Environmental Management Act No. 20, 2004);* na

(iii) Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Maji, Na. 11 ya Mwaka 2009 *(The Water Resources Management Act No. 11, 2009)*.

Kwa ujumla, maudhui na matamko ya Sera ya Taifa ya Mazingira na Sera ya Taifa ya Maji yanatoa mwongozo mzuri na sheria zinaweka misingi na utaratibu mzuri wa usimamizi wa rasilimali hizo. Kasoro za kiutendaji za sera zilizojitokeza zinachangia kuendelea kukua na kuibuka kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kasoro za kiutekelezaji katika sekta zinazohusika na usimamizi wa rasilimali maji na mazingira, zimefafanuliwa katika Juzuu ya Pili. Baadhi ya kasoro hizo ni:-

(i) Kutoshirikishwa kwa makundi ya watumiaji wa maji katika kupanga matumizi ya maji, kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji;

(ii) Udhaifu katika utekelezaji wa mipango ya Sekta ya Maji; na

(iii) Kutosimamiwa kwa Mkakati kuhusu utengaji wa maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria ya Uwekezaji. Kamati ilichambua Sera ya Taifa ya Kuhamasisha Uwekezaji pamoja na Mwongozo wa Uwekezaji wa mwaka 2013 *(The Tanzanian Investment Guide, 2013)*. Uchambuzi huo uliiwezesha Kamati kubaini dosari za kiutekelezaji zifuatazo:-

(i) Utwaaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji bila ya kuwashirikisha wananchi;

(ii) Kutokuwalipa wananchi fidia stahiki wakati maeneo yao yanapotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji *(Makofi)*

(iii) Kubadilisha matumizi ya ardhi ya uwekezaji kinyume na Mkataba; na

(iv) Utelekezwaji wa ardhi iliyotolewa kwa ajili ya Uwekezaji bila Serikali kuchukua hatua zozote.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Na. 26 ya mwaka 1997 iliyotungwa mahsusi kwa ajili ya kuweka utaratibu wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uhamasishaji wa Uwekezaji ya mwaka 1996. Sheria imeanzisha Kituo cha Uwekezaji ili kurahisisha shughuli za uwekezaji . Moja ya majukumu ya Kituo ni kubainisha fursa zilizopo katika sekta ya Kilimo.

Aidha, Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya mwaka 1999 inazuia wawekezaji wasio wazawa kujipatia ardhi kwa shughuli ambazo si za uwekezaji, na kuweka utaratibu maalumu wa kupata ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuwekezaji . Katika uchunguzi wake Kamati imebaini kuwepo kwa dosari za kiutekelezaji katika suala la uwekezaji kama ifuatavyo:-

(i) Umilikishaji ardhi kwa wawekezaji wageni usiofuata taratibu za kisheria;

(ii) Serikali za Vijiji kugawa kwa wawekezaji maeneo makubwa kinyume cha sheria; na

(iii) Wawekezaji kutumia mashamba bila kuwa na hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla kuhusu matokeo ya uchambuzi wa sera, mikakati na sheria. Uchambuzi wa sera umeainisha kasoro mbalimbali za kiutekelezaji. Mbali na kasoro hizo, Kamati ilibaini mambo ya jumla yanayohusu sera zinazozungumzia matumizi ya ardhi. Mambo hayo ni:-

(i) Kutegemeana kwa sera, mikakati na sheria ziliyopitiwa ni suala la msingi katika kuongoza udhibiti na uzuiaji wa migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Maudhui ya sera, mikakati na sheria hizo yanadhihirisha uwepo wa kutegemeana katika usimamizi wa shughuli za sekta za ardhi, kilimo, mifugo, uwekezaji, mazingira na maji.

(ii) Sera, mikakati na sheria za ardhi zinasimamia matumizi ya ardhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji, uwekezaji, miundombinu ya maji na nyinginezo zinazoendeshwa na watumiaji mbalimbali wa ardhi. Kimsingi, sera kuu inayosimamia matumizi ya ardhi kwa shughuli zote hizo chini ya sekta mbalimbali ni Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997, iliyowekewa mikakati na kutungiwa sheria za ardhi.

(iii) Kutofautiana kwa msisitizo miongoni mwa sera. Sera ni mwongozo wa msingi katika usimamizi wa shughuli za kiuchumi, kijamii na uendelezaji wa sekta mbalimbali. Msisitizo wa sera za taifa kwa kawaida haupaswi kutofautiana katika jambo moja.

Uchambuzi wa sera umeonesha kuwa kuna kutofautiana baina ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997, na Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 katika suala la ufugaji wa kuhamahama. Wakati sera ya ardhi 1997 inashawishi msisitizo katika kuzuia ufugaji wa kuhamahama, Sera ya Mifugo ya 2006 inahimiza ufugaji wa kuhamahama.

Aidha, kutoendana *(not aligned)* kwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 ni jambo lililojitokeza. Mtafiti Lugoe (2011) alipata kueleza:

*"The Livestock Policies are not aligned to the Land Policy on the land resource available for distribution among major users. Whereas, land policy advances the notion that the bulk of land is "difficult to manage" for various reasons as also acknowledged elsewhere, the livestock policies call such lands as "a large untapped resource base."*

Kwa maelezo hayo, Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997, haziendani *(Not aligned)* katika suala la ardhi iliyopo nchini ambayo kwa sasa haitumiki. Sera hizo hazina upatanifu wa mwongozo katika suala la ardhi isiyotumika kwa sasa.

Kwa hali hiyo, haikuwa vigumu kwa sekta ya ardhi na sekta ya mifugo kutofautiana katika kuweka msisitizo juu ya suala la ardhi kubwa isiyotumika kwa sasa *(a large untapped resource base)* jambo ambalo si la kawaida katika utekelezaji bora wa sera za taifa.

(iv) Wizara zinazohusika na usimamizi wa sera, mikakati na sheria
zilizochambuliwa ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara hizo na sera zimeanishwa katika jedwali linalofuata hapo, (ambalo Waheshimiwa Wabunge bila shaka wanaweza kuipitia), lakini pia kwa muundo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu inahusika na uratibu *(coordination)* wa kushughulikia shughuli za Serikali, katika utekelezaji wa Sera, Mikakati na sheria zilizochambuliwa.

Dhana ya uratibu katika lugha ya kiingereza inaweza kufafanuliwa kama ilivyoelezwa na mwandishi Newman, katika kitabu chake cha "*Administrative action*" ukurasa wa

403, kitabu cha mwaka 53, aliyenukuliwa na Bhagwan na Bhushan katika kitabu chake cha "Public Administarion" cha mwaka 2010 ukursa wa 225, akisema:

*"Coordination is "the orderly synchronization of efforts to provide the proper amount, timing and directing of execution resulting in harmornious and unified actions to a stated objective".*

Kwa tafsiri isiyo rasmi yaweza kusemwa kuwa "uratibu" ni utaratibu mzuri wa kuchakata na kuwianisha juhudi katika utekelezaji kwa namna inayoweza kutoa kiasi sahihi cha matokeo ya utekelezaji unaounganisha na kuoanisha hatua mbalimbali za kufikia lengo lililoainishwa.

Tukizingatia maelezo hayo pamoja na Tangazo la Serikali, Na. 494 lililochapishwa tarehe 17 Disemba, 2010, Ofisi ya Waziri Mkuu inahusika na kuwianisha, kuoanisha na kupatanisha juhudi za Wizara hizo zinazohusika na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria kuhusiana na matumizi ya ardhi ili malengo mazuri ya sera yaweze kufikiwa.

Aidha, Halmashauri nchini chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zinahusika na usimamizi wa rasilimali zinazotumika katika utekelezaji wa sera mbalimbali kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya rejea ya pili, mapitio ya taarifa za kamati au Tume zilizowahi kuundwa. Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Tume ya Rais ya kuchunguza masuala ya ardhi *(The Presidential Commission of Inquiry into Land Matters)* iliyoundwa tarehe 03, Januari, 1991 chini ya Mwenyekiti Profesa Issa Shivji kutoka Kitivo cha Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akisaidiana na Makamishna Kumi na Mmoja.

Tume ilikabidhi Taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais mnamo Tarehe 11, Novemba, 1992. Taarifa ya Tume ina sura 25, zinazoelezea matokeo ya uchunguzi. Kamati hii imepitia sura za Juzuu ya Kwanza ya taarifa hiyo kwa kuzingatia

matokeo yanayohusiana na migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Katika Taarifa hiyo, Tume iliripoti kuwa ilipokea malalamiko zaidi ya elfu moja yanayohusiana na migogoro ya ardhi . Migogoro hiyo, kwa kiasi kikubwa imeleta hali ya sintofahamu *(uncertainty)* kwa wananchi, ikizingatiwa kuwa ardhi ndiyo nguzo kuu ya uzalishaji mali *(major means of production)* katika nchi yetu. Ufafanuzi zaidi wa maudhui ya taarifa hiyo umewekwa katika Juzuu ya Pili ya maelezo ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa kuhusiana na namna ya kuepusha migogoro ya ardhi, Kamati ilipitia maoni ya Tume ambayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuna ugumu wa kupata huduma za vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi (mabaraza ya ardhi na Mahakama),

(ii) Kumekuwepo na ucheleweshaji katika utoaji wa maamuzi ya migogoro ya ardhi,

(iii) Kutokuwa na hakika *(uncertainty)* na pia kutokamilika *(lack of finality)* kwa maamuzi ya migogoro ya ardhi,

(iv) Kumekuwepo na msigano na muingiliano wa kimamlaka katika utekelezaji wa majukumu ya vyombo mbalimbali, hali inayosababisha kutolewa kwa maamuzi yanayokinzana au ucheleweshaji wa maamuzi,

(v) Mfumo wa kimahakama uliopo na namna uongozi wa Serikali unavyoshughulikia masuala ya ardhi, vinaashiria kupoteza uhalali (legitimacy) machoni pa wananchi. Wengi wao hawana imani na jinsi mamlaka husika zinavyoshughulikia migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, maoni hayo, Tume ya Rais (Tume ya Shivji) ilitoa mapendekezo yafuatayo:-

(i) Kiundwe chombo huru chenye kuaminika kwa Wananchi *(Independent and impartial)*, ambacho kitakuwa na jukumu la kutatua migogoro ya ardhi,

(ii) Wajumbe wa chombo cha kutatua migogoro ya ardhi wasitokane na viongozi wa Vijiji, Wilaya au Mkoa, bali wachaguliwe kutoka miongoni mwa wananchi na wawe ni watu wenye maadili na weledi,

(iii) Viongozi wa kijadi na kimila watumiwe katika kutatua migogoro ya ardhi

(iv) Hati miliki za ardhi kwa matumizi mbalimbali zitolewe,

(v) Upimaji na ramani za vijiji upewe kipaumbele,
(vi) Upangaji wa Miji uzingatiwe,
(vii) Pawepo na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika ngazi za vijiji, Kata,Wilaya na Taifa,

(viii) Kuimarisha hatua za uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma katika idara ya ardhi wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na wasiokuwa na maadili katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na Taarifa ya Tume ya Rais ya kuchunguza masuala ya ardhi, Kamati inabainisha mambo sita (6) ya kuzingatiwa kuhusiana na hali ya migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi kama ifuatavyo:-

(i) Sababu za migogoro ya ardhi zilizobainishwa na Tume ya Profesa Shivji zinashabihiana kwa kiasi kikubwa na sababu za migogoro ya ardhi zilizobainishwa na Kamati hii,

(ii) Kwa kiasi kikubwa sababu za kihistoria za migogoro zinaweza kutokana na sera ya Vijiji ya mwaka 1974 ambapo Vijiji vingi vilipata ardhi bila kuzingatia sheria.

(iii) Vyombo vya utatuzi wa migogoro vimeundwa kwa baadhi ya sehemu lakini haviko huru na havina rasilimali za kutosha kutimiza majukumu yake, kama ulivyobainika katika uchunguzi wa Kamati hii.

(iv) Mabaraza ya ardhi kwa baadhi ya maeneo hayaaminiki kutokana na tuhuma za rushwa na kukosa wataalamu wa kutosha.

(v) Mashauri ya ardhi yanachukua muda mrefu kama inavyothibitishwa na kesi ya Kijiji cha Kambala inayoendelea kusikilizwa kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya mkoani Morogoro tangu mwaka 2009, na

(vi) Kutoheshimiwa kwa maamuzi ya vyombo vya kutoa haki kumeendelea kuonekana hadi sasa. Mfano ni baadhi ya viongozi wa Serikali na raia kutoheshimu maamuzi ya mahakama kuhusu ardhi. Jambo hilo limedhihirika katika kijiji cha Mabwegere wilaya ya Kilosa, Mkoani Morogoro na pia katika eneo la Emboley Murtangos, wilayani Kiteto, na eneo la vilima vitatu, Babati, Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Tathmini ya Matatizo Yaliyotokana na Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza. Taarifa hiyo, inayohusu tathmini ya matatizo, yaliyotokana utekelezaji wa kazi wa operesheni Tokomeza. Taarifa hiyo ilitokana na kazi iliyofanywa na Kamati Ndogo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, iliyopewa Hadidu za Rejea Nne.

Miongoni mwa Hadidu za Rejea, Hadidu Namba Nne iliitaka Kamati hiyo kuchunguza migogoro ya ardhi inayohusu wakulima, wafugaji na wawekezaji kwenye maeneo yanayozunguka maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ilikamilisha jukumu ililopewa na Bunge lako. Mnamo tarehe 18 Desemba, 2013 iliwasilisha Bungeni Taarifa, iliyoeleza matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa Operesheni Tokomeza. Taarifa hiyo ilifafanua mambo mbalimbali ikiwemo tathmini ya migogoro ya ardhi kati ya wananchi na mamlaka au wasimamizi wa maeneo ya hifadhi.

Migogoro hii inatokana na kupanuliwa kwa maeneo ya mapori ya akiba na ya hifadhi, bila kuwashirikisha wananchi wanaoishi au kufanya shughuli zao kwenye maeneo hayo.

Mifano iliyotolewa na Kamati hii, ni pamoja na migogoro ya ardhi katika maeneo ya:-

(i) Wilaya ya Bunda katika Pori la Akiba la Gurumeti;

(ii) Kata ya Iputi na Lupiro dhidi ya Hifadhi ya Taifa ya Selous wilayani Ulanga; na

(iii) Vijiji Kegonga na Masanga katika kata ya Nyanungu, wilaya ya Tarime wakigombea bonde lililopo kwenye eneo la Bonde la Hifadhi iliyoongezwa na *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na tathmini iliyofanywa na Kamati hiyo kuhusiana na migogoro inayowahusisha wakulima, wafugaji, wawekezaji dhidi ya mamlaka na wasimamizi wa Mapori ya akiba na maeneo ya hifadhi ilitoa mapendekezo. Kama yafuatayo:-

(i) Kamati hiyo ilibaini kwamba, katika baadhi ya maeneo yaliyoko Mipakani mfano; Karagwe, Idara ya Uhamiaji hutoa vibali kwa raia wa nchi jirani vya kuishi, kufuga na kulima hapa nchini, vibali ambavyo havina udhibiti wala tija kwa nchi, na usababisha migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji lakini pia uharibifu wa

mazingira kwa kuingiza mifugo hifadhini, Kamati ilipendekeza Bunge liazimie kwamba;

- Serikali isitishe mara moja zoezi la kutoa vibali hivyo, na kufuta vilivyopo na kuwataka raia hao wa kigeni wenye vibali kuondoka nchini mara moja . *(Makofi)*

(ii) Kamati ilibaini kwamba, zaidi ya asilimia 25 ya eneo la Nchi ni hifadhi, na mipaka ya maeneo mengi yaliyohifadhiwa haikuainishwa, na kwa kuwa Serikali haina uwezo wa (rasilimali watu na fedha) wa kusimamia na kulinda Mipaka ya maeneo haya kikamilifu, Kwa hiyo basi, Kamati ililiomba Bunge liazimie kuitaka; Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuridhia Idara ya Wanyamapori na Wakala wa Huduma ya Misitu kuajiri idadi ya watumishi wanaotakiwa kama Serikali bado inaendelea kuyahifadhi maeno hayo;

- Kuainisha mipaka ya mapori yote ya akiba, hifadhi za taifa na Misitu ya Serikali kwa alama maalumu na za kudumu, ili kuepusha Wananchi kuingia katika maeneo hayo kwa kutojua mipaka; na

- Kuyaachia mapori ya Serikali ambayo yamekosa sifa, ili yatumike kwa kilimo na ufugaji kwa ajili ya kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi

(iii) Kamati ilibaini kuwepo wa maeneo ya mapori na Hifadhi ambayo yana migogoro ya muda mrefu, ambapo wananchi wameishi katika maeneo hayo kwa muda mrefu. Kamati ililiomba Bunge liazimie kwamba;

- Serikali irekebishe mipaka husika au iwahamishie Wananchi hao kwenda kwenye maeneo mengine yenye miundombinu.

- Serikali iwaagize Mawaziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutembelea maeneo yote yenye migogoro

nchini na kuitafutia ufumbuzi ili wananchi waweze kuelewa hatma yao katika maeneo hayo kwani wamekuwa katika hali ya sintofahamu kwa muda mrefu.

(iv) Kamati ilibaini kwamba, migogoro wanayokumbana nayo wafugaji kutokana na kuingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi pamoja na kero nyingine inatokana na kukosekana kwa miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo, na kwa kuwa, Mheshimiwa Rais aliunda Wizara mahususi kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini akitambua umuhimu wa Sekta hiyo kwa uchumi wa Taifa.

Kamati hii Teule inaendelea kusisitiza kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo ya Bunge yakitekelezwa kikamilifu yanaweza kuwa suluhisho kwa migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi iliyokithiri hapa nchini. Kamati Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasli na Mazingira ilipendekeza Bunge liitake Serikali:-

(i) Kusitisha mara moja utoaji wa vibali kwa raia wa nchi jirani wanaoishi nchini na mifugo, hali inayosababisha migogoro baina ya wakulima na wafugaji kutokana na uhaba wa ardhi na uharibifu wa mazingira;

(ii) Kuainisha mipaka ya mapori ya akiba na maeneo ya hifadhi za Taifa na misitu ya Serikali ili kuepusha mamlaka na wasimamizi wa mapori ya akiba na maeneo ya hifadhi kuingia kwenye migogoro na wakulima na wafugaji kutokana na mipaka kutotambulika;

(iii) Kuyaachia mapori yasiyo na sifa ili yatumike kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa nia ya kuepusha migogoro ya ardhi;

(iv) Kuweka utaratibu utakaowezesha viongozi wa Serikali kutembelea maeneo yenye migogoro ya mara

kwa mara kuhusu matumizi ya ardhi na kuipatia ufumbuzi; na

(v) Serikali iweke mkazo katika kusimamia sera na mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu ili kuimarisha sekta za mifugo na kilimo kwa kuweka miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo na mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana mapitio ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Kamati hii Teule ina maoni kuwa migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi na hifadhi au mapori ya akiba inaweza kutatuliwa kwa hatua za muda mfupi, wa kati na muda mrefu kama inavyoainishwa katika Juzuu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, Tamko la Mtowisa la tarehe 17 Septemba, 1998: Tamko hilo liliitwa "*Tamko la Mtowisa*" lilitolewa katika Mkutano uliofanyika kijiji cha Mtowisa, Tarafa ya Mtowisa, Wilaya ya Sumbawanga Mkoani Rukwa. Mkutano huo ulihudhuriwa na watu wapatao elfu mbili (2000) na ulijumuisha wafugaji, wakulima pamoja na viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya tamko la Mtowisa yanafanana kwa kiasi kikubwa na mapendekezo yaliyotolewa pia katika Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira pamoja na mapendekezo ambayo yametolewa na Profesa Shivji katika Tume yake hiyo. Kwa maana hiyo naomba mapendekezo hayo ya Mtowisa yaliyopo mahali hapo yaweze kuingia katika Hansard kama yalivyo katika taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa Tamko la Mtowisa Kamati imebaini kwamba sababu za kuwepo kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji zinafahamika Serikalini kwa muda mrefu. Pamoja na sababu mbalimbali, kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya

ardhi za vijiji, ni kichocheo kikubwa cha mwingiliano wa shughuli za kilimo na ufugaji.

Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba maazimio yaliyoafikiwa katika Mkutano wa Mtowisa yalilenga kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Licha ya kuwekwa kwa utaratibu mzuri wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa maazimio hayo, mambo yafuatayo yameendelea kuwa changamoto:-

(i) Kutokukamilishwa kwa zoezi la upimaji wa ardhi na utengaji wa maeneo ya kilimo na ufugaji kwa baadhi ya vijiji nchini;

(ii) Kutokufanyika kwa sensa ya Taifa ya mifugo na kutokuwepo kwa Daftari la Kumbukumbu za Mifugo;

(iii) Kutokuwepo kwa utaratibu madhubuti wa ukusanyaji wa kodi au ushuru unaotokana na mifugo kwa maendeleo ya mifugo;

(iv) Kutokutolewa ipasavyo kwa elimu ya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara kwa wafugaji;

(v) Usimamizi hafifu wa sheria mama na sheria ndogo; na

(vi) Kutotatuliwa kikamilifu kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya Rejea ya Tatu: Uchambuzi wa Mikakati ya Kusuluhisha migogoro: Uchambuzi wa mikakati ya Serikali ya kusuluhisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji nchini ulilenga kutathmini maudhui yake pamoja na utekelezaji.

Uchambuzi huo ulikusudia pia kubainisha namna mikakati hiyo inavyoweza kusaidia kuondoa na kuzuia migogoro miongoni mwa wakulima na wafugaji. Matokeo

ya uchambuzi huo yanaonesha mambo makuu mawili kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana kwa mkakati mahususi wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, Serikali haina Mkakati mahsusi uliotayarishwa, uliosambazwa au unaotumika kitaifa kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, Kamati ilibaini kuwepo kwa Rasimu ya Mkakati wa kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji nchini ya mwaka 2009. Rasimu hiyo inayopendekeza njia mbalimbali za kutatua migogoro haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, ushahidi uliowasilishwa mbele ya Kamati umebainisha kuwa migogoro inayoendelea baina ya wakulima na wafugaji inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutokuwepo kwa mkakati mahsusi wa Serikali wa kuzuia na kuondoa migogoro hiyo.

Kutokuwepo kwa mkakati wa Serikali wa kuondoa migogoro na kutofahamika kwa Rasimu ya Mkakati huo kunathibitishwa na ushahidi wa baadhi ya Mashahidi walioitwa mbele ya Kamati. Kwa mfano, baadhi ya mashahidi wenye nyadhifa katika Wizara wakiwemo Mawaziri walieleza kwamba hawajawahi kuiona wala kufanyia kazi Rasimu ya Mkakati wa Serikali wa mwaka 2009 unaolenga kumaliza migogoro baina ya wakulima na wafugaji licha ya kwamba ni wa mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, njia za utatuzi wa migogoro hazitoi suluhisho la kudumu, kutokana na kukosekana kwa mkakati mahsusi kwa ajili ya kutatua migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi, Serikali hutumia njia mbalimbali za kuitatua migogoro hiyo. Mara nyingi njia hizo hazitoi suluhisho la kudumu na hivyo migogoro hiyo inaendelea kuwepo. Mfano, kuna nyakati Jeshi la Polisi hutumika kutuliza ghasia zinazotokana na migogoro

hiyo huku chanzo cha migogoro hiyo kikiendelea kuwepo. *(Makofi)*

Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba migogoro inayoibuka mara kwa mara katika Wilaya za Mvomero na Kiteto haijapatiwa suluhisho la kudumu na badala yake Serikali imekuwa ikitumia Jeshi la Polisi kutuliza ghasia wakati wa migogoro hiyo bila kushughulikia chanzo cha tatizo.

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya Rejea ya Nne: Uchambuzi wa Mikakati ya kulinda vyanzo vya maji: Kamati ilichambua mikakati iliyolenga kuhifadhi vyanzo vya maji na kuzuia uharibifu wa Mazingira. Mikakati iliyochambuliwa ni:-

(i) Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa Mwaka 2006,

(ii) Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Maji wa Mwaka 2006

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa mikakati hiyo miwili, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(i) Mkakati wa kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji uliandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau na sekta nyingine. Lengo la mkakati huo ni kuzuia uharibifu wa mazingira ambao ni kiini cha kuenea kwa hali ya jangwa na ukame pamoja na kukauka kwa vyanzo vya maji nchini. Ushahidi wa kukauka kwa vyanzo vya maji unathibitishwa na takwimu za vyanzo vya maji hususan Bwawa la Mtera. Takwimu hizo zinaonesha kuwa kina cha juu cha maji cha Bwawa la Mtera, kimekuwa kikishuka kutoka mita 695.8 mwaka 2003, hadi mita 690.5 mwaka 2004 hadi mita 689 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kwa kiasi kikubwa husababishwa na mambo yafuatayo:-

(ii) Shughuli za kilimo kisicho endelevu zinazofanywa katika maeneo ya vyanzo vya maji ikiwa ni

pamoja na kwenye vilele na miteremko ya safu za milima. Shughuli hizo ni kama vile ukataji miti hovyo, uchomaji moto misitu, umwagiliaji usio endelevu katika shughuli za kilimo na kadhalika,

(iii) Uhamaji wa makundi makubwa ya mifugo kutoka eneo moja kwenda jingine kwa nia ya kutafuta malisho, maji pamoja na dhana ya kuepuka magonjwa ya mifugo. Hali hii huchangia uharibifu mkubwa wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji na hivyo kusababisha kuongezeka kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa rasilimali ardhi na maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua mikakati ya Serikali katika kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu. Baadhi ya mikakati hiyo ni kuainisha maeneo ya vyanzo vya maji nchini, kubainisha maeneo yaliyovamiwa na wafugaji ifikapo Juni, 2006 na kubainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji ifikapo mwaka 2006.

Mikakati mingine iliyochambuliwa ililenga kutoa taarifa sahihi kuhusu uwezo wa malisho, aina na idadi ya mifugo ifikapo Juni, 2006; kuandaa na kutekeleza utaratibu wa kuwaondoa wafugaji na mifugo kwenye maeneo waliyovamia kwenda kwenye maeneo yanayofaa ifikapo Juni, 2006; na Kuendeleza njia za asili za hifadhi ya malisho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, mikakati ililenga kusimamia utekelezaji wa programu za hifadhi ya mazingira na mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ifikapo Julai 2007, kuhakikisha mipaka ya vijiji 6,000 inapimwa na vyeti vya ardhi ya kijiji vinatolewa, kuandaa na kutekeleza Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi na kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa dosari mbalimbali ambazo zimeelezwa katika Juzuu ya Pili. Dosari hizo ni:-

(i) Kutobainishwa kwa maeneo ya ufugaji,

(ii) Kukosekana kwa taarifa sahihi kuhusu uwezo wa malisho (*carrying capacity*) aina na idadi ya mifugo,

(iii) Kuendelea kuwepo kwa uvamizi wa shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji,

(iv) Utaratibu usiofaa wa kuwaondoa wakulima na wafugaji katika maeneo waliyoyavamia,

(v) Kutojengwa kwa malambo, visima na mabwawa,

(vi) Kutotekelezwa kwa Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi,

(vii) Athari zilizotokana na kuyafanya baadhi ya maeneo kuwa hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya Rejea ya Tano: Mapendekezo ya kuondoa migogoro iliyopo na kudumisha uhusiano mzuri kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi; Baada ya uchambuzi wa kina na kwa kuzingatia hadidu za rejea, Kamati inatoa mapendekezo katika makundi makuu matatu kwa kigezo cha muda wa utekelezaji.

Makundi hayo ni kundi la mapendekezo ya muda mfupi (miaka 0-2), kundi la muda wa kati (miaka 2-5) na kundi la muda mrefu (miaka 5-15). Vilevile, Kamati imeainisha viwango vya athari za kutotekelezwa kwa mapendekezo yaliyotolewa (*Risk*) katika aina kuu mbili ambazo ni Athari ya juu (*High Risk*) na athari ya kati (*Average Risk*). Madhumuni ya kuainisha mapendekezo katika makundi na kueleza viwango vya athari ya utekelezaji ni kubainisha umuhimu wa mapendekezo hayo kufanyiwa kazi pamoja na kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Muda Mfupi: Mapendekezo haya yanalenga kutafuta ufumbuzi wa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini. Katika mapendekezo haya yapo yanayotakiwa kufanyiwa kazi haraka ambayo ni:

(i) Usuluhishi wa migogoro ya ardhi katika Wilaya ya Kiteto;

KWA KUWA, Mgogoro wa ardhi katika Wilaya ya Kiteto unazidi kuendelea na kusababisha mauaji ya watu ndani ya Wilaya hiyo na migongano kati ya Uongozi wa Wilaya ya Kiteto na Wilaya za jirani, mathalan, Kongwa na Chemba,

NA KWA KUWA, Migogoro hiyo ni hatari kwa mustakabali wa amani, usalama, umoja na utangamano wa Taifa na kwamba kuna hukumu iliyotolewa na Mahakama kuwa eneo hilo lisitumike kwa shughuli za kilimo wala ufugaji.

KWA HIVYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali:-

(a) Kuharakisha usuluhishi wa mgogoro baina ya wakulima na wafugaji wanaogombea maeneo ya ardhi Wilayani Kiteto ili kuzuia mauaji ya wenyewe kwa wenyewe yanayoendelea kutokea.

(b) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa hukumu ya Mahakama iliyoamua kuhusu matumizi ya eneo linalogombewa la (*Emboley Murtangos*).

(ii) Mheshimiwa Spika, Kudhibiti uswagaji wa mifugo:

KWA KUWA, Mheshimiwa Rais alitoa agizo kupitia waraka Namba 01 wa mwaka 2002, lililokataza kuswaga mifugo kutoka eneo moja la nchi kwenda lingine bila kufuata utaratibu unaopaswa kuzingatiwa,

NA KWA KUWA, kuendelea kuswaga mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine ni ishara ya kutozingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, na hivyo uswagaji huo wa mifugo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro na uharibifu wa mazingira,

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba, Bunge liitake Serikali kusimamia kikamilifu:-

(a) Utekelezaji wa haraka wa maelekezo ya Waraka wa Mheshimiwa Rais, unaoelekeza uhamishaji wa mifugo ufanyike kwa kutumia magari au reli (kwa ng'ombe wanaohamishwa kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine) badala ya kuswaga; hili ni vizuri lieleweke ni ng'ombe wanaotoka masafa ya mbali kwenda maeneo mengine ya mbali ambao wanakatisha Wilaya moja kwenda nyingine, siyo ng'ombe waliopo kwenye malisho.

(b) Kusimamia kikamilifu sheria zinazoweka masharti ya kuwa na vibali wakati wa kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine; na

(c) Kila Halmashauri ya Wilaya inatakiwa kutenga njia maalum za kupitisha mifugo *(stock route)* na kuweka utaratibu utakaowezesha mifugo kupitishwa kwenda kwenye malisho, majosho au minadani.

(iii) Kutenga njia za kupitisha mifugo

KWA KUWA, kuwekwa kwa njia za kupitisha mifugo kwenda kutafuta maji, malisho majosho au minada ni muhimu kwa ajili ya kuepusha mwingiliano wa shughuli za ufugaji, wakulima na shughuli nyingine za watumiaji wa ardhi,

NA KWA KUWA, kukosekana kwa njia mahsusi kwa ajili ya kupitisha mifugo, kunachangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kutokana na mifugo kuingia kwenye mashamba na kuharibu mazao,

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kutenga njia za kupitisha mifugo kwa ajili ya kufuata malisho, majosho na maji kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (1) – (3) cha Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula, Na. 12, ya mwaka 2010.

(iv) Hatua dhidi ya uvamizi wa wageni kutoka nchi jirani:

KWA KUWA, Katika mikoa ya Rukwa, Kigoma na Kagera inayopakana na nchi jirani, kuna wimbi la wavamizi kutoka nchi jirani wanaoingia nchini wakiwa na idadi kubwa ya mifugo kwa ajili ya kutafuta malisho,

NA KWA KUWA, Kamati imebaini kwamba hali hii huongeza mahitaji ya ardhi na hivyo kusababisha uharibifu wa mazingira, kueneza magonjwa ya mifugo, wananchi kukosa ardhi ya kutosha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za kilimo na ufugaji pamoja na kuhatarisha hali ya utulivu, amani na usalama nchini,

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za haraka dhidi ya uvamizi huo.

(v) Kutenga maeneo ya Ardhi ya vijiji

KWA KUWA, kutojulikana kwa idadi ya mifugo yote iliyomo nchini, na ukubwa wa ardhi inayofaa kwa shughuli mbalimbali ni jambo muhimu katika kuainisha matumizi ya ardhi kwa lengo la kuondoa mwingiliano wa shughuli za sekta mbalimbali,

NA KWA KUWA, kutojulikana kwa ukubwa wa ardhi inayofaa kwa kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za kiuzalishaji kumechangia ugumu wa kuainisha ardhi inayofaa kwa kilimo, ufugaji, hifadhi na shughuli nyingine hapa nchini, na hivyo kusababisha mwingiliano wa shughuli hizo na migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi,

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kupima na kuainisha ukubwa wa ardhi inayofaa na inayohitajika kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo, hifadhi na shughuli nyingine na na kumilikisha ardhi hiyo kwa kuzingatia mahitaji ya uzalishaji.

(vi) Kutotekelezwa kwa masharti ya uvunaji wa mifugo;

KWA KUWA, Kifungu cha 20 cha Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula, Na. 13 ya mwaka 2010 kimeweka utaratibu kwamba ili yawepo malisho ya kutosha na idadi ya mifugo inayoendana na malisho, utaratibu wa kuvuna mifugo unapaswa kutekelezwa,

NA KWA KUWA, kuwepo kwa idadi kubwa ya mifugo isiyoendana na upatikanaji wa malisho ya mifugo katika eneo moja husababisha uwiano usiokuwa sawa wa idadi ya mifugo na malisho, hali inayolazimisha wafugaji na wakulima kuhamia maeneo yanayotumiwa kwa shughuli nyingine, hivyo kuchochea migogoro baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi,

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa, Bunge liitake Serikali kufanya sensa ya mifugo na kuainisha aina na idadi ya mifugo yote nchini.

(vii) Mheshimiwa Spika, Chombo cha kuratibu na kusimamia masuala ya ardhi;

KWA KUWA, Matumizi ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji, uwekezaji na matumizi mengine, yanasimamiwa na kuratibiwa na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi pamoja na Wizara na Idara mbalimbali zinazohitaji uratibu na mawasiliano madhubuti na yenye tija baina yao zaidi ya ilivyo sasa,

NA KWA KUWA, Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa kuna udhaifu katika uratibu, usimamizi na mawasiliano miongoni mwa Wizara, ofisi, idara mbalimbali zinazohusika, hali inayochochea kuibuka kukua na kuendelea kuwepo kwa migogoro ya ardhi inayoathiri maendeleo, amani na utulivu nchini,

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liafiki kuitaka Serikali:-

(a) Kuiimarisha Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kuipatia vitendea kazi na watumishi wa kutosha wenye weledi katika tasnia ya ardhi;

(b) Kufungua Ofisi za Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi katika ngazi za Mikoa kwa ajili ya kuwezesha usimamizi na upangaji, upimaji na umilikaji wa ardhi katika Wilaya za Mikoa husika kwa karibu na kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, nane, ni upimaji wa ardhi ya Mkoa wa Morogoro.

KWA KUWA Mkoa wa Morogoro umebainika kukumbwa na migogoro mikubwa ya ardhi ya mara kwa mara inayosababishwa na mwingiliano wa shughuli za wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi,

NA KWA KUWA, migogoro hiyo imesababisha madhara makubwa kama vile kukwama kwa shughuli za uzalishaji mali katika maeneo yenye migogoro, vifo, uharibifu wa mali, uharibifu wa mazingira na kukosekana kwa amani na utulivu kwa wananchi wanaoishi ndani na nje ya mkoa huo;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kupima ardhi ya vijiji vya Mkoa wa Morogoro kwa utaratibu wa mkakati wa dharura ili kufanikisha dhana ya mipango ya matumizi bora ya ardhi na kupunguza mwingiliano wenye madhara kiuhusiano kati ya shughuli za kilimo na zile za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, tisa, migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Serikali.

KWA KUWA Kamati imebaini kuwa ipo baadhi ya migogoro inayowahusisha:-

(a) Wananchi na baadhi ya watendaji wa Serikali kutokana na watendaji hao kuvamia maeneo ya ardhi ya vijiji na kuendesha shughuli zilizo kinyume na mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika kijiji cha Itaswi Wilayani Kondoa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa alibainika kuwa katika mgogoro na wananchi wa kijiji cha Itaswi kutokana na yeye kuendesha shughuli za kilimo katika eneo la ardhi ya kijiji lililotengwa kuwa ardhi ya akiba.

(b) Mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kata ya Bagara Ziwani dhidi ya Halmashauri ya Mji wa Babati kutokana na baadhi ya wananchi hao kutolipwa fidia stahiki; na

(c) Migogoro ya ardhi kati ya wananchi wa maeneo mbalimbali kwenye kambi za jeshi.

NA KWA KUWA migogoro hiyo imekuwa ikiwaathiri wananchi hao kiuchumi na kuwafanya wakose imani na Serikali yao;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali:-

(a) Kufanya uchunguzi wa watendaji wa Serikali wanaohusika na kubadilisha matumizi ya ardhi kama yalivyopangwa katika Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi za Vijiji na kuchukua hatua stahiki dhidi yao;

(b) Kutoa fidia stahiki na kwa wakati kwa wananchi ambao ardhi yao inakuwa imetwaliwa kwa ajili ya matumizi mengine; na

(c) Ni kupata suluhu ya kudumu ya migogoro ya mipaka kati ya wananchi na kambi mbalimbali za jeshi chini.

Mheshimiwa Spika, kumi, mashamba yaliyobinafsishwa na kutelekezwa.

KWA KUWA imebainika kwamba mashamba mengi yaliyobinafsishwa kwa baadhi ya wawekezaji hayajaendelezwa na yameachwa katika hali ya kutelekezwa kabisa na mengine yamebadilishwa matumizi yaliyokusudiwa;

NA KWA KUWA mashamba hayo yanawavutia wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kuyatumia kuendesha shughuli zao, jambo linalosababisha kuibuka kwa migogoro miongoni mwao;

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali:-

(a) Kufuta hati za umiliki wa mashamba yaliyobinafsishwa kwa wawekezaji ambayo yametelekezwa au kubadilishwa matumizi yaliyokusudiwa na kugawa kwa wananchi; na

(b) Kupima upya mashamba yote yanayohodhiwa bila kuendelezwa (mashamba pori) ambayo hati za umiliki zimefutwa ili kuyagawa kwa wananchi wenye uhitaji.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kuwemo kwenye hatari ya kufungiwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani.

KWA KUWA Kamati imebaini kuwa Tanzania iko hatarini kufungiwa kusafirisha nje ya nchi mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa, siagi, jibini na ngozi kutokana na kutozingatia ipasavyo miongozo ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani;

NA KWA KUWA, nchi yetu ikifungiwa na Shirika hilo itasababisha sekta ya mifugo kuendelea kuwa duni na ufugaji kutokuwa wa kisasa, jambo litakaloendelea kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liazimie kwamba Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi iweke mipango mahsusi ya kusimamia

utekelezaji wa maelekezo ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani ili sekta ya mifugo iwe ya uzalishaji wenye tija kwa taifa. Aidha, mipango hiyo iwasilishwe bungeni ili Bunge lijiridhishe na maudhui ya mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili kupima upya maeneo ya vijiji vyenye migogoro ya mipaka;

KWA KUWA imebainika kwamba zoezi la usajili wa baadhi ya vitongoji kuwa vijiji ama upimaji wa baadhi ya vijiji nchini lilifanyika bila ya kushirikisha kikamilifu kijiji mama au vijiji jirani;

NA KWA KUWA kasoro hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi miongoni mwa vijiji hivyo;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa, Bunge liitake Serikali;

(a) Kuyapima upya maeneo ya vijiji vyote vyenye migogoro ya mipaka inayoleta migongano kwa kushirikisha vijiji vyote vinavyohusika ili kuondoa kabisa migogoro hiyo;

(b) Serikali itafute utaratibu wa kisheria wa utatuzi wa migogoro ya mipaka kwenye vijiji vyenye migogoro iliyokwisha amuliwa na Mahakama; na

(c) Serikali ilete Bungeni Taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo hayo ndani ya kipindi cha miezi sita (6).

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, viongozi wa vijiji kugawa maeneo yanayozidi ekari 50 kwa wawekezaji.

KWA KUWA Kanuni ya 76(3) ya Kanuni za Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114, inaweka ukomo kwa Mamlaka za Vijiji kugawa ardhi kuwa isizidi eneo la ukubwa wa ekari 50, lakini imebainika kwamba kuna baadhi ya mamlaka hizo za vijiji zinagawa maeneo zaidi ya ekari 50 kwa watu binafsi au kwa wawekezaji kinyume cha sheria;

NA KWA KUWA utaratibu wa kugawa maeneo ya ardhi ya kijiji kiholela umekuwa ni chanzo cha kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi;

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kwamba Bunge liishauri Serikali kufanya uchunguzi kuhusu wawekezaji waliomilikishwa zaidi ya ekari 50 za ardhi na viongozi wa Serikali za Vijiji na ichukue hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kutwaa ardhi hizo na igawe maeneo hayo kwa wananchi waliokosa ardhi.

Mheshimiwa Spika, upanuzi mkubwa wa ardhi kwa ajili ya Maeneo ya Hifadhi.

KWA KUWA hadi sasa asilimia 27 ya ardhi iliyopo ya nchi kavu ni maeneo yanayohifadhiwa (hifadhi za Taifa, maeneo ya mapori tengefu, mapori ya akiba na hifadhi za misitu);

NA KWA KUWA kumekuwa na jitihada za Serikali za kupanua mipaka ya maeneo ya hifadhi, hali inayochangia kupungua kwa ardhi inayotumika kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji, makazi na uchimbaji wa madini, hivyo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa watumiaji hao wa ardhi.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali;

(a) Kufanya utafiti wa kina wa kuangalia ulazima, faida, athari na matokeo ya upanuzi wa mipaka ya maeneo ya hifadhi ili kuepusha migogoro ya ardhi inayotokea mara kwa mara miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi.

(b) Ni kuainisha maeneo yote yaliyokuwa ya hifadhi na ambayo kwa sasa yamepoteza hadhi hiyo kutokana na muingiliano wa matumizi mbalimbali ya kilimo, ufugaji, makazi, uchimbaji madini na kuchukua hatua stahiki ili kuzuia migogoro ya ardhi iliyopo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni kuyafuta maeneo ya hifadhi yaliyopoteza sifa.

KWA KUWA yapo maeneo ya hifadhi yanayotumiwa na wananchi kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji kwa zaidi ya miaka 50 na mfano wa maeneo hayo ni Kona Nne na Kangeme huko Kaliua, Kiteto, Kimotoro huko Simanjiro.

NA KWAKUWA maeneo hayo hayana sifa za kuwa hifadhi, na wananchi wameyaendeleza kwa kuyapatia huduma muhimu za jamii kama vile hospitali, shule, nyumba za kuabudu na barabara; pia maeneo hayo yameonesha kuchangia kwa kiasi kikubwa mapato kwenye Halmashauri husika;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kuridhia maeneo hayo yaendelee kutumika kama ardhi kwa ajili ya makazi ya watu na shughuli za kilimo na ufugaji kwa kuyafuta kutoka kwenye orodha ya maeneo yaliyotengwa kuwa hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dosari ya tafsiri ya neno "*movement*" katika Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010.

KWA KUWA Kifungu cha 3 cha Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, Na. 12 ya mwaka 2010 kinatafsiri neno uhamishaji wa mifugo *(movement)* kuwa ni kuongezeka au kupungua kwa mifugo kutoka shamba la mifugo kunakohusisha kuzaliwa, kuchinjwa, vifo na kuhamisha, kupotea kwa wanyama au mazao ya wanyama.

NA KWA KUWA tafsiri hiyo haihusishi mifugo inayohamishwa kutoka eneo moja kwenda eneo lingine lililopo nje ya shamba la mifugo ili kutafuta malisho, maji au kukimbia magonjwa ya mifugo, na hivyo tafsiri hiyo haisaidii kudhibiti ufugaji wa kuhamahama.

KWA HIVYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri Serikali kuandaa Muswada wa Sheria ili kuboresha

Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, Na. 12 ya mwaka 2010, kwa ajili ya kudhibiti ufugaji wa kuhamahama.

Mheshimiwa Spika, dosari katika utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo.

KWA KUWA vifungu vya 14 – 18 vya Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 vimeweka mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mazao ya mifugo na kuweka uwiano unaotakiwa wa malisho yaliyopo na idadi ya mifugo.

NA KWA KUWA Kamati imebaini kwamba ipo dosari katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, Na. 12 ya mwaka 2010, jambo linalosababisha mazao ya mifugo kuwa duni na kuwepo kwa uhaba wa maeneo ya malisho na hivyo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro kutokana na wafugaji kuingia kwenye ardhi inayotumiwa na watumiaji wengine.

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali;

(a) Isimamie ipasavyo Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, ili kuitambua, kuisajili na kutunza kumbukumbu za mifugo ili kuboresha upatikanaji wa mazao ya mifugo, upatikanaji wa malisho ya kutosha na kuepusha migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi; na

(b) Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji usiozingatia mipaka ya vijiji.

KWA KUWA Kamati imebaini kwamba migogoro ya ardhi katika mashamba ya *Kapunga Rice Farm* lililopo Mbarali mkoani Mbeya, Efata lililopo mkoani Rukwa, Ranchi

ya Misenyi iliyopo mkoani Kagera na Shamba la Gidagamond la mkoani Manyara, imesababishwa na watendaji wa Serikali waliobinafsisha mashamba hayo na ranchi pasipo kuzingatia mipaka halisi ya maeneo hayo na vijiji vilivyo jirani.

NA KWA KUWA kutozingatia mipaka ya vijiji vinavyozunguka mashamba na ranchi wakati wa zoezi la ubinafsishaji kumesababisha wananchi wa vijiji vilivyo jirani kukosa maeneo ya kufanyia shughuli zao na hivyo kuvamia mashamba hayo na ranchi kwa ajili ya kuendesha shughuli zao, hali inayochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro baina ya wawekezaji na wananchi wa vijiji husika.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali itwae maeneo yanayolalamikiwa na wananchi kwamba yamebinafsishwa bila ya kuzingatia mipaka halisi ya vijiji na kuirejesha ardhi hiyo kwa wananchi baada ya kulipa fidia kwa wawekezaji kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dosari katika utaratibu wa kupima na kusajili vijiji.

KWA KUWA vifungu vya 22 hadi 28 vya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982 vinampa mamlaka Msajili wa Vijiji kusajili na kuvitangaza vijiji vilivyosajiliwa katika Gazeti la Serikali baada ya kuzingatia idadi ya kaya zinazotosha kuwa kijiji na eneo la ardhi linalotosha kwa ajili ya kuendesha shughuli za wananchi.

NA KWA KUWA Kamati ilibaini kuwepo kwa dosari ya kisheria ambapo Msajili wa Vijiji halazimiki kuzingatia mambo mengine muhimu katika usajili kama vile kujiridhisha na mipaka halisi kati ya kijiji kinachotakiwa kusajiliwa na vijiji jirani, uwepo wa ardhi ya kutosha katika kijiji tarajali, asili ya kijiji kinachosajiliwa na uwepo wa huduma muhimu za kijamii, ni kichocheo cha kuibuka kwa migogoro miongoni mwa wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na hata kijiji na kijiji.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali:-

(a) Kuleta mapendekezo ya marekebisho ya sheria ili kuweka vigezo vya usajili wa kijiji kujumuisha ukaguzi wa mipaka ya kijiji tarajiwa, mipaka ya kijiji na vijiji vya jirani, uwepo wa ardhi ya kutosha, kuangalia asili na historia ya kijiji na uwezekano wa kijiji kipya kupata huduma muhimu za kijamii; na mwisho

(b) Ni kufanya uhakiki ili kubaini kama usajili wa vijiji vyenye migogoro ya ardhi ulikidhi vigezo na kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo katika Halmashauri nchini.

KWA KUWA imebainika kuwa sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto ya miundombinu ya huduma duni za ugani kutokana na ufinyu wa bajeti katika ngazi za Halmashauri nchini.

NA KWA KUWA ukosefu huo wa miundombinu na huduma bora za ugani, ni miongoni mwa sababu za kuwepo kwa ufugaji wa kuhamahama unaochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuzielekeza Halmashauri zote nchini zinazokusanya ushuru kutokana na shughuli za ufugaji, zianzishe Mfuko Maalum wa Maendeleo ya Mifugo *(Livestock Development Fund-LDF)* kwa kuwashirikisha wenyewe. Mfuko huo utatokana na kiwango maalum cha ushuru husika ili fedha hizo zitumike mahsusi kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya ufugaji (majosho, mabwawa,) na huduma za ugani kama vile tiba mifugo na elimu kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wanaokodisha mashamba kwa wananchi.

KWA KUWA uamuzi wa Serikali kuwapatia wawekezaji maeneo ya ardhi ulilenga kuwapa fursa ya kuboresha shughuli za kilimo na ufugaji ili kuchangia kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

NA KWA KUWA Kamati ilibaini kwamba wawekezaji wengi waliouziwa mashamba kwa ajili ya uwekezaji kama vile wawekezaji waliouziwa *Southern Highlands* nimeondoa mashamba ya *RIVACU,* kama wengine watakuwa wameiona pale kwa sababu haikuuzwa ilikuwa ni *typing error*. *Southern Highlands* Wilaya ya Mbarali na shamba la Patel Wilaya ya Kilosa hawayatumii mashamba hayo kama ilivyokusudiwa bali wanayakodisha kwa wananchi kwa gharama kubwa, jambo linalochochea migogoro baina ya wawekezaji na wafugaji na wakulima baada ya wananchi hao kuvamia maeneo ya wawekezaji.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali:-

(a) Kufuta umiliki wa mashamba ambayo wawekezaji wanayakodisha kwa wananchi kama vile mashamba ya *Southern Highland* Wilaya ya Mbarali na shamba la Patel katika Wilaya ya Kilosa na yanayofanana na hayo na kuyagawa kwa wananchi. *(Makofi)*

(b) Kuchunguza mashamba mengine yote ambayo wawekezaji wanayakodisha kwa wananchi, kufuta umiliki wake na kuyatwaa kuyagawa kwa wananchi. Huko nyuma tumeorodhesha tumeambatanisha orodha ya mashamba pori yaliyoko ambayo yamekaa ambayo hayo ndiyo tunayapendkeza yafutwe na wananchi waweze kugawiwa mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya muda wa kati, kundi hili ni mapendekezo yanayohitaji kutekelezwa ndani ya kipindi kisichozidi miaka mitano. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

Moja, kukosekana kwa masoko ya uhakika kwa mazao ya kilimo na mifugo.

KWA KUWA kumekuwepo na ukosefu wa masoko ya uhakika ya mazao ya mifugo na kilimo.

NA KWA KUWA ukosefu wa masoko ya uhakika wa mazao ya mifugo umesababisha kuwepo kwa ongezeko la mifugo inayoshindwa kupata malisho ya uhakika na pia ukosefu wa masoko ya uhakika wa mazao ya kilimo umesababisha mazao mengi kuozea katika maghala na hivyo kusababisha wakulima na wafugaji na Taifa kwa ujumla kushindwa kufaidika na mazao hayo kiuchumi.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuhakikisha panakuwepo na soko thabiti la mazao ya mifugo *(meat commisision)* na kilimo *(commodity exchange market)* ili kuchochea uvunaji wa mifugo kwa mujibu wa sheria na pia kuwawezesha wakulima na wafugaji kuinua hali zao kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pili, ni upungufu wa rasilimali watu na fedha.

KWA KUWA rasilimali fedha na rasilimali watu ni muhimu katika kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi.

NA KWA KUWA uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa upo upungufu mkubwa wa rasilimali watu na fedha unaosababisha mipango mingi kutokamilishwa ikiwemo upimaji wa ardhi za vijiji na Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kutenga bajeti ya kutosha kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya kuajiri wataalam na kugharamia shughuli za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ongezeko la idadi ya watu.

KWA KUWA ongezeko la idadi ya watu hapa nchini ni kubwa kufikia wastani wa 2.82% kwa mwaka na kusababisha upungufu wa ardhi iliyopo kwa ajili ya matumizi ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

NA KWA KUWA ongezeko hili linachangia kuibuka kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji na wawekezaji kutokana na kugombea rasilimali ardhi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kibinadamu,

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali:-

(a) Kupunguza kasi ya ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa kigeni kwa kuwa, vipo viashiria kuwa katika miaka michache ijayo, migogoro ya ardhi itaongezeka kutokana na kuwepo kwa ongezeko la idadi ya watu.

(b)Kuendelea kuelimisha wananchi wazingatie uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Spika, nne, fidia kwa wananchi wanaohamishwa.

KWA KUWA Sera na Sheria za ardhi zinaelekeza kuwa malipo ya fidia stahiki na kwa wakati ni haki ya wananchi ambao ardhi yao inatwaliwa na Serikali au kupewa wawekezaji.

NA KWA KUWA kushindwa au kuchelewa kulipa fidia kwa wananchi mara baada ya kuwahamisha ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa wananchi kutokana na kukosa maeneo ya kuishi na kuendeshea shughuli za kilimo, ufugaji au matumizi mengine.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali;

(a) Kuhakikisha kwamba inalipa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kwenye maeneo wanayoishi au kuyatumia kihalali kabla ya maeneo hayo kutwaliwa na Serikali.

(b) Wananchi walipwe kwa wakati fidia inayoendana na thamani ya ardhi, makazi na mali zao kwa wakati huo mara wanapoondolewa kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, tano ni kuwafidia wawekezaji halali wa mashamba yenye migogoro.

KWA KUWA ardhi ni muhimu kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali zikiwemo za kilimo, ufugaji na uwekezaji, baadhi ya wakulima na wafugaji wanaoishi maeneo yanayozunguka mashamba ya wawekezaji wanakosa ardhi kutokana na ardhi iliyokuwepo kugawiwa kwa wawekezaji wakati wa zoezi la ubinafsishaji, hivyo kutoweza kuhimili ongezeko la watu na shughuli za kibinadamu.

NA KWA KUWA ukosefu wa ardhi kwa ajili ya wananchi kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji umesababisha baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya wawekezaji na kusababisha uharibifu wa mali za wawekezaji kama ilivyotokea katika Wilaya ya Babati, shamba la Kiru na katika maeneo mengine nchini.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kushauriana na wawekezaji ambao maeneo waliyopewa yana migogoro ardhi kati yao wananchi wanaoishi jirani na maeneo yao kutokana na kutokuwa na ardhi ya kuendesha shughuli zao ili wayaachie kwa wananchi kwa kuzingatia makubaliano yenye tija kati yao na Serikali; kwa maana ya kupata fidia, wananchi ambao hawana ardhi wapate.

Mheshimiwa Spika, sita, ukosefu wa miundombinu ya mifugo.

KWA KUWA ukosefu wa miundombinu ya mifugo kama vile malambo na majosho ni sababu za msingi zinazochangia kuwepo kwa mfumo wa ufugaji wa kuhamahama,

NA KWA KUWA ufugaji wa kuhamahama unachangia kuwepo kwa uharibifu wa mazingira na kuibuka kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuanzisha miundombinu ya mifugo kama vile malambo na majosho katika maeneo yote yaliyotengwa rasmi kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, namba saba ni uhaba wa maji.

KWA KUWA maji ni rasilimali muhimu katika uendeshaji wa sekta ya kilimo na mifugo na kwa ajili ya kuchangia maendeleo na kuboresha shughuli za wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

NA KWA KUWA imebainika kwamba kuna uhaba mkubwa wa rasilimali maji katika baadhi ya maeneo hapa nchini unaosababisha muingiliano wa shughuli za wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi unaochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwao.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali:-

(a) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali ya maji katika maeneo yenye uhaba wa maji.

(b) Kuhakikisha kwamba wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi wanapata fursa sawa ya kutumia maji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, nane, dosari katika utunzaji wa mazingira;

KWA KUWA utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa lengo la kuboresha hali ya maisha na shughuli mbalimbali katika kukidhi mahitaji ya kibinaadamu na viumbe hai vingine.

NA KWA KUWA Kamati imebaini kuwepo kwa dosari katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Namba 20 ya mwaka 2004 zinazochangia kukauka kwa vyanzo vya maji, kuharibiwa kwa kingo za mito, Delta ya Bonde la Mto Rufiji, Bonde la Mto Kilombero, kupotea kwa uoto wa asili kutokana na wakulima na wafugaji kuvamia maeneo hayo, hivyo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuimarisha utunzaji wa mazingira, vyanzo vya maji, mabonde na kingo za mito na bahari, delta na mabwawa.

Mheshimiwa Spika, namba tisa ni kuimarisha Mabaraza ya Ardhi.

KWA KUWA uwepo wa Mabaraza ya Ardhi katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya umekumbwa na changamoto kubwa zinazokwamisha usuluhisi wa migogoro ya ardhi kwa kukosekana wataalamu na rasilimalil za kutekeleza majukumu yao.

NA KWA KUWA imebainika kwamba changamoto hizo zimesababisha kuendelea kuibuka na kukua kwa migogoro ya ardhi katika maeneo mengi hapa nchini.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kupitia upya Sheria inayoanzisha Mabaraza ya Ardhi ili kuhakikisha kuwa wajumbe wanaoteuliwa kwenye Mabaraza husika ni wale tu wenye sifa zitakazosaidia utatuzi wa migogoro na pia kuhakikisha kwamba mabaraza husika yanakuwa na uwezo wa kuratibu shughuli nzima zinazohusiana na ugawaji wa ardhi katika maeneo husika.

KWA KUWA Kamati imebaini kuwa ni chini ya 10% ya vijiji vyote vilivyopo hapa nchini hadi kufikia Novemba, 2012 ambavyo vimepimwa.

NA KWA KUWA uwepo wa vijiji vingi ambavyo havijapimwa umesababisha mgongano wa watumiaji mbalimbali wa ardhi kama vile wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi hali inayosababisha migogoro ya ardhi baina yao kwa wao kutotambua mipaka ya kufanya shughuli zao.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuwa na mpango mahsusi wa kuharakisha upimaji wa vijiji vyote ambavyo havijapimwa ili kuepusha nchi na migogoro ya ardhi inayoweza kuepukika.

Mheshimiwa Spika, katika kundi la mapendekezo ya muda mrefu, Kamati imeainisha mambo ambayo utekelezaji wake utafanyika kwa kipindi cha miaka sita hadi kumi na tano. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kusimamia kilimo na ufugaji wa kisasa na wa kibiashara.

KWA KUWA kilimo na ufugaji wa kisasa na biashara *(intensive agriculture)* ni shughuli zinazoweza kuepusha mifumo ya uzalishaji unaosababisha mwingiliano wa shughuli hizo na migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

NA KWA KUWA wakulima na wafugaji wengi hapa nchini wanaendelea na kilimo na ufugaji wa kuhamahama, jambo linalochangia kuibuka kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini kutokana na mwingiliano wa shughuli hizo wakati wa kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza Bunge liitake Serikali:-

(i) Kuelimisha wakulima na wafugaji kuhusu kilimo cha kisasa na kibiashara pamoja na kuhakikisha kuwa wakulima wanatumia teknolojia ya kisasa inayowezesha uzalishaji wenye tija katika eneo dogo; na

(ii) Kuelimisha wakulina na wafugaji kuhusu ufugaji wa kisasa na wa kibiashara unaoendana na matumizi ya eneo dogo kwa uzalishaji wenye tija kutokana na matumizi ya aina bora za mifugo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti kwa ajili ya miundombinu ya kilimo na mifugo.

KWA KUWA uendelezaji wa miundombinu kwa ajili ya ufugaji hutegemea upatikanaji wa fedha zilizokadiriwa katika Bajeti kwa ajili hiyo, lakini mwenendo wa Bajeti umeendelea kutokidhi mahitaji ya uendelezaji wa miundombinu.

NA KWA KUWA ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya ufugaji na kilimo umesababisha kutokuwepo kwa miundombinu jambo linalochangia kuibuka, kuendelea na kukua kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza kuwa Bunge liiitake Serikali kutenga fedha zakutosha na kuheshimu Bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miundombinu ya kilimo na mifugo.

(iii) Kuanzisha Bodi ya Maendeleo ya Miundombinu ya Ufugaji.

KWA KUWA imebainika kwamba hakuna chombo mahsusi kilichoundwa kwa ajili ya kusimamia miundombinu ya ufugaji kama vile majosho na malambo, sekta ya mifugo imekuwa ikikumbwa na changamoto mbalimbali,

NA KWA KUWA kukosekana kwa chombo kinachosimamia maendeleo ya miundombinu ya ufugaji

kunachangia kuendelea kuwepo kwa mfumo wa ufugaji wa kuhamahama unaoharibu mazingira na vyanzo vya maji na kusambaza magonjwa ya mifugo, hali inayosababisha wafugaji kuvamia maeneo ya watumiaji wengine wa ardhi.

NA KWA HIYO BASI Kamati inapendekeza Bunge liitake Serikali:-

(a) Kuanzisha Bodi ya Maendeleo ya Miundombinu ya Ufugaji *(The Livestock Infrastructure Development Board)* kwa ajili ya kusimamia na kuratibu ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya ufugaji kwa nchi nzima; na

(b) Kuheshimu bajeti itanayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya rejea namba sita ni kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na utendaji.

Mheshimiwa Spika, hadidu ya rejea ya sita iliitaka Kamati kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na kiutendaji. Jukumu hili si dogo na linahitaji kujiridhisha bila ya shaka yoyote kuhusu uhusika wa wahusika, namna walivyohusika na sababu za kuhusika kwao.

Vilevile msukumo katika kuhusika kwao pamoja na manufaa ya kibinafsi na kitaifa yanayoweza kupatikana kwa hatua za uwajibikaji zitakazopendekezwa ama kuchukuliwa ni mambo yanayohitaji kujiridhisha nayo. Aidha, hatua hii inapaswa kufikiwa baada ya kujiridhisha pasipo na shaka yoyote juu ya dhima na wajibu wa Bunge katika mustakabali mzima wa kulitumikia Taifa na watu wake.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa kwa kiasi kikubwa sababu za migogoro ya ardhi na matatizo ya uhifadhi wa mazingira ambavyo huchangia

migogoro ya ardhi ni masuala mtambuka ambayo asili, athari na namna zinavyotokea zinategemeana na kunasibiana miongoni mwa sekta, idara, asasi mbalimbali za Serikali na pia wananchi kwa ujumla. Kwa mfano, ipo migogoro ya ardhi na uharibifu wa mazingira inayotokana na kutosimamiwa kikamilifu kwa sheria. Migogoro mingine inatokana na kuchelewa kutolewa kwa uamuzi na vyombo vya kutoa maamuzi kama vile mahakama au kuchelewa kwa Serikali kutekeleza maamuzi ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, maelezo haya yanaakisi hali iliyojitokeza Wilayani Kiteto ambako yapo maamuzi ya mahakama yanayobainisha namna ardhi inayogombewa inavyopasa kutumika, maamuzi hayo hadi sasa hayajatekelezwa kikamilifu na hali hii inachangia kuendelea kutokea kwa migogoro ya mara kwa mara baina ya wakulima na wafugaji na hivyo kusababisha uvunjifu wa amani katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, migogoro mingine inatokana na mawasiliano duni miongoni mwa watendaji. Vilevile ipo migogoro inayotokana na kukosekana kwa elimu ya matumizi ya ardhi na uhifadhi wa mazingira na sababu nyingine kama migogoro inayotokana na usimamizi hafifu wa sheria za ardhi, mifugo, kilimo, maji, uwekezaji na mazingira. Aidha, ongezeko la idadi ya watu na mabadiliko ya tabia ya nchi vinachangia kutokea kwa mivutano na migogoro katika matumizi ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali. Kamati ilibaini kuwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi inagusa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali pamoja na wananchi wenyewe katika maeneo yenye migogoro.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, hekima na busara za Kibunge *(Parliamentary wisdom)* katika Kamati ziliiongoza Kamati kuandaa taarifa hii ili kulishauri Bunge kwa mujibu wa maelekezo katika hadidu ya rejea hii. Jambo muhimu ni kwamba endapo ushauri huu utaridhiwa na Bunge lako Tukufu, utaweka misingi madhubuti ya Bunge kuisimamia Serikali katika kutatua migogoro ya ardhi katika

maeneo mengi nchini ambayo imekuwa mingi kwa sasa na hata kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika kuishauri Serikali na kusimamia uwajibikaji wake yote haya ni majukumu ya Bunge. Katika kutumia madaraka ya Bunge na katika kutekeleza majukumu yake, majukumu ya kushauri na kusimamia Serikali yanaweza kwenda kwa pamoja au moja laweza kutekelezwa baada ya lingine. Kwa mfano, Bunge linaweza kuishauri Serikali na baadae Bunge laweza kuitaka Serikali kuchukua hatua za kutaka uwajibikaji unaotokana na utekelezaji wa ushauri uliotolewa na hivyo kufikia hatua ya Bunge kuweka maazimio yake.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo yote hayo, Kamati inapendekeza hadidu ya rejea hii isomwe kwa pamoja na mapendekezo ya Kamati ushauri uliotolewa uliwezeshe Bunge lako kuweka misingi imara itakayowezesha migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini kufikia ukomo na kuweka utaratibu utakaokidhi matarajio ya wananchi katika jambo hili kwa namna yenye kuleta tija na yenye kuzingatia haki.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa ujumla, madhara yanayotokana na migogoro miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi ni makubwa. Na inaleta athari nyingi za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Migogoro inayowahusisha wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi inapaswa kudhibitiwa na Serikali ili isiendelee kuleta athari hizo.

Aidha, Kamati inapendekeza kuwa ili kuhakikisha kwamba migogoro hii inakwisha kabisa, Bunge liiendelee kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha taarifa hii, naomba nikushukuru wewe mwenyewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kutupa heshima kubwa ya kuwa Wajumbe wa Kamati Teule ya Bunge. Nawashukuru pia Waheshimiwa

Wabunge wote, mashahidi na marafiki waliofika mbele ya Kamati Teule kwa ajili ya majadiliano, kutupatia mawazo, ushauri wao na mahojiano pia kwa kutuletea nyaraka mbalimbali tulizoziomba au kuzihitaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inathamini sana mchango wao katika kufanikisha taarifa hii. Tunaamini kwamba yote hayo yalifanyika kwa mapenzi mema waliyonayo kwa nchi yetu. Tunapenda kuwaeleza kwamba mchango wao umetusaidia sana kutekeleza jukumu hili.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuzishukuru Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Manyara, Arusha, Kigoma, Tabora, Kagera, Rukwa, Katavi na Mbeya kwa namna zilivyosaidia Kamati kukamilisha ziara za kiuchunguzi katika baadhi ya Wilaya za Mikoa hiyo kwa usalama. Aidha, napenda kutambua ushirikiano mzuri tulioupata kutoka kwa wawekezaji na wananchi wa vijiji vilivyotembelewa na Kamati kwa ajili ya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa kufanya kazi na Kamati kwa muda wote, kwa ushauri wake makini uliowezesha kuhakikisha kuwa uratibu wa shughuli za Kamati unaenda vizuri na unaimarika wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, naishukuru timu nzima ya Sekretarieti ya Kamati Teule kwa utendaji wao wa kitaalam uliosaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuthamini kazi yao naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo, Ndugu Athuman Hussein - Kiongozi wa Sekretarieti, Ndugu Dickson Bisile - Mjumbe Kamati ya Sekretarieti, Ndugu Zainab Issa Mjumbe wa Sekretarieti, Ndugu Lina Kitosi - Mjumbe wa Sekretarieti, Ndugu Pius Mboya - Mjumbe wa Sekretarieti, Ndugu Prudence Rweyongeza - Mjumbe wa Sekretarieti, Ndugu Erick Maseke - Mjumbe wa Sekretarieti na Ndugu Mathew Kileo - Mjumbe wa Sekretarieti. Aidha, nawashukuru kwa dhati watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao katika uratibu wa shughuli za Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa Hoja naomba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Simanjiro kwa kuendelea kunivumilia wakati tulipokuwa katika shughuli za Kamati na nikiwataja wananchi wa Simanjiro ni pamoja na wananchi wa Majimbo ya Wajumbe wote wa Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA YA KAMATI TEULE YA BUNGE ILIYOUNDWA KUCHUNGUZA SABABU ZA MIGOGORO BAINA YA WAKULIMA, WAFUGAJI, WAWEKEZAJI NA WATUMIAJI WENGINE WA ARDHI NCHINI KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**ORODHA YA VIAMBATISHO**

**A: VIELELEZO**

**Kielelezo Na. 01:** Orodha ya vijiji vilivyotembelewa

**Kielelezo Na. 02:** Orodha ya mashahidi waliohojiwa na Kamati pamoja na marafiki wakiwemo Wabunge waliojadiliana na Kamati kuanzia tarehe 28 Novemba, 2013 hadi tarehe 4 Februari, 2014

**B: JEDWALI**
Jedwali kuonesha wizara zinazosimamia utekelezaji wa sera, mikakati na sheria zilizochambuliwa.

**C: JUZUU**
**JUZUU YA I:** Hali ya migogoro na mapitio ya Sera, Mikakati na Sheria
**JUZUU YA II:** Mambo yaliyobainika na mapendekezo yake.

**D: RANDAMA**: Matokeo ya uchunguzi

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 122 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

**Mheshimiwa Spika,**

Bila ya kuathiri Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inayohusu muundo wa Taarifa ya Kamati Teule, Taarifa hii inasomwa pamoja na Juzuu mbili za maelezo ya matokeo ya uchunguzi uliofanywa na Kamati Teule zikiwa na viambatisho vyake.

Viambatisho hivyo, ni:

i) Randama ya yaliyojitokeza wakati Kamati ilipofanya ziara ya kiuchunguzi;

ii) Orodha ya Mashamba yaliyotelekezwa kwa muda mrefu bila kuendelezwa; na

iii) Nakala za Taarifa Rasmi za Bunge zinazohusu majadiliano ya Kamati wakati wa uchunguzi.

### 1.1 Chanzo cha Kuundwa kwa Kamati Teule

**Mheshimiwa Spika,**

Chanzo cha Kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge[1] ni Hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge iliyotolewa Bungeni na Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, mnamo tarehe 01 Novemba, 2013.

Hoja hii ilifuatiwa na michango mbalimbali ya waheshimiwa Wabunge kuhusu kero na madhara yanayotokana na migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Miongoni mwa Wabunge waliochangia ni pamoja na Mheshimiwa Said Juma Nkumba (Mb), Mheshimiwa Alphaxard

[1]Hansard ya Tarehe 01 Novemba, 2013

Kangi Ndege Lugola (Mb), Mheshimwa Pauline P. Gekul (Mb), Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani (Mb) na Mheshimiwa Saidi Amour Arfi (Mb) walizungumzia migogoro iliyopo baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya michango mbalimbali ya waheshimiwa Wabunge, mtoa hoja, Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla (Mb), alipewa nafasi ya kuhitimisha hoja yake na kueleza:

> NUKUU: "*Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa niliyoitoa leo asubuhi wakati wa kuchangia hoja ya kuahirisha shughuli ... naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lako Tukufu, likubali kuunda Kamati Teule ya kuchunguza na kuchambua Sera mbalimbali zinazohusu masuala ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji, Wanyama pori, na uwekezaji ili kubaini kasoro zilizomo katika matumizi ya ardhi na hatimaye kuleta mapendekezo Bungeni ambayo yakitekelezwa na Serikali yatapunguza na kuondoa migogoro ya muda mrefu inayoendelea kati ya Wafugaji na Wakulima, na hifadhi, Wawekezaji na Watumiaji wengine wa ardhi*"

Maelezo ya Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla (Mb) yalitaka kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge kwa ajili ya kuchunguza migogoro miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi na kutoa mapendekezo Bungeni. Baada ya maelezo hayo, Hoja iliungwa mkono na kuafikiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati Teule ya Bunge iliundwa na wajumbe wake kutangazwa tarehe 09 Novemba, 2013, chini ya Kanuni ya 120 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 kwa ajili ya kuchunguza sababu za kuwepo kwa migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Wajumbe walioteuliwa na kutangazwa siku hiyo ni:-

1) Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla, (Mb)

2) Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb)
3) Mhe. Magdalena Hamis Sakaya, (Mb)
4) Mhe. Joseph Roman Selasini, (Mb)
5) Mhe. Christopher Olenyokie Ole-Sendeka, (Mb)

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya uteuzi huo, katika kikao chao cha kwanza, Wajumbe walimchagua Mheshimiwa Christopher Olenyokie Ole-Sendeka, (Mb) kuwa Mwenyekiti wa Kamati, kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

**Mheshimiwa Spika,**
Mnamo tarehe 19 Januari, 2014 Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kutokana na uteuzi huo, Mheshimiwa Spika alimteua Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu (Mb), kujaza nafasi hiyo.

**1.2 Hadidu za Rejea**
Kamati Teule ya Bunge ilipewa Hadidu za Rejea zifuatazo:-

i) Kuchambua Sera mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi ili kubainisha kasoro zilizomo na kuchunguza mikakati ya utekelezaji wa Sera hizo iliyowekwa na Serikali,

ii) Kufanya mapitio ya taarifa nyingine za Kamati na Tume zilizoundwa huko nyuma kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji,

iii) Kuchambua mikakati yote ya Serikali ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji,

iv) Kuchambua mikakati ya kulinda vyanzo vya maji pamoja na uharibifu wa mazingira,

v) Kutoa mapendekezo yatakayoondoa migogoro iliyopo na kudumisha uhusiano mzuri na utangamano kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi,

vi) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na utendaji,

vii) Mambo mengine yoyote ambayo Kamati itakayoona yanafaa.

**1.3 Namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake**

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilitumia njia mbalimbali kutekeleza majukumu yake. Njia hizo ni pamoja na:-

i) Kupitia machapisho mbalimbali kuhusiana na migogoro ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi;

ii) Kukutana na kujadiliana na wadau mbalimbali wakiwemo wanataaluma na Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE) na marafiki wengine wa Kamati kama vile Waheshimiwa Wabunge na vyama vya wakulima na wafugaji;

iii) Kuwahoji mashahidi kutoka taasisi za Serikali;

iv) Kuchambua nyaraka mbalimbali zilizowasilishwa na mashahidi na marafiki wa Kamati wakati wa majadiliano na mahojiano;

v) Kutembelea baadhi ya sehemu zilizoathirika na migogoro na kuchaguliwa kama sampuli *(Sample)* katika uchunguzi. Kamati ilitembelea wilaya kumi na tisa (19) za mikoa kumi na moja (11) ambayo ni: Pwani, Morogoro, Dodoma, Manyara, Arusha, Kigoma, Tabora, Kagera, Rukwa, Katavi, na Mbeya.

vi) Kufanya mikutano ya hadhara katika vijiji 53 vya wilaya za mikoa hiyo kwa lengo la kupata taarifa na maelezo kutoka kwa wananchi wanaoishi kwenye baadhi ya maeneo yenye migogoro ya ardhi. Orodha ya vijiji hivyo ni **Kielelezo Na. 01.**

Orodha ya Mashahidi waliohojiwa na Kamati pamoja na Marafiki wakiwemo Wabunge waliojadiliana na Kamati kuanzia tarehe 28 Novemba, 2013 hadi tarehe 4 Februari, 2014 ni **Kielelezo Na. 02.**

**1.4 Hali ya Migogoro**

**Mheshimiwa Spika,**
Hali ya migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi imeelezwa katika Juzuu ya Kwanza ya Maelezo kuhusu hali ya migogoro na mapitio ya sera, mikakati na sharia.

Kwa muhtasari, mapitio ya nyaraka zilizofanyiwa kazi na Kamati yameonesha kuwa hali hiyo imedumu kwa muda mrefu sasa licha ya kuwepo kwa Sera, Mikakati na Sheria madhubuti kwa ajili ya kusimamia masuala ya ardhi

**Mheshimiwa Spika,**
Migogoro baina ya wakulima na wafugaji itaendelea kudumu kwa muda mrefu zaidi endapo haitapatiwa ufumbuzi, ikiwamo jitihada za viongozi kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

Hali ya sasa ya migogoro hiyo ni mbaya zaidi na inatishia kutoweka kwa amani, umoja na utangamano wa wananchi katika maeneo yenye migogoro na taifa kwa ujumla.
Hivi sasa katika maeneo yenye migogoro, uhasama baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi umefikia kiwango cha juu; ambapo imekuwa vigumu kwa jamii hizo kukaa pamoja katika mikutano, kushirikiana katika shughuli za ujenzi wa taifa au za kijamii, kutumika kwa lugha za kibaguzi na ukabila na hivyo kusababisha mapigano ya mara kwa mara na hata mauaji miongoni mwao.

**Mheshimiwa Spika,**
Katika kudhihirisha kuwa tatizo hili lilifahamika Serikalini, barua ya tarehe 19 Februari, 1986 yenye Kumb. Na. PMO/DSM/A.40/01/01, kutoka kwa Msaidizi wa Waziri Mkuu na Makamu wa

Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwenda kwa Mkuu wa wilaya ya Morogoro vijijini, inathibitisha zaidi. Kwa mujibu wa barua hiyo, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Joseph S. Warioba) alitaka kuona mgogoro baina ya wakulima na wafugaji wa kijiji cha Kambala kilichopo katika wilaya ya Mvomero mkoa wa Morogoro, unapatiwa ufumbuzi wa kudumu ifikapo tarehe 01 Machi, 1986, kama inavyodhihirika katika nukuu ya barua hiyo:-

> **NUKUU "*... pamoja na barua hii Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais atapenda kuona suala hilo linapatiwa ufumbuzi wa kudumu na hatua za haraka zinachukuliwa mara moja kumaliza uhasama uliopo kati ya wafugaji na wakulima*."**

Kwa barua hiyo, bila shaka, Mkuu wa Wilaya alitakiwa kuhakikisha kuwa mgogoro unakwisha kabisa ili kuondoa uhasama uliokuwepo baina ya makundi hayo ya watumiaji wa ardhi katika kijiji cha Kambala. Nakala ya barua hiyo ni **Kielelezo Na. 01 kwenye Juzuu ya I.**

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa sasa ni takriban miaka 28, mgogoro kati ya wakulima na wafugaji wa kijiji cha Kambala umeendelea kukua na kusababisha vifo, uharibifu wa mali, uvunjifu wa amani na kuathiri shughuli za maendeleo.

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu migogoro hiyo kwa lengo la kubaini kiini, sababu na namna ya kutatua tatizo la msingi. Maelezo ya kina kuhusu matokeo ya baadhi ya tafiti hizo yameelezwa katika **Juzuu ya II.**

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa hali halisi ya migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini, Serikali na wananchi kwa ujumla hawana budi kujitathmini wajibu wao katika kudumisha amani, usalama na maendeleo ya Taifa. Endapo migogoro hii itaendelea, Taifa lisitarajie

kufanikisha Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN[2]) katika shughuli za kiuchumi na kijamii na kukua kwa uzalendo na mshikamano miongoni mwa wananchi. Ni vema hatua madhubuti zikachukuliwa sasa kama ilivyo katika mapendekezo ya Kamati hii.

## 2.0 AINA NA SABABU ZA MIGOGORO
### 2.1 Aina za Migogoro

**Mheshimiwa Spika,**
Ili kuchambua vema kiini halisi cha migogoro ya ardhi miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi, uchambuzi wa Kamati umeainisha migogoro hiyo katika aina tano zifuatazo:-

i) Migogoro baina ya Wakulima na Wafugaji
ii) Migogoro baina ya Wakulima na Wawekezaji
iii) Migogoro baina ya Wafugaji na Wawekezaji
iv) Migogoro baina ya Wakulima/ Wafugaji dhidi ya maeneo ya Hifadhi
v) Migogoro baina ya Wananchi na Serikali

Chanzo cha migogoro ya aina zilizotajwa hutofautiana kutoka aina moja na nyingine na sehemu moja na nyingine. Aidha, aina moja ya mgogoro inaweza kusababisha kuibuka kwa aina nyingine ya mgogoro.

### 2.2 Sababu za Migogoro baina ya Wakulima, Wafugaji, Wawekezaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilibaini kuwepo kwa sababu mbalimbali za kuibuka, kukua na kuendelea kuwepo kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Sababu hizo zimeelezwa katika **Juzuu ya I,** ambazo baadhi yake ni:-

a) Vijiji kutokuwa na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi,

[2] Big Results Now – Mpango Maalum uliozinduliwa na Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete mnamo Februari, 2013 wenye lengo la kuleta mabadiliko katika sekta mbalimbali ili kuleta maendeleo na kukuza uchumi wa Taifa.

b) Kutokutengwa kwa Maeneo Mahsusi kwa ajili ya Kilimo na Ufugaji
c) Kutotengwa kwa maeneo mahsusi kwa ajili ya malisho
d) Kilimo na Ufugaji wa kuhamahama
e) Kutambua umuhimu na thamani ya ardhi na kuongezeka kwa Mahitaji ya Ardhi kunakosababishwa na:

i) Ongezeko kubwa la idadi ya watu na idadi ya mifugo,
ii) Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya shughuli za ufugaji,
iii) Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya kilimo,
iv) Upanuzi wa maeneo ya hifadhi za Taifa,
v) Kupanuka na kuanzishwa kwa miji mipya,
vi) Ongezeko la vitalu vya uchimbaji madini na uwindaji,
vii) Kupungua kwa ardhi inayofaa kwa uzalishaji kutokana na Mabadiliko ya tabia nchi na ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa mazingira

a) Kutokupimwa na kubainishwa kwa mipaka kati ya vijiji
b) Watu wachache kumilikishwa maeneo makubwa ya

ardhi

c) Kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa sera na sheria. Mfano wa maeneo yasiyosimamiwa vizuri kwa mujibu wa maelezo ya wadau mbalimbali ni:-

*i) Tamko la Sheria ya Ardhi za Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999* kuhusu kutengwa maeneo mahsusi kwa ajili ya shughuli za ufugaji;

ii) Utaratibu wa kupunguza mifugo *uliowekwa na Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo, Na. 13* (2010);

iii) Utaratibu wa vibali maalumu wakati wa kuhamisha mifugo kutoka sehemu moja kwenda nyingine *uliowekwa na Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo*, Na. 12 ya mwaka 2010; na

iv) Maelezo ya Sera ya Maji kuhusu uvunaji, uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa ajili ya matumizi ya mifugo na kilimo.

d) Kutokuwepo kwa chombo cha kuratibu matumizi ya Ardhi

e) Upungufu na ukosefu wa Maji

f) Dosari za Maudhui ya Sera na Sheria

g) Uwekezaji Usiofuata Sheria na Taratibu ambapo baadhi ya wawekezaji:-

i) Wamepewa au kumilikishwa maeneo ya ardhi bila wananchi wa maeneo husika kushirikishwa na bila ya kufuata taratibu zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria[3].

ii) Wameyatelekeza mashamba jambo linalosababisha wakulima/wafugaji kuvutiwa kufanya shughuli zao katika mashamba hayo wakiamini kuwa ni ardhi isiyo na mmiliki.

iii) Wawekezaji wanakodisha maeneo yao kwa wakulima au wafugaji badala ya kuyaendeleza kama ilivyokusudiwa. Katika utaratibu huu, wawekezaji huyakodisha mashamba hayo kwa gharama kubwa ambazo wakulima wadogo au wafugaji hushindwa kuzimudu. Utaratibu huu unachangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro baina yao na wawekezaji[4].

iv) Wamepewa mashamba pasipo kufuata taratibu za kisheria.

Kwa mujibu wa *Sheria ya Uwekezaji* ya mwaka 1997, wawekezaji wanatakiwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kabla ya kupewa ardhi kwa ajili ya mashamba. Utaratibu uliopo kwa sasa, unamwezesha mwekezaji kupata ardhi kupitia mojawapo kati ya Wizara ya Ardhi au TIC.

[3] Hansard: Mahojiano ya tarehe 06 Disemba, 2013 na Mhe. Prof. Anna Tibaijuka, Majadiliano ya tarehe 28 Novemba 2013 na Prof. Davis Mwamfupe, Rufaa ya *Udaghwenga Bayay na Wenzake dhidi ya Halmashauri ya Kijiji cha Vilima Vitatu.* Rufaa Na. 77 ya mwaka 2012 Mahakama ya Rufaa,ya Tanzania-Arusha.

[4]Hansard: Majadiliano ya tarehe 5 Disemba, 2013 na MVIWATA

m) Kutozingatiwa kwa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi,

n) Kauli za baadhi ya viongozi wa serikali na viongozi wa kisiasa kusigana na kukinzana kuhusiana na migogoro baina ya wakulima na wafugaji,

i) Rushwa kwa baadhi ya Watendaji wa Serikali katika ngazi mbalimbali;

ii) Mila na Desturi za Wakulima/Wafugaji zinazochochea Migogoro ya Ardhi.

**3.0 MATOKEO YA UCHUNGUZI**

**Mheshimiwa Spika,**
Matokeo ya uchunguzi wa Kamati Teule kuhusu migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi yamefafanuliwa kwa kina katika Juzuu ya II kwa kufuata mtiririko wa Hadidu za Rejea. Aidha, uchambuzi na matokeo hayo unaainishwa kama ifuatavyo:

**3.1 Hadidu ya Rejea ya kwanza: Uchambuzi wa Sera na mikakati ya utekelezaji**

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilifanya uchambuzi wa Sera mbalimbali ili kubaini na kuainisha namna sera hizo zinavyohusiana na migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Kamati ilibaini kuwa, Sera hizo zinatoa mwongozo wa masuala mbalimbali yakiwemo, matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji, uhamasishaji katika uwekezaji na uboreshaji wa sekta za kilimo na mifugo.

Katika hatua hii ya uchunguzi, Kamati ilichambua sera zifuatazo:-

i) Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997;

ii) Sera ya Taifa ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997;
iii) Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013;
iv) Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006,
v) Sera ya Maji ya Mwaka 2002,
vi) Sera ya Uhamasishaji wa Uwekezaji ya mwaka 1996, na
vii) Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997.

### 3.1.1 Uchambuzi wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati imebaini kuwa Sera ya Taifa ya Ardhi imedumu kwa zaidi ya miaka 18, lakini migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuwepo na kuongezeka licha ya sera hiyo kuwa na maudhui yanayodhibiti kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro.

Maudhui ya Sera ya Taifa ya Ardhi, pamoja na mambo mengine, yanatambua uwepo wa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi kama inavyotamkwa na Sera ya Taifa ya Ardhi, katika Aya namba 7.3:-

> *NUKUU: "Kumekuwa na ongezeko la migogoro ya kijamii, hofu ya uharibifu wa mazingira na migongano ya matumizi ya ardhi kutokana na ugawaji hovyo wa maeneo ya Wafugaji kwa Wakulima wa mashamba makubwa. Hali hii imepunguza maeneo ya malisho…"*[5].
> *"Uhamaji holela wa Wafugaji na mifugo yao husababisha migogoro ya umilikaji ardhi na migongano ya matumizi ya ardhi katika maeneo yenye jamii za makazi ya kudumu..."*[6]

Aidha, maudhui ya jumla ya sera yanabainisha vichocheo mbalimbali vinavyoibua migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Vichocheo hivyo ni vifuatavyo:-
i) Ongezeko kubwa la watu,

[5] Aya ya 7.3.0, Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997
[6] Aya ya 7.3.2, Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997

ii) Ongezeko la mifugo,
iii) Kupungua kwa maeneo ya malisho,
iv) Uhamishaji wa mifugo kutoka kwenye maeneo yasiyo na malisho na maji ya kutosha kwenda kwenye maeneo yenye mahitaji hayo,
v) Ukuaji wa miji,
vi) Utekelezaji wa Sera ya uwekezaji,
vii) Uanzishaji, upangaji upya na upanuzi wa vijiji na miji,
viii) Kuwepo kwa ongezeko la mahitaji makubwa ya ardhi,
ix) Kubadilika kwa aina ya umiliki wa ardhi kimila kuwa wa aina ya umiliki binafsi wa ardhi, na
x) Baadhi ya hukumu za Mahakama kuhusu uhalali wa miliki za kimila za ardhi.

Maudhui ya Sera hizo yanaonesha nia ya kuendeleza sekta ya ardhi, na kuepusha migongano miongoni mwa wamiliki na watumiaji mbalimbali wa ardhi. Kwa kuzingatia maudhui hayo, Serikali inaweza kulinda rasilimali za ardhi na kuwawezesha watumiaji mbalimbali kuwa na haki sawa katika kupata na kutumia ardhi.

**Mheshimiwa Spika,**
Pamoja na ubora wa Sera ya Taifa ya Ardhi kuna kasoro mbalimbali za kiutekelezaji zinazotokana na kutozingatiwa kwa matamko ya sera katika masuala mbalimbali yanayohusu umiliki na utumiaji wa ardhi. Kasoro hizo zimefafanuliwa kwenye **Juzuu ya II** sehemu ya maelezo ya matokeo ya uchambuzi na uchunguzi wa Kamati.

**Miongoni mwa kasoro hizo ni pamoja na:-**

i) Kutokulipa fidia kwa wananchi ambao ardhi yao imetwaliwa na Serikali. Pia kutolipwa kwa kiwango wanachostahili na kwa wakati kulingana na thamani ya ardhi;
ii) Uangalizi na usimamizi duni wa matumizi ya Ardhi;
iii) Kutozingatiwa kwa uamuzi wa Serikali za vijiji katika masuala ya ardhi;
iv) Ugumu katika kupata, kumiliki na kutumia ardhi;
v) Matumizi ya ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji;

vi) Udhaifu katika usimamizi wa sheria za ardhi
vii) Wananchi kutoshirikishwa ipasavyo katika utoaji wa ardhi kwa wawekezaji;
viii) Kutozingatiwa kwa utunzaji wa maeneo ya hifadhi;
ix) Kutokuwa na chombo madhubuti cha utatuzi wa migogoro ya ardhi;
x) Kutokuwepo kwa ramani ya maeneo yaliyopimwa;
xi) Kutoainishwa kwa mipaka halisi ya vijiji; na
xii) Kutokuwepo kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini.

**Mheshimiwa Spika,**
Ufafanuzi na mifano halisi ya kasoro hizo umeainishwa na Kamati kwenye Juzuu ya II.

Aidha, uchambuzi wa baadhi ya sheria zinazohusika na matumizi ya ardhi umewekwa kwenye Juzuu hiyo. Sheria hizo ni:

i) Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999;
ii) Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999;
iii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982;
iv) Sheria ya Utwaaji Ardhi Na. 47 ya mwaka 1967; na
v) Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007.

Aidha, zipo kasoro katika utekelezaji wa sheria hizo pamoja na mkakati wake wa utekelezaji umebainika kuwa na kasoro hizo zinazochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi miongoni mwa wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

### 3.1.2 Uchambuzi wa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mkakati wa utekelezaji wake

**Mheshimiwa Spika,**
Matamko ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na kuweka mazingira mazuri yatakayotoa fursa ya kuboresha sekta ya mifugo kwa kuongeza uzalishaji na kubadilisha ufugaji kuwa wa kisasa na kibiashara hivyo kukuza ajira.

Mkakati wa utekelezaji umefafanua namna ya kutekeleza matamko ya sera. Katika uchambuzi, Kamati imebaini kuwa licha ya kuwepo matamko hayo na mkakati uliowekwa, zipo kasoro katika maeneo mbalimbali ya kiutekelezaji kama zilivyofafanuliwa katika Juzuu ya II.

Baadhi ya kasoro hizo ni:-

i) Kushindwa kuugeuza ufugaji wa asili kuwa wa kisasa na wa kibiashara,
ii) Kutokutengwa kwa maeneo mahsusi kwa ajili ya shughuli za ufugaji,
iii) Kutokuzingatiwa kwa uwiano wa mifugo na malisho,
iv) Kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo; na
v) Kutokuwepo kwa huduma madhubuti kwa ajili ya tiba na kinga za magonjwa ya mifugo.

**Mheshimiwa Spika,**
Ili kufahamu mfumo wa kisheria wa utekelezaji wa sera ya taifa ya Mifugo, Kamati ilichambua Sheria zifuatazo:-

i) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula, Na. 13 ya Mwaka 2010;
ii) Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya Mwaka 2010;
iii) Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003; na
iv) Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008.

Uchambuzi wa Sheria hizo ulionesha kuwa, kama ilivyo kwa Sera, zipo kasoro pia katika utekelezaji na usimamiaji wa Sheria.

**3.1.3 Uchambuzi wa Sera na Sheria za Maji na Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilichambua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002. Vile vile Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria zifuatazo:-

h) Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009 (*The Water Supply and Sanitation Act, No. 12, 2009*);

ii) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 (*The Environmental Management* Act No. 20, 2004); na

iii) Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Maji, Na. 11 ya Mwaka 2009 (*The Water Resources Management Act No. 11, 2009).*

Kwa ujumla, maudhui na matamko ya Sera ya Taifa ya Mazingira na Sera ya Taifa ya Maji yanatoa mwongozo mzuri na Sheria zinaweka misingi na utaratibu mzuri wa usimamizi wa rasilimali hizo. Kasoro za kiutendaji za sera zilizojitokeza zinachangia kuendelea kukua na kuibuka kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi.

**Mheshimiwa Spika,**
Kasoro za kiutekelezaji katika sekta zinazohusika na usimamizi wa rasilimali maji na mazingira zimefafanuliwa katika Juzuu ya Pili. Baadhi ya kasoro hizo ni:-

i) Kutoshirikishwa kwa makundi ya watumiaji wa maji katika kupanga matumizi ya maji, kulinda na kuhifadhi vyanzo vya maji;

ii) Udhaifu katika utekelezaji wa mipango ya Sekta ya Maji; na

iii) Kutosimamiwa kwa Mkakati kuhusu utengaji wa maeneo ya kilimo na malisho ya mifugo.

### 3.1.4 Matokeo ya Uchambuzi wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji na Sheria ya Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilichambua Sera ya Taifa ya Kuhamasisha Uwekezaji pamoja na Mwongozo wa Uwekezaji wa mwaka 2013 *(The Tanzanian Investment Guide, 2013)*. Uchambuzi huo uliiwezesha Kamati kubaini dosari za kiutekelezaji zifuatazo:-

i) Utwaaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji bila ya kuwashirikisha wananchi;

ii) Kutokuwalipa wananchi fidia stahiki wakati maeneo yao yanapotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji; na

iii) Kubadilisha matumizi ya ardhi ya uwekezaji kinyume na Mkataba; na

iv) Utelekezwaji wa ardhi iliyotolewa kwa ajili ya Uwekezaji bila serikali kuchukua hatua zozote.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilichambua Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Na. 26 ya mwaka 1997 iliyotungwa mahsusi kwa ajili ya kuweka utaratibu wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uhamasishaji wa Uwekezaji ya mwaka 1996. Sheria imeanzisha Kituo cha Uwekezaji ili kurahisisha shughuli za uwekezaji[7]. Moja ya majukumu ya Kituo ni kubainisha fursa zilizopo katika sekta ya Kilimo[8].

Aidha, Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya mwaka 1999 inazuia wawekezaji wasio wazawa kujipatia ardhi kwa shughuli ambazo si za uwekezaji[9] na kuweka utaratibu maalumu wa kupata ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuwekezaji[10]. Katika uchunguzi wake Kamati imebaini kuwepo kwa dosari za kiutekelezaji katika suala la uwekezaji kama ifuatavyo:-

i) Umilikishaji ardhi kwa wawekezaji wageni usiofuata taratibu za kisheria;

ii) Serikali za vijiji kugawa kwa wawekezaji maeneo makubwa kinyume cha sheria; na

iii) Wawekezaji kutumia mashamba bila kuwa na hatimiliki.

[7] Kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwekezaji, Sura 38
[8] Kifungu cha 6 (c ) cha Sheria ya Uwekezaji.
[9] Kifungu cha 20 (1)cha Sheria ya Ardhi
[10] Kifungu cha 20 (2) Sheria y a Ardhi

## 3.2 Maelezo ya jumla kuhusu matokeo ya uchambuzi wa sera, mikakati na sheria

**Mheshimiwa Spika,**
Uchambuzi wa sera umeainisha kasoro mbalimbali za kiutekelezaji. Mbali na kasoro hizo, Kamati ilibaini mambo ya jumla yanayohusu sera zinazozungumzia matumizi ya ardhi.

Mambo hayo ni:-

i) Kutegemeana kwa sera, mikakati na sheria ziliyopitiwa ni suala la msingi katika kuongoza udhibiti na uzuiaji wa migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Maudhui ya sera, mikakati na sheria hizo yanadhihirisha uwepo wa kutegemeana katika usimamizi wa shughuli za sekta za ardhi, kilimo, mifugo, uwekezaji, mazingira na maji.

ii) Sera, mikakati na sheria za ardhi zinasimamia matumizi ya ardhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji, uwekezaji, miundombinu ya maji na nyinginezo zinazoendeshwa na watumiaji mbalimbali wa ardhi. Kimsingi, sera kuu inayosimamia matumizi ya ardhi kwa shughuli zote hizo chini ya sekta mbalimbali ni Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997 iliyowekewa mikakati na kutungiwa sheria za ardhi.

iii) Kutofautiana kwa msisitizo miongoni mwa Sera
Sera ni mwongozo wa msingi katika usimamizi wa shughuli za kiuchumi, kijamii na uendelezaji wa sekta mbalimbali. Msisitizo wa sera za taifa kwa kawaida haupaswi kutofautiana katika jambo moja.

Uchambuzi wa sera umeonesha kuwa kuna kutofautiana baina ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 katika suala la ufugaji wa

kuhamahama. Wakati sera ya ardhi 1997 inashawishi msisitizo katika kuzuia ufugaji wa kuhamahama, Sera ya mifugo ya 2006 inahimiza ufugaji wa kuhamahama.

Aidha, kutoendana (*not aligned*) kwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 ni jambo lililojitokeza.

Mtafiti Lugoe (2011) alipata kueleza:

> **NUKUU:** *The Livestock Policies are not aligned to the Land Policy on the land resource available for distribution among major users. Whereas, land policy advances the notion that the bulk of land is "difficult to manage" for various reasons as also acknowledged elsewhere, the livestock policies call such lands as "a large untapped resource base***".**

Kwa maelezo hayo, Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006 na Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997, haziendani (*Not aligned*) katika suala la ardhi iliyopo nchini ambayo kwa sasa haitumiki. Sera hizo hazina upatanifu wa mwongozo katika suala la ardhi isiyotumika kwa sasa.

Kwa hali hiyo, haikuwa vigumu kwa sekta ya ardhi na sekta ya mifugo kutofautiana katika kuweka msisitizo juu ya suala la ardhi kubwa isiyotumika kwa sasa (*a large untapped resource base)* jambo ambalo si la kawaida katika utekelezaji bora wa sera za taifa.

iv) Wizara zinazohusika na usimamizi wa sera, mikakati na sheria Wizara zinazohusika na usimamizi wa sera, mikakati na sheria zilizochambuliwa ni zifuatazo:-

**Jedwali: Wizara zinazosimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na sheria zilizochambuliwa.**

| NA | SERA, MIKAKATI NA SHERIA | WIZARA INAYOHUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997, Mikakati ya utekelezaji na sheria zake | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi |
| 2. | Sera ya Taifa ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1995, Sera ya Kilimo ya mwaka 2013 Mikakati ya utekelezaji na sheria zake | Wizara ya Kilimo, Chakula na ushirika |
| 3. | Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, Mikakati ya Utekelezaji na sheria zake | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi |
| 4. | Sera ya Taifa ya Uhamasishaji Uwekezaji ya mwaka 1995, Mikakati ya utekelezaji na sheria zake | Ofisi ya Waziri Mkuu-Uwezeshaji |
| 5. | Sera ya Taifa ya Mazingira, Mikakati ya Utekelezaji | Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira |
| 6. | Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2006, Mikakati ya Utekelezaji na sheria zake | Wizara ya Maji |
| 7. | Uratibu wa shughuli za Serikali | Ofisi ya Waziri Mkuu: Sera, Uratibu na Bunge |

**Chanzo:** ***Tangazo la Serikali, Na. 494 lililochapishwa tarehe 17 Desemba, 2010, (ISSN. 0856 – 034X)***

Kwa muundo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu inahusika na uratibu *(coordination*) wa shughuli za Serikali katika utekelezaji wa sera, mikakati na sheria. Dhana ya uratibu katika lugha ya kiingereza inaweza kufafanuliwa kama ilivyoelezwa na mwandishi Newman[11] (1953:uk.403) aliyenukuliwa na Bhagwan[12] na Bhushan (2010:uk.225) akisema:

> **Nukuu:** *Coordination is "the orderly synchronization of efforts to provide the proper amount, timing and directing of execution resulting in harmornious and unified actions to a stated objective***".**

Kwa tafsiri isiyo rasmi yaweza kusemwa kuwa "uratibu" ni utaratibu mzuri wa kuchakata na kuwianisha juhudi katika

[11] Newman, W.H.(1953) **Administrative Action**: The techniques of Organization & Management, Englewood Cliffs, NJ:Prentice – Hall,,

[12] Bhagwan and Bhushan (2010) **Public Administration**, S. CHAND &COMPANY LTD, New Delhi [ISBN- 81-219-0340-8]

utekelezaji kwa namna inayoweza kutoa kiasi sahihi cha matokeo ya utekelezaji unaounganisha na kuoanisha hatua mbalimbali za kufikia lengo lililobainishwa.

Tukizingatia maelezo hayo pamoja na Tangazo la Serikali, Na. 494 lililochapishwa tarehe 17 Disemba, 2010, Ofisi ya Waziri Mkuu inahusika na kuwianisha, kuoanisha na kupatanisha juhudi za Wizara hizo zinazohusika na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria kuhusiana na matumizi ya ardhi ili malengo mazuri ya sera yaweze kufikiwa.

Aidha, halmashauri nchini chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zinahusika na usimamizi wa rasilimali zinazotumika katika utekelezaji wa sera mbalimbali kwenye maeneo yao.

### 3.3 Hadidu ya Rejea ya Pili: Mapitio ya Taarifa za Kamati au Tume zilizowahi kuundwa

Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Tume ya Rais ya kuchunguza masuala ya ardhi *(The Presidential Commission of Inquiry into Land Matters)* iliyoundwa tarehe 03, Januari, 1991 chini ya Mwenyekiti Profesa Issa Shivji kutoka Kitivo cha Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akisaidiana na Makamishna Kumi na Mmoja.

Tume ilikabidhi Taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais mnamo Tarehe 11, Novemba, 1992. Taarifa ya Tume ina sura 25 zinazoelezea matokeo ya uchunguzi. Kamati hii imepitia sura za Juzuu ya Kwanza ya taarifa hiyo kwa kuzingatia matokeo yanayohusiana na migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Katika Taarifa hiyo, Tume iliripoti kuwa ilipokea malalamiko zaidi ya elfu moja (1000) yanayohusiana na migogoro ya ardhi[13]. Migogoro hiyo, kwa kiasi kikubwa imeleta hali ya sintofahamu *(uncertainty)* kwa wananchi ikizingatiwa kuwa ardhi ndiyo nguzo kuu ya uzalishaji mali *(major means of*

[13] The Presidential Commission of Inquiry into Land Matters page 101

*production)* katika nchi yetu. Ufafanuzi zaidi wa maudhui ya taarifa hiyo umewekwa katika Juzuu ya Pili ya maelezo ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Ili kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa kuhusiana na namna ya kuepusha migogoro ya ardhi, Kamati ilipitia maoni ya Tume ambayo ni pamoja na yafuatayo:-

i) Kuna ugumu wa kupata huduma za vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi (mabaraza ya ardhi na mahakama),
ii) Kumekuwepo na ucheleweshaji katika utoaji wa maamuzi ya migogoro ya ardhi,
iii) Kutokuwa na hakika *(uncertainty)* na pia kutokamilika *(lack of finality)* kwa maamuzi ya migogoro ya ardhi,
iv) Kumekuwepo na msigano na muingiliano wa kimamlaka katika utekelezaji wa majukumu ya vyombo mbalimbali, hali inayosababisha kutolewa kwa maamuzi yanayokinzana au ucheleweshaji wa maamuzi,
v) Mfumo wa kimahakama uliopo na namna uongozi wa Serikali unavyoshughulikia masuala ya ardhi, vinaashiria kupoteza uhalali *(legitimacy)* machoni pa wananchi. Wengi wao hawana imani na jinsi mamlaka husika zinavyoshughulikia migogoro ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**
Kwa maoni hayo, Tume ya Rais (Tume ya Shivji) ilitoa mapendekezo yafuatayo:-

i) Kiundwe chombo huru chenye kuaminika kwa Wananchi *(Independent and impartial)* ambacho kitakuwa na jukumu la kutatua migogoro ya ardhi,
ii) Wajumbe wa chombo cha kutatua migogoro ya ardhi wasitokane na viongozi wa vijiji, wilaya au Mkoa, bali wachaguliwe kutoka miongoni mwa wananchi na wawe ni watu wenye maadili na weledi,
iii) Viongozi wa kijadi na kimila watumiwe katika kutatua migogoro ya ardhi;
iv) Hati miliki za ardhi kwa matumizi mbalimbali zitolewe,
v) Upimaji na ramani za vijiji upewe kipaumbele,

vi) Upangaji wa miji uzingatiwe,
vii) Pawepo na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika ngazi za vijiji, kata,wilaya na Taifa,
viii) Kuimarisha hatua za uwajibikaji kwa watumishi wa umma katika idara ya ardhi wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na wasiokuwa na maadili katika kutekeleza majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na Taarifa ya Tume ya Rais ya kuchunguza masuala ya ardhi, Kamati inabainisha mambo sita (6) ya kuzingatiwa kuhusiana na hali ya migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi kama ifuatavyo:-

i) Sababu za migogoro ya ardhi zilizobainishwa na Tume ya Profesa Shivji zinashabihiana kwa kiasi kikubwa na sababu za migogoro ya ardhi zilizobainishwa na Kamati hii,

ii) Kwa kiasi kikubwa sababu za kihistoria za migogoro zinaweza kutokana na sera ya vijiji ya mwaka 1974 ambapo vijiji vingi vilipata ardhi bila kuzingatia sheria.

iii) Vyombo vya utatuzi wa migogoro vimeundwa kwa baadhi ya sehemu lakini haviko huru na havina rasilimali za kutosha kutimiza majukumu yake, kama ulivyobainika katika uchunguzi wa Kamati hii,

iv) Mabaraza ya ardhi kwa baadhi ya maeneo hayaaminiki kutokana na tuhuma za rushwa na kukosa wataalamu wa kutosha,

v) Mashauri ya ardhi yanachukua muda mrefu kama inavyothibitishwa na kesi ya kijiji cha Kambala inayoendelea kusikilizwa kwenye Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya mkoani Morogoro tangu mwaka 2009, na

vi) Kutoheshimiwa kwa maamuzi ya vyombo vya kutoa haki kumeendelea kuonekana hadi sasa. Mfano ni baadhi ya

viongozi wa Serikali na raia kutoheshimu maamuzi ya mahakama kuhusu ardhi. Jambo hilo limedhihirika katika kijiji cha Mabwegere wilaya ya Kilosa, Mkoani Morogoro na pia katika eneo la Emboley Murtangos, wilayani Kiteto, Mkoa wa Manyara.

**3.4 Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Tathmini ya Matatizo yaliyotokana na Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza**

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilipitia Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira iliyohusu Tathmini ya Matatizo Yaliyotokana na Utekelezaji wa Operesheni Tokomeza.

Taarifa hiyo ilitokana na kazi iliyofanywa na Kamati Ndogo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira iliyopewa Hadidu za Rejea Nne. Miongoni mwa Hadidu za Rejea, Hadidu Namba Nne iliitaka Kamati hiyo kuchunguza migogoro ya ardhi inayohusu wakulima, wafugaji na wawekezaji kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilikamilisha jukumu ililopewa na Bunge lako. Mnamo tarehe 18 Desemba, 2013 iliwasilisha Bungeni Taarifa iliyoeleza matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa Operesheni Tokomeza. Taarifa hiyo ilifafanua mambo mbalimbali ikiwemo tathmini ya migogoro ya ardhi kati ya wananchi na mamlaka au wasimamizi wa maeneo ya hifadhi.

Migogoro hii inatokana na kupanuliwa kwa maeneo ya mapori ya akiba na ya hifadhi bila kuwashirikisha wananchi wanaoishi au kufanya shughuli zao kwenye maeneo hayo.

Mifano iliyotolewa na Kamati ni pamoja na migogoro ya ardhi katika maeneo ya:
i) Wilaya ya Bunda katika Pori la Akiba la Gurumeti;
ii) Kata ya Iputi na Lupiro dhidi ya Hifadhi ya Taifa ya Selous wilayani Ulanga; na

iii) Vijiji Kegonga na Masanga katika kata ya Nyanungu, wilaya ya Tarime wakigombea bonde lililopo kwenye eneo la Bonde la Hifadhi iliyoongezwa na TANAPA

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na tathmini iliyofanywa na Kamati hiyo kuhusiana na migogoro inayowahusisha wakulima, wafugaji, wawekezaji dhidi ya mamlaka na wasimamizi wa Mapori ya akiba na maeneo ya hifadhi ilitoa mapendekezo.

Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa ni kama yafuatayo:-

i) Kamati hiyo ilibaini kwamba, katika baadhi ya maeneo yaliyoko mipakani mfano; Karagwe, Idara ya Uhamiaji hutoa vibali kwa raia wa nchi jirani vya kuishi, kufuga na kulima hapa nchini, vibali ambavyo havina udhibiti wala tija kwa nchi, na kusababisha migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji lakini pia uharibifu wa mazingira kwa kuingiza mifugo hifadhini, Kamati ilipendekeza Bunge liazimie kwamba;

· Serikali isitishe mara moja zoezi la kutoa vibali hivyo, na kufuta vilivyopo na kuwataka raia hao wa kigeni wenye vibali kuondoka nchini mara moja[14].

ii) Kamati ilibaini kwamba, zaidi ya asilimia 25 ya eneo la Nchi ni hifadhi, na mipaka ya maeneo mengi yaliyohifadhiwa haikuainishwa, na kwa kuwa Serikali haina uwezo wa (rasilimali watu na fedha) wa kusimamia na kulinda mipaka ya maeneo haya kikamilifu, Kwa hiyo basi, Kamati ililiomba Bunge liazimie kuitaka; Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

· Kuridhia Idara ya Wanyamapori na Wakala wa Huduma ya Misitu kuajiri idadi ya watumishi wanaotakiwa kama Serikali bado inaendelea kuyahifadhi maeno hayo;

· Kuainisha mipaka ya mapori yote ya akiba, hifadhi za taifa na Misitu ya Serikali kwa alama maalumu na za kudumu ili kuepusha Wananchi kuingia katika maeneo hayo kwa kutojua mipaka; na

[4] Pendekezo Namba x la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira

· Kuyaachia mapori ya Serikali ambayo yamekosa sifa, ili yatumike kwa kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi[15].

iii) Kamati ilibaini uwepo wa maeneo ya mapori na Hifadhi ambayo yana migogoro ya muda mrefu, ambapo wananchi wameishi katika maeneo hayo kwa muda mrefu. Kamati ililiomba Bunge liazimie kwamba;

· Serikali irekebishe mipaka husika au iwahamishie Wananchi hao kwenda kwenye maeneo mengine yenye miundombinu; na

· Serikali iwaagize Mawaziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maliasili na Utalii na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutembelea maeneo yote yenye migogoro nchini na kuitafutia ufumbuzi ili wananchi waweze kuelewa hatma yao katika maeneo hayo kwani wamekuwa katika hali ya sintofahamu kwa muda mrefu[16].

iv) Kamati ilibaini kwamba, migogoro wanayokumbana nayo wafugaji kutokana na kuingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi pamoja na kero nyingine inatokana na kukosekana kwa miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo, na kwa kuwa, Mheshimiwa Rais aliunda Wizara mahususi kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini akitambua umuhimu wa Sekta hiyo kwa uchumi wa Taifa.
Aidha, Taarifa ya Kamati ilibainisha kuwa, Tanzania ni ya Pili (2) kwa wingi wa mifugo Barani Afrika, hivyo ni wazi kwamba adha wanazokumbana nazo wafugaji ni matokeo ya kutokuwepo kwa sera na mipango madhubuti ya muda mfupi na muda mrefu[17].

Kamati hii Teule inaendelea kusisitiza kuwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo ya Bunge yakitekelezwa kikamilifu yanaweza kuwa suluhisho kwa migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi iliyokithiri hapa nchini. Kamati Kudumu ya

[15] Pendekezo Namba xi khj
[16] Pendekezo Namba xii khj
[17] Pendekezo Namba xv la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira

Bunge ya Ardhi, Maliasli na Mazingira ilipendekeza Bunge liitake serikali:

i) Kusitisha mara moja utoaji wa vibali kwa raia wa nchi jirani wanaoingia nchini na mifugo, hali inayosababisha migogoro baina ya wakulima na wafugaji kutokana na uhaba wa ardhi na uharibifu wa mazingira;

ii) Kuainisha mipaka ya mapori ya akiba na maeneo ya hifadhi za Taifa na misitu ya serikali ili kuepusha mamlaka na wasimamizi wa mapori ya akiba na maeneo ya hifadhi kuingia kwenye migogoro na wakulima na wafugaji kutokana na mipaka kutotambulika;

iii) Kuyaachia mapori yasiyo na sifa ili yatumike kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa nia ya kuepusha migogoro ya ardhi;

iv) Kuweka utaratibu utakaowezesha viongozi wa serikali kutembelea maeneo yenye migogoro ya mara kwa mara kuhusu matumizi ya ardhi na kuipatia ufumbuzi; na

v) Serikali iweke mkazo katika kusimamia sera na mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu ili kuimarisha sekta za mifugo na kilimo kwa kuweka miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo na mazao ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana mapitio ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Kamati hii Teule ina maoni kuwa migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi na hifadhi au mapori ya akiba inaweza kutatuliwa kwa hatua za muda mfupi, wa kati na mrefu kama inavyobainishwa katika Juzuu ya Pili.

**3.5 Tamko la Mtowisa la tarehe 17 Septemba, 1998**

**Mheshimiwa Spika**

Tamko hilo liliitwa "*Tamko la Mtowisa*" lilitolewa katika Mkutano uliofanyika kijiji cha Mtowisa, Tarafa ya Mtowisa, Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa.

Mkutano huo ulihudhuriwa na watu wapatao elfu mbili (2000) na ulijumuisha wafugaji, wakulima pamoja na viongozi wa serekali na vyama vya siasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Chimbuko la hali iliyosababisha tamko hilo limefafanuliwa katika Juzuu ya Pili ya Maelezo ya Kamati. Kubwa katika chimbuko la tamko hilo ni kukithiri kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji mkoani Rukwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Mkutano wa Mtowisa uliotoa Tamko hilo, ulihitimishwa kwa kuweka maazimio 15 kama ifuatavyo:-

i) Kila Mamlaka ya Halmashauri za Mkoa zianzishe na kusimamia kuwepo kwa rejista za wafugaji katika kila kijiji. Regista hizo zionyeshe jina la mfugaji na idadi ya mifugo aliyonayo kila mwaka,

ii) Kila mwaka kijiji kiendeshe sensa ya mifugo na kuingiza kwenye rejista. Hii ni kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka za Halmashauri kwenye bajeti na pia kwa ajili ya kumbukumbu za kijiji kwa matumizi yao ya baadaye,

iii) Vijiji viunde Kamati za kusimamia, kupanga na kuratibu matumizi bora ya ardhi, kutoa maamuzi ya ruhusa ya kupokea mifugo kutoka nje ya wilaya/mikoa na taratibu zingine,

iv) Mamlaka za Halmashauri, Serikali za Vijiji na vyombo vya dola wasimamie kikamilifu utekelezaji wa sheria zilizopo (sheria mama na sheria ndogo) zinazodhibiti usafirishaji wa mifugo, matumizi bora ya ardhi, hifadhi ya mazingira n.k,

v) Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, (Halmashauri za Wilaya) zipitie na kufanya marekebisho baadhi ya sehemu au vipengele vya sheria zake ambavyo vinaonekana kupitwa na wakati. Kwa mfano *"Cattle Grazing Act,* Cap 155" juu ya uendelezaji wa Nyanda za Malisho na "*Animal Diseases Ordinance,* Cap 156" juu ya udhibiti wa magojwa ya mifugo,

vi) Mamlaka za Halmashauri zikishirikiana na Serikali ziweke utaratibu mzuri wa kukusanya kodi au ushuru wa mifugo ikiwa ni pamoja na kushirikisha Serikali za vijiji kama wakala,

vii) Kila Mamlaka za Halmashauri zianzishe mifuko ya kuendeleza mazao ya kilimo na mifugo *Crops and Livestock Development Funds (CDLF)*. Fedha itokane na makato ya 10% - 2% ya kodi/ushuru kutoka vyanzo vilivyo chini ya sekta hizo,

viii) Mamlaka za Halmashauri zitoe elimu kwa wafugaji juu ya kuvuna baadhi ya mifugo yao ili kuwawezesha kufanya shughuli zingine za kiuchumi au kimaendeleo licha ya shughuli za ufugaji. Mfano kubuni mfumo wa kodi ya mifugo kulingana na ongezeko la mifugo, kuongeza kujenga minada, upatikanaji wa vifaa vya ujenzi n.k,

ix) Halmashauri za Wilaya/Mji ziainishe maeneo yaliyoathirika zaidi na uharibifu wa mazingira ili kuangalia uwezekano wa kuwataka wafugaji kuhamisha mifugo yao kutoka maeneo hayo. Sambamba na zoezi hilo, Halmashauri ziandae maeneo watakayohamia wafugaji hao,

x) Serikali kuu inaombwa kutoa taratibu za kisheria zitakazotoa muafaka wa mawasiliano ya awali kati ya Mikoa inayopokea na Mikoa inayotarajia kuingiza mifugo ili kuafikiana idadi ya mifugo inayoweza kuhamishwa,

xi) Wananchi wote wakulima na wafugaji waliojenga na kuishi maeneo ya vyanzo vya maji wahamishwe/wahame maeneo hayo mara moja. Maeneo hayo yaendelee kutunzwa kwa njia zozote zile mfano kupanda miti na kuweka wigo,

xii) Serikali Kuu na Halmashauri ziendelee kukamilisha zoezi la kupima maeneo ya vijiji na kusimamia upatikanaji wa hati miliki za maeneo yao,

xiii) Halmashauri zibainishe njia za mifugo zilizopo au zitengenezwe nyingine *(stock routes),*

xiv) Wakulima na wafugaji kuheshimiana na kuheshimu mali za kila upande, na

xv) Wakulima na wafugaji kuendelea kuishi kwa amani na utulivu na udugu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na uchambuzi wa Tamko la Mtowisa Kamati imebaini kwamba sababu za kuwepo kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji zinafahamika Serikalini kwa muda mrefu. Pamoja na sababu mbalimbali, kukosekana kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji, ni kichocheo kikubwa cha mwingiliano wa shughuli za kilimo na ufugaji.

Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba maazimio yaliyoafikiwa katika Mkutano wa Mtowisa yalilenga kutatua migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Licha ya kuwekwa kwa utaratibu mzuri wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa maazimio hayo, mambo yafuatayo yameendelea kuwa changamoto:-

i) Kutokukamilishwa kwa zoezi la upimaji wa ardhi na utengaji wa maeneo ya kilimo na ufugaji kwa baadhi ya vijiji nchini;

ii) Kutokufanyika kwa sensa ya taifa ya mifugo na kutokuwepo kwa Daftari la Kumbukumbu za Mifugo;

iii) Kutokuwepo kwa utaratibu madhubuti wa ukusanyaji wa kodi au ushuru wa mifugo;

iv) Kutokutolewa ipasavyo kwa elimu ya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara kwa wafugaji;

v) Usimamizi hafifu wa sheria mama na sheria ndogo; na

vi) Kutotatuliwa kikamilifu kwa migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

### 3.6 Hadidu ya Rejea ya Tatu: Uchambuzi wa Mikakati ya Kusuluhisha migogoro

**Mheshimiwa Spika,**
Uchambuzi wa mikakati ya Serikali ya kusuluhisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji nchini ulilenga kutathmini maudhui yake pamoja na utekelezaji. Uchambuzi huo ulikusudia pia kubaini namna mikakati hiyo inavyoweza kusaidia kuondoa na kuzuia migogoro miongoni mwa wakulima na wafugaji.

Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha mambo makuu mawili kama ifuatavyo:-

#### 3.6.1 Kukosekana kwa mkakati mahususi wa serikali

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilibaini kuwa, Serikali haina Mkakati mahsusi uliotayarishwa, uliosambazwa au unaotumika kitaifa kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, Kamati ilibaini kuwepo kwa Rasimu ya Mkakati wa kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji nchini ya mwaka 2009. Rasimu hiyo inaoyopendekeza njia mbalimbali za utatuzi wa migogoro haijaanza kutumika.

Ushahidi uliowasilishwa mbele ya Kamati umebainisha kuwa migogoro inayoendelea baina ya wakulima na wafugaji inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutokuwepo kwa mkakati mahsusi wa serikali wa kuzuia na kuondoa migogoro hiyo.

Kutokuwepo kwa mkakati wa serikali wa kuondoa migogoro na kutofahamika kwa Rasimu ya Mkakati huo kunathibitishwa na ushahidi wa baadhi ya Mashahidi

walioitwa mbele ya Kamati. Kwa mfano, baadhi ya mashahidi wenye nyadhifa katika Wizara walieleza kwamba hawajawahi kuiona wala kufanyia kazi Rasimu ya Mkakati wa Serikali wa mwaka 2009 unaolenga kumaliza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

### 3.6.2 Njia za utatuzi wa migogoro hazitoi suluhisho la kudumu

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na kukosekana kwa mkakati mahsusi kwa ajili ya kutatua migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi, Serikali hutumia njia mbalimbali za kuitatua migogoro hiyo. Mara nyingi njia hizo hazitoi suluhisho la kudumu na hivyo migogoro hiyo inaendelea kuwepo. Mfano, kuna nyakati Jeshi la Polisi hutumika kutuliza ghasia zinazotokana na migogoro hiyo huku chanzo cha migogoro hiyo kikiendelea kuwepo.

Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba migogoro inayoibuka mara kwa mara katika wilaya za Mvomero na Kiteto haijapatiwa suluhisho la kudumu na badala yake Serikali imekuwa ikitumia Jeshi la Polisi kutuliza ghasia wakati wa migogoro hiyo.

### 3.7 Hadidu ya Rejea ya Nne: Uchambuzi wa Mikakati ya kulinda vyanzo vya maji

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilichambua mikakati iliyolenga kuhifadhi vyanzo vya maji na kuzuia uharibifu wa Mazingira. Mikakati iliyochambuliwa ni:

i) Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa Mwaka 2006,

ii) Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Maji wa Mwaka 2006

**Mheshimiwa Spika,**
Katika uchambuzi wa mikakati hiyo miwili, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

i) Mkakati wa kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji uliandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau na Sekta nyingine.

Lengo la Mkakati huo ni kuzuia uharibifu wa mazingira ambao ni kiini cha kuenea kwa hali ya jangwa na ukame pamoja na kukauka kwa vyanzo vya maji nchini.

Ushahidi wa kukauka kwa vyanzo vya maji unathibitishwa na takwimu za vyanzo vya maji hususan bwawa la Mtera. Takwimu hizo zinaonesha kuwa kina cha juu cha maji cha Bwawa la Mtera, kimekuwa kikishuka kutoka mita 695.8 mwaka 2003, mita 690.5 mwaka 2004 hadi mita 689 mwaka 2005.

**Mheshimiwa Spika,**
Uharibifu wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kwa kiasi kikubwa husababishwa na mambo yafuatayo:-

i) Shughuli za kilimo kisicho endelevu zinazofanywa katika maeneo ya vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kwenye vilele na miteremko ya safu za milima. Shughuli hizo ni kama vile ukataji miti hovyo, uchomaji moto misitu, umwagiliaji usio endelevu katika shughuli za kilimo n.k., na

ii) Uhamaji wa makundi makubwa ya mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine kwa nia ya kutafuta malisho, maji pamoja na dhana ya kuepuka magonjwa ya mifugo. Hali hii huchangia uharibifu mkubwa wa mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji na hivyo kusababisha kuongezeka kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa rasilimali ardhi na maji.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilichambua mikakati ya Serikali katika kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu. Baadhi ya mikakati hiyo

ni kuainisha maeneo ya vyanzo vya maji nchini, kubainisha maeneo yaliyovamiwa na wafugaji ifikapo Juni, 2006 na kubainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji ifikapo Juni, 2006.

Mikakati mingine iliyochambuliwa ililenga kutoa taarifa sahihi kuhusu uwezo wa malisho, aina na idadi ya mifugo ifikapo Juni, 2006; kuandaa na kutekeleza utaratibu wa kuwaondoa wafugaji na mifugo kwenye maeneo waliyovamia kwenda kwenye maeneo yanayofaa ifikapo Juni, 2006; na Kuendeleza njia za asili za hifadhi ya malisho.

**Mheshimiwa Spika,**
Pamoja na hayo, mikakati ililenga kusimamia utekelezaji wa programu za hifadhi ya mazingira na mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ifikapo Julai 2007, kuhakikisha mipaka ya vijiji 6,000 inapimwa na vyeti vya ardhi ya kijiji vinatolewa, kuandaa na kutekeleza Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi na kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati imebaini kuwepo kwa dosari mbalimbali ambazo zimeelezwa katika Juzuu ya Pili. Dosari hizo ni:-

i) Kutobainishwa kwa maeneo ya ufugaji,

ii) Kukosekana kwa taarifa sahihi kuhusu uwezo wa malisho (*carrying capacity*) aina na idadi ya mifugo,

iii) Kuendelea kuwepo kwa uvamizi wa shughuli za kilimo kwenye vyanzo vya maji,

iv) Utaratibu usiofaa wa kuwaondoa wakulima na wafugaji katika maeneo waliyoyavamia,

v) Kutojengwa kwa malambo, visima na mabwawa,

vi) Kutotekelezwa kwa Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi,

vii) Athari zilizotokana na kuyafanya baadhi ya maeneo kuwa hifadhi za taifa.

**3.8 Hadidu ya Rejea ya Tano: Mapendekezo ya kuondoa migogoro iliyopo na kudumisha uhusiano mzuri kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi**

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya uchambuzi wa kina na kwa kuzingatia hadidu za rejea, Kamati inatoa mapendekezo katika makundi makuu matatu kwa kigezo cha muda wa utekelezaji.

Makundi hayo ni kundi la mapendekezo ya muda mfupi (miaka 0-2), kundi la muda wa kati (miaka 2-5) na kundi la muda mrefu (miaka 5-15).

Vile vile, Kamati imeainisha viwango vya athari za kutotekelezwa kwa mapendekezo yaliyotolewa (*Risk*) katika aina kuu mbili ambazo ni:-

Athari ya juu (*High Risk*) na athari ya kati (*Average Risk*).

Madhumuni ya kuainisha mapendekezo katika makundi na kueleza viwango vya athari ya utekelezaji ni kubainisha umuhimu wa mapendekezo hayo kufanyiwa kazi pamoja na kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wake.

### 3.8.1 MAPENDEKEZO YA MUDA MFUPI

**Mheshimiwa Spika,**
Mapendekezo haya yanalenga kutafuta ufumbuzi wa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini. Katika mapendekezo haya yapo yanayotakiwa kufanyiwa kazi haraka ambayo ni:

**1. Usuluhishi wa migogoro ya ardhi katika wilaya ya Kiteto;**

**KWA KUWA,** Mgogoro wa ardhi katika wilaya ya Kiteto unazidi kuendelea na kusababisha mauaji ya watu ndani ya wilaya hiyo na migongano kati ya Uongozi wa wilaya ya Kiteto na wilaya za jirani, mathalan, Kongwa na Chemba,

**NA KWA KUWA,** Migogoro hiyo ni hatari kwa mustakbali wa amani, usalama, umoja na utangamano wa Taifa na kwamba kuna hukumu iliyotolewa na Mahakama kuwa eneo hilo lisitumike kwa shughuli za kilimo wala ufugaji.

**HIVYO BASI**, Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali:

*Athari ya Juu (High Risk)*

a) Kuharakisha usuluhishi wa mgogoro baina ya wakulima na wafugaji wanaogombea maeneo ya ardhi wilayani Kiteto ili kuzuia mauaji ya wenyewe kwa wenyewe yanayoendelea kutokea.

b) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa hukumu ya Mahakama iliyoamua kuhusu matumizi ya eneo linalogombewa (*Emboley Murtangos*).

**2. Kudhibiti uswagaji wa mifugo**

**KWA KUWA,** Mheshimiwa Rais alitoa agizo kupitia waraka Namba 01 wa mwaka 2002, lililokataza kuswaga mifugo kutoka eneo moja la nchi kwenda lingine bila kufuata utaratibu unaopaswa kuzingatiwa,

**NA KWA KUWA**, kuendelea kuswaga mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine ni ishara ya kutozingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, na hivyo uswagaji huo wa mifugo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro na uharibifu wa mazingira,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kwamba, Bunge liitake Serikali kusimamia kikamilifu:-

*Athari ya wastani (Average Risk)*

a) Utekelezaji wa haraka wa maelekezo ya Waraka wa Mheshimiwa Rais unaoelekeza uhamishaji wa mifugo ufanyike kwa kutumia magari au reli (kwa ng'ombe wanaohamishwa kutoka wilaya moja kwenda wilaya nyingine) badala ya kuswaga;

b) Kusimamia kikamilifu sheria zinazoweka masharti ya kuwa na vibali wakati wa kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine; na

c) Kila halmashauri ya wilaya inatakiwa kutenga njia maalum za kupitisha mifugo *(stock route)* na kuweka utaratibu utakaowezesha mifugo kupitishwa kwenda kwenye malisho, majosho au minadani.

**3. Kutenga njia za kupitisha mifugo**

**KWA KUWA,** kuwekwa kwa njia za kupitisha mifugo kwenda kutafuta maji, malisho majosho au minada ni muhimu kwa ajili ya kuepusha mwingiliano wa shughuli za ufugaji, wakulima na shughuli nyingine za watumiaji wa ardhi,

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa njia mahsusi kwa ajili ya kupitisha mifugo, kunachangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kutokana na mifugo kuingia kwenye mashamba na kuharibu mazao,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kutenga njia za kupitisha mifugo kwa ajili ya kufuata malisho, majosho na maji kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (1) – (3) cha *Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula, Na. 12, ya mwaka 2010*.

**4. Hatua dhidi ya uvamizi wa wageni kutoka nchi jirani:**

**KWA KUWA,** Katika mikoa ya Rukwa, Kigoma na Kagera inayopakana na nchi jirani, kuna wimbi la wavamizi kutoka nchi jirani wanaoingia nchini wakiwa na idadi kubwa ya mifugo kwa ajili ya kutafuta malisho,

**NA KWA KUWA,** Kamati imebaini kwamba hali hii huongeza mahitaji ya ardhi na hivyo kusababisha uharibifu wa mazingira, kueneza magonjwa ya mifugo, wananchi kukosa ardhi ya kutosha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za kilimo na ufugaji pamoja na kuhatarisha hali ya utulivu, amani na usalama nchini,

*Athari ya Juu*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za haraka dhidi ya uvamizi huo.

**5. Kutenga maeneo ya Ardhi ya vijiji**

**KWA KUWA** kutojulikana kwa idadi ya mifugo yote iliyomo nchini, na ukubwa wa ardhi inayofaa kwa shughuli mbalimbali ni jambo muhimu katika kuainisha matumizi ya ardhi kwa lengo la kuondoa mwingiliano wa shughuli za sekta mbalimbali,

**NA KWA KUWA** kutojulikana kwa ukubwa wa ardhi inayofaa kwa kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za kiuzalishaji kumechangia ugumu wa kuainisha ardhi inayofaa kwa kilimo, ufugaji, hifadhi na shughuli nyingine hapa nchini, na hivyo kusababisha mwingiliano wa shughuli hizo na migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kupima na kuainisha ukubwa wa ardhi inayofaa na inayohitajika kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo, hifadhi na shughuli nyingine na na kumilikisha ardhi hiyo kwa kuzingatia mahitaji ya uzalishaji.

*Athari ya Juu (High Risk)*

**6. Kutotekelezwa kwa masharti ya uvunaji wa mifugo;**

**KWA KUWA,** Kifungu cha 20 cha *Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula*, Na. 13 ya mwaka 2010 kimeweka utaratibu kwamba ili yawepo malisho ya kutosha na idadi ya mifugo inayoendana na malisho, utaratibu wa kuvuna mifugo unapaswa kutekelezwa,

**NA KWA KUWA,** kuwepo kwa idadi kubwa ya mifugo isiyoendana na upatikanaji wa malisho ya mifugo katika eneo moja husababisha uwiano usiokuwa sawa wa idadi ya mifugo na malisho, hali inayolazimisha wafugaji na wakulima kuhamia maeneo yanayotumiwa kwa shughuli nyingine, hivyo kuchochea migogoro baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa, Bunge liitake Serikali kufanya sensa ya mifugo na kuainisha aina na idadi ya mifugo yote nchini.

*Athari ya wastani*

**7. Chombo cha kuratibu na kusimamia masuala ya ardhi;**

**KWA KUWA,** Matumizi ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji, uwekezaji na matumizi mengine, yanasimamiwa na kuratibiwa na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi pamoja na Wizara na Idara mbalimbali zinazohitaji uratibu na mawasiliano madhubuti na yenye tija baina yao zaidi ya ilivyo sasa,

**NA KWA KUWA,** Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa kuna udhaifu katika uratibu, usimamizi na mawasiliano miongoni mwa wizara, ofisi, idara mbalimbali zinzohusika, hali inayochochea kuibuka kukua na kuendelea kuwepo kwa migogoro ya ardhi inayoathiri maendeleo, amani na utulivu nchini,

*Athari ya Juu* **KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liafiki kuitaka Serikali;

a) Kuiimarisha Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa kuipatia vitendea kazi na watumishi wa kutosha wenye weredi katika tasnia ya ardhi;

b) Kufungua ofisi za Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi katika ngazi ya Mikoa kwa ajili ya kuwezesha, usimamizi na upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi katika wilaya za mikoa husika kwa karibu na kwa haraka zaidi.

**8. Upimaji wa Ardhi ya Mkoa wa Morogoro**

**KWA KUWA,** Mkoa wa Morogoro umebainika kukumbwa na migogoro mikubwa ya ardhi, ya mara kwa mara, inayosababishwa na mwingiliano wa shughuli za wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi,

**NA KWA KUWA,** Migogoro hiyo imesababisha madhara makubwa kama vile, kukwama kwa shughuli za uzalishaji mali katika maeneo yenye migogoro, vifo, uharibifu wa mali, uharibifu wa mazingira na kukosekana kwa amani na utulivu kwa wananchi wanaoishi ndani na nje ya mkoa huo,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa, Bunge liitake Serikali kupima ardhi ya vijiji vya mkoa wa Morogoro kwa utaratibu wa Mkakati wa Dharura ili kufanikisha dhana ya mipango ya matumizi bora ya ardhi na kupunguza mwingiliano wenye madhara kiuhusiano kati ya shughuli za kilimo na zile za ufugaji.

*Athari ya Juu (High Risk)*

**9. Migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Serikali**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa ipo baadhi ya migogoro inayowahusisha:

(a) Wananchi na baadhi ya watendaji wa Serikali kutokana na watendaji hao kuvamia maeneo ya ardhi ya vijiji na kuendesha shughuli zilizo kinyume na mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji hivyo. Kwa mfano; katika kijiji cha Itaswi wilayani Kondoa, Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Kondoa alibainika kuwa katika mgogoro na wananchi wa kijiji cha Itaswi kutokana na yeye kuendesha shughuli za kilimo katika eneo la ardhi ya kijiji lililotengwa kuwa ardhi ya akiba.

(b) Mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kata ya Bagara Ziwani dhidi ya Halmashauri ya Mji wa Babati kutokana na baadhi ya wananchi hao kutolipwa fidia stahiki; na

(c) Migogoro ya ardhi kati ya wananchi wa maeneo mbalimbali kwenye kambi za jeshi,

**NA KWA KUWA,** migogoro hiyo imekuwa ikiwaathiri wananchi hao kiuchumi na kuwafanya wakose imani na Serikali yao,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali:

*Athari ya Juu (High Risk)*

(a) Kufanya uchunguzi wa watendaji wa Serikali wanaohusika na kubadilisha matumizi ya ardhi kama yalivyopangwa katika Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi za vijiji na kuchukua hatua stahiki dhidi yao;

(b) Kutoa fidia stahiki na kwa wakati kwa wananchi ambao ardhi yao inakuwa imetwaliwa kwa ajili ya matumizi mengine; na

(c) Kupata suluhu ya kudumu ya migogoro ya mipaka kati ya wananchi na kambi mbalimbali za jeshi chini.

**10. Mashamba yaliyobinafsishwa na kutelekezwa**

**KWA KUWA,** imebainika kwamba mashamba mengi yaliyobinafsishwa kwa baadhi ya wawekezaji hayajaendelezwa na yameachwa katika hali ya kutelekezwa kabisa, na mengine yamebadilishwa matumizi yaliyokusudiwa,

**NA KWA KUWA,** mashamba hayo yanawavutia wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi kuyatumia kuendesha shughuli zao, jambo linalosababisha kuibuka kwa migogoro miongoni mwao,

*Athari ya Juu*

**KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza kuwa, Bunge liishauri Serikali:

a) Kufuta hati za umiliki wa mashamba yaliyobinafsishwa kwa wawekezaji ambayo yametelekezwa au kubadilishwa matumizi yaliyokusudiwa na kugawa kwa wananchi; na

b) Kupima upya mashamba yote yanayohodhiwa bila kuendelezwa (*mashamba pori*) ambayo hati za umiliki zimefutwa ili kuyagawa kwa wananchi wenye uhitaji.

**11. Tanzania kuwemo kwenye hatari ya kufungiwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE);**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa Tanzania iko hatarini kufungiwa kusafirisha nje ya nchi mazao ya mifugo kama vile, nyama, maziwa, siagi, jibini na ngozi kutokana na kutozingatia ipasavyo miongozo ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani,

**NA KWA KUWA,** nchi yetu ikifungiwa na Shirika hilo, itasababisha sekta ya mifugo kuendelea kuwa duni na ufugaji kutokuwa wa kisasa, jambo litakaloendelea kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liazimie kwamba Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi iweke mipango mahsusi ya kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, ili sekta ya mifugo iwe ya uzalishaji wenye tija kwa taifa. Aidha, mipango hiyo iwasilishwe bungeni ili Bunge lijiridhishe na maudhui ya mipango hiyo. *Athari ya Juu*

**12. Kupima Upya maeneo ya vijiji vyenye migogoro ya mipaka**

**KWA KUWA,** imebainika kwamba zoezi la usajili wa baadhi ya vitongoji kuwa vijiji ama upimaji wa baadhi ya vijiji nchini lilifanyika bila ya kushirikisha kikamilifu kijiji mama au vijiji jirani.

**NA KWA KUWA,** kasoro hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi miongoni mwa vijiji hivyo,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa, Bunge liitake Serikali; *Athari ya Juu*

a) Kuyapima upya maeneo ya vijiji vyote vyenye migogoro ya mipaka inayoleta migongano kwa kushirikisha vijiji vyote vinavyohusika ili kuondoa kabisa migogoro hiyo;

b) Serikali itafute utaratibu wa kisheria wa utatuzi wa migogoro ya mipaka kwenye vijiji vyenye migogoro iliyokwisha amuliwa na Mahakama; na

c) Serikali ilete Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa mapendekezo hayo ndani ya kipindi cha miezi sita (6).

### 13. Viongozi wa vijiji kugawa maeneo yanayozidi Ekari 50 kwa wawekezaji

**KWA KUWA,** Kanuni ya 76(3) ya Kanuni za Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114, inaweka ukomo kwa Mamlaka za Vijiji kugawa ardhi kuwa isizidi eneo la ukubwa wa ekari 50, lakini imebainika kwamba kuna baadhi ya mamlaka hizo zinagawa maeneo zaidi ya ekari 50 kwa watu binafsi au wawekezaji kinyume cha sheria,

**NA KWA KUWA,** utaratibu wa kugawa maeneo ya ardhi ya kijiji kiholela umekuwa ni chanzo cha kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi,

*Athari ya wastani (**Average risk**)*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kwamba, Bunge liishauri Serikali kufanya uchunguzi kuhusu wawekezaji waliomilikishwa zaidi ya ekari 50 za ardhi na viongozi wa serikali za vijiji na ichukue hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kutwaa ardhi hiyo, na igawe maeneo hayo kwa wananchi waliokosa ardhi.

### 14. Upanuzi mkubwa wa ardhi kwa ajili ya Maeneo ya Hifadhi

**KWA KUWA,** hadi sasa asilimia 27 ya ardhi iliyopo nchi kavu ni maeneo yanayohifadhiwa (hifadhi za taifa, Maeneo tengefu, Mapori ya akiba na hifadhi za Misitu),

**NA KWA KUWA,** kumekuwa na jitihada za Serikali za kupanua mipaka ya maeneo ya hifadhi, hali inayochangia kupungua kwa ardhi inayotumika kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji, makazi na uchimbaji wa madini, hivyo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa watumiaji hao wa ardhi.

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa, Bunge liitake serikali;

d) Kufanya utafiti wa kina wa kuangalia ulazima, faida, athari na matokeo ya upanuzi wa mipaka ya maeneo ya hifadhi ili

kuepusha migogoro ya ardhi inayotokea mara kwa mara miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi.

e) Kuanisha maeneo yote yaliyokuwa ya hifadhi na ambayo kwa sasa yamepoteza hadhi hiyo kutokana na muingiliano wa matumizi mbalimbali (kilimo, ufugaji, makazi, uchimbaji madini n.k) na kuchukua hatua stahiki ili kuzuia migogoro ya ardhi iliyopo katika maeneo husika.

**15. Kuyafuta Maeneo ya Hifadhi yaliyopoteza sifa**

**KWA KUWA,** yapo maeneo ya hifadhi yanayotumiwa na wananchi kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji kwa zaidi ya miaka 50 (mfano wa maeneo hayo ni Kona Nne na Kangeme – Kaliua),

**NA KWAKUWA,** maeneo hayo hayana sifa za kuwa hifadhi, na wananchi wameyaendeleza kwa kuyapatia huduma muhimu za jamii kama vile hospitali, shule, nyumba za kuabudu na barabara; pia maeneo hayo yameonesha kuchangia kwa kiasi kikubwa mapato kwenye halmashauri husika,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kuridhia maeneo hayo yaendelee kutumika kama ardhi kwa ajili ya makazi ya watu na shughuli za kilimo na ufugaji kwa kuyafuta kutoka kwenye orodha ya maeneo yaliyotengwa kuwa hifadhi. *Athari ya juu*

**16. Dosari ya tafsiri ya neno *"Movement"* katika Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010**

**KWA KUWA,** Kifungu cha 3 cha *Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo*, Na. 12 ya mwaka 2010 kinatafsiri neno uhamishaji wa mifugo (*movement*) kuwa ni kuongezeka au kupungua kwa mifugo katika shamba la mifugo kunakohusisha kuzaliwa, kuchinjwa, vifo, kuhamisha kupotea kwa wanyama au mazao ya wanyama,

**NA KWA KUWA,** tafsiri hiyo haihusishi mifugo inayohamishwa kutoka eneo moja kwenda eneo lingine lililo nje ya shamba la mifugo ili kutafuta malisho, maji au kukimbia magonjwa ya mifugo, na hivyo tafsiri hiyo haisaidii kudhibiti ufugaji wa kuhamahama,

*Athari ya juu*

**KWA HIVYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liishauri serikali kuandaa Muswada wa sheria ili kuboresha *Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo*, Na. 12 ya mwaka 2010, kwa ajili ya kudhibiti ufugaji wa kuhamahama.

**17. Dosari katika Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo**

**KWA KUWA,** vifungu vya 14 – 18 vya *Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo*,Na. 12 ya mwaka 2010 vimeweka mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mazao ya mifugo na kuweka uwiano unaotakiwa wa malisho yaliyopo na idadi ya mifugo,

*Athari ya juu*

**NA KWA KUWA,** Kamati imebaini kwamba, ipo dosari katika usimamizi na utekelezaji wa *Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo*, Na. 12 ya mwaka 2010, jambo linalosababisha mazao ya mifugo kuwa duni na kuwepo kwa uhaba wa maeneo ya malisho,na hivyo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro kutokana na wafugaji kuingia kwenye ardhi inayotumiwa na watumiaji wengine,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali;

a) Isimamie ipasavyo Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, ili kuitambua, kuisajili na kutunza kumbukumbu za mifugo ili kuboresha upatikanaji wa mazao ya mifugo, upatikanaji wa malisho ya kutosha na kuepusha migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi; na

b) Kusimamia utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo kwa mujibu wa sheria,

**18.Ubinafsishaji usiozingatia mipaka ya vijiji**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini kwamba migogoro ya ardhi katika mashamba ya Kapunga Rice Farm lililopo Mbarali mkoani Mbeya, Efata lililopo mkoani Rukwa, Ranchi ya Misenyi iliyopo mkoani Kagera na Shamba la Gidagamond la mkoani Manyara, imesababishwa na watendaji wa Serikali waliobinafsisha mashamba hayo na Ranchi pasipo kuzingatia mipaka halisi ya maeneo hayo na vijiji vilivyo jirani,

**NA KWA KUWA,** kutozingatia mipaka ya vijiji vinavyozunguka mashamba na ranchi wakati wa zoezi la ubinafsishaji kumesababisha wananchi wa vijiji vilivyo jirani kukosa maeneo ya kufanyia shughuli zao, na hivyo kuvamia mashamba hayo na ranchi kwa ajili ya kuendesha shughuli zao, hali inayochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro baina ya wawekezaji na wananchi wa vijiji husika,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake serikali itwae maeneo yanayolalamikiwa na wananchi kwamba yamebinafsishwa bila ya kuzingatia mipaka halisi ya vijiji na kuirejesha ardhi hiyo kwa wananchi baada ya kulipa fidia kwa wawekezaji.

*Athari ya wastani*

**19. Dosari katika utaratibu wa kupima na kusajili vijiji**

**KWA KUWA,** vifungu Na. 22 – 28 vya *Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya)* Na. 7 ya mwaka 1982 vinampa mamlaka Msajili wa vijiji kusajili na kuvitangaza vijiji vilivyosajiliwa katika Gazeti la Serikali baada ya kuzingatia idadi ya kaya zinazotosha kuwa kijiji na eneo la ardhi linalotosha kwa ajili ya kuendesha shughuli za wanakijiji,

**NA KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwepo kwa dosari ya kisheria ambapo Msajili wa vijiji halazimiki kuzingatia mambo mengine muhimu katika usajili, kama vile; kujiridhisha na mipaka halisi kati ya kijiji kinachotakiwa kusajiliwa na vijiji jirani, uwepo wa ardhi ya kutosha katika kijiji tarajali, asili ya kijiji kinachosajiliwa na uwepo wa huduma muhimu za kijamii, ni kichocheo cha kuibuka kwa migogoro miongoni mwa

wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi na hata kijiji na kijiji,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake serikali:

a) Kuleta mapendekezo ya marekebisho ya sheria ili kuweka vigezo vya usajili wa kijiji kujumuisha: ukaguzi wa mipaka ya kijiji tarajiwa, mipaka ya kijiji na vijiji jirani, uwepo wa ardhi ya kutosha, kuangalia asili na historia ya kijiji na uwezekano wa kijiji kipya kupata huduma muhimu za kijamii; na

b) Kufanya uhakiki ili kubaini kama usajili wa vijiji vyenye migogoro ya ardhi ulikidhi vigezo na kuchukua hatua stahiki.

**20. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo katika Halmashauri nchini**

**KWA KUWA,** imebainika kuwa Sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto ya miundombinu na huduma duni za ugani kutokana na ufinyu wa bajeti katika ngazi za Halmashauri nchini,

**NA KWA KUWA,** Ukosefu huo wa Miundombinu na huduma bora za ugani, ni miongoni mwa sababu za kuwepo kwa ufugaji wa kuhamahama unaochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuzielekeza halmashauri zote nchini zinazokusanya ushuru kutokana na shughuli za ufugaji, zianzishe Mfuko maalum wa maendeleo ya mifugo *(Livestock Development Fund-LDF)*.

Mfuko huo utatokana na kiwango maalumu cha ushuru husika ili fedha hizo zitumike mahsusi kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya ufugaji (Majosho, mabwawa,) na huduma za ugani kama vile, tiba mifugo na elimu kwa wafugaji.

**21. Wawekezaji wanaokodisha mashamba kwa wananchi**

**KWA KUWA**, uamuzi wa serikali kuwapatia wawekezaji maeneo ya ardhi ulilenga kuwapa fursa ya kuboresha shughuli za kilimo na ufugaji ili kuchangia kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii,

**NA KWA KUWA,** Kamati imebaini kwamba wawekezaji wengi waliouziwa mashamba kwa ajili ya uwekezaji kama vile wawekezaji waliouziwa mashamba ya RIVACU, wilaya ya Babati, Southern Highlands wilaya ya Mbarali na shamba la Patel wilaya ya Kilosa, hawayatumii mashamba hayo kama ilivyokusudiwa bali wanayakodisha kwa wananchi kwa gharama kubwa, jambo linalochochea migogoro baina ya wawekezaji na wafugaji au wakulima baada ya wananchi hao kuvamia maeneo ya wawekezaji,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali: *Athari ya wastani*

a) kufuta umiliki wa mashamba ambayo wawekezaji wanayakodisha kwa wananchi kama vile mashamba ya RIVACU yaliyopo wilayani Babati, *Southern Highlands* wilaya ya Mbarali na shamba la Patel wilaya ya Kilosa, na kuyagawa kwa wananchi; na

b) Kuchunguza mashamba mengine yote ambayo wawekezaji wanayakodisha kwa wananchi, kufuta umiliki wake au kuyatwaa kuyagawa kwa wananchi.

**3.8.2 MAPENDEKEZO YA MUDA WA KATI**

**Mheshimiwa Spika,**
Kundi hili ni mapendekezo yanayohitaji kutekelezwa ndani ya kipindi kisichozidi miaka mitano. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

**1. Kukosekana kwa masoko ya uhakika kwa mazao ya Kilimo na mifugo**

**KWA KUWA,** kumekuwepo na ukosefu wa masoko ya uhakika ya mazao ya mifugo na kilimo,

**NA KWA KUWA,** ukosefu wa masoko ya uhakika wa mazao ya mifugo umesababisha kuwepo kwa ongezeko la mifugo inayoshindwa kupata malisho ya uhakika na pia ukosefu wa masoko ya uhakika wa mazao ya kilimo umesababisha mazao mengi kuozea katika maghala na hivyo kusababisha wakulima na wafugaji na Taifa kwa ujumla kushindwa kufaidika na mazao hayo kiuchumi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuhakikisha panakuwepo na soko thabiti la mazao ya mifugo *(meat commisision)* na kilimo *(commodity exchange market)* ili kuchochea uvunaji wa mifugo kwa mujibu wa sheria na pia kuwawezesha wakulima na wafugaji kuinua hali zao kiuchumi.

**2. Upungufu wa Rasilimali watu na fedha**

**KWA KUWA,** rasilimali fedha na rasilimali watu ni muhimu katika kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi nchini,

**NA KWA KUWA,** uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa upo upungufu mkubwa wa rasilimali watu na fedha unaosababisha mipango mingi kutokamilishwa, ikiwemo upimaji wa ardhi za vijiji na Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kutenga bajeti ya kutosha kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya kuajiri wataalamu na kugharamia shughuli za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi.

**3. Ongezeko la idadi ya watu**

**KWA KUWA,** ongezeko la idadi ya watu hapa nchini ni kubwa kufikia wastani wa 2.82% kwa mwaka na kusababisha upungufu wa ardhi iliyopo kwa ajili ya matumizi ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi,

**NA KWA KUWA,** ongezeko hili linachangia kuibuka kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji na wawekezaji kutokana na kugombea rasilimali ardhi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kibinadamu,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali; *Athari ya wastani*

a) Kupunguza kasi ya ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji kwa kuwa vipo viashiria kuwa, katika miaka michache ijayo, migogoro ya ardhi itaongezeka kutokana na kuwepo kwa ongezeko la idadi ya watu; na

b) Kuendelea kuelimisha wananchi wazingatie uzazi wa mpango.

**4. Fidia kwa wananchi wanaohamishwa**

**KWA KUWA,** Sera na sheria za ardhi zinaelekeza kuwa malipo ya fidia stahiki na kwa wakati ni haki ya wananchi ambao ardhi yao inatwaliwa na serikali au wawekezaji,

**NA KWA KUWA,** kushindwa au kuchelewa kulipa fidia kwa wananchi mara baada ya kuwahamisha ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa wananchi hao kutokana na kukosa maeneo ya kuishi na kuendeshea shughuli za kilimo, ufugaji au matumizi mengine,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake serikali: *Athari ya wastani*

a) Kuhakikisha kwamba inalipa fidia kwa wananchi wanaohamishwa kwenye maeneo wanayoishi au kuyatumia kihalali kabla ya maeneo hayo kutwaliwa na serikali; na

b) Wananchi walipwe kwa wakati fidia inayoendana na thamani ya ardhi, makazi na mali zao kwa wakati huo mara wanapoondolewa kwenye maeneo yao.

**5. Kuwafidia wawekezaji halali wa mashamba yenye migogoro**

**KWA KUWA,** ardhi ni muhimu kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali zikiwemo za kilimo, ufugaji na uwekezaji, baadhi ya wakulima na wafugaji wanaoishi maeneo yanayozunguka mashamba ya wawekezaji wanakosa ardhi kutokana na ardhi iliyokuwepo kugawiwa kwa wawekezaji wakati wa zoezi la ubinafsishaji, kutoweza kuhimili ongezeko la watu na shughuli za kibinadamu,

**NA KWA KUWA,** ukosefu wa ardhi kwa ajili ya wananchi kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji umesababisha baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya wawekezaji na kusababisha uharibifu wa mali za wawekezaji kama katika wilaya ya Babati *(shamba la Kiru Six)* na katika maeneo mengine nchini,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake serikali kushauriana na wawekezaji ambao maeneo waliyopewa yana migogoro ardhi kati yao wananchi wanaoishi jirani na maeneo yao kutokana na kutokuwa na ardhi ya kuendesha shughuli zao ili wayaachie kwa wananchi kwa kuzingatia makubaliano yenye tija kati yao na serikali.

**6. Ukosefu wa miundombinu ya mifugo**

**KWA KUWA,** ukosefu wa miundombinu ya mifugo kama vile malambo na majosho ni sababu za msingi zinazochangia kuwepo kwa mfumo wa ufugaji wa kuhamahama,

**NA KWA KUWA,** ufugaji wa kuhamahama unachangia kuwepo kwa uharibifu wa mazingira na kuibuka kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake serikali kuanzisha miundombinu ya mifugo kama vile malambo na majosho katika maeneo yote yaliyotengwa rasmi kwa ajili ya shughuli za ufugaji. *Athari ya wastani*

**7. Uhaba wa maji**

**KWA KUWA,** maji ni rasilimali muhimu katika uendeshaji wa sekta za kilimo na mifugo kwa ajili ya kuchangia maendeleo na kuboresha shughuli za wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi,

**NA KWA KUWA,** imebainika kwamba, kuna uhaba mkubwa wa rasilimali maji katika baadhi ya maeneo hapa nchini unaosababisha mwingiliano wa shughuli za wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi unaochangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwao,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake serikali:- *Athari ya wastani*

a) Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali ya maji katika maeneo yenye uhaba wa maji; na

b) Kuhakikisha kwamba wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi wanapata fursa sawa ya kutumia maji yaliyopo.

**8. Dosari katika utunzaji wa mazingira**

**KWA KUWA,** utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa lengo la kuboresha hali ya maisha na shughuli mbalimbali katika kukidhi mahitaji ya kibinaadamu na viumbe hai vingine,

**NA KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwepo kwa dosari katika utekelezaji wa *Sheria ya Usimamizi wa Mazingira*, Na. 20 ya mwaka 2004 zinazochangia kukauka kwa vyanzo vya maji, kuharibiwa kwa kingo za mito, Delta ya Bonde la Mto Rufiji,

Bonde la mto Kilombero na kupotea kwa uoto wa asili, kutokana na wakulima na wafugaji kuvamia maeneo hayo, hivyo kuchangia kuibuka, kukua na kuendelea kwa migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa *Sheria ya Usimamizi wa Mazingira* na kuimarisha utunzaji wa mazingira, vyanzo vya maji, mabonde na kingo za mito na bahari, Delta, na mabwawa.

**9. Kuimarisha Mabaraza ya Ardhi**

**KWA KUWA,** uwepo wa mabaraza ya ardhi katika ngazi za vijiji, kata na wilaya umekumbwa na changamoto kubwa zinazokwamisha usuluhisi wa migogoro ya ardhi kwa kukosa wataalamu na rasilimalil za kutekeleza majukumu yao,

**NA KWA KUWA,** imebainika kwamba changamoto hizo zimesababisha kuendelea kuibuka na kukua kwa migogoro ya ardhi katika maeneo mengi hapa nchini,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kupitia upya sheria inayoanzisha mabaraza ya ardhi ili kuhakikisha kuwa wajumbe wanaoteuliwa kwenye mabaraza husika ni wale tu wenye sifa zitakazosaidia utatuzi wa migogoro na pia kuhakikisha kwamba mabaraza husika yanakuwa na uwezo wa kuratibu shughuli nzima zinazohusiana na ugawaji wa ardhi katika maeneo husika.

**10. KWA KUWA,** Kamati imebaini kuwa ni chini ya asilimia 10 ya vijiji vyote vilivyopo hapa nchini ( hadi kufikia Novemba, 2012) ambavyo vimepimwa,

**NA KWA KUWA,** uwepo wa vijiji vingi ambavyo havijapimwa umesababisha mgongano wa watumiaji mbalimbali wa ardhi kama vile; wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi hali inayosababisha migogoro

ya ardhi baina yao kwa wao kuto tambua mipaka ya kufanya shughuli zao,

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kuwa na mpango mahsusi wa kuharakisha upimaji wa vijiji vyote ambavyo havijapimwa ili kuepusha nchi na migogoro ya ardhi inayoweza kuepukika.

### 3.8.3 MAPENDEKEZO YA MUDA MREFU

**Mheshimiwa Spika**,
Katika kundi la mapendekezo ya muda mrefu, Kamati imeainisha mambo ambayo utekelezaji wake utafanyika kwa kipindi cha miaka sita hadi kumi na tano. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

**1. Kusimamia kilimo na ufugaji wa kisasa na kibiashara:**

**KWA KUWA** kilimo na ufugaji wa kisasa na biashara (Intensive Agriculture) ni shughuli zinazoweza kuepusha mifumo ya uzalishaji unaosababisha mwingiliano wa shughuli hizo na migogoro baina ya wakulima na wafugaji,

**NA KWA KUWA** wakulima na wafugaji wengi hapa nchini wanaendelea na kilimo na ufugaji wa kuhamahama, jambo linalochangia kuibuka kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini, kutokana na mwingiliano wa shughuli hizo wakati wa kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine,

**KWA HIYO BASI** Kamati inapendekeza Bunge liitake Serikali; *Athari ya wastani*

i) Kuelimisha wakulima na wafugaji kuhusu kilimo cha kisasa na kibiashara pamoja na kuhakikisha kuwa wakulima wanatumia teknolojia ya kisasa inayowezesha uzalishaji wenye tija katika eneo dogo; na

ii) Kuelimisha wakulina na wafugaji kuhusu ufugaji wa kisasa na kibiashara unaoendana na matumizi ya eneo dogo kwa

uzalishaji wenye tija kutokana na matumizi ya aina bora za mifugo.

**2. Bajeti kwa ajili ya miundombinu ya kilimo na mifugo**

**KWA KUWA** Uendelezaji wa miundombinu kwa ajili ya ufugaji hutegemea upatikanaji wa fedha zilizokadiriwa katika Bajeti kwa ajili hiyo, lakini mwenendo wa Bajeti umeendelea kutokidhi mahitaji ya uendelezaji wa miundombinu,

**NA KWA KUWA,** ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya ufugaji na kilimo umesababisha kutokuwepo kwa miundombinu jambo linalochangia kuibuka, kuendelea na kukua kwa migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi,

*Athari ya wastani*

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kuwa Bunge liiitake serikali kuheshimu Bajeti inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miundombinu ya kilimo na mifugo.

**3. Kuanzisha Bodi ya Maendeleo ya Miundombinu ya Ufugaji**

**KWA KUWA**, imebainika kwamba hakuna chombo mahsusi kilichoundwa kwa ajili ya kusimamia miundombinu ya ufugaji kama vile majosho na malambo, sekta ya mifugo imekuwa ikikumbwa na changamoto mbalimbali,

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa chombo kinachosimamia maendeleo ya miundombinu ya ufugaji kunachangia kuendelea kuwepo kwa mfumo wa ufugaji wa kuhamahama unaoharibu mazingira na vyanzo vya maji na kusambaza magonjwa ya mifugo, hali inayosababisha wafugaji kuvamia maeneo ya watumiaji wengine wa ardhi; na

**KWA HIYO BASI,** Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake serikali;

a) Kuanzisha Bodi ya Maendeleo ya Miundombinu ya Ufugaji

(*The Livestock Infrastructure Development Board*) kwa ajili ya kusimamia na kuratibu ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya ufugaji kwa nchi nzima; na

b) Kuheshimu bajeti itakayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu.

**3.9 Hadidu ya rejea ya Sita: Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na utendaji:**

**Mheshimiwa Spika,**
Hadidu ya rejea ya sita iliitaka Kamati kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na kiutendaji.

Jukumu hili si dogo na linahitaji kujiridhisha bila ya shaka yoyote kuhusu uhusika wa wahusika, namna walivyohusika na sababu za kuhusika kwao. Vilevile msukumo katika kuhusika kwao pamoja na manufaa ya kibinafsi na kitaifa yanayoweza kupatikana kwa hatua za uwajibikaji zitakazopendekezwa ama kuchukuliwa ni mambo yanayohitaji kujiridhisha nayo.

Aidha, hatua hii inapaswa kufikiwa baada ya kujiridhisha pasipo na shaka yoyote juu ya dhima na wajibu wa Bunge katika mustakabali mzima wa kulitumikia taifa na watu wake.

**Mheshimiwa Spika,**
Uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa kwa kiasi kikubwa sababu za migogoro ya ardhi na matatizo ya uhifadhi wa mazingira ambavyo huchangia migogoro ya ardhi ni masuala mtambuka ambayo asili, athari na namna zinavyotokea zinategemeana na kunasibiana miongoni mwa sekta, idara, asasi mbalimbali za Serikali na pia wananchi kwa ujumla.

Kwa mfano, ipo migogoro ya ardhi na uharibifu wa mazingira, inayotokana na kutosimamiwa kikamilifu kwa sheria. Migogoro mingine inatokana na kuchelewa kutolewa kwa uamuzi na vyombo vya kutoa maamuzi kama vile Mahakama au kuchelewa kwa serikali kutekeleza maamuzi ya kisheria.

Maelezo haya yanaakisi hali iliyojitokeza wilayani Kiteto ambako yapo maamuzi ya mahakama yanayobainisha namna ardhi inayogombewa inavyopasa kutumika, maamuzi ambayo hadi sasa hayajatekelezwa. Hali hii inachangia kuendelea kutokea kwa migogoro ya mara kwa mara baina ya wakulima na wafugaji na hivyo kusababisha uvunjifu wa amani.

**Mheshimiwa Spika,**
Migogoro mingine inatokana na mawasiliano duni miongoni mwa watendaji. Vilevile, ipo migogoro inayotokana na kukosekana kwa elimu ya matumizi ya ardhi na uhifadhi wa mazingira na sababau nyingine kama, migogoro inayotokana na usimamizi hafifu wa sheria za ardhi, mifugo, kilimo, maji, uwekezaji na mazingira.

Aidha, ongezeko la idadi ya watu na mabadiliko ya tabia ya nchi vinachangia kutokea kwa mivutano na migogoro katika matumizi ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali.
Kamati ilibaini kuwa, migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi inazigusa wizara na idara mbalimbali za Serikali pamoja na wananchi wenyewe katika maeneo yenye migogoro.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na maelezo hayo, hekima na busara za kibunge (*Parliamentary wisdom*) katika Kamati ziliiongoza Kamati kuandaa taarifa hii ili kulishauri Bunge kwa mujibu wa maelekezo katika Hadidu ya rejea hii.

Jambo muhimu ni kwamba endapo ushauri huu utaridhiwa na Bunge lako Tukufu, utaweka misingi madhubuti ya Bunge kuisimamia Serikali katika kutatua migogoro ya ardhi katika

maeneo mengi nchini ambayo imekuwa mingi kwa sasa na hata kwa siku zijazo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa hakika, kuishauri Serikali na kusimamia uwajibikaji wake yote haya ni majukumu ya Bunge. Katika kutumia madaraka ya Bunge na katika kutekeleza majukumu yake, majukumu ya kushauri na kusimamia serikali yanaweza kwenda kwa pamoja au moja laweza kutekelezwa baada ya lingine.

Kwa mfano, Bunge linaweza kuishauri serikali na baadae Bunge laweza kuitaka Serikali kuchukua hatua za kutaka uwajibikaji unaotokana na utekelezaji wa ushauri uliotolewa na hivyo kufikia hatua ya Bunge kuweka maazimio yake.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa maelezo yote hayo, Kamati inapendekeza Hadidu ya Rejea hii isomwe kwa pamoja na mapendekezo ya Kamati ushauri uliotolewa uliwezeshe Bunge lako kuweka misingi imara itakayowezesha migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini kufikia ukomo na kuweka utaratibu utakaokidhi matarajio ya wananchi katika jambo hili kwa namna yenye kuleta tija na yenye kuzingatia haki.

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa ujumla, madhara yanayotokana na migogoro miongoni mwa watumiaji mbalimbali wa ardhi ni makubwa. Na inaleta athari nyingi za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Migogoro inayowahusisha wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi inapaswa kudhibitiwa na serikali ili isiendelee kuleta athari hizo.

Aidha Kamati inapendekeza kuwa, ili kuhakikisha kwamba migogoro hii inakwisha kabisa, Bunge liiendelee kuisimamia serikali katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kabla ya kuhitimisha Taarifa hii, naomba nikushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kutupa heshima kubwa ya kuwa Wajumbe wa Kamati Teule ya Bunge. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote, mashahidi na marafiki wa waliofika mbele ya Kamati kwa ajili ya majadiliano, kutupatia mawazo, ushauri wao na mahojiano pia kwa kutuletea nyaraka mbalimbali tulizoziomba au kuhitaji.

Kamati inathamini sana mchango wao katika kufanikisha taarifa hii. Tunaamini kwamba, yote hayo yalifanyika kwa mapenzi mema waliyonayo kwa nchi yetu. Tunapenda kueleza kwamba mchango wao umetusaidia sana kutekeleza jukumu hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba pia kuzishukuru Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Manyara, Arusha, Kigoma, Tabora, Kagera, Rukwa, Katavi na Mbeya kwa namna zilivyosaidia Kamati kukamilisha ziara za kiuchunguzi katika baadhi ya wilaya za mikoa hiyo kwa usalama. Aidha, napenda kutambua ushirikiano mzuri tulioupata kutoka kwa wawekezaji na wananchi wa vijiji vilivyotembelewa na Kamati kwa ajili ya uchunguzi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kipekee kabisa napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt.Thomas Kashililah kwa kufanya kazi na Kamati kwa muda wote, kwa ushauri wake makini uliowezesha kuhakikisha kuwa uratibu wa shughuli za Kamati unaenda vizuri na unaimarika wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Aidha, naishukuru timu nzima ya Sekretarieti ya Kamati Teule kwa utendaji wao wa kitaalam uliosaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Kwa kuthamini kazi yao naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1)Ndg. Athuman Hussein | - | Kiongozi wa Sekretarieti |
| 2)Ndg. Dickson Bisile | - | Mjumbe wa Sekretarieti |
| 3)Ndg. Zainab Issa | - | Mjumbe wa Sekretarieti |
| 4)Ndg. Lina Kitosi | - | Mjumbe wa Sekretarieti |
| 5)Ndg. Pius Mboya | - | Mjumbe wa Sekretarieti |
| 6)Ndg. Prudence Rweyongeza | | Mjumbe wa Sekretarieti |
| 7)Ndg. Erick Maseke | - | Mjumbe wa Sekretarieti |
| 8)Ndg. Mathew Kileo | - | Mjumbe wa Sekretarieti |

Aidha, nawashukuru kwa dhati watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao katika uratibu wa shughuli za Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Christopher Olonyokie Ole – Sendeka,
**MWENYEKITI**
**KAMATI TEULE YA BUNGE**
6 Februari 2015

**REJEA ZILIZOTUMIKA**

A: **SERA**

1) Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996

2) Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997

3) Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1997

4) Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997

5) Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002

6) Sera ya Taifa ya Mifugo ya Mwaka 2006

7) Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013

**B: SHERIA**

1) Sheria ya Ardhi Na. 4, ya Mwaka 1999

2) Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5, ya Mwaka 1999 *(The Village Land Act)*

3) Sheria ya Mahakama (Usuluhishi wa Migogoro) ya Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2002 *(The Courts (Land Disputes Settlements) Act NA. 2, 2002)*

4) Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya Mwaka 2009 *(The Water Supply and Sanitation Act, No. 12, 2009)*

5) Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6, 2007 *(The Land Use Planning Act No. 6, 2007)*

6) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula Vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010 *(The Grazing – Land and Animal Feed Resources Act No. 13, 2010)*.

7) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya ) Na. 7 ya Mwaka 1982 *(The Local Government (Local Authorities) Act, No. 7, 1982*

8) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 *(The Environmental Management Act No. 20, 2004)*

9) Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Maji, Na. 11 ya Mwaka 2009 *(The Water Resources Management Act No. 11, 2009)*.

10) Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008 *(The Animal Welfare Act No. 19)*

11) Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo, Na. 12 ya mwaka 2010 *(The Livestock Identification, Registration and Traceability Act No. 12, 2010)*.

12) Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, Na. 47 ya mwaka 1967, *(The Land Acquisition Act. No. 47, 1967)*

13) Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Na 26 ya mwaka 1997 (The Tanzania *Investment Act No. 26, 1997)*

**C: HUKUMU ZA MAHAKAMA**

*1) Rufaa ya Halmashauri ya kijiji cha Mabwegere dhidi ya Hamisi (Shaban) Msambaa na wenzake 32,* Rufaa Na. 53 ya mwaka 2010, katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania iliyoketi Dar es salaam.

*2) Udahwenga Bayay na Wenzake 16 dhidi ya Halmashauri ya Kijiji cha Vilima Vitatu,* Rufaa Na. 77 ya mwaka 2012 katika Mahakama ya Rufaa Tanzania iliyoketi Arusha. Shauri hili lilianzia Baraza la Ardhi la Wilaya, Mahakama Kuu ya Tanzania Arusha na kisha likasikilizwa katika Mahakama ya Rufaa.

**D: REJEA NYINGINE**

1) Tangazo la Serikali, Na. 494 lililochapishwa tarehe 17 Desemba, 2010, (ISSN. 0856 – 034X);

2) Newman, W.H.(1953) **Administrative Action**: The techniques of Organization & Management, Englewood Cliffs, NJ:Prentice – Hall;

3) Bhagwan and Bhushan (2010) **Public Administration**, S. CHAND &COMPANY LTD, New Delhi [ISBN- 81-219-0340-8].

***KIAMBATISHO NA. 01***

## ORODHA YA VIJIJI VILIVYOTEMBELEWA

| NA. | KIJIJI | WILAYA | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabwegere | Kilosa | MOROGORO |
| 2. | Kimamba | | |
| 3. | Mkata Station | | |
| 4. | Twatwatwa | | |
| 5. | Kidogobasi | | |
| | | Kilombero | |
| 6. | Chita | | |
| 7. | Namawala | | |
| 8. | Idete | | |
| 9. | Mlimba | | |
| | | Mvomero | |
| 10. | Hembeti | | |
| 11. | Mtibwa | | |
| 12. | Kambala | | |
| 13. | Mkindo | | |
| 14. | Kwa boga | | |
| 15. | Kidudwe | | |
| 16. | Lugenge | | |
| | | Morogoro (V) | |
| 17. | Bwakira chini | | |
| 18. | Dakawa | | |
| 19. | Bonye | | |
| 20. | Mbwade | | |
| 21. | Bonyabise | | |
| 22. | Mvuha | | |
| | | Rufiji | PWANI |
| 23. | Muhoro | | |
| 24. | Kilimani | | |
| | | Kiteto | MANYARA |
| 25. | Namelok | | |
| 26. | Olpopong | | |
| | | Hanang' | |
| 27. | Murbadaw | | |
| 28. | Gawidu | | |
| 29. | Ming'enyi | | |
| | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 30 | Vilima vitatu | | |
| 31. | Mwada (Shamba la RIVACU) | | |
| 32. | Bagara ziwani | | |
| 33. | Kiru six | | |
| 34. | Rolkisale | Monduli | ARUSHA |
| 35. | Itaswi | Kondoa | DODOMA |
| 36. | Mwambani | Chunya | MBEYA |
| 37. | Kapunga | Mbarali | |
| 38. | Ubaruku | | |
| 39. | Misenyi Ranchi | Misenyi | KAGERA |
| | Chabuhora | | |
| | Kashanda | | |
| | Nkansi | Sumbawanga | RUKWA |
| 40. | Nkundi | | |
| 41. | Malonje | | |
| 42. | Sikaunga | | |
| 43. | Fyongeleja | | |
| 44. | Kabungu | Mpanda | KATAVI |
| | | | TABORA |
| 45. | Kangeme | Urambo | |
| 46. | North Ugala | | |
| | | Kaliua | |
| 47. | Kona nne (King'wangoko) | | |
| 48. | Itebula | Uvinza | KIGOMA |
| 49. | Bweru | | |
| 50. | Malagarasi | | |

***KIAMBATISHO NA. 02***

## ORODHA YA MASHAHIDI WALIOHOJIWA NA KAMATI PAMOJA NA MARAFIKI WAKIWEMO WABUNGE WALIOJADILIANA NA KAMATI KUANZIA TAREHE 28 NOVEMBA, 2013 HADI TAREHE 4 FEBRUARI, 2014

| NA. | JINA | TAASISI | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Vitalis Mnyanga | Taasisi ya Maendeleo ya Usimamizi wa maji | Director of Research and Consultancy |
| 2 | Prof. Davis Mwamfupe | Chuo Kikuu - Dodoma | Ag. Principal |
| 3 | Prof. Dominic Kambarage | Sokoine University of Agriculture (SUA) | Professor |
| 4 | Anes Lukanga | TGNP | P.O. EJ |
| 5 | Yefred Myenzi | HAKIARDHI | Mkurugenzi Mtendaji |
| 6 | Joseph Chiombola | HAKIARDHI | Advocate |
| 7 | Geofrey Chambua | LHRC | Member |
| 8 | Susan L. Aloyce Kiwanga, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Viti Maalum |
| 9 | Sophia Elias Kaduma | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika | Katibu Mkuu |
| 10 | Eliezer Chuma | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika | PAO |
| 11 | Jumanne A. Maghembe | Wizara ya Maji | Waziri |
| 12 | Bashiri Mrindoko | Wizara ya Maji | Katibu Mkuu |
| 13 | Kaika Saning'o Telele | Bunge la Tanzania | Mbunge - Ngorongoro |
| 14 | Suma T. Mbyopyo | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Ag. AC ® |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15 | Eng. Christopher Chiza, Mb | Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika | Waziri |
| 16 | Jayson M. Kami | Tume ya Mipango, Matumizi Bora ya Ardhi | Ag. DG |
| 17 | Alphayo J. Kidata | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Katibu Mkuu |
| 18 | Aloyce Mwogofi | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | DAP |
| 19 | Gasper V. Luanda | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Ag. CL |
| 20 | Dome P. Malosha | CHC | Ag. DG |
| 21 | Stephen A. Ruvuge | MVIWATA | Mkurugenzi |
| 22 | Abdu Tumbo | MVIWATA | Mkulima |
| 23 | Zawadi Chande | MVIWATA | Mkulima |
| 24 | Abdulla Iddi | MVIWATA | Mwezeshaji |
| 25 | Hamisi J. Funge | MVIWATA | Mkulima |
| 26 | Dhamiru S. Ndiuwa | MVIWATA | Mkulima |
| 27 | Shomari S. Msumi | MVIWATA | Mkulima |
| 28 | Dr. S. Y. Sinare | TPSF | Chairman |
| 29 | Hawa A. Ghasia | TAMISEMI | Waziri |
| 30 | Dr. Yohana L. Budeba | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi | K/KM |
| 31 | Dr. David Mathayo, Mb | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi | Waziri |
| 32 | Prof. Anna Tibaijuka, Mb | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | Waziri |
| 33 | Maimuna K. Tarishi | Wizara ya Maliasili na Utalili | Katibu Mkuu |
| 34 | Khamis S. Kaghasheki | Wizara ya Maliasili na Utalii | Waziri |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 35 | Jumanne A. Sagini | TAMISEMI | Katibu Mkuu |
| 36 | George S. Kifuko | Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) | Katibu Mkuu |
| 37 | Deusdedith M. Duncan | CCWT | Mwanasheria |
| 38 | Gesso Heghon Bajuta | CCWT | Mjumbe |
| 39 | Ally Hamis Lumiye | CCWT | Mwenyekiti |
| 40 | Malema C. Mpyila | CCWT | Mwanasheria |
| 41 | Charles Mwijage, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Muleba Kaskazini |
| 42 | Mustafa H. Mkulo, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Kilosa |
| 43 | Innocent Edward Kalogeris, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Morogoro Kusini |
| 44 | Moshi S. Kakoso, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Mpanda Vijijini |
| 45 | Said Juma Nkumba, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Sikonge |
| 46 | Prof. Juma Kapuya, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Urambo Magharibi |
| 47 | Vita R. Kawawa, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Namtumbo |
| 48 | Ezekiel Maige, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Msalala |
| 49 | Modestus D. Kilufi, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Mbalali |
| 50 | Alphaxard Kangi Lugola, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Mwibara |
| 51 | Amos G. Makalla, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Mvomero |
| 52 | Dr. Titus M. Kamani, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Busega |
| 53 | Murtaza A . Mangungu, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Kilwa Kaskazini |
| 54 | Kuruthum J. Mchuchuli, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Viti Maalum |
| 55 | Richard Mganga Ndassa, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Sumve |
| 56 | Abdul Jabiri Marombwa, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Kibiti |
| 57 | Saidi Amour Arfi, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Mpanda Mjini |
| 58 | Jitu Vrajlal Soni, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Babati Vijijini |
| 59 | Job Yustino Ndugai, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Kongwa |
| 60 | Rose Kamili Sukum, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Viti Maalum |
| 61 | Benedict N. Ole-Nangoro, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Kiteto |
| 62 | David Zacharia Kafulila, Mb | Bunge la Tanzania | Mbunge - Kigoma Kusini |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 63 | Audax Mwendabantu | RAMSAR - Kilombero | Meneja |
| 64 | Maj. Msabaha Y. Yamawe | 837 KJ CHITA | Kamanda wa Kikosi |
| 65 | Aloyce Masanja | RUBADA | DG |
| 66 | Wallace Karia | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero | DED |
| 67 | Majaliwa Jafari | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero | DLPU |
| 68 | Anthony Mtaka | Wilaya ya Mvomero | DC |
| 69 | F. C. Shilogile | Polisi Morogoro | RPC |
| 70 | William V. Lukuvi | Ofisi ya Waziri Mkuu | Waziri wa Nchi (SUB) |
| 71 | Joel J. Bendera | Mkoa wa Morogoro | RC |
| 72 | Julieth Kairuki | TIC | CEO |
| 73 | Revocatus Arbogast | TIC | IFM (P) |
| 74 | Ildefonce Ndemela | TIC | PLO |
| 75 | Elias Tarimo | Wilaya ya Kilosa | DC |
| 76 | Arnold C. Mzigo | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero | Ag. DLNREO |
| 77 | Violeth J. Kimeme | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | P.L. Officer |
| 78 | Dkt. Rehema J. Nchimbi | Mkoa wa Dodoma | RC |
| 79 | Omar S. Kwaangw' | Wilaya ya Kondoa | DC |
| 80 | Sylvester M. Ambokile | Idara ya Uhamiaji, Makao Makuu | PCIS |
| 81 | Dawson Mongi | Idara ya Uhamiaji, Makao Makuu | Kamishna |
| 82 | A. Kh. Abdallah | Idara ya Uhamiaji, Makao Makuu | Kamishna |
| 83 | I.J. Mwalongo | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa | DED |
| 84 | Alexander N. Songorwa | Wizara ya Maliasili na Utalii | Mkurugenzi/ Wanyamapori |
| 85 | Deusdedith Mayomba Duncun | PINGOS Forum | Mjumbe/Wakili |
| 86 | Hayte M. Samo | Mwenyekiti - PINGOS | Daktari |
| 87 | Isaya N. Olesaiblu | PINGOS, Director of Programmes | PINGOS |
| 88 | Navaya Ndasko | PINGOS | Researcher |
| 89 | Emmanuel Saringe | PINGOS Forum | |
| 90 | Kusundwa Wawalwa | PINGOS Forum | |
| 91 | Edward Porokisa | PINGOS Forum | Mkurugenzi |
| 92 | Elie Chansa | PINGOS Forum | Msaidizi Habari |

**SPIKA:** Ahsante. Hiyo hoja ni ya Kamati Teule hamna namna! Tuliiunga mkono wakati ule basi kwa hiyo, ndiyo taarifa inayotoka. Sasa huyu ndiyo ni Mjumbe wa Kamati Teule! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemruhusu..., naomba mumpigie tu makofi. Wapigieni makofi Wajumbe wa Kamati wote wapate faraja tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama mmesikiliza vizuri hii taarifa ya Kamati Teule na hata hadidu rejea tulizowapa zilikuwa ni kujaribu kuchambua maudhui yote yanayoleta migogoro nchini kwetu kuhusiana na matatizo haya yaliyotajwa humu na kwamba sisi ni watu ambao tunatakiwa katika kuingia kutunga yaani kusimamia Serikali katika kutunga sera ambazo zile zinaweza kusaidia kufanya mambo bora zaidi kwa kizazi hiki kuliko tulikotoka.

Kwa hiyo, mimi ninachoomba tumezoea sisi Wabunge na najua ni kipindi cha lala salama najua hiyo, sasa lala salama muiache leo, tuzungumzie ripoti hii ambayo imefanyika kazi nzuri sana, tuache lala salama zetu zile naamini unaanza kuzungumzia sana sana unaweza kuwa unatoa mfano kusema kwa mfano kuunga mkono kuliko kwenda ile lala salama mimi sijui hakuna atakayekujibu hapa. Hapa tunasema kwamba tunataka kufanya kitu hiki tuseme kwamba hali iliyopo hii hairidhishi twende wapi nadhani ndiyo kubwa tunalotakiwa kufanya na ikiwezekana tufikishe mahali Bunge hili liweze kusaidia Serikali kuja na kitu ambacho kinaeleweka wafugaji wanajijua, wakulima wanajijua, wawekezaji wanafahamu, wahifadhi wanafahamika angalau tuwe na vitu hataunavyokuja kusimamia Serikali mnasimamia katika mambo ambayo tutayatungia sheria pengine watakavyoleta.

Lakini tukileta hapa lala salama zetu huko kwa kweli hatutakuwa tumeisaidia nchi yetu na watu wanaandika wanasema Wabunge wanalalamika tu, wanalalamika tu hebu tuache safari hii kulalamika tuzungumze. Tuzungumze yale ambayo tunafikiri tunaweza kuifanya nchi yetu ikawa

bora zaidi kuliko ilivyo sasa na mambo yetu ya siasa hii taarifa hii nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii wameifanya bila kujala siasa ya vyama vyao. *(Makofi)*

Sasa tukijenga hii, hili ni suala la ardhi na maslahi ya Watanzania wote bila kujali chama wanachotoka na wanakokwenda tunataka Watanzania wa leo na vitoto vyote vya miaka miaka viweze kuridhika kwamba sisi tuliwahi kufanya kazi mambo haya yalikuwa yamevurugika hapa katikati sasa yanyooke na wakuonyosha ni ninyi.

Kwa hiyo, mimi leo uchangiaji nataka ile habari ya kulalamika nitakukalisha chini, ripoti ndiyo hii hapa, ripoti ipo hapa na wameiandika kitaalamu kweli kweli. Nawashukuru sana Sekretarieti ile imefanya kazi nzuri sana, nawashukuru sana na nawashukuru na Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba ni Wabunge makini sana hawa wangeweza kupigana huko huko, lakini hawakufanya hivyo maana Ole-Sendeka mifugo, nani sijui mkulima, nani wangepigana tu akina Selasini kule mifugo haipo wangepigana lakini hawakufanya hivyo, wamekuja na kitu kizuri. Kwa hiyo, kwa muda nilionao hapa napenda achangie Mheshimiwa Joseph Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

Ni dakika zile zile kumi, msijali tunajadili leo na kesho mpaka saa sita kwa hiyo nilishafanya hesabu hapa tunaweza kufika watu zaidi ya thelathini na ngapi sijui.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia taarifa hii ya Kamati Teule.

Kabla sijatoa mchango wangu na mimi nipende kukushukuru kwa kuniteua kuwa mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati hii na nilishukuru sana Bunge kukubali kuiunda Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote yaliyosema katika taarifa ya Kamati Teule ningeomba sote kwa pamoja na kama ulivyosisitiza tukubali kwamba tunalo tatizo katika nchi

yetu ambalo kwa pamoja lazima tulitatue kama Bunge la nchi yetu. Katika siku hizi mbili leo na kesho Bunge linayo nafasi ya kuhitimisha matatizo, magomvi na mauaji yanayoendelea katika nchi yetu kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, Bunge lina nafasi hiyo kwa kujadili kwa kina mapendekezo yaliyotolewa na Kamati Teule na kuisaidia Serikali iweze kuchukua hatua zinazostahili za muda mfupi, za muda wa kati na za muda mrefu kama Kamati ilivyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuweka msisistizo katika mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba katika nchi yetu tuna tatizo kubwa sana na bajeti yetu, lakini imefika wakati lazima kama Bunge, kama nchi tuipime ardhi yetu ili tuweze kujua ardhi yetu ina ukubwa gani, wakulima eneo lao liko wapi, wafugaji eneo lao ni lipi na watumiaji wengine wa ardhi eneo lao ni lipi. Bila kufanya namna hiyo muingiliano huu wa shughuli kati ya wakulima na wafugaji ukiendelea hatutaweza kutatua mgogoro uliopo na mauaji kati ya wakulima na wafugaji hayatakoma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo katika ziara yetu ya uchunguzi tumetembelea baadhi ya vijiji katika nchi yetu kati ya vijiji karibu 12,000 ni vijiji elfu moja kama na mia mbili hivi ambavyo vimepimwa na baadhi ya hivyo 1000 ni vichache sana ambavyo vipo katika mpango wa matumizi bora ya ardhi. Hili ni tatizo lazima vilevile tuangalie namna ya kuweza kupata njia ya kupima vijiji vyote na kuweza kuhakikisha kwamba mpango wa matumizi bora ya ardhi umeenezwa katika vijiji vyote katika nchi yetu. Ushahidi uliopo mgogoro wa kijiji cha Kambala na majirani zake kwa mfano kijiji cha Mkindo ni matokeo ya upimaji ambao haukufanywa katika vijiji vingine vilivyo jirani na kijiji cha Kambala na vilevile ni matokeo ya kutokuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, mgogoro ulio katika kijiji cha Mabwegere ambao umesababisha mauaji kwa muda mrefu vilevile ni matokeo ya upimaji ambao unalalamikiwa na upimaji ambao vijiji vingine havijaweza kuzingatia. Ni ushauri wa Kamati na ni maoni yetu kwamba kama Serikali au kwa kutafuta upatanishi au kwa kutumia njia zozote zile za busara vijiji hivi mipaka yake ikaonekana upya kwa makubaliano na vijiji vyote jirani na mpango wa matumizi bora ya ardhi ukazingatiwa kwa kiasi kikubwa sana tutaweza kutatua tatizo hili ambalo linaendelea na shida na migogoro hii ni karibu katika vijiji vyote ambavyo vina mgogoro.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda Wilaya ya Kilombero, tumekwenda Tarafa ya Mlimba, tumekwenda Chita vijiji vya Namawala, Chitete na karibu mwambao huo mpaka Wilaya ya Ulanga vijiji karibu 22 vina matatizo yanayotokana na vijiji kutopimwa na kutozingatiwa kwa matumizi bora ya ardhi, ndiyo maana naliomba Bunge na Serikali kuhakikisha kwamba njia pekee, njia muhimu sana ambayo itatuondolea migogoro kati ya wakulima wa nchi yetu na wafugaji wa nchi yetu ni kuhakikisha ardhi za vijiji zimepimwa na tumekuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni mashamba pori na mashamba ambayo yanamilikiwa na wawekezaji wa ndani na nje. Ni kweli baadhi ya wawekezaji wa ndani na nje wamechukua mashamba makubwa yaliyokuwa ya *NAFCO* na taasisi nyingine lakini hawayaendelezi. Tumefika kwa mfano Kilosa pale tummekuta Mwenyekiti wa Halmashauri ana shamba analikodisha kwa wananchi wake na analikodisha kwa gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Pia tumekuta Wachina pale Kilosa wana shamba katika nchi yetu wanalikodisha halafu wao wanafuga sungura wakati wananchi jirani wanahangaika, ni kwa sababu hii tunaishauri Serikali kwa nia njema kabisa ipitie maeneo haya, iangalie wale ambao mashamba yale hawayatumii wayachukue kwa sababu yanaleta kishawishi

kwa wananchi majirani ambao hawana ardhi kwa wafugaji majirani ambao hawana ardhi kuvamia yale mashamba.

Jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni namna ambavyo Wizara ya Ardhi itawatumia wale watendaji wake kwenye Halmashauri, kwa sababu tulichogundua ni kama baada ya ugatuaji wa madaraka wale Maafisa Ardhi kwenye Halmashauri hawana *link* na Wizara, kule kwenye Halmashauri wako wamekaa peke yao tu hawana uwezo wa kutoa maamuzi na wakati mwingine wakitoa yale maamuzi, maamuzi yanasigana kule juu na Wizara. Kwa hiyo ni kwa sababu hii tukasema ni vizuri Wizara ya Ardhi iangalie namna ambavyo itashirikiana na watendaji kwenye Halmashauri ili kuweza kufanya kazi zao sawasawa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa muda, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Sakaya kwa muda uliobakia.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu, lakini pia nikushukuru kwa kuniteua kwenye Kamati hii na niwashukuru Wabunge wote kwa kuweza kuridhia nikaweza kuwa Mjumbe wa kamati hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchangia tu kwenye mambo machache kwa sababu mapendekezo yote tumeyatoa sisi kama Kamati. Ukiangalia kwa ujumla ripoti nzima ya Kamati Teule tumegundua kwamba matatizo mengi sana ya migogoro ambayo iko ndani ya nchi yetu imesababishwa kwanza kabisa kutofuatwa kwa sheria ambazo tunazo, lakini pili kutokuatwa kwa sera ambazo zipo wazi na ziko *clear,* lakini tatu kutokuwajibika kwa viongozi kwa nafasi zao kwa maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la kukosekana kwa masoko. Tumeshuhudia kwamba

tumetembea maeneo mengi na tumeona kweli wafugaji wanayo mifugo mingi sana na mingine ni dhaifu na tukiangalia idadi ya mifugo na maeneo ya kufuga haiendani na wafugaji tumejaribu kuongea nao wako tayari kabisa kupunguza mifugo yao, lakini wanauliza tupunguzie wapi Waheshimiwa Wabunge? Hatuna masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, leo ndani ya nchi yetu hatuna kiwanda hata kimoja cha kusindika nyama, hatuna viwanda vya ngozi vyote vimekufa, vilivyobinafsishwa vyote vimegeuka kuwa ni ma-*godown* ya magari vingine vinafugia kondoo ndiyo hapo tulipofika na ukiangalia wafugaji wanasema Waheshimiwa Wabunge ng'ombe ukimchukua kuanzia pembe ni *product*, ukija kwato ni *product,* ngozi ni *product*, nyama ni *product*, mifupa ni *product* Serikali haioni haya, haioni kwamba mifugo inayozurura ni mali kwa Taifa hili?

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho nilikuwa naomba sana ni lazima Serikali yetu kwa mapendekezo ambayo tumeyatoa, Serikali iache kujiondoa kusema kwamba tunaendelea kusubiri wawekezaji waje wajenge viwanda kwa sababu asilimia 80 ya Watanzania ni wafugaji na wakulima, leo mifugo inazurura hatujapata wawekezaji wa kuwekeza kwenye viwanda hivyo. Tumezungumza kwenye taarifa yetu kuna baadhi ya nchi kwa mfano Zimbabwe wanayo *commodity exchange market* wanashughulika na mambo ya mazao ya mifugo na mazao ya kilimo Zimbabwe kwa hiyo Serikali ina *commission* yake maalum kwa ajili ya kuhusika na mazao ya mifugo na kilimo.

Mheshimiwa Spika, Sudan na wenyewe wana kitu kinaitwa *Meat Commission* wenyewe ni *commission* ya Serikali inashughulika na kuhakikisha kwamba mazao ya mifugo yanapata masoko mazuri na ni *commission* muhimu kwa ajili hiyo. Kwa nini nchi yetu tusiwe na vitu kama hivyo, hii habari ya kusubiri wawekezaji hatuwezi kuendelea wakati mifugo inazurura. Naomba sana kwenye mapendekezo kwenye hilo Serikali lazima ihakikishe kwamba inaingia hapo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la maeneo yaliyokosa sifa za kuweza kuwa hifadhi. Ni kweli tumetembea maeneo mbalimbali, kuna maeneo kwa kweli ukiambiwa ni hifadhi unashangaa, maeneo mengi tuliyotembea ambayo yamekuwa na malalamiko mengi tumekwenda Wabunge wameona. Maeneo ndani ya vitabu vya Serikali na ramani kweli ni hifadhi ukienda kwenye *ground* hakuna mti, hakuna kichaka, hakuna ngendere, hakuna swala kule kuna *guest house*, kule kuna masoko, kule kuna nyumba za ibada, kule misikiti, kuna makanisa, kuna shule, kuna maji na mambo kama hayo.

Sasa maeneo kama haya Serikali imeendelea kuwa na migogoro na wananchi ambao tayari pale na vijiji hivi vimesajiliwa kisheria, wanaosajili ni Serikali yenyewe, wanaopeleka huduma za maji kule ni Serikali, wanaopeleka barabara ni Serikali. Ifike mahali maeneo kama haya sasa tumependekeza yaondolewe kwenye hifadhi huwezi kuendelea kung'ang'ania kwamba hii ni hifadhi wakati hakuna hifadhi. Tumetoa hifadhi kwa wachache mifano imetolewa maeneo ya Kaliuwa ambayo miaka yote napigana nayo, Kangeme, Shela, Kona Nne huku Sikonge kuna maeneo kibao, Uyui, Mkoa wa Tabora tu kwa tathmini iliyokuwa imefanyika mwaka 1967 vijiji zaidi ya 60 viko ndani ya hifadhi na vimesajiliwa kisheria. Tumependekeza maeneo haya Serikali ione kwamba yaondolewe kwenye hifadhi ili kuondoa migogoro ambayo imekuwepo miaka mingi.

Suala lingine ni suala la wawekezaji kupewa mashamba bila kufuata taratibu. Tunayo sera nzuri sana na nashukuru kwa fursa uliyotupa tumepitia sera za nchi hii ni nzuri ajabu, tatizo ni utekelezaji tu. Tunayo sera inayosema Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 wawekezaji wote wapitie *TIC* kuweza kupata maeneo kwa ajili ya kuwekeza, lakini cha ajabu Serikali haifuati kile ambacho kipo kwenye sheria iko *clear* sasa hivi mwekezaji ana *option* mbili, anaweza akapitia *TIC* au anaweza akapitia Wizara ya Ardhi na tulivyoongea na watu wa *TIC* asilimia kidogo sana ndiyo wanaopitia *TIC* wengi wanapitia Wizara ya Ardhi huku ardhi sasa ndiyo kuna rushwa, wanapata kiholela wanakwenda kurubuni wananchi

kule vijijini matokeo yake migogoro imeendelea. Kwa nini Serikali tumeshaweka tayari tuna sheria yetu tuifuate kila mwekezaji apitie *TIC* kwa sababu *TIC* wanafanya utafiti, wanakwenda kuangalia maeneo, wanayapima vizuri mwekezaji anapewa eneo ambalo halina migogoro. Kwa hiyo, hili nalo tunaomba sana kwamba Serikali ifanyiwe kazi.

Suala lingine ni suala la Watendaji wa Serikali, ilitushangaza sana kuna mkakati mzuri ulioandaliwa tangu 2009 mzuri ajabu ukiusoma unapendekeza na umendaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na ni mkakati ambao kama ungefuatwa ungeondoa changamoto na matatizo yote ya migogoro ambayo ipo tangu mwaka 2009 mpaka 2014 mpango upo, mkakati upo Watendaji Wakuu wa Serikali hawaujui wala hawajaufanyia kazi. Sasa ukiangalia mpango unaandaliwa kwa rasilimali, vikao vimekaa, wamezunguka maeneo mbalimbali, wameuchukua wameweka kwenye *draw,* kwa mwendo wa kutofanyia kazi mikakati yetu kama Serikali tutaendelea tu kuongea Bungeni hapa. Tutaendelea kupiga kelele, tunaomba Serikali mipango ikishapangwa, mikakati ikiandaliwa wachukue waisambaze ili ifanyiwe kazi kuweza kuondoa changamoto ambazo zimeendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu ni hayo machache nikushukuru sana kwa nafasi hii ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nawashukuru nilitaka waanze wenyewe wa-*set pace* maana yake mnaona walivyoongea mpaka wote mnasikia hamu kuwasikiliza mara mbili, tatu. Sasa na hiyo mnaweza wote kila mtu si anatoka eneo lake anakajua kuna matatizo yanayofanana. Kwa hiyo nawategemea kabisa mchana mtajadili kwa nguvu sana na kwa lengo la kupata kitu kimoja kizuri sana kwa ajili ya nchi yetu tuondokane na matatizo yaliyopo hapa.

Waheshimiwa kwa sababu muda wenyewe umekwisha nisitishe shughuli mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Lediana M. Mng'ong'o) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, atafuatiwa Mheshimiwa Lucy Nkya na Mheshimiwa Capt. John Chiligati, kama wapo wajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee nianze kwa kukupongeza kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetu. Ni hakika kama ambavyo sisi tuna imani na wewe basi utaendelea kulitendea haki Bunge hili na kutuongoza katika kutengeneza mambo yaliyo mazuri kwa mustakabali wa maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Ole-Sendeka na Kamati nzima kwa kazi kubwa ambayo wamekwishaifanya na kwa kweli binafsi naona sasa mwanga katika kutatua migogoro mikubwa inayotukabili sisi ambao katika maeneo yetu tuna mchanganyiko mkubwa sana wa wakulima na wafugaji hasa katika eneo hili la migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo nilikuwa nataka nichangie, kubwa zaidi ni juu ya jinsi gani tunaweza kupunguza kama siyo kuondoa kabisa migogoro ya ardhi iliyopo katika maeneo yetu. Nishukuru Kamati imeweza kuainisha maeneo ambayo yanaonekana kwamba yana matatizo makubwa sana. Pia niwashukuru kwa kuona kwamba eneo la Mkoa wa Pwani hususan Jimbo la Chalinze ni moja ya maeneo yenye matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya yameelezwa katika lugha ambayo niseme labda kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti Sendeka alikuwa anatupa *summary* maana nikiri pia kwamba kumekuwa na tatizo kubwa sana la upatikanaji wa hizi taarifa maana *book* lile ni kubwa sana. Kama tungepewa mapema maana yake tungeweza kwenda *deep*

zaidi lakini niseme kwamba kwa kazi nzuri waliyoifanya mimi kwangu nataka nianze katika eneo la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunayo matatizo na katika eneo la rushwa hili pamoja na taarifa nzuri aliyotupa Mheshimiwa Sendeka lakini tuna matatizo makubwa sana kwa Wenyeviti wetu wa Vijiji. Mimi niwashukuru wananchi ambao waliamua kuwahukumu wale ambao wamekuwa ni sehemu kubwa ya tatizo katika jamii zetu. Maana wako Wenyeviti kule kwangu wameondolewa, mimi binafsi yangu niliwashukuru wananchi walipochaguliwa hawa wapya kwa sababu wamekuwa ni sehemu kubwa sana ya kupokea rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wetu wanachukua rushwa mchana kweupe, wakati mwingine inapofika kwenye mikutano ile ya wananchi kutaka kujua nini kinachoendelea taarifa wanazotoa zinakinzana na hali halisi. Maana haiwezekani mifugo ikaja kula shamba la mtu halafu Mwenyekiti anaulizwa lugha anayotoa anasema kwamba, bwana mimi sikuja kama kuna mifugo imeingia. Hili linatokana na ukweli kwamba hata Watendaji wetu pia wameshindwa kusimamie ile mipango mizuri ya Serikali iliyowekwa. Maana imewekwa taratibu kwa mfano kule kwangu, maeneo yametengwa ya wakulima na wafugaji, lakini unakuta watu wetu wanashiriki kusimamia kugawa tena ardhi zilezile ambazo zimetengwa kwa ajili ya wafugaji kwenda kuwapa watu wengine waweze kufanya shughuli nyingine ambazo siyo za malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nianze na hili ikiwa ni sehemu kutoa wito kwa Serikali kuendelea kusisitiza katika watendaji wetu na viongozi wetu wanaopewa dhamana za Kiserikali wasimamie sheria. Maana kama wao hawatasimamia sheria sisi wananchi itakuwaje? Naogopa sana kufikia hatua ambayo wenzetu katika maeneo mengine wamefikia. Kwa mfano, nimewahi kusikia siku moja watu wa Kilosa kwamba watu wanachomana mishale katika maana ya kulinda rasilimali ardhi zao. Imefika sehemu maeneo mengine kama Kiteto watu wanauliwa katika

migogoro ya ardhi. Mimi nataka nitoe rai hii kwa Serikali, waendelee kutoa elimu lakini pia waendelee kuwasisitizia wenzetu hawa ambao wamepewa dhamana wasimamie rasilimali hizi na watimize wajibu wao kama ambavyo waliahidi katika viapo vyao vya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, yako matatizo mengine ambayo naita matatizo yanayosababishwa na watu wenyewe au viongozi wetu au watu waliopewa dhamana ya kutotambua dhamana zao. Hapa nataka nijikite katika eneo la Bagamoyo na Chalinze. Tunalo eneo linaitwa Makurunge. Pale Makurunge kuna hadithi moja ambayo Bunge hili likisikia linaweza likashtuka kidogo. Kuna eneo walipewa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaitwa Razaba halafu kuna eneo wamepewa watu wanaitwa *EcoEnergy* kwa ajili ya kilimo cha miwa halafu katika eneo hilohilo kuna eneo amepewa Mzungu, mwekezaji ambaye wanakijiji pale Makurunge wanasema hawajawahi kumuona na eneo hilohilo wamepewa *NARCO* kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sehemu moja ya sikitiko kubwa sana kwangu mimi, wananchi hawaelewi wafanye nini. Eneo alilopewa huyu bwana ni kubwa sana ni *almost* karibu heka 5000 au 10,000 lakini eneo hilohilo ukiangalia ni ule utaratibu wa kutoa hati juu ya hati. Kwa sababu leo hii wako wenzetu wa mbuga ya Saadan wanasema kwamba eneo lao limeanzia kwenye Mto Wami pale limekuja mpaka Makurunge. Eneo hilohilo ambalo mbuga ya Saadan wanasema ni la kwao ndiyo eneo hilohilo ambalo watu wa *EchoEnergy* wamepewa kama sehemu ya wao kufanya kilimo cha miwa. Upande wa pili wa barabara inayotoka Bagamoyo kwenda Kiwangwa, kwenda mpaka Msata, kuna eneo lingine la kijiji pia ambalo kuna Mzungu mwekezaji amepewa, yeye anasema eneo lile ni la kwake kapewa la uwekezaji lakini hapohapo alipokuja mama Mahiza kipindi hicho akiwa Mkuu wa Mkoa alitoa taarifa kwamba eneo lile ni eneo la ranchi ya *NARCO*, hawa wenzetu wa hapa Mlandizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maeneo ambayo kama hatukuweza kuyashughulikia mapema, yanaweza kusababisha mgogoro mkubwa sana siku zijazo. Siyo tu katika maana ya kwamba wananchi wangu au wananchi wetu wa Bagamoyo wanaweza kukosa eneo kwa ajili ya kufanya shughuli zao za kilimo na maendeleo lakini pia inaweza kusababisha hata yale maendeleo kwa jumla yake yakakosekana. Ni wito wangu na natambua kwamba sasa tunaye Waziri wa Ardhi ambaye anakwenda mbio kwelikweli, mtu makini, ndugu yangu, kaka yangu, baba yangu Mheshimiwa Lukuvi, ni imani kwamba katika eneo hili ataangalia jinsi gani anaweza akawaelekeza watu wa Halmashauri, watu wa Ardhi katika maeneo yote haya ili waweze kuyasimamia na kuona jinsi gani wanaweza wakatatua matatizo haya na hata ikibidi kuondoa hati nyingine ambazo zinaonekana kwamba zinaweza zikasababisha migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni eneo la ardhi katika Mahakama. Utaratibu tulionao sasa hivi mashauri yote yanapelekwa katika Mabaraza ya Ardhi. Moja ya tatizo kubwa ambalo tunalipata hasa nikizungumzia kwa jiografia ya Mkoa wa Pwani, leo hii mtu akiwa na tatizo kule Delta - Rufiji analazimika atembee umbali mrefu mpaka Kibaha kwenda kupata haki. Kibaya zaidi sheria ambayo inaanzisha Mabaraza hayo haielezi hivyo, sheria yenyewe inaelekeza Mabaraza yafunguliwe katika kila Wilaya. Natambua *may be* huenda ni changamoto ambazo zinatokana na fedha na mambo mengineyo lakini ni wakati sasa umefika wa Serikali yetu ambayo mimi naamini kwamba ni Serikali sikivu kuliangalia jambo hili kwa ukaribu zaidi ili wananchi wetu hawa waweze kujipatia haki yao wanaostahili kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana sisi kwenye sheria tunaamini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba haki ifanyike. *(Makofi)*

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hili tatizo ambalo limewakoroga Watanzania kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii niwape pole wale wote ambao wamepoteza maisha, wamepoteza ndugu zao kwenye migogoro ya wakulima na wafugaji, sehemu yoyote pale Tanzania lakini hususan katika Wilaya ya Mvomero Morogoro, bado tatizo lipo na linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri sasa wakati umefika kwamba yale maeneo ambayo yamekuwa na matatizo makubwa na naona yanaliletea Taifa letu dosari kwamba kunakuwepo na kuvunjika kwa haki za binadamu na mambo mengine, Serikali ipange mkakati maalum wa kwenda katika Wilaya ya Mvomero, wahakikishe kwamba wanapitia upya ile mipaka ya vijiji, kijiji cha Kambala, kijiji cha Mabwegere na kila mmoja aelewe mwisho wake ni wapi na viongozi wale wapate elimu. Baada ya hapo naamini kwamba sisi Watanzania siyo adui kati ya mkulima na mfugaji, lakini hasira na jazba zinapanda pale ambapo kila mmoja anaona mali yake inaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni namna ambavyo vyombo vya ulinzi na usalama vina-*handle* hiyo *problem* inapojitokeza. Mara nyingi unakuta kwamba hawa walinzi wetu wa amani wengine wanachukua upande, wanakuwa upande wa wengine, sasa hilo linafanya wananchi wanakuwa na hasira zaidi. Kumbe wao kazi yao ni kuhakikisha kwamba hizi pande mbili zinazogombana zinakaa mahali zinazungumza na wao wakiwa kama viongozi wao ili tuweze kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba hata maeneo mengine ya Morogoro katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Jimbo la Morogoro Kusini bado kuna harufu ya ugomvi. Hata juzi tu ameuliwa mkulima katika eneo la Bwakila. Mambo siyo shwari. Kwa sababu mambo siyo shwari, naomba sasa Serikali itamke leo ndani ya Bunge hili kwamba maeneo hayo ni maeneo ambayo tunataka waende wakafanye operesheni maalum, operesheni maalum maana yake ni kwamba wakahakikishe hawa wanaogombana kila mtu anakaa kwake lakini ardhi ipimwe na matumizi yake yajulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo, naomba Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wapate semina ya kuelewa kwamba wao mamlaka yao ya kugawa ardhi yanaishia wapi. Kweli kabisa, matatizo tuliyokuwa nayo Morogoro yanatokana na kutokujua wajibu wa Serikali za Vijiji kwamba wana uwezo wa kugawa ardhi kiasi gani. Unakuta tu Mwenyekiti wa Kitongoji anakwenda anamgawia mtu hekari 200 au 300, mamlaka hayo kayapata wapi? Yule akishapata anakwenda anaweka mipaka yake, anaanza kufanya kazi, wewe ukienda kulalamika kwamba shamba langu limeliwa yule anajua kwamba kauza shamba lako hachukui hatua yoyote anakaa nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa ni kuheshimu Sheria Ndogo ambazo zimewekwa kwenye kila kijiji na zimepata baraka ya Halmashauri, kwa Morogoro imekuwa ni ngumu. Kuna makabila mengine wanasema hapana hamwezi kutuwekea sisi sharia! Sasa inapofika hapo kesi zinakwenda Mahakamani, naomba niseme kwamba na vyombo vya kutoa haki vimechangia sana kukua kwa mgogoro kati ya wakulima na wafugaji hasa katika Mkoa wa Morogoro. Unamkamata mtu shambani kwako, mnakamata ng'ombe anakuja Afisa Kilimo anafanya mahesabu ya hasara uliyopata anaitwa kwenye usuluhishi mwenye ng'ombe anakataa. Mnaondoka mnapelekwa Mahakamani, mkifika Mahakamani wananchi wangu wanasema kwamba ule umeshakuwa mradi tayari wa Mahakimu wa ngazi ya Wilaya pamoja na wale wa Kata,

hakuna kesi inayoshinda hata moja, wakulima wote wanashindwa. Unakuta mtu shamba lake hekari 10 limeliwa na wanyama lakini hakuna anayechukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaposubiri mpaka mambo yanakuwa mabovu, yanakuwa ni magumu ndiyo sasa tunaingilia matokeo yake ni kwamba wananchi wanakuwa wakaidi wanaanza kuwaona kwamba walinzi wao wa amani siyo ndugu zao, wanaanza ugomvi, ndiyo unasikia kwamba mwananchi kapigwa risasi kafa, ndiyo unasikia kwamba Askari kapigwa, ndiyo! Morogoro imekuwa mbaya zaidi, wamegombana Kambala, mtu wa bodaboda kauliwa kule, bodaboda wa Morogoro baada ya mazishi wakaamua kwamba na sisi kichwa cha mfugaji yeyote ambaye ataonekana Morogoro Mjini ni chetu, wakaanza kuua. Hata hivyo, wale ambao waliua wangeenda kukamatwa mara moja, wakapelekwa mbele ya haki, sidhani kwamba vijana wa bodaboda wangeanza kuua Wamasai kule mjini? Hii imekuwa siyo haki kwa akina mama wa Kimasai, siyo haki hata kwa Mmasai ambaye hakuhusika na lile jambo amekwenda kuuliwa. Mimi naomba vyombo vyote vya ulinzi na usalama vinaposikia kwamba kuna tatizo, nendeni mkamkamate yule mhusika, msiende kulinda wengine, kamata aliyehusika kwa sababu siyo jamii nzima imehusika kumuua mtu wa bodaboda mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba Mkoa wa Morogoro tuna matatizo, Morogoro Vijiji tuna matatizo, Mvomero kuna matatizo, Kilosa kuna matatizo, matatizo ya Kilosa ni kijiji cha Mabwegere ambacho kimeambiwa mipaka yake irekebishwe na irekebishwe kijiji mama kikiwepo na wao wawepo, hakuna anayechukua hatua hiyo. Mimi naomba Serikali isikie hilo na ikachukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni Kambala, Kambala kulikuwa na kijiji lakini ikafika mahali kuna mtu aliamua kusema kwamba Kambala imeongezeka mpaka imefika kwenye mradi wa mpunga. Kwa hiyo, ina maana kwamba mashamba ya mpunga, mashamba yote ya

Mgongola yamekwenda kwenye Kijiji cha Kambala. Ukitaka kulima unatakiwa ukakodishe sasa kutoka kwenye jamii ya Wamasai. Haikuwa hivyo, walikuwa wanaishi kwa amani tangu zamani, nani ameleta matatizo hayo Mwenyekiti? Tunaomba hilo liangaliwe na tulijue lakini naomba kusema kwamba hii hali ya hatari ambayo bado imesimama kwenye maeneo haya mawili ichukuliwe hatua mapema iwezekanavyo, Mabwegere Kilosa pamoja na Kambala kule Mvomero na kijiji cha Dala pamoja na Bwakila Juu na Bwakila Chini katika Jimbo la Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunaomba basi tuweke msimamo kwamba tunaenda kufanya upimaji wa vijiji vyote na matumizi ya ardhi kwa sababu sisi kama Wilaya hatuna hela, tunaomba msaada wenu kwa sababu tunataka amani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimuite Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa kwa sababu simuoni Mheshimiwa Chiligati.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu waliochangia kabla yangu kukupongeza kwa kukalia hicho Kiti. Tunaomba utukumbuke katika ufalme wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lililo mbele yetu siku ya leo lilianzia kwenye Kamati yetu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Nashukuru Bunge kwamba mlikubaliana na sisi kwamba tuunde Tume ambayo matokeo yake ndiyo haya tunayajadili siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya matukio ya migogoro kati ya wafugaji na wakulima imekuwa sehemu ya maisha ya Taifa letu. Kila baada ya miezi michache tunapata taarifa, tunasikitika halafu tunasahu lakini tunasahau kwamba yanaacha makovu mengi sana kwa watu wanaohusika, watu wanakufa, amani ni tete. Kwa hiyo, hii Kamati ilifanya kazi mwaka mmoja uliopita, nilishangaa imechukua muda wote huu bila ripoti yao kuletwa hapa Bungeni lakini kawia ufike. Nashukuru kwamba leo imeletwa hapa na napenda nimpongeze Mwenyekiti na Kamati yake kwa hii ripoti ya kina na uwasilishaji mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kunapotokea mgogoro wa wafugaji na wakulima, hulka ya Mtanzania ni kumlaumu mfugaji kama ndiyo mkorofi. Ng'ombe tunawahitaji, mashamba tunayahitaji, sasa tunapowalaumu wafugaji halafu huwaonyeshi eneo mbadala la kwenda kufuga nadhani hapa ni makosa, tunawaonea, wakafugie wapi? Sisi kama Kamati tumeishauri Serikali mara nyingi kwamba hili suala la wafugaji siyo la Wizara ya Kilimo peke yake, Wizara ya Maji inahusika, Ardhi, TAMISEMI, Kilimo, Usalama wa Taifa, Mambo ya Ndani, Mazingira, ningeweza kuendelea ungekuta kwamba ni *cabinet* nzima. Kwa hiyo, ushauri ambao tumekuwa tukitoa kwa Serikali ni kwamba ije na mkakati shirikishi ambao utahusisha Wizara, sekta na wadau mbalimbali kwa dhana nzima ya *multisectoral approach*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini uzoefu tunao kwa janga hili la Ukimwi. Ugonjwa huu ulipoingia nchini mwaka 1983 ilifikiriwa kwamba ni ugonjwa, kwa hiyo, Wizara ya Afya ingehusika lakini huu ugonjwa tulipoona kwamba pia unaleta matatizo ya kijamii, kiuchumi, kisiasa hatukuweza kuiachia Wizara ya Afya peke yake, tukawa na hii *multisectoral approach*, watu wote walihusika, wadau mbalimbali, *NGOs* na mafanikio tunayoyaona katika kupambana na Ukimwi yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na kujumuisha nguvu za taasisi mbalimbali. Kwa hiyo, ombi na wazo ambalo sisi kama Kamati tulikuwa nalo ni kuishauri Serikali kwamba tusing'ang'anie tu Wizara ya Kilimo, tunajua baadhi ya Mawaziri wamepoteza kazi kwa sababu ya mifugo lakini hili

ni suala la Serikali nzima waje na mpango shirikishi ili tuweze kutafuta jawabu la tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tulifanya ziara ya mafunzo Ethiopia. Kieneo Ethiopia ni kubwa kuliko nchi yetu na hata idadi ya watu wako 85,000,000 sisi tuko 45,000,000 na wanyama wanaowafuga wako wengi, maradufu kuliko wa kwetu lakini maeneo yanayofaa kwa kilimo na ufugaji sisi tunayo mengi zaidi kuliko Ethiopia. Tulipofika kule tukawauliza Wanakamati wenzetu, je, na wenyewe wana matatizo ya migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima? Wakasema hakuna kitu kama hicho. Tukawauliza wamefanikiwaje? Wakasema wakulima na wafugaji wote mahitaji yao ni sawa, wanahitaji maji, mkulima anahitaji maji, mfugaji anahitaji maji lakini pia wanahitaji ardhi inayofaa na ardhi inayofaa kwa kilimo ni ardhi inayofaa kwa mfugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wali-*identify* maeneo hayo, wakayapima, wakayagawa na wakaweka miundombinu stahiki. Mkulima akashawishiwa, akafundishwa na akawezeshwa kuwa mfugaji. Kwa hiyo, akawa mfugaji na wakati huohuo ni mkulima na ufugaji wenyewe wa kisasa na mfugaji vilevile akashawishiwa, akafundishwa na akawezeshwa kuwa mkulima. Kwa hiyo, hii inaitwa *agro-pastoralism*, mkulima huyohuyo ndiyo mfugaji. Sasa huyo mfugaji ana shamba, hawezi kuhama na mifugo akaacha mashamba yake, hivyo hili jambo kwa wenzetu halipo. Kama nilivyosema hii ziara ilikuwa ya mafunzo, ina maana ni mambo tunakwenda kutizama ni yepi yanaweza yakatusaidia hapa kwetu. Tatizo letu kubwa ni kwamba maeneo yetu hayajapimwa. Leo asubuhi tumeambiwa vijiji vilivyopimwa hapa Tanzania ni asilimia kumi tu. Najua kwamba inahitaji rasilimali fedha lakini muhimu zaidi ni kwamba tuwe na sera. Kusema kweli haitatokea hata siku moja Serikali ikasema ina hela za kutosha lakini tukiona hili ni tatizo kubwa, tupime nchi, tutenge haya maeneo na labda tumfundishe mkulima awe mfugaji kusema kweli tunaweza tukasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunatenga bajeti kubwa kwa ajili ya chakula cha kupambana na njaa kwa wenzetu ambao wanaishi kwenye maeneo ya ukame lakini pia *NFRA* tunatenga hela nyingi sana na mwaka jana ilikuwa shilingi bilioni thelathini na mbili na mwaka huu ni shilingi bilioni mia moja na kumi. Nikawa najiuliza, *suppose* tunafanya uamuzi mgumu kwamba tujenge mabwawa au majosho kumi kila mwaka kwenye maeneo ambayo ni kame, tuchukue kiasi cha pesa hizi na tutafute na zingine ili tujenge haya mabwawa. Mimi nadhani katika muda ambao si mrefu sana tunaweza tukawafanya wafugaji wakae hukohuko, kwa sababu kinachowaondoa huko kwenye maeneo yao ya asili ni kutafuta maji na malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la *NFRA* kutenga shilingi bilioni mia moja na kumi, azma ya kwanza ilikuwa tuwe na akiba ya chakula kwa ajili ya watu wenye njaa lakini sasa Serikali imejigeuza kuwa ndiyo soko kwenda kununua mazao ya wananchi halafu hatuwalipi ambapo tungejikita katika kutafuta masoko…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii iliyoundwa na Spika wetu kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la msingi katika nchi yetu na kama hili hatujakabiliana nalo, tutapata matatizo katika mambo mengi. Tatizo kubwa ni usimamizi kwa sababu inapofikia hali mpaka watu wanapoteza roho

na sisi tunaona ni jambo la kawaida tu, mtu anasema aah waliokufa si Wamasai, si wamepeleka ng'ombe kusudi, *no,* hivi ni vitu ambavyo tunahitaji kuvisimamia. Wanauwawa wakulima mtu anasema aah sasa si wanafanya zogo wenyewe, haiwezekani, lazima Serikali ichukue nafasi yake ya ku-*protect* maisha ya watu. Huwezi ku-*protect* maisha ya watu bila kuwa na utaratibu. Ardhi kweli ni mali ya Watanzania wote lakini si katika ujumla wake ati, ni katika sehemu ambayo mtu kapewa kaambiwa hii ni yako. Sasa kama hukupima ardhi ukampa mtu, matokeo yake unamfanya awe katika hali ya hatari kumbe ungeweza kumsaidia. Tunaiomba Serikali, zoezi hili la kupima ardhi na kuwamilikisha watu lifanywe kwa haraka kwa sababu jambo hili limewezekana katika nchi nyingi duniani. Ni kweli nchi yetu ni kubwa lakini si kubwa sana ya kuwa hilo haliwezekani, tatizo ni usimamizi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema vitu viwili vinatuumiza sana, kwanza ni kupuuza, yaani anaona *it is a laissez faire* wacha iende tu. La pili ambalo ni *syndrome* mbaya sana ni rushwa. Hii rushwa imefika mahali mpaka sasa kila mtu anaona mimi naweza kuchukua rushwa nikaachia jambo hili likaharibika wala hakuna mtu wa kunigusa. Bahati nzuri tuna vyombo vingi tulivyoviunda vinalalamikia juu ya jambo hili lakini ukitizama katika uhalisi wa mambo, bado rushwa ni tatizo kubwa hasa katika maeneo haya ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima ilinde watu, kama haikulinda watu watakuwa katika hatari kubwa. Mfano, hii Kamati moja katika kazi yake ilitakiwa pia iangalie wawekezaji. Wawekezaji wamepewa ardhi na ile ardhi maana yake waitumie na wengi wao wanaitumia kwa kilimo. Mambo mawili, ukitumia ardhi kwa kilimo maana yake lazima upate pesa ya kuendeleza ardhi hiyo. Pesa hizo wengi wa wanyonge hawa Watanzania wenzetu hawa waliowekeza wanachukua benki. Mkulima analima, *it is a risk,* mara nyingine anakosa mvua, anakosa mambo chungu mzima lakini anachukua benki mkopo ili aweze kufanya lile ambalo alikusudia kwa kutafuta ile ardhi aliyopewa. Kama hukumlinda, utapata tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nataka nitoe mfano hai wa wakulima wa miwa. Mwaka 1996 wakulima wa miwa walikuwa wachache sana ni kama 5000 leo tunao wakulima wasiopungua 15,000, wale wakulima wadogo wadogo tu wa miwa. Mwaka 1996 sukari ilikuwa ikizalishwa hapa tani kama 96,000 hivi, leo inazalishwa tani 320,000. Wanaozalisha sukari hii ni wale ambao tumewapa ardhi walime, wajenge kiwanda cha kutengeneza sukari, wauze sukari hiyo hapa. Nini kinachofanyika? Serikali inashindwa kama nilivyosema mwanzo kuwalinda watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnasikia katika mitaa watu wanaleta sukari wanavyotaka, wale wakulima wawekezaji ambao ndiyo tunawakaribisha kwetu waje wawekeze ili watu wetu wapate ajira na nchi yetu ipate mapato wanashindwa kuuza sukari yao kwa sababu tumeruhusu. Hatuwalindi na wanaotoa ruhusa hii bila shaka itakuwa ni Serikali, ama kwa makusudi au kwa kuona jambo linaharibika bila kulisimamia. Huwezi kuniambia mimi nikaamini hata siku moja kuwa katika mwaka huu ulioisha wa 2014, sukari iliyoingizwa nchini ni tani 150,000 na hapakutolewa kibali hata cha kuingiza kilo moja. Sukari hiyo inaonekana hapa ndani ya nchi na viongozi wanaiona, sasa sisi tunajiuliza mambo mawili tu, wanakusudia kuwaangamiza hawa wenye viwanda na mashamba ya sukari au ni kwa sababu wanapata fungu lao, wanapata pesa kwa wauzaji hawa wanaoleta sukari bila vibali ndiyo maana wananyamaza kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *it is even more dangerous* kuona baadhi ya wauzaji hawa wa sukari wana ujanja wa ajabu sana ya kuwaangamiza hawa wawekezaji. Kuna sukari inaletwa kutoka nje inafikia Zanzibar kwa sababu labda aliyeleta sukari amesajili biashara yake Zanzibar, anatoa ndani ya meli anapakia ndani ya lori anaingiza ndani ya meli nyingine analeta Dar es Salaam, ammbo yameenda kienyeji tu hivyohivyo. Serikali inakosa mapato au mnachukua chochote wakubwa niwaulize kwa wafanyabiashara hawa, mnagawiwa chochote hivi? Haiwezekani kama hamchukui chochote mnaachia na kwani sukari hamuioni katika

maduka mpaka mnanyamaza kimya au mnasema hamna habari au muunde Tume?

**MBUNGE FULANI:** Ufisadi tu huo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Kwani hamuioni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasikitika sana, usimamizi katika nchi yetu umekuwa wa kutisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye mada sasa nataka nizungumzie ardhi na wafugaji. Wafugaji tunahitaji kuwaelimisha. Mimi sidhani kama ni jambo la fahari sana kumuachia mfugaji anamiliki ng'ombe 5000, mtu mmoja anamiliki ng'ombe 5000. Mimi niliwahi kwenda mara moja kule Ihefu kwa kazi nyingine lakini nikaona ile kasheshe iliyopo ya wafugaji. Tuwaelimishe wafugaji wetu kuwa fahari si kuwa na ng'ombe 5000 ni kuwa na ng'ombe ambao watakuzalishia tija. Mtu ana ng'ombe 5000 lakini ukiwatizama ng'ombe wengine kwa macho tu utahesabu mbavu zake zote ndani ya mwili ng'ombe huyo, sasa wa nini kuwa na ng'ombe wa namna hiyo? Tukiwaelimisha wakaweza kufuga ng'ombe kidogo wenye kuwa na tija kubwa, wao wenyewe watafaidika, watapata pesa, watajenga na watafanya kila kitu na ng'ombe wale wachache watakaowafuga, itawasaidia hata kuweza kuwalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama una ng'ombe 5000 maana yake unahitaji eneo kubwa sana kuweza kuwalisha na si mtu mmoja basi. Ukienda kwa Wasukuma rafiki zangu wapo watu wenye ng'ombe wa kiwango hicho, ukija kwa Wamasai, siku moja mtu mmoja wa Zanzibar alijisifu mbele ya Mmasai akasema mimi nafuga. Akaulizwa una ng'ombe wangapi? Akasema nina ng'ombe wanne bwana. Akaambiwa wewe una wazimu ng'ombe wanne au mia nne? Akasema wanne. Sasa kwetu sisi Zanzibar kufuga ng'ombe wanne ni mfugaji huyo lakini kwa huku Bara ng'ombe wanne ni nyama ya kula kwenye sherehe ya harusi tu. Sasa ndugu zangu tuwaelimishe wafugaji wetu kuwa hoja

si kufuga ng'ombe wengi ni kufuga wachache ambao watazalisha tija. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwaelimishe wakulima na wafugaji wetu kuwa nchi yetu hii, kufuga au kulima isiwe ndiyo sababu ya kutoana roho. Kama vijijini kuna watu wanatumia mamlaka yao kwa kuwapa watu ardhi kienyeji ili watu wauwane, hebu anzeni na hao! Anzeni na viongozi hao wa vijiji na ndiyo wenye matatizo makubwa. Mimi siamini kuwa mtu anakwenda akapata ardhi kirahisi rahisi lazima katoa pesa mbili, tatu, mtu mmoja tu anasema tumekaa Mkutano wa Kijiji kumbe haujakaliwa, mtu anapata ardhi wenyewe wananchi wakija wakiigusa ni vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, lazima tuwaelimishe wananchi wetu wanaokaa katika maeneo ya ardhi za uwekezaji. Ukishampa mtu ardhi, hutakiwi tena kwa mujibu wa taratibu za kimataifa kumbugudhi tena kwa sababu ulimpa kwa kufuata sheria. Sasa mwekezaji umempa ardhi halafu unamgeukia unakwenda kuchukua ardhi, akisema, unasema yule Mzungu. Hata kama Mzungu au kabila gani lakini si ulimpa? Nchi yenye utawala bora kama yetu si jambo la fahari hata kidogo kuwa na hali kama hiyo. Kama tunaona taabu kuwapa wawekezaji moja kwa moja tubadilishe Sheria yetu ya Uwekezaji, iwe mwekezaji hawezi kuwekeza mpaka apate *partnership* ya mzalendo. Ikitokea hiyo tutaondoa matatizo mengi tu lakini uhasama huu mimi naomba Serikali yetu iwe makini sana, ukidharau mwiba mguu utakujaota tende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Capt. John Chiligati atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikuombe radhi uliniita sikuwepo nilichelewa nilikuwa kwenye kikao kingine cha

mambo ya Bunge hayahaya lakini nakushukuru kwa huruma yako nafasi yangu umehifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niipongeze Kamati Teule imefanya kazi nzuri, imeleta mapendekezo mazuri ambayo mimi niseme tu mwanzoni kabisa nayaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Kamati kwamba nchi yetu tumebarikiwa tuna ardhi kubwa sana, kilometa za mraba laki tisa na nusu ukiondoa zile zenye maji, ardhi inabaki karibu laki nane, Mungu ametupa eneo kubwa ambalo ni jambo zuri. Jambo zuri usipolipanga vizuri linageuka badala ya kuwa baraka linakuwa balaa. Sasa hili jambo zuri kwamba tuna ardhi kubwa kwa sababu ya mipango yetu siyo mizuri linataka kugeuka kuwa balaa badala ya baraka. Tatizo letu tu ni kwamba ardhi hii imekaa kiholeholela, nakubaliana kabisa na Kamati Teule, imekaa kiholelaholela. Kitu kikishakuwa holela basi kila mtu mahali popote atafanya jambo lolote, matumizi yanagongana ndiyo hii migogoro tunayoiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati kwamba, kwanza ardhi yetu ipangiwe matumizi bora ya ardhi. Kuwe na mpango wa Kitaifa, Mkoa, Wilaya, Kijiji, maeneo yote yabainishwe, ya kilimo yabainishwe na mipaka yake, ya ufugaji yabainishwe na mipaka yake, ya viwanja yabainishwe na mipaka yake, ya hifadhi yabainishwe, ya misitu yabainishwe, kila eneo libainishwe na mipaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, sasa lipimwe, likishapangwa linapimwa na kuwekwa mipaka. Kwa hiyo, kila shughuli eneo lake linawekewa mipaka yake. La tatu, wale wenye maeneo yale wamilikishwe ili wapate hati miliki. Tulishafanya hayo, tukisharasimisha namna hiyo, migogoro mingi itapungua kama haitakwisha kabisa kwa sababu kila mtu anajua eneo hili ni la mifugo na mipaka yake ni hii. Hili ni shamba la fulani, mipaka yake ni hii, hili la shughuli hii,

mipaka yake ni hii na sheria inalinda pale. Kwa hiyo, mtu kutoka katika eneo kwenda eneo 'B' anavunja sheria na anakamatwa anashughulikiwa. Kwa hiyo, hilo naunga mkono kabisa Serikali ifanye hima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini iko changamoto, kwa nini upimaji na umilikishaji hauendi haraka sambamba na matakwa ya Watanzania. Sasa hivi kila mkulima, kila mfugaji anataka eneo lake apate hati. Changamoto kubwa ni mbili, ya kwanza ni gharama. Sasa hizi kilomita za mraba laki nane, kuzifanyia mpango wa matumizi, kuzipima, kuzimilikisha ni gharama kubwa sana. Sasa hivi tunategemea bajeti ya Serikali lakini angalia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi angalia bajeti inayopata ni kidogo sana, haiwezi! Halmashauri zetu na sisi wote ni Madiwani, tuna fedha kiasi gani za kupima ardhi katika Wilaya zetu, haiwezekani! Hata kile chombo ambacho sasa hivi ndiyo kinachosimamia cha MKURABITA, bajeti yao ya kupima ardhi ya maendeleo kwa mwaka ni shilingi bilioni tatu! Sasa ardhi kilomita laki nane, unazipima kwa shilingi bilioni, haiwezekani, itatuchukua miaka mingi, mingi tukienda na utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza na haya mapendekezo nitayaandika ili kesho tunapopitisha mapendekezo ya Kamati na haya mapendekezo yangu yajadiliwe. La kwanza, tuanzishe Mfuko Maalum wa Urasimishaji wa Ardhi. Tunaweza tukasema tu Mfuko wa Urasimishaji Rasilimali za Watanzania na rasilimali kubwa kabisa ni ardhi. Zipo rasilimali nyingine za biashara ndogo ndogo na wenyewe Mfuko utawasaidia hata hawa Wamachinga, lakini uwe ni Mfuko wa Urasimishaji ili vyanzo mbalimbali, ambavyo sheria itavitambua, vichangie huo Mfuko ili kazi ya Mfuko huo iwe ni moja tu, urasimishaji wa rasilimali za Watanzania na hasa wanyonge. Mfuko huu ukae benki, Serikali ipeleke benki, iwe ni dhamana, halafu zile benki zinatumia hela zao kukopesha mara tatu ya zile fedha za dhamana. Halmashauri ziende zikakope huko, zikishamaliza kurasimisha vile viwanja kama ni mashamba ziko gharama ambazo watapata wanarudisha kwenye Mfuko huo ili uwe

wa kuzunguka *(Revolving Fund)*. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sasa hivi ina Mfuko huo, lakini una fedha kidogo mno halafu hazizunguki. Wakishakopa Halmashauri hawarudishi lakini zikikaa benki, mabenki wana utaratibu wao wa kufanya fedha zirudi na zitarudi. Kwa kufanya hivi Mfuko huu utaharakisha upimaji na umilikishaji uende harakaharaka kuliko kutegemea bajeti ya Serikali. Hili ni pendekezo ambalo nitaliandika nililete ili kesho vilevile tulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili, ni chombo cha urasimishaji. Sasa hivi chombo cha urasimishaji ardhi ni MKURABITA, ni kidogo mno, kina watu 27 tu. Watu 27 watapima kweli kilomita laki nane! Kinapata fedha kidogo mno, shilingi bilioni tatu, halafu hakina nguvu ya kisheria ya kumbana mtu yeyote katika urasimishaji. Kwa hiyo, napendekeza MKURABITA huyu tumfanyie mabadiliko makubwa kabisa ili tuwe na Tume ya Urasimishaji, ni chombo ambacho sasa kitakuwa kina nguvu ya kisheria, ni chombo ambacho kitakuwa kinawasimamia hawa wanaorasimisha, ni chombo ambacho kitasimamia hata huo Mfuko ili kweli kazi hii iende tunavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiambie tu Serikali, hii Katiba Mpya kama itapita, mle ndani ile Katiba imesema kwamba Serikali ipime ardhi, iwamilikishe, iwape hati miliki wakulima na wafugaji ili wawe na uhakika na mali yao na watumie zile kama dhamana kukopa katika mabenki. Nina hakika wakulima na wafugaji watafanya juu chini Katiba hii ipite ili haya yatekelezeke! Kwa hiyo, Serikali msipojipanga vizuri, msipopima na kumilikisha, mtapelekwa Mahakamani mmevunja haki za msingi za hawa wakulima na wafugaji, kwa hiyo, ni lazima tujiandae, kifedha kuwa na Mfuko na chombo kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imelia nimalizie na la mwisho, nakubaliana na pendekezo la Kamati Teule, kwamba yale maeneo ambayo yameshapitwa na wakati, ile hifadhi yenyewe imeshakwisha. Unakuta eneo la

hifadhi lakni kuna vijiji mle, kuna shule, kuna barabara, kuna zahanati, naomba sana Serikali hayo maeneo tuyaache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu, watu wameongezeka, shughuli zimeongezeka, hata mipaka hii ya hifadhi iangaliwe upya. Kule kwangu nina mfano, mwaka 1995, hifadhi ilitoka ilikokuwa ikasogea kwenye vijiji. Sasa wanavijiji wameongezeka sana, wanaomba mpaka urudi ulivyokuwa mwaka 1995. Tumepeleka ombi Serikalini, nimemkaribisha Waziri, nadhani atakuja ama Naibu Waziri, aje aone. Vitu kama hivi Serikali tusiwe *rigid*, tusikatae kwa sababu ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tena naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWONGOZO**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa *list* ya wachangiaji ambayo tumeipata, tumeona wako watu 26 *so far*. Mimi niombe mwongozo wako kuhusu utaratibu unaotumika kuandika hayo majina kwa sababu kuna watu hawajawahi kuchangia hata mara moja tangu tumeanza lakini kuna watu ambao wameomba kuchangia asubuhi hata kabla Bunge halijaanza saa tatu, wamewahi sana kwa sababu hii ripoti ni muhimu sana kwa maeneo yao. Mfano, mimi ambaye natoka Babati, ripoti imenigusa kabisa nimewahi leo asubuhi lakini hata jina halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, ni utaratibu gani umetumika kuandika hayo majina na

orodha ni hiyo tu au kuna orodha nyingine tujue. Kwa sababu hili *group* lote unaloliona hapa, majina hayapo na tumewahi asubuhi kabisa, tunaomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitajibu baadaye kwa sababu nimeingia Mezani na orodha nimeikuta hapa, jibu nitawapa baadaye. Tuendelee, Mheshimiwa Ishengoma!

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia taarifa ambayo imeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ni nzuri sana na naiunga mkono. Wameweza kuichambua na kuiangalia vizuri, wamekwenda kwenye Mikoa mbalimbali na wameweza kuona matatizo yaliyopo na kuwahoji na kupata mambo mazuri. Kwa kweli ni taarifa nzuri sana naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba na wewe nikupe pongezi, nilikuwa sijakupa pongezi, pamoja na Mheshimiwa Kidawa kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wetu na kuendesha Bunge letu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo hasa ya wakulima na wafugaji yamekuwa ya muda mrefu na hasa kwenye Mkoa wa Morogoro nikizungumzia upande wa Mvumero na Wilaya zingine zote za Morogoro, Kilosa, Morogoro Vijijini, Ulanga pamoja na Kilombero, imekuwa ni matatizo makubwa sana. Nashukuru sana kuwa njia ya kutatua haya matatizo hasa kwa Wilaya ya Mvomero imeanza kuonekana ingawaje bado ni matatizo makubwa. Serikali kwa kusaidiana na Mbunge wao na viongozi wengine wote wa Serikali, wameanza kupima vijiji vya Wilaya ya Mvomero ingawaje bado kuna matatizo, tunayaona mara kwa mara, watu wanapigana, watu wameuana, watu wanafunga njia mpaka barabara haipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda Kilosa, tumeona vijiji vya Mbigili mpaka sasa hivi navyoongea ni msimu wa kilimo lakini wakulima wameshindwa kulima kwa sababu ya matatizo ya wakulima na wafugaji. Mabwegere, kwa upande wa mipaka, imekuwa matatizo lakini naamini, tatizo kubwa sana ni kwa sababu, ardhi haiongezeki, watu wanaongezeka, mifugo inaongezeka. Kwa hiyo, hapa, jambo la kutatua matatizo haya, hasa ni matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umefika, tumesikia matatizo ya Kiteto, tumesikia matatizo ya Mkoa wa Pwani, tumesikia matatizo ya Mikoa mingine mpaka Kagera. Naomba sana Serikali iweke mkakati wa kipaumbele wa kuona jinsi ya kutatua matatizo haya hasa ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Nashukuru sana Kamati imefanya mambo mazuri sana, imetoa mapendekezo yao ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi. Naomba sana tuyaangalie, kusudi tuweze kuwanusuru wananchi wanaoteseka, wananchi wanaopigwa, wananchi wanaokufa! Nawapa pole kweli wote waliopoteza maisha yao. Juzi juzi mmewaona wengine wamefunga bandeji lakini ndiyo hivyo, kwa hiyo, naomba mapendekezo ya Kamati yafuatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa lingine, naomba sana, wafugaji na wakulima waheshimiane, wakiheshimiana wakakaa pamoja kama Kamati ilivyosema, kwa kutumia viongozi wa kimila, wanaweza wakatatua matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naliunga mkono kabisa, ni wafugaji waweze kupata elimu, Mabwana Shamba tunao, Maafisa Kilimo tunao, Maafisa Mifugo tunao, kama hawatoshi, tuajiri zaidi! Kila kijiji waweze kupata Bwana Mifugo na Bwana Kilimo kusudi tuweze kutatua haya matatizo kwa kuwapa elimu wafugaji na wakulima waweze kufuga ufugaji wa kisasa na wenye tija, mifugo michache ambayo inatoa mazao yenye tija. Kwa

mfano, ng'ombe mmoja ukimlisha vizuri anaweza akatoa maziwa lita 36 kwa siku. Kwa nini uhitaji ng'ombe wengi kama ng'ombe mmoja anatoa maziwa lita 36 kwa siku? Kwa hiyo, nawaomba sana tuweze kuwapa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu nyingine ambapo hawa Mabwana Shamba na Mabwana Mifugo na viongozi wengine ambao wanaweza kuwapatia elimu wafugaji wetu, ni kuhusu malisho mazuri ambayo yanaweza kuzalishwa kwa urahisi. Mbegu zipo, naamini Nane Nane huwa mnakwenda, mnakwenda kwenye tafiti, *research centers,* kuna mbegu ambazo tunaweza tukazitumia kwa kupata malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo tumeliona kwa wafugaji, ingawaje tunasema wanahamahama, wafugaji tunawapenda, wakulima tunawapenda, kwa sababu wote tunashabihiana. Wakulima wanalima chakula, wafugaji na wenyewe wanapata chakula, wafugaji wanafuga tunapata maziwa, nyama na tunapata mbolea. Kwa hiyo, naomba tuwatimizie mahitaji yao kwa sababu kilio cha wafugaji kimekuwa kikubwa na ndiyo kinachopelekea matatizo na migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ni Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza ya Ardhi naomba yatende haki. Mara kwa mara likitokea tatizo kwa wafugaji kuhusu ardhi au kuhusu mambo yao ya mifugo, *experience* yangu wafugaji ndiyo wanaoshinda na yenyewe hiyo inatokana na Mabaraza ya Ardhi. Kwa hiyo, naomba sana tuyaangalie. Naiomba Serikali yangu, iweze kuona ni jambo gani la kufanya kusudi tuweze kutatua haya matatizo ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye utunzaji wa mazingira, mifugo imekwenda kwa wingi sana kwenye mabonde! Wakienda kwenye vyanzo vya maji, maji yanakauka tumeona bonde la Ihefu, sasa hivi bonde la

Kilombero. Kwa hiyo, nawaomba sana upande wa Serikali tuweze kusimamia vizuri kuona tunafanyaje kusudi kuepukana na migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Machael Laizer.

**MWONGOZO**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Nimemuita Mheshimiwa Michael Laizer, baadaye.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba mwongozo.

**MWENYEKITI:** Nasema naomba ukae nimemuita Mheshimiwa Michael Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mwongozo baada ya mimi kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie taarifa hii. Kwanza niwapongeze sana Kamati, wamefanya kazi kubwa, taarifa yao kwa kweli ni nzuri, haijaegemea upande wowote, imetenda haki, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, naomba suala hili tusilifanye la kisiasa kama ilivyo kule kwenye vijiji, kwenye Majimbo, hapa tusifanye jambo la siasa. Tusifanye jambo la siasa kwa sababu jambo hili watu wengi wamepoteza maisha, watu wengi wamepoteza mali zao, makazi ya watu yamechomwa, yameteketezwa, kwa hiyo, siyo jambo la kuweka siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Serikali wamenyamaza kimya kwa muda mrefu. Kwa sababu kuna Tume mbalimbali zimesomwa na Kamati, Tume ya Shivji, Tume ya Rais ya kuangalia masuala ya ardhi, Tume ya Tokomeza, zote zimeleta taarifa za Tume zao. Kamati wameeleza wametoa mapendekezo mazuri lakini hayajafanyiwa kazi. Naomba kwenye Bunge hili, taarifa na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati yafanyiwe kazi ili wananchi tena wasiuane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu, maeneo ambayo hayajatekelezwa, mgogoro wa ardhi katika kijiji cha Kambala, ni kijiji chenye hati miliki lakini kimevamia na ile hati miliki yake haijazingatiwa, haijaonekana kwamba ni hati, haijaonekana kwamba kijiji kimepimwa, sijui upimaji huu sasa tunaotaka ni upimaji wa aina gani kama upimaji uliotangulia hauheshimiwi? Kijiji cha Mabwegere, kilichoko Wilaya ya Kilosa, kina hati, kimevamiwa bado Mahakama imewapa kijiji haki lakini bado ile haki yao pamoja na hukumu ya Mahakama hayajazingatiwa. Emborey ya Murtangos, Mahakama imetoa hukumu lakini bado Serikali yenyewe ndiyo inavunja sheria na kutaka kuwapeleka wakulima katika maeneo hayo. Naomba maeneo yote hayo matatu, ndiyo yapewe kipaumbele, yafanyiwe kazi haraka sana na uamuzi ufanyike katika hayo maeneo matatu ambayo watu wamekufa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo, nashangaa wakulima wakisema kwamba wafugaji wapunguze mifugo lakini bado mwekezaji mmoja anapewa heka elfu hamsini lakini halionekani kwamba eneo hili ni eneo kubwa kwa mwekezaji mmoja. Hivi kwa nini unaona kwamba mifugo ni mingi kuliko eneo hili lote ambalo linamilikiwa na mwekezaji mmoja, unamuona mfugaji ndiye amechukua eneo kubwa. Naomba na maeneo hayo ya wawekezaji ambao nao wamechukua maeneo makubwa yaangaliwe na hata wakulima. Kama ni kusema kwamba tupunguze mifugo ni lazima wakulima nao waangaliwe kwa sababu na wenyewe nao wanahodhi maeneo makubwa, maeneo hayo nayo yapunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa vijiji ni lazima na ni lazima uheshimiwe. Bado sijui kwa nini kuna mgogoro katika maeneo haya! Mkoa wa Arusha, Kilimanjaro, kuna wafugaji na wakulima; kwa nini wasigombane? Kwa nini wasiuane? Nilisema wakati mwingine tuangalie kuna tatizo gani hapa Morogoro; kwa sababu sisi tuna wakulima wengi tu na wafugaji lakini hakuna mauaji, wala hakuna ugomvi, tunaheshimiana. Lazima na hawa waheshimiane, wakulima wawaheshimu wafugaji na wafugaji wawaheshimu wakulima na kuona kilimo ni mali, ndiyo tegemeo, ndiyo uchumi wao. Kwa hiyo, ni lazima waheshimiane, bila kuheshimiana kwa kweli itakuwa ni vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu angalizo, tunaona wafugaji katika nchi hii ni watu ambao wamenyanyasika sana, inaonekana si Watanzania. Pamoja na kwamba wafugaji ni wengi, lakini kabila moja la Wamaasai ndiyo wamekuwa tatizo katika nchi hii. Tunataka tujue kwa nini makabila yote yaliyoko Tanzania, sehemu kubwa ya makabila wanamwona Mfugaji Mmaasai ndiyo tatizo katika nchi hii?

Nipende kusema kwamba, Wamaasai ni Watanzania kama makabila mengine, wanastahili nao kutumia ardhi iliyoko katika nchi hii kama wafugaji wengine na kama wakulima wengine.

Naomba hili Serikali ilisikilize kwa makini, hatutaki tena umwagaji wa damu. Mapendekezo mengi mmepewa na Kamati, mkiyafanyia kazi nadhani mgogoro utapungua na wakulima na wafugaji wataheshimiana. Bahati mbaya sana, viongozi walioko ngazi ya chini, walioko mkoani na walioko wilayani, ufugaji umekuwa ni *deal*. *(Makofi)*

Aibu kabisa ukimsikia *DC* anawapeleka wakulima katika maeneo ya wafugaji na kwenda kusimamia eti walime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja; kule kwetu kuna mwekezaji mmoja alipelekwa kuwekwa katika eneo la malisho, ambayo yanatumiwa na Wilaya ya Siha na

Wilaya ya Longido. Amewekwa pale aanzishe *National Park*. Sijawahi kusikia *National Park* ya mtu mmoja tena mwekezaji! Hakuna ng'ombe kuingia, hakuna mtu kuingia, yaani hakuna tofauti, ni Sheria za *National Park,* tena bila kuulizwa sisi.

Naomba Waziri wa Ardhi na Waziri wa Mifugo, nendeni mkaangalie eneo hilo, kwa sababu huko nako umeanza mgogoro. Amechomewa hiyo kambi yake na magari na bado mgogoro huo utaendelea. Mwekezaji huyo aondolewe pale, asipoondolewa bado mgogoro utaendelea, kwa sababu yuko katika eneo la malisho la miaka na miaka. Eneo la Endarakwai, panaitwa *Endarakwai Farm* ambapo vijiji viwili vya Wilaya ya Siha kwa Mwanri na vijiji viwili vya Wilaya ya Longido, Wabunge wawili. Wapiga kura wetu wamenyang'anywa eneo ili mwekezaji kutoka sijui Marekani sijui Uingereza ndiyo ana hati miliki ya eneo la malisho, sisi tuondoe mifugo yetu katika eneo hilo! *(Makofi)*

Kadhalika na wawekezaji walioko katika maeneo mengine ambao wanawanyanyasa wafugaji na hilo liangaliwe watoke. Ukienda Babati ni hivyo hivyo, kuna wawekezaji ambao wamemilikishwa eneo, watoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Gervas Mbassa.

## MWONGOZO WA MWENYEKITI

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Sabreena Sungura!

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, ningependa Bunge lako litambue kwamba, Bunge letu linaendeshwa kwa utaratibu na uzoefu wa Bunge hili na Mabunge mengine Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu wa Bunge hili unaonesha mtu akiomba kuchangia, akipata mara moja au mara mbili, *next time* wanaokuwa *considered* ni watu ambao hawajawahi kuchangia hata mara moja. Ninasikitika hata wale Mawaziri Vivuli wenye dhamana, Mheshimiwa Halima Mdee ni Waziri Kivuli wa Ardhi, lakini jina lake halimo kabisa kwenye *list*. Mimi ni Naibu Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na watu wengine ambao ni *senior* kabisa humu ndani hawamo kwenye *list*.

Sasa tunaomba utaratibu, kuna mtu ameomba mwongozo hapa ukasema utatoa mwongozo baadaye, lakini unavyozidi kuvuta muda unapoteza haki za watu. Kuna Mheshimiwa Esther Matiko, kuna Mheshimiwa Pauline Gekul, kuna Mheshimiwa Cecilia Paresso, wote hao kwenye *list* hawamo. Kuna akina Silinde, akina Suzan Lyimo, wamechangia zaidi ya mara mbili, sisi wengine hatuonekani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sabreena…

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Kiti chako kinafanyaje maamuzi Mheshimiwa Mwenyekiti, kinayumba, Makatibu wako wanatuangusha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sabreena, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge, orodha inaletwa na Vyama na inaletwa kwa uwiano.

*(Hapa Wajumbe fulani walipiga kelele kuonesha kutokubaliana na Kiti)*

**MWENYEKITI:** Naomba nisikilizeni, naomba mheshimu Kiti. Uwiano ni watatu kwa mmoja. Nimeanza watatu, nikaita mwakilishi kutoka *CUF,* nimerudia watatu nimemwita mwakilishi kutoka CHADEMA. Majina ninayo na mmeshaniletea vikaratasi vingi hapa, sasa mimi siwezi kuvunja Kanuni kwa kuita Mjumbe ambaye hayuko kwenye orodha hii. Naomba tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, tuambie Mbassa ametoka kwenye karatasi ipi?

**MWENYEKITI:** Naomba ukae Esther. Esther Matiko naomba ukae!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Nawaomba mkae!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hiyo orodha tuione.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul naomba ukae, naomba uheshimu Kiti. Naomba Dkt. Mbassa uendelee.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hata mimi nilipata wasiwasi kidogo na mimi nilikuandikia ki-*note*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuishukuru Kamati na kuipongeza kwa kazi kubwa waliyoifanya.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Dkt. Mbassa, siyo kweli, ndiyo wewe uliyekuwa unafuata, siyo kwa kuniletea ki-*note*. *(Kicheko)*

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hivyo hivyo tuendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Wanakamati, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Ninajua ni sehemu ndogo tu ya Wilaya na Mikoa waliyoweza kuizungukia kubaini matatizo ya ardhi, mifugo, maji na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikijiuliza mara nyingi lakini nikaja kugundua kwamba, msingi wa mambo

haya yote ni Serikali kutokuweza kueleza bayana mipaka ya Viongozi wetu tunaowachagua. Nimekuwa nikijiuliza mara nyingi Wenyeviti wetu wa Vijiji, Wenyeviti wetu wa Vitongoji, je, wanapewa mafunzo kujua majukumu yao? Wajumbe wa Serikali za Vijiji wanaochaguliwa wanapewa mafunzo kujua majukumu yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya ardhi imekuwa ikijitokeza pale Wenyeviti wa Vijiji wanapoungana na Wenyeviti wa Vitongoji katika kuunda ile Kamati ya Uchumi, Mipango na Fedha, ile Kamati Ndogo na matokeo yake wanauza ardhi na wananchi hawapewi taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuuliza mara nyingi hapa na nimekuwa nikifuatilia katika chaguzi zote zilizopita kama watu hawa wamewahi kujengewa uwezo; inaonekana hakuna. Ikumbukwe kwamba, migogoro hii inapoanza au kesi hizi zinapoanza, wao ndiyo wanageuza kiti tena kuwa mahakimu wa kuweza kusuluhisha migogoro hiyo. Kwa hiyo, hapo hakuna nafasi pekee itakayojitokeza ya kuweza kukwepa rushwa katika mazingira haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya ardhi hususan ya wakulima na wafugaji, inasababishwa na Viongozi wetu. Leo hii ni jambo ambalo halipingiki, unamkuta mfugaji ana nguvu, ana *power*. Pale inapotokea tatizo, mfugaji anao uwezo wa kuweza ku-*combat* kile kikao na matokeo yake maamuzi yakawa ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ningeliomba Serikali iweze kwenda *deeper* zaidi kwa ajili ya kuwasaidia watu hawa. Elimu itolewe na Viongozi hawa wafundishwe mipaka yao ya kazi. Sehemu nyingine inafika mahala hata maamuzi yanayotolewa na Viongozi wetu yanakuwa siyo sahihi na inakatisha tamaa pale mfugaji anapojitahidi kufuga kwa nguvu zake zote na uwezo wake wote, lakini mara mifugo yake inapoporwa anachokuja kufidiwa aidha ni mifugo kidogo au kutoipata kabisa. Katika kauli hiyo, naomba niwape pole akina mama wa pale Morogoro, wale wajane, waliochukuliwa mifugo yao ikapelekwa Kituo cha

Polisi lakini inaonekana wanapewa mifugo kidogo sana tofauti na iliyotolewa kwenye mazizi yao; poleni sana ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajiuliza, kama vyombo vinavyopaswa kutenda haki, kulinda raia na mali zao, leo hii ndiyo wamechukua mifugo na mifugo inapatikana kidogo; hiyo mifugo imepotelea wapi? Kuna mazizi mengine ya ziada walikopeleka au walipaswa kulinda ile mifugo ili amani ipatikane wenye mifugo warudishiwe mifugo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haikubaliki. Tumeona kwenye Operesheni Tokomeza, watu wamechukuliwa mifugo yao imepelekwa mpaka leo hii kesi zimekuwa za kusuasua, haki haitendeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii sidhani kama tutapata utulivu wa kifikra au tutapata amani. Haiwezekani, lazima mfugaji huyu naye atalazimika kutumia mbinu atakazoweza ili apate fidia ya mifugo yake iliyoibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii ninaweza nikasema Serikali imechangia. Pamoja na kwamba, kuna maelezo yaliyotolewa na Wanakamati, nashukuru sana. Katika Bunge hili nimekuwa nikiongelea sana mipaka baina ya vijiji na hifadhi. Unakuta kijiji kimesajiliwa, kina Viongozi, kuna Mtendaji wa Kijiji yuko pale, shule imejengwa imesajiliwa watoto wanasoma, lakini leo hii imeibuka hoja kijiji kipo ndani ya hifadhi; hivi nini kimeanza hifadhi au kijiji? Bado suala limeendelea, Serikali haichukui hatua zozote za kufuatilia kujua mpaka wa hifadhi uko wapi.

Tunaambiwa tu kinadharia kwamba hili ni Pori la Akiba, lakini ukiingia kwenye hilo Pori la Akiba unakuta ni mbuga kiasi kwamba, inayobaki ni kazi ndogo tu ya kuondoa vile visiki hata ndege inaweza ikatua bila matatizo yoyote! Tunahifadhi nini? *(Makofi/*

*Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiliongea suala hili mara nyingi sana. Katika Jimbo langu la Biharamulo, Kijiji cha Mpago, Kata ya Kaniha, tarehe 21 Agosti, 2014, ninamshukuru sana Kanali Mstaafu Fabian Massawe; tuliongozana kwenda kwenye kijiji kile, baada ya suala la migogoro ya vijiji na mipaka ya hifadhi kuwa limekithiri sana. Tumefika pale mpaka tulioneshwa siyo mpaka wa kijiji kile na wananchi wale wakamwonesha kijiji chao kinaishia mahali fulani. Haya twende porini tukaangalie hilo Pori la Akiba, waliyoyakuta kule ilikuwa ni majanga tu. Majanga majanga, imewekwa *barrier* barabarani huku *semi-trailer* zinakatiza kwenda kubeba mkaa, hakuna Pori la Hifadhi lililoko mahala pale! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala mtambuka, Wizara zinazohusika zinafahamika. Leo hii tuombe Viongozi wa Wizara msikae Wizarani, mnaletewa taarifa nyingine ambazo ni *fake*, teremkeni mkaangalie uhalisia wa mambo haya ukoje ili wananchi waondokane na matatizo haya. *TFS* wanaweka mabango pale ni marufuku kulima, kuendeleza shughuli, sijui kufanya nini, sasa huyu mwananchi ataishije; ana familia, ana watoto wanahitaji wasome na kipato pekee anakipata kutokana na huo ufugaji mdogo mdogo? Kipato pekee anachokitegemea ni kutokana kilimo cha jembe la mkono kisichokuwa na tija, leo hii unamzuia asifanye kazi hiyo, unategemea nini kama si kuwaweka wananchi wetu katika maisha ambayo ni ya rehani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Viongozi hawa wa Wizara wateremke chini waangalie matatizo yaliyoko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni jinsi gani Serikali itaweka utaratibu wa kutafsiri hizi *GN* kwa Watendaji au Viongozi walioko katika Halmashauri zetu. Migogoro mingine inaletwa na Viongozi walioko kule. Katika Jimbo langu la Biharamulo Magharibi, Kijiji cha Kiruruma, kuna Kitongoji kimeanzishwa kinaitwa Nyalwambo, pale kuna watu zaidi ya 155 hata kupiga kura kwenye Uchaguzi wa

Serikali za Mitaa wamekataliwa eti wao ni wavamizi. Kimsingi, wamepokelewa kwa kutumia taratibu zote za kupokea wageni katika kijiji; wamelipa viingilio, ukimuuliza una risiti anakwamba sina ila mchango nilimpa Mwenyekiti wa Kijiji. Mwenyekiti kachukua Wajumbe kaenda kule kukagua lile eneo na wamepewa, lakini eneo walilopewa liko kwenye *buffer zone,* linapakana na hifadhi. Leo hii watu wa hifadhi wakichukua hatua zinazostahili wananchi wale wanapaswa waondoke, wabomolewe nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama na Viongozi wameshiriki kufanya hili, ni tatizo kubwa sana.

Namshukuru Mzee Michael Laizer hapa amesema, kuna sehemu imefikia mahala hata Wakuu wa Wilaya wanakwenda wanasema kwa hili ninyi mtaelewana tu na Mwenyekiti wa Kijiji; ebo kwa utaratibu gani! Hakuna suala la kuelewana, sheria ichukue mkondo wake, tujue kabisa kama huyu anapaswa kupewa eneo halali lijulikane na Serikali za Vijiji zinafahamu kabisa wanapaswa kugawa mwisho ekari ngapi. Inakuwa ni makusudi mazima, mtu anaambiwa basi wewe utalima tu, utafuga utakapoishia, sasa hakuna mipaka?

Maeneo yaliyoko ndani ya vijiji, Viongozi wetu Wenyeviti wa Vijiji wameuza na anayeuziwa bahati mbaya unakuta siyo raia wa mahala pale. Sasa na yeye anakuwa mungu mtu, anashika mjeledi anaanza kuchapa viboko wenyeji waondoke kusudi abaki yeye peke yake ndiyo analishia katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vurugu hizi hatuwezi kuziepuka hata siku moja. Naomba hata Kamati zetu za Ulinzi na Usalama, *DCs* wapo, *RCs* wapo, hebu chunguzeni. Nilikuwa nasoma hili kabrasha la viambatisho kuonesha jinsi gani wageni wanavyoingia kiharamu katika Pori la Burigi Kimisi lakini wana hati wamepewa *permit* za kuingia mle ndani; hivi hizi *permit* zinatolewa na nani? Hawa Maafisa Uhamiaji ni Wajumbe kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama, kwa nini tusiwahoji hizi *permit* zinatoka wapi?

Inafika mahala mtu kapewa *permit* hiyo hawamfuatilii kumwambia *permit* yako imekwisha, aidha ufuate utaratibu unaokubalika au basi urudi; hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema maneno haya, lakini mgogoro najua tunauendeleza sisi wenyewe. Haya kama yangeweza kufanyiwa kazi, hakika yangelikwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida!

**MHE. BENEDICT N. OLE NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe na Mheshimiwa Kidawa Saleh, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge; hongereni sana. *(Makofi)*

Pili, ningependa kuishukuru Kamati yako Teule, wamefanya kazi nzuri ya kitaalam na ya kina na wametuchorea Ramani ya Tanzania na migogoro ilipo na ilivyokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii Teule imebainisha vyanzo vya matatizo yanayosababishwa na matumizi ya ardhi yanayokinzana na wamefanya kazi nzuri sana. Wametuonesha hata na mikoa ambayo hali hii ni mbaya kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ndiyo rasilimali kubwa kuliko rasilimali nyingine zote na kila mtu anaihitaji na anaitumia. Ardhi hii kama wachangiaji wengine walivyosema, inaonekana ni kubwa na kweli ni kubwa, lakini bila kuipangia, bila kuisimamia, ukubwa huo hautakuwa wa manufaa kwetu. Kila mtu ardhi ni chanzo cha maisha yake. Migogoro hii pamoja na kuchukua sura nyingi, lakini ardhi ndiyo chimbuko la migogoro kati ya wakulima na wafugaji ama wanavijiji na watumiaji wengine hasa wawekezaji, wachimbaji madini pamoja na hifadhi pia. *(Makofi)*

Migogoro hii si kwamba imeleta tu uvunjifu wa amani, lakini watu wengi wamepoteza maisha. Vyanzo vinafahamika, Serikali ina taarifa. Kwa upande wa Sera tuko vizuri, kwa sababu Sera yetu hasa Toleo la Pili. Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 97, Toleo hilo la Pili ni nzuri na imeweka wazi kwamba, ardhi yetu mwelekeo wake wa kumiliki, wa kutumia na wa usimamizi ukoje; lakini kumekuwepo na udhaifu mkubwa hasa katika usimamizi wa sheria.

Sheria nazo hasa zile kuu, Sheria ya Jumla na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999, hizi zote ziko vizuri na zipo wazi. Tatizo linakuja katika usimamizi, hatuwezi kusimamia ardhi isiyobainishwa, kwa maana ya kupimwa na ramani kuchorwa. Hapa kuna upungufu mkubwa, kwa sababu zoezi ni la gharama, kuna uhaba wa vifaa, uhaba wa rasilimali watu na uhaba wa fedha. Tatizo hili kama limekuwa kubwa na linatishia amani kwa nini Serikali isichukue programu kama ya sasa ya kujenga Maabara na kusema tutapima ardhi ya kila kijiji kwenye nchi hii tukaimaliza?

Pili, tujenge masjala, maana huwezi kuwa na mafaili ya kitu muhimu kama ardhi na hakuna ofisi wala hakuna mahala pa kuhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni la muhimu sana. Kwa sasa teknolojia imerahisisha uchoraji wa ramani na hata upimaji. *GPS* wanaweza wakafundishwa vijana walioko vijijini, wakatumia bila hata kuwa na kisomo kikubwa. Kinachonishangaza zaidi ni kwamba, kuna vitu viwili; kuna uhaba wa ardhi kupita kiasi na vijana wawe wakulima, wafugaji, wachimbaji wadogo wadogo, hawa wana tatizo hawana maeneo ya kufanyia kazi za uzalishaji. Wakati huo huo kuna ardhi tupu inayokaliwa, inayomilikiwa kwa majina, bila kutumika na bila kufuata taratibu za sheria na masharti ya kuendeleza ardhi.

Kuna mashamba pori kwenye kila eneo, iwe ni Mvomero, iwe ni Kilosa. Kuna Ranchi na Vitalu hewa upande wa Kagera na ndiyo maana inawezekana kuingiza mifugo ya kigeni. Kwangu Kiteto kuna eneo kubwa ambalo

halimilikiwi, lakini linatumiwa na watu wanaojificha kwenye migongo ya watu wachache. Bahati mbaya sana wengi ni viongozi, ni watu wenye dhamana ya kuwa viongozi wa umma. Orodha ipo Serikalini, lakini Serikali imekuwa inasita kuwachukulia hatua. Badala yake wamekuwa wanamtafuta mchawi wa tatizo la ugomvi Kiteto ni nani! Nani anayechochea na huku umepewa orodha ya watu wanatumia zaidi eka 160,000, majina yapo wanafahamika na hawa ndiyo wamekuwa kikwazo katika kusimamia sheria hasa hukumu ya Mahakama ya Rufaa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali isimamie sheria hasa pale ambapo ardhi inajulikana imepimwa, imepangiwa matumizi na sheria iko wazi, hakuna mgogoro kwenye milki maana ni ardhi ya vijiji, mgogoro unakuja kwenye matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 60 ya ardhi ni ardhi ya vijiji inamilikiwa na wanakijiji na inatumiwa na wanakijiji, wawe wakulima au wafugaji. Ardhi ile kwa taratibu za sheria zetu, Afisa Ardhi Kijijini ni Mtendaji wa Kijiji. Kuwa Mtendaji wa Kijiji ni kazi ya pekee ambayo haidai taaluma yoyote. Tunasema mtu awe ni *form four leaver,* awe na *diploma,* lakini ni taaluma gani inayotakiwa ili mtu aweze kushika wajibu na kusimamia kazi muhimu kama hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna mgogoro, kwa sababu Taasisi za kusimamia Ardhi kwenye ngazi ya kijiji ni dhaifu. Afisa mwenyewe hajui majukumu yake, haifahamu Sera wala haifahamu hiyo Sheria; tunawezaje kumpa mtu kama huyu dhamana? Kwa hiyo, si bure kwamba uhalifu unatokea, ardhi inagawanywa kama njugu, taratibu hazifuatwi na unaweza ukakuta mtu inasemekana kapewa eneo kijijini ekari 6,000 mpaka 10,000 na huku sheria iko wazi kwamba mwisho wa uwezo wa kijiji kutoa ardhi ni ekari 50 tu.

Hapa ni lazima Serikali itazame hili na ichukue hatua mara moja kwa sababu hatuwezi kuboresha milki ya ardhi, matumizi ya ardhi, tukamaliza mgogoro kati ya wakulima,

wafugaji, wanakijiji na wawekezaji, bila kuweka mkazo kwa wasimamizi pamoja na Taasisi nyingine zilizopewa dhamana ya kusimamia ardhi ya kijiji.

Mabaraza ya adhi ni hivyo hivyo, yawe ngazi ya kijiji, ngazi ya Kata na hata ngazi ya Wilaya. Ya Wilaya ndiyo kuna taaluma ya kisheria, lakini kila mahali hasa ambapo ardhi inamilikiwa kijadi, sheria hizo nazo zina upungufu, kwa sababu sheria zilizopo hasa zinazotumika kwenye Mabaraza ya Wilaya ya Ardhi, kidogo milki ya jadi haikupata nafasi ya kutosha.

Nitoe tu mwito Serikalini, naomba upimaji ardhi uwekewe mkazo na usimamizi wa ardhi na sheria iwe ni kwa kila mtu. Ingelipaswa kuwa rahisi zaidi kwa Watendaji Serikalini, wawe kwenye Mhimili, iwe ni Bunge, Mahakama ama Serikalini, ni rahisi kuwachukulia hatua hasa wanapokuwa chanzo cha migogoro kwenye ardhi, iwe upande wa Mabwegere, Kiteto na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ninamwita Mheshimiwa Riziki Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nakupongeza kwa kusimamia vizuri Kiti chako na Mungu akupe nguvu na uendelee kuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na mimi kuchangia katika hoja iliyopo Mezani. Nitangulize Wosia wa Baba wa Taifa juu ya Ardhi ya Watanzania, ambao aliutoa mwaka 1958. Ninaomba kunukuu: "Katika nchi kama yetu, ambamo Waafrika ni maskini na wageni ni matajiri, kuna uwezekano mkubwa kwamba, Mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi yake katika miaka ya 80 au miaka 100 ijayo, ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni na wenyeji watakuwa watwana." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaendelea tena kusema: "Lakini hata kama wageni wasipokuwa matajiri, litaibuka tabaka la Watanganyika matajiri, wajanja. Tukiruhusu ardhi yetu iuzwe kama njugu, katika muda mchache kutakuwa na kundi dogo la Waafrika, wakiwa na ardhi kubwa na walio wengi watakuwa watwana na maskini." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayaona sasa hivi, Watanzania maskini wamekuwa watwana ndani ardhi yao. Hii inatokana na baadhi ya wajanja kuhakikisha hawa maskini hawahitajiki na hawahitaji kuwa na fursa ya ardhi. Inatia uchungu, inaudhi, inatia kichefuchefu na hautakiwi tena kuendelea mfumo kuwakandamiza watu maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya ardhi ndani ya Tanzania hii inaongozwa na baadhi ya Viongozi na Watendaji wa Serikali ambao wanatanguliza maslahi binafsi bila kuangalia haki, sheria na kanuni inasema nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007, kulikuwa kuna matatizo makubwa sana ya umeme kukatika, wakahamishwa wafugaji kutoka Ihefu wakapelekwa Lindi. Cha kushangaza hii Kamati haikwenda Lindi, Mtwara wala Ruvuma. Hata Kamati ya Maliasili inapozunguka, inazunguka Serengeti, Ngorongoro, maeneo ya raha raha yale! Nendeni kwenye maeneo magumu ambako ndiko kwenye matatizo makubwa, mkaone kuna nini Lindi, Mtwara na Ruvuma kuwa kule hakuna migogoro.

Sasa hivi Mkoa wa Lindi unaongoza kwa migogoro ya ardhi. Wananchi wa Lindi sasa hivi ni watwana katika ardhi yao. Leo hii tuchukue mfano, unamtoa mwananchi kwa shilingi 400,000, wewe unaiuza ardhi ile shilingi milioni 8 mpaka milioni 36; huyu mwananchi aende wapi hana *re-settlement? (Makofi)*

Leo utasema mwananchi yule ananufaika nini na ardhi yake. Tunalazimisha migogoro iendelee kusambaa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kuongea mengi kwa vile nilishaongea siku zilizopita, lakini ninataka Serikali iiangalie hii haki iko wapi? Shilingi 400,000; jeneza unaweza kulinunua kwa shilingi 400,000? Mwananchi ananyanyasika na shilingi 400,000, haikubaliki kabisa. Hii hali inamfanya mtu anakuwa mnyonge, mwingine mpaka anazirai anakufa tunanyamaza, haikubali.

Mimi ninajisikia huzuni hata nikimwona mtu ananyanyasika, unampeleka wapi kwa shilingi 400,000? Itathminiwe ardhi. Wananchi wetu waangaliwe kwa huruma, tusifikirie biashara na mazingira ya matumbo yetu binafsi, tukawaacha wale watu wakikandamizwa; hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kuna watu wanaodharau uhifadhi. Uhifadhi duniani kote ni muhimu, bila hifadhi hakuna mvua. Leo Tanzania tunategemea kilimo kwa kutegemea mvua. Tunahitaji maeneo yetu yapate maji, lakini vyanzo vya maji vimeharibiwa, misitu imekatwa; je, tunakwenda wapi?

Wafugaji wamewatoa Mbeya Ihefu na mimi wakati huo nilikuwa katika Kamati ya Maliasili na Mazingira, wamepelekwa Lindi, hakuna miundombinu iliyopelekwa Lindi. Leo hii Mto Mbwemkulu umekauka, Mto Matandu umekauka, Mto Rufiji unaendelea kukauka na Mto Lukuledi ndiyo haupo kabisa watu wanacheza mpira ndani ya mto. *(Makofi)*

Tulikuwa tuna *Lake Mkoe* halipo, unaona katika *Google* tu kwamba hapa palikuwa na Ziwa, lakini hakuna, ni kwa ajili ya uharibifu wa mazingira. Wafugaji baada ya kwenda kule, wanahama kila sehemu, wanahamia hapa wanakata pori, anakwenda pale wanakata pori, unaona kama siasa vile. Haisaidii, tunaiua nchi yetu kwa kutumia mazingira magumu ambayo yako katika nafsi zetu. Wale wafugaji wamepelekwa kule jiulize kuna majosho hakuna; kuna malambo, hakuna! Wanahama sasa hivi mpaka wanahamia Mozambique, tunakwena wapi? Tutengeneze

mazingira kuhakikisha wafugaji wanawekewa mazingira mazuri waache kuhamahama. *(Kicheko)*

Migogoro haitakwisha kama mfugaji anahama kutoka Mwanza mpaka anafika Lindi. Mwanza jangwa, ukija Dodoma jangwa, Singida jangwa, Monduli jangwa, Kiteto jangwa; jamani leo Tanzania ilikuwa katika *heavy forest* ya Msitu wa *Tropical,* leo Tanzania ukiingia katika *Google* iko katika jangwa! Tuko wapi? Tunaangalia siasa au tunataka kuangalia maendeleo ya nchi baada ya miaka 50 kutoka leo? Hakuna misitu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vijijini, sasa hivi miti migumu inakatwa kwa ajili ya mkaa; je, hakuna Diwani? Hakuna Mtendaji? *DC* yuko wapi? Misitu imekwisha. *(Makofi)*

Tulitembelea Liwale, Liwale sasa hivi ni jangwa kuliko hata Singida au Dodoma, lakini ndiyo lilikuwa eneo kubwa la misitu mikubwa. Watendaji wa kule wameshikamana kuhakikisha leo Liwale hakuna msitu. Wanatumia mbinu moja, mimi nikawauliza kwa nini wakatuambia hizi mbao tunazozikata tunapeleka katika Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Bunge wanatengeneza samani kwa ajili ya Ofisi za Wafanyakazi wa Bunge.

Mimi sikukubali maneno hayo, nikapiga simu Ofisi ya Bunge, wakasema siyo kweli ni Magereza wanafanya uhuni katika kila eneo wanasema sisi tumepewa *tender* ya kutengeneza samani kwa ajili ya Ofisi za Bunge. Hivi sasa wanakata misitu, macherezeo yako maporini na wakitoka pale wanatembea na vibali kuwa mbao hizi tunakwenda kutengenezea samani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenye Dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi, aje atupe majibu kwa nini yanatendeka mambo kama hayo, misitu inakwisha kwa kutumia vibali vya uwongo. Watupe tathmini na ni nani anayefanya hivyo. Ninaomba tena zile mbao zilizokamatwa Liwale, zipelekwe katika mashule, wanafunzi wapatiwe madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanakaa chini Liwale, wanafunzi wanakaa chini Lindi, lakini mbao zinaletwa Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya biashara; haikubaliki. Misitu Tanzania imekwisha. Halafu kila siku mkikaa Wabunge nataka maji Ludewa, nataka maji Sumbawanga, maji yatapatikana wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa John Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumzia jambo hili muhimu sana.

Ninaanza kwa kuwashukuru na pia kuwapa hongera kubwa sana Mwenyekiti na Kamati hii Teule, kwa kutuandikia Taarifa nzuri kama hii. Taarifa hii kwa maoni yangu kwa Serikali, ina kila kitu; ina matatizo na ina suluhu na pia imetoa maoni ni jinsi gani mambo ambayo yameorodheshwa yanaweza yakatatuliwa. Mimi ninataka kuongeza mambo ambayo ninaona ni muhimu kwa sasa hivi.

La kwanza kabisa na ninawaomba hili Watanzania tusilibeze, kuna mtindo ambao unaanza kuingia katika Taifa hili nao ni wa kubaguana. Hivi sasa kama Morogoro yale ambayo tunayaona kwenye taarifa za habari, yale tunayoyaona kwenye television, mtu mwenye bodaboda anaweza akalipwa pesa amfuate mtu yeyote aliyevaa rubega anayefanana na Wamaasai amwondoe; tunaenda kubaya! *(Makofi)*

Kama ni sumu, ninawaambia sumu haionjwi. Yale mauaji tuliyoyasikia ya *genocide* Rwanda yalianza kidogo kidogo hivi hivi. Mnaanza kuangalia ni kabila gani tuliondoe, hakuna kabila hapa la kuliondoa. Sisi sote ni Watanzania na sote tuna haki ya kutumia ardhi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu moja kwa moja na zaidi kwa upande wa Morogoro, kama kuna mwanasiasa anayefikiri anaweza kuwaondoa wafugaji kwa njia ya kulipalipa vipesa kwa bodaboda, huyu sasa hivi aache mchezo huo na Serikali iangalie na ihakikishe jambo hili linakoma mara moja. *(Makofi)*

Ukianzisha Morogoro, utayakuta haya Arusha, utayakuta Dar es Salaam. Dar es Salaam sasa hivi nyumba zote zinalindwa na Wamaasai. Tukianza kuwachokoza na mimi ninawaomba na Mwenyezi Mungu abariki ombi langu, ninawaomba Wazee wa Kimaasai wawaombe kabisa vijana hawa wasipandishe mori na wao waanze kulipiza kisasi, hapana. *(Makofi)*

Wakianza hivyo, sisi ambao tunalindwa, wengi wetu wako Dar es Salaam na sehemu nyingine, hatutakuwa na maisha. Kwa hiyo, nimeona hili niliseme. Imezungumzwa juu ya amani na maana ya amani siyo kuizungumza tu, ni lazima tuchukue hatua tunapoona kuna dalili ya kutokuwa na amani na kuishi pamoja katika Taifa letu. *The bottom line* kila mmoja ana haki ya kuishi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nilishawaambia siku nyingi, ng'ombe hazungumzi, lakini ninyi Waheshimiwa Wabunge mnaopenda kubezabeza mambo ya ng'ombe, ng'ombe ana laana. Kama unataka kurudi kwenye Bunge hili acha mambo ya kudharau ng'ombe. *(Makofi)*

Unaagiza mpaka mishikaki mitano, ng'ombe hawafai, biashara ya wapi hiyo! Mimi ninataka maziwa, ng'ombe huwataki, maana yake nini! Ng'ombe kwa wafugaji, hawa wafugaji siyo maskini. Nimeona hapa tumeanza sasa na *TASAF II,* sijui *TASAF* ngapi kutafuta watu maskini. Wale uliowaona hapa wamevaa wanaweza wasivae vile unavyopenda wewe *suite,* lakini wale watu siyo maskini. Mfugaji mwenye ng'ombe 100, ndiyo kusema anayo akiba siyo chini ya shilingi milioni 30.

Hebu niwaulize Waheshimiwa Wabunge tukaangalie akaunti zetu; nani aliyekaa na shilingi milioni 30 ndani ya benki? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hamna!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Hawa wameshavuka *level* ya kuitwa maskini na kama unatafuta *Big Results Now (BRN)* au Matokeo Makubwa Sasa, hawa ndiyo kila mwaka wanazalisha mara mbili ya walichonacho, unatafuta nini tena?

Kilichotushinda ni namna ya kutafuta utaratibu wa kuishi pamoja wafugaji na wakulima; hili ndiyo tatizo! Mambo ya kubezanabezana hayawezi kutufikisha mahali popote, tutafute *formula* ya kuishi pamoja. Tatizo la wafugaji la kwanza, wao wanatafuta mahali pa kulisha na mahali pa kunywesha ng'ombe wao. Ufugaji ndiyo maisha yao, tatizo lao ni malisho na mtu anayehodhi malisho mengi ni Serikali; ina ranchi kubwa, imefukuza wafugaji, imeweka ardhi ambayo haina ng'ombe. Hili siyo jambo jipya.

Serikali 27% ni hifadhi, hakuna anayebeza hifadhi wala hakuna anayekataza hifadhi, lakini kwa kuwa tulianza tukiwa watu milioni 8 na leo tupo milioni 48 na ardhi ni ileile, lazima tuangalie je, inawezekana tukaendelea kuwa na hifadhi ya 27% ya ardhi yote? Haya ndiyo mambo ya kuzungumza na kupanga. Bila kufanya hivyo, tutaendelea kugombana mwisho tufike mahali watu waseme waondoe hawa, hakuna anayeondoka hapa! Tutengeneze utaratibu tu wa kuweza kuishi pamoja. *(Makofi)*

Siyo hivyo tu, jambo lingine ambalo naliona ni matumizi ya ardhi. Matumizi ya ardhi pia Serikali ina mkono mkubwa mno. Juzi hapa kwa mfano, Serikali ilitaka Kigamboni, kila mmoja anaambiwa simamisha maendeleo ya ardhi yako. Serikali inaanza kutafuta fedha, miaka 10, miaka 20, pale *airport*, utaratibu huu lazima tuukataze kwa sheria. Kama wewe Serikali unataka ardhi yangu, katayarishe kwanza pesa, ukishapata fedha ya kutosha, basi uje uchukue

mali yangu, kwa sababu tumesema hata kwa sheria kwamba, ardhi ni mali, *land has value*. Usitumie sheria tu mimi nataka hapa kuanza kupatengeneza, kuanza kuendesha maendeleo, lakini fedha huna.

Watu wa Kigamboni unawaambia wasiendeleze nyumba zao Serikali haina fedha na Waziri aliyepita anajua hilo. Kwa hiyo, hata Serikali yenyewe inaleta migogoro, wewe ukitaka ardhi yangu lete *cash* mkono kwa mkono, unanipa mapesa yangu nakwenda mahali na hii iko kila mahali, ukitaka mji, watu wapewe *compensation* wakati ambapo wanahitaji.

Si hivyo tu, kuna mapori mengine, kwa mfano, mimi natoka *Maswa Game Reserve*. Wewe unaitengeneza *hunting block,* unawapa watu wachache wa kuja na bunduki kutafuta simba, kutafuta wanyama na mambo kama hayo, mbona Ngorongoro wanyama pamoja na ng'ombe wanaweza kulisha kwa pamoja? Vipi kwa *Game Reserve* yote ya Maswa, kwa nini wanyama wasilishe pamoja na ng'ombe? *(Makofi)*

Ukiwa Mbunge wa sehemu kama ya Itilima ninakotoka mimi, kila siku ni kesi ya ng'ombe wamekamatwa na Maafisa wa Pori na wakiwakamata wanakwenda kuwafungia kwenye zizi, hakuna maji wala malisho. Mheshimiwa Waziri wa Mifugo namwona hapa, tumetunga sheria kwamba, ng'ombe ana haki ya kupewa maji na malisho. Huwezi kuwa na sheria moja tu ambayo unaitaka kwamba, ni Sheria ya Hifadhi na ukaacha sheria nyingine inayohusu ng'ombe. Kama wewe unawakamata ng'ombe wangu basi hakikisha unawapa malisho na pia unawapa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Samahani nilimtaja Mheshimiwa Jitu Soni, naomba uendelee!

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwanza kabisa, naomba nikupongeze wewe na Mheshimiwa Kidawa, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu na pia tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu, muweze kufanya kazi zenu vizuri. Ninaamini uwezo huo mnao. *(Makofi)*

Nampongeza pia Mheshimiwa Spika, kwa kukubali kuunda Kamati Teule. Kamati hii imefanya kazi yake kwa uadilifu na imezingatia utaifa mbele na kuangalia maslahi ya Taifa kwa ujumla, badala ya kuangalia masuala ya vyama au itikadi mbalimbali. Nawapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mfano mzuri waliouonyesha ni pale walipofika Babati; nimpongeze Mheshimiwa Selasini, hakuonyesha kabisa masuala ya itikadi na alifanya kazi ile na kukemea masuala mbalimbali, hata alipoona mtu ambaye yuko katika chama chake hakujali hayo, yeye alijali maslahi ya Taifa na katika maeneo mengi wamefanya hivyo ikiwemo Babati. *(Makofi)*

Mimi nawaomba Wabunge wenzangu wote, ushauri ambao umetolewa na Kamati, tuendelee kuuboresha ili migogoro ya ardhi iliyopo katika nchi yetu iishe na mauaji ya watu na kutokuelewana viondoke na turudi katika Taifa letu kama tulivyokuwa huko nyuma, tuishi kwa amani na upendo. Muhimu kuliko yote, tusipoangalia suala hili tayari tumeshaanza kuingiza ukabila.

Leo hii maeneo mengi vita vimeanza kuzuka baina ya makabila mbalimbali; kwa mfano kule Morogoro, tukija Babati tayari wafugaji wa Kibarbaig wanapigana na wale ambao ni wakulima wa eneo la Mwada. Tayari baada ya kuwa na vita baina ya mtu na mtu, sasa inachukuliwa tafsiri kwamba ni ya makabila ya Wambugwe na Wabarbaig, Wamasai na Wabarbaig au fulani na fulani. Tunakoelekea siyo kuzuri, ninaomba wote tushirikiane tuhakikishe haya matatizo tunayamaliza kwa kuweka misimamo mizuri. Sera

ipo nzuri na sheria zipo, tatizo kubwa ni utekelezaji wa hizo sheria, tumekosa watu wa kutekeleza sheria na usimamizi wa sheria, haupo kabisa. Tukizisimamia hizi sheria ambazo zipo, ninaamini kwamba matatizo haya yote yataisha.

Jambo lingine ambalo ningeshauri ni kwamba, ule Muswada wa kuweka Sheria za Ardhi mbalimbali uletwe haraka. Kwa mfano, ardhi ya kilimo iwe na sheria yake, yaani matumizi ya ardhi, ardhi ya ufugaji, ardhi ya uvuvi na hata ardhi ya makazi iwe na sheria yake, ili ukitaka kubadilisha kutoka sheria moja kwenda nyingine iwe ngumu, kwa sababu bila hivyo bado hii migogoro itaendelea kuwepo. Leo hii ardhi nyingi sasa ya kilimo na mifugo imegeuzwa kuwa ya makazi kiholela na itafika mahali tutakuwa na makazi kila mahali bila kuwa na mpangilio wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia tuangalie namna ya kuhakikisha maeneo yote ambayo yametajwa katika eneo hili yenye migogoro, ni mifano tu lakini inachukuliwa kwamba hiyo sasa ikitungiwa sera na sheria, itamaliza matatizo katika nchi yetu.

Naomba niishukuru Kamati, ilipokuja Babati, kwanza, katika eneo la Kiru wametoa ushauri mzuri kabisa kwamba, baadhi ya yale mashamba wawekezaji wafidiwe ili ule mgogoro uishe na wananchi wapewe maeneo. Tayari Serikali imeanza kutekeleza, niipongeze kwa hilo na ninaamini kabisa kuwa hatua stahiki zitaendelea kufuata.

Niendelee kusisitiza kwamba, kuna maeneo kwa mfano Shamba la Rivaku kule Dareda, ni shamba ambalo limetajwa hapa na kila siku tunalitaja; kuna baadhi ya maeneo mashirika yanahodhi ardhi na wanaendelea kukodisha. Ardhi ile Rivaku inakodishwa, tunashauri vijiji ambavyo vinazunguka lile shamba ambao tayari wako ndani ya eneo hilo la *lease* ya Dareda; Vijiji vya Ari, Dohom, Singu na Endasagu, wote walipewa lakini yale maeneo ambayo kuna migogoro ya ardhi, basi wale watu waweze kupatiwa hayo maeneo.

Kuna shamba ambalo Kamati ililitembelea, Shamba la Mwada la Rivaku ambalo Rivaku imenyang'anya kwa nguvu eneo la wananchi Shamba la Mwada, ambalo kijiji kilitoa kwa ajili ya majaribio ya pamba, lakini matokeo yake Rivaku sasa imefanya lile shamba ni mali yake. Naomba kama Tume hii ilivyoshauri lile shamba lote lirudi kwa wananchi.

Tatizo kubwa ambalo tunalipata ni Tume, ziumeundwa nyingi, ushauri unatolewa mzuri ili kumaliza migogoro, lakini utekelezaji wake utafanyika? Mimi naamini kabisa kwamba, huu utekelezaji ukifanyika tutapata suluhisho.

Kwetu kuna eneo karibu na Tarangire, eneo la Kijiji cha Kakoi, maeneo ya wafugaji kule Mdorii ambayo yalikuwa ya ufugaji rasmi, ambako kuna maeneo yanaitwa *Veterinary,* unakuta eneo lote sasa limegeuzwa kuwa *WMA* na leo wafugaji wanafukuzwa hawana pa kwenda. Wenyeviti wa Vijiji wanakamatwa wanawekwa ndani bila sababu yoyote, kisa wale wawekezaji wanashirikiana na Uongozi kuhakikisha hawafanikiwi.

Niendelee kushauri kuwa maeneo ya Gedamar, Ayamango na Gedajabong, ambayo yana mgogoro na Tarangire, yaendelee kubakizwa. Wananchi wako pale, hili eneo ni kubwa, waendelee kubaki kama eneo la mifugo na wale wachache ambao ni wakulima, basi watafutiwe eneo mbadala kwenye Shamba la Galapo Estate na pale Rivaku ili wale ambao wana nia ya kulima walime na hili eneo liendelee kubaki kuwa la wafugaji. Kipindi cha kilimo wafugaji waweke mifugo yao pale na kipindi cha kiangazi warudi kwenye mashamba yao na lile eneo liwe linakaa kwa muda ili tatizo hilo liwe limekwisha.

Eneo lingine ni eneo la Vilima Vitatu, mgogoro upo wa aina hiyohiyo. Mtu alipewa *hunting block* kwa ajili ya uwindaji, ambapo wananchi kipindi ambacho siyo cha uwindaji walikuwa wanaingiza mifugo yao, wanakata miti, wanakata majani au nyasi za kuezekea, huduma mbalimbali

na miti shamba. Leo hii lile eneo limegeuzwa kuwa eneo la *photographic,* yaani utalii wa picha na hakuna mwananchi anayeruhusiwa kuingia huko. Je, hao wananchi waliotoa eneo lao kuwa *WMA* waende wapi na mifugo yao?

Mara nyingi unakuta wafugaji ndiyo wanaendelea kunyanyaswa na hawana pa kwenda, kwa sababu wapo wachache na walio wengi wakiwezeshwa kidogo basi unakuta kila kitu kinaenda kwa maslahi ya watu wachache.

Pale kwetu kuna mfano; kijiji kimetoa eneo dogo, ni sawa kutokana na sheria, lakini wameweka *buffer zone* ya *one square kilometer* kutoka mahali ambapo mtu ameweka hoteli. *Square kilometer* moja ni ekari ngapi? Ni eneo kubwa kiasi gani? Na humo pia wafugaji maboma yao 17 yalichomwa moto pamoja na mifugo midogo yote ilichomwa moto, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Naomba mchango wangu wa maandishi uingie kwenye *Hansard. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Selemani Jafo, atafuatiwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kukushukuru sana. Kubwa zaidi, niwaombe Wabunge wenzangu, hili jambo lililoko mbele yetu hapa ni *sensitive* kidogo. Jambo *sensitive* kwa sababu wakati tukijadili hapa, kuna watu wana makovu, wengine wana majeraha na kuna watu wana kumbukumbu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuwaomba Wabunge wenzangu tu kwamba, mjadala wetu tuufanye

huku tukijua tunapojadili inawezekana tunagusa hisia na familia za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunafanya *analysis* za kuangalia kiwango cha vifo Tanzania, inawezekana ajali kubwa sana sasa hivi zinaongozwa na ajali za pikipiki. Ajali za pikipiki kwa siku zingekuwa zinakuwa *recorded* na chombo maalum, basi inawezekana kila siku tunapoteza mabasi matatu au manne ambayo yanapata ajali. Vifo vingine ambavyo haviko rasmi ni vifo baina ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni tete sana na hili ndiyo maana nasema tusizungumze kwa hisia kali sana kwa sababu huko, hata leo hii kuna askari mmoja ambaye ameenda kugombelezea ugomvi amefariki na maiti inasafirishwa inaenda Songea. Hali ni tete sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujifunze hapa, kuna maeneo tunafikiria kama Mkoa wa Kilimanjaro na baadhi ya maeneo ya Arusha, suala zima la migogoro kati ya wakulima na wafugaji jambo hilo huwezi kuligusa sana. Kuna baadhi ya mikoa kiasilia zamani ilikuwa si mikoa ya ufugaji. Ukizungumzia Mkoa wa Morogoro, Pwani na Lindi hata ufugaji ulikuwepo lakini siyo *large scale* kama hivi sasa ilivyo. Kwa hiyo, ina maana hapo ni lazima tujiulize kwa nini hali imekuwa hivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwaangalia wafugaji hawa ndiyo hapa tunapata *analysis* kutokana na watu mbalimbali wanavyochangia kwamba, inawezekana hatujajipanga vizuri katika baadhi ya maeneo. Hili lazima tujue kwamba, hali siyo shwari, kama Wabunge na kama Serikali, tuangalie jinsi gani tutatoka hapa tufike mahali salama.

Katika mikoa mbalimbali ukichukua mkoa wangu wa Pwani, Wilaya yangu ya Kisarawe hali ni mbaya. Zamani mifugo kule watu walikuwa wanaita mng'onyo, yaani ni

mdudu, leo hii wanapopata ng'ombe na nini, basi changamoto inakuwa kubwa sana.

Mauaji baina ya wakulima na wafugaji, nikiangalia Mvomero katika vyombo vya habari hali inatisha sana. Katika jambo hili lazima tupate majibu hapa. Nashukuru Kamati imekuja na mawazo mazuri sana, lakini ni lazima tuyafanyie maamuzi na lazima tukayatekeleze. Inawezekana mawazo yakawa mazuri utekelezaji wake ukawa hafifu, tutakuwa tunazungumza historia hii miaka yote. Kamati mbalimbali zinaweza zikaundwa, lakini utekelezaji wake tusije tukafikia mafanikio yale tunayokusudia.

Mimi nafikiri tuwe katika kipindi sasa hivi tuangalie ni jinsi gani tunaenda katika *transformation* ya jinsi gani tunakwenda. Mimi naomba nikupe changamoto kaka yangu Kamani, wewe ni mfugaji *by nature* na Naibu Waziri wako, naomba ikiwezekana mjitahidi jinsi gani mtatututatulia hapa tulipo. Ikiwezekana katika suala zima la Sekta ya Mifugo na sekta nyingine na Wizara nyingine, inawezekana wakati mwingine hatuzungumzi lugha moja, ndiyo tatizo tunalolipata hapa. Mimi naomba sana, ikiwezekana Wizara ya Mifugo, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi, zikae pamoja wajadili hili jambo. *(Makofi)*

Mimi nina imani ya kutosha, kama tungekuwa tunafanya maamuzi, kwanza, siamini kama Tanzania yote inaweza kuwa eneo la ufugaji, siamini hivyo. Mimi siamini kama kila eneo tutakuwa tunafuga, lakini naamini tukipanga maeneo tunaweza tukapata maeneo ya kilimo na maeneo ya ufugaji. Vilevile siamini kama mapori tengefu, hifadhi zetu na kila kitu, kutokana na wingi wa mifugo tuliyonayo, kama Watanzania wakati mwingine tunashindwa kufanya maamuzi kama kuna baadhi ya eneo tunaweza tukalitenga maalum kwa ajili ya wafugaji. Inawezekana Waziri wa Mifugo anazungumza lugha nyingine na Waziri wa Maliasili na Utalii anazungumza lugha nyingine, hatuwezi kufika mahali pamoja.

Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba, kama kuna eneo linaonekana ni pori limetengwa, ambalo tunaweza tukalibadilisha, tukaweka miundombinu ya kutosha, wafugaji kwa wingi wao tunawapeleka pale na tukatengeneza *facilities* zote mifugo tukaiingiza pale, tufanye hivyo. Hii ni nchi yetu sisi wenyewe, tusihitaji mtu mwingine aje kutupangia matumizi ya nchi yetu.

Tusiwe *rigid* katika maamuzi yetu, kama kuna pori kubwa limekaa bure; hivi pori hili kwa nini tusiamue sasa tunafanya maamuzi japo lilikuwa pori tengefu au hifadhi sasa tunasema tunaweka miundombinu ya kutosha, tunatengeneza na kiwanda, wafugaji tunawapeleka pale kwa wingi wao waweze kufuga mifugo yao. *(Makofi)*

Hili jambo linawezekana ndugu zangu, lakini kama hatufanyi maamuzi hayo, vifo vya wakulima na wafugaji hatuwezi kuvisitisha.

Hili ni jambo kubwa, kwa sababu leo mkulima amelala, asubuhi anaamka anakuta shamba lake limeliwa, tena anaulizwa shamba lako limeliwa nikupe fedha kiasi gani! Hapo ndiyo matatizo yanapotokea. Mapori yetu tungeamua tufanye maamuzi, hii ni nchi ya kwetu, tupange maamuzi ya kwetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jitu kuna kitu alikuwa anakizungumza katika maeneo mbalimbali, kumbe kuna maeneo mengine inawezekana tunayalazimisha lazima yawe maeneo ya hifadhi, lakini vilevile tuna wafugaji. Hivi hatuwezi tukaamua kwamba kuna sehemu fulani tufanye *concentration*, haya maeneoya hifadhi tuyaweke vizuri yawe hifadhi, lakini maeneo mengine tuweke fursa hata wafugaji waweze kufuga mifugo yao; yanawezekana hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuna-*push* wafugaji wetu wanajikuta kwamba hata yale maeneo yao ya asili ambayo mwanzo walikuwa wanakaa lakini sasa hivi hawawezi kukaa, ndiyo maana wanaenda kuvamia baadhi ya maeneo mengine na migogoro inaanza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namwomba sana Waziri wa Mifugo, tufanye mabadiliko sasa. Ninaamini Wizara ya Maliasili na Utalii ikikaa vizuri, ikabainisha maeneo yake na kutenga maeneo mengine, ikikaa vizuri na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, watakuja kutupa tangazo hapa kwamba Serikali imeamua eneo fulani tunaenda kutenga kwa ajili ya wafugaji na tutaweka miundombinu yote. Hata *concentration* ya miundombinu itakaa vizuri pale. Lakini kila mtu akisema jangu jangu, yaani kila mtu aseme la kwangu, la kwangu; mimi maliasili yangu, mifugo yangu, hatufiki! Kwa kweli hatufiki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naiomba sana Serikali, Kamati imeleta mapendekezo mazuri sana, tuyafanyie kazi.

Mimi hapa nazungumza kwa uchungu sana kwa sababu najua siyo muda mrefu sana wafugaji wenyewe kwa wenyewe; Wasukuma na nanii waliuana kule Kisarawe; siyo muda mrefu sana na nyie mnakumbuka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mangungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza nianze kwa kukupongeza wewe kwa kupata nafasi hiyo uliyonayo hivi sasa. Tunaamini kwamba utatuongoza vile ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo Watanzania wote tunatakiwa tulifahamu kwa mifano ya Mataifa mengine, maeneo mengine na tukumbuke Mwenyezi Mungu

hakutuumba sisi tuje duniani kwa namna yoyote ili tuje kufarakana au kugombana.

Nasema hivi kwa sababu wapo watu ambao wanaishi wakiamini kwamba wakichochea migogoro, wakitengeneza migogoro ama migogoro ikiwa inaendelea, ndipo ambapo wao wanapata maslahi yao. Ukisikiliza maelezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati hii teule, Mheshimiwa Ole-Sendeka na Wajumbe wake, taarifa iliyoandikwa, unaona kabisa matatizo ya mapigano, mabishano, mvurugano baina ya wakulima na wafugaji yanasababishwa na watu kutotekeleza majukumu waliyokabidhiwa inavyotakikana. Sheria nzuri zipo, lakini watu wanaangalia upande mmoja ule ambao utawafanya wao wawe wananufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo wa jambo hili mpaka ikaundwa Kamati Teule ilitokana na madhira ambayo wafugaji waliyapata, matatizo ambayo yanatokea kila siku ndani ya nchi yetu, mapigano baina ya wakulima na wafugaji, Bunge likaona liunde Kamati Teule ili ilete mapendekezo. Kwa bahati mbaya sana, sina hakika kama mapendekezo haya, hao ambao tunawazungumzia hapa watakuwa tayari kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tukio moja ambalo nililiona kwenye televisheni jana na juzi. Kama ilivyotokea kipindi cha Operesheni Tokomeza, wananchi ambao tunawawakilisha katika maeneo yetu, waliteswa walinyanyaswa, walipigwa wakadhalilishwa na wakafanyiwa vitendo vya kinyama ambavyo hata hao wanyama wenyewe hawajawahi kufanyiwa. Mwisho wa siku hakuna fidia ambayo wamelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii umeanza uharamia mpya ambapo Polisi wanashirikiana na makundi mengine; hatuwezi kusema ni Jeshi zima la Polisi, lakini kunaweza kukawa na kikundi cha wachache, wanakwenda kukamata mifugo, mathalani wamekamata ng'ombe 170 wamewafikisha kituoni ng'ombe wakiwa wako 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kila siku tunazungumzia suala la kuwawezesha wananchi, hii tunawawezesha au tunawanyang'anya?

**MJUMBE FULANI:** Tunawawezesha!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hii ambayo imewasilishwa, tunaona kabisa msamiati huu wa watawala wapya kwamba kuna wawekezaji. Wawekezaji hawa wanakuwaje wawekezaji ndani ya hii nchi bila ya kuwekeza?

Maeneo ambayo *NARCO* walikuwa wanayamiliki kulikuwa na sababu gani za msingi kwenda kuwakabidhi watu wengine kutoka nje ya nchi ambao wao wana uwezo mkubwa wa uwekezaji wa kujenga miundombinu, kuweka visima vya maji na majosho ili waweze kuwekeza kama wanavyotaka, maeneo yale wapewe wananchi ambao ndio waliowezesha kujengwa kwa zile ranchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zile zilikuwa ni za walipa kodi, ndizo zilizopelekea kujengwa ranchi. Ranchi zimeshindwa kuendeshwa, sasa wapewe wenyewe walipa kodi waziendeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha na la kustaajabisha sana, mwaka 2012/2013 ukame mkubwa ulipojitokeza maeneo yanayozunguka ranchi; Kongwa, Kibaha, maeneo ya Karagwe, wale wanaoendesha zile ranchi walikataa kuwaingiza ng'ombe kwenda kupata nyasi na kunywa maji, kama vile wao ndio walioumba nyasi na ardhi ile iliyoko pale. Tunafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ambao tunauendesha sasa, inawezekana kabisa Wabunge wengi wamechangia na wakasema kwamba, maeneo ya hifadhi yameshakuwa ni makubwa zaidi ukilinganisha na mahitaji ya wananchi. Idadi ya wananchi inakua kila siku, tuangalie yale maeneo yasiyohitajika kufanywa hifadhi, waachiwe wananchi wayatumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanyamapori wanaonekana kwamba wana thamani zaidi kuliko wanadamu, haiwezekani! Hili ni jambo ambalo halitakubalika na sisi kama Bunge hatuwezi kukubali kuwapa haki wanyamapori kuliko wanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani? Matatizo yaliyotokea kwa kipindi hicho cha mwaka 2013/2014 ilionekana kwamba mtu kuingia ndani ya hifadhi ataweka hatari kwa wanyamapori kuliko yeye mwanadamu ambaye anaenda labda kuchimba dawa au kufanya kitu kingine. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufuata ripoti hii iliyowasilishwa, tunaiomba sana Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Viwanda na Biashara, mkae pamoja kutatua matatizo, siyo kwamba kila upande unatetea mambo yake. Mnawapa mzigo mkubwa sana wenzetu wa Serikali za Mitaa kushughulika na migogoro wakati wajibu ni wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo haya ni lazima tuseme ukweli, hamjatengeneza mfumo mzuri wa masoko kwa ajili ya kuuza bidhaa zetu za nyama na mifugo kwenda nje; hamjatengeneza mfumo mzuri wa kusaidia upatikanaji wa pembejeo kwa maana ya kuweka malisho; hamjatengeneza mfumo mzuri wa kuwasaidia wakulima kuweza kujua namna ya kuweza kuongeza thamani ya mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la aibu sana leo hii Wasukuma wanapata adhabu ya kutembea na ng'ombe nchi nzima na hapo hapo tunatoa vibali vya kuagiza nyama kutoka Brazil na nchi nyingine. Haiwezekani! Timizeni wajibu wenu, tengenezeni mfumo mzuri bado ng'ombe wana thamani na Watanzania bado soko la ndani peke yake halijitoshelezi. Maeneo mengine nyama imekaa, ng'ombe hawajachinjwa lakini maeneo mengine kuna upungufu

mkubwa wa nyama, kilo inafika mpaka Sh. 8,000/= hadi Sh.10,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tengenezeni mfumo mzuri kwa kufuata na kuzingatia ripoti hii, itaweza kutuondolea matatizo mengi hasa upande wa ardhi kupimwa na wananchi wakaanishiwa maeneo ambayo yanastahili kufanyiwa shughuli zinazokusudiwa kama mpango unavyoonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninakuombea Mungu wewe na Wabunge wote, tuweze kufanya kazi kwa kushirikiana kwa pamoja ili tuweze kuisaidia nchi yetu. Ahsante, sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ngonyani!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kama Mwenyekiti wa Bunge. Vilevile nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati Teule ambayo leo imenifariji sana, Mheshimiwa Ole-Sendeka. Kwa kweli hapa tunahitaji tumpongeze kwa kazi nzuri ambayo umeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kesi ya wakulima na wafugaji. Toka wakati wa uhuru Wakulima na Wafugaji walikuwa ni watu ambao wanakaa sehemu moja, wanashirikiana; huyu akitoa unga, huyu anatoa maziwa; au huyu akitoa maziwa, huyu anatoa mboga. Lakini hapa katikati, napenda sana kuwalaumu wanasiasa. Wanasiasa ndio wametufikisha hapa tulipo. *(Makofi)*

Nasema hivi kwa sababu Jimboni kwangu, Mkoa wa Tanga Wakulima na Wafugaji kwa miaka yote walikuwa wanakaa katika kushirikiana, wanafanya kazi wote pamoja, wanashirikiana kwa kila kitu. Lakini kinachoshangaza sana, inafika mahali wanakuwa maadui. Kwanini? Kwa sababu kuna baadhi ya wanasiasa wanatafuta umaarufu kupitia kwa

wakulima; kuna baadhi ya wanasiasa wanatafuta umaarufu kupitia kwa wafugaji. Leo hii kuna baadhi ya wafugaji ambao wamekaa toka uhuru…

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Wamekaa katika maeneo ambayo wanashirikiana na wakulima, lakini cha kushangaza watu wanakuja kupima eneo hilo, halafu wanaambiwa hii ni sehemu ya hifadhi, waondoke. Waondoke hapo, wanakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo linajitokeza sasa hivi ni kwamba, kuna baadhi ya Watendaji wa Vijiji ndio wanaotufikisha hapa tulipo.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Wakulima na wafugaji wamepewa maeneo, lakini wanakuja wafugaji wengine kutoka maeneo mengine tofauti, hawakai kwenye Serikali za vijiji kuwashauri kwamba wapewe maeneo gani ya kufuga. Wanatoa maeneo, wakija kwenye mikutano ya hadhara, tayari wameshapewa ng'ombe mbili au tatu, watu wanawahukumu wafugaji, wao wanakuja kutafuta ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kumlaumu mfugaji anayetafuta ardhi kwa ajili ya malisho, lakini baadhi ya Viongozi wa Serikali wanakuwa ni walafi, wanataka kuwavuruga wananchi wawachukie wafugaji, kitu ambacho sasa hivi kinakuwa ni kigumu sana. *(Makofi)*

Naomba Mwenyekiti wa Kamati teule, angalia sana Mkoa wa Tanga. Mkoa huu una eneo kubwa sana, walikuwa wanaishi katika mazingira mazuri, lakini sasa hivi imekuwa ni kichaka. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Vilevile tunakuja katika mambo ya ardhi. Nimeshangaa sana mambo ya ardhi. Ardhi imeongelewa sana katika Mikoa yote Mwenyekiti wa Kamati Teule, lakini Mkoa wa Tanga hawajazungumzia mahali popote wakati ndiyo penye kiini cha matatizo ya ardhi. Kama kuna Mkoa ambao una wakulima wanapata shida, wanayumbishwa ni Tanga. Lakini katika taarifa ya Kamati hii sijaona mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia Mkoa wa Morogoro, Mikoa mingine, Wabunge wamehojiwa; Mkoa wa Tanga ni Mbunge gani ambaye amehojiwa, aweleze shida za Mkoa wa Tanga, awaeleze matatizo ya Mkoa wa Tanga jinsi wananchi wanavyopata shida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga sasa ni wakati wa kulima. Kwanza niwashukuru watu wa *Katani Limited*, wametusaidia kwa kiwango fulani, wametoa maeneo yao, wamewapa wakulima, wanalima. Lakini leo hii kuna baadhi ya vijiji watu wanapokonywa maeneo.

Serikali ilikuja wakati wa vijiji wananchi wakapewa maeneo, kwamba haya maeneo mtayatumia kwa sababu ya kukosekana kwa ardhi, lakini cha kushangaza leo hii mwekezaji anakuja kuwapokonya ardhi watu ambao wako tayari wanataka kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakulima ambao wamekaa kwa muda mrefu ambao wanategemea Serikali yao sikivu inaweza kuwasaidia, watakwenda kulima wapi? Nasema hayo yametokea Makuyuni, Mswaha, Kwalukonge, Shemshi na kuna mashamba makubwa katika Mkoa wa Tanga ambayo yalitakiwa yapewe wananchi, lakini mpaka leo hii ukiuliza hati, unaambiwa iko mezani kwa Mheshimiwa Rais. Lakini ukiuliza hati, yanakutwa mashamba ya Wilaya moja ambayo ni juhudi binafsi za Mheshimiwa Mntangi amefanya kazi hiyo mpaka yale mashamba yamegaiwa kwa wananchi. Je, hizi Wilaya nyingine za Mkoa wa Tanga, wananchi hawahitaji kulima, kufuga au ardhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, sisi wengine tunaipenda sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ndiyo iliyotufikisha hapa, lakini hatuko tayari kuikosoa Serikali yetu.

Hata hivyo, nasema hivi, Waziri wa Ardhi uliyepewa nafasi hiyo, una uwezo mkubwa, Mheshimiwa Dkt. Kamani una uwezo mkubwa! Nendeni Mkoa wa Tanga hata kesho tukiahirisha Bunge, mkaone mazingira ya wananchi wa Mkoa wa Tanga, hasa Wilaya ya Korogwe, Mjini na Vijijini tunavyonyanyaswa na wawekezaji ambao wametelekeza mashamba, lakini mkulima akienda kulima anakuja anapokonywa, mtu anakuja kupanda mkonge. Hii kama siyo dhambi ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka naingia Bunge hili mwaka 2010 ni kilio cha mashamba, mashamba, mashamba! Naonekana kama vile ninapiga ramli! *(Kicheko/Makofi)*

**MJUMBE FULANI:** Si ndiyo kazi yako! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Inashangaza! *(Kicheko/Makofi)*

**MJUMBE FULANI:** Ndiyoooo, kweli! *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naonekana kama napiga ramli hapa ndani ya Bunge!

**MJUMBE FULANI:** Na ndiyo kazi yako!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Kazi yetu sisi Wabunge ni nini? Kuwatetea wanyonge au kuja kusinzia tu kwenye makochi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mawaziri husika, Mwenyekiti wa Kamati Teule ambaye umefanya kazi nzuri sana ambayo inatupa matumaini sisi watu wa chini, hebu waambie waende Mkoa wa Tanga wakatembee Wilaya

hadi Wilaya. Wenzetu walikuwa wanakuja, wanakomea Wilaya moja, wanaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kuongea, ila naomba sana, Mkoa wa Tanga ni Mkoa ambao umekuwa na watu wavumilivu mno. Kama ni vita vya wakulima na wafugaji vingeanzia Mkoa wa Tanga, lakini wananchi wa Mkoa wa Tanga hawako tayari kuona damu ya mtu inamwagika kwa sababu ya kugombea ardhi. Wanawapenda sana wafugaji na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngonyani. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa heshima hii niweze kuzungumzia hili suala la wakulima na wafugaji. Ingawa natoka kwenye eneo lenye ardhi ndogo na watu wengi, lakini migogoro hiyo pia ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Kijiji cha Mawala ambako wapo Wamasai, wafugaji wazuri na tuko wakulima wazuri. Sasa naona tatizo kubwa linalojitokeza ni la utawala. Kwa mfano, huko Mawala, Serikali ilifanya kazi nzuri sana huko nyuma kwa kutenga eneo la wafugaji na wakulima. Kazi nzuri sana na ramani wanayo kwa miaka mingi. Kwa hiyo, wakulima na wafugaji walikuwa wanaishi vizuri, lakini pakajitokeza tajiri mmoja akavamia lile eneo la wafugaji akajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale wafugaji hawakuweza kuvumilia na wenyewe wakaenda kutetea eneo lao. Kilichotokea ni kwamba, watoto wa Kimasai walikamatwa wakishitakiwa kwa *trespass* kwamba wamevamia eneo la tajiri, halafu Serikali imekaa kimya.

Kwa hiyo, la kwanza ninaloliona ni kwamba Serikali ingekuwa macho, ingekuwa sambamba na wale wakulima na wafugaji, huyu tajiri alipovamia hilo eneo la wafugaji, Serikali ingejitokeza. Kwa sababu wale vijana baada ya kukamatwa, walipelekwa Polisi, wanateseka, dhamana imezuiwa na Serikali ya Kilimanjaro inajua eneo lile walikwishaligawa, wafugaji kwao na wakulima kwao. Tukakutana na wale wafugaji, tumeshitakiwa Polisi, ikabidi niende kubembeleza Polisi ili vijana wale wasisote kule ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, huyo aliyevamia shamba akafungua kesi Mahakamani, yeye ana Wakili, wale Wamasai hawana. Hela hawana. Ikabidi tukutane, tukachangisha fedha kuweka Wakili *(Advocate)*. Sasa wale wakapelekwa Mahakamani. Wanateseka kila siku, kiguu na njia Mahakamani wanashtakiwa. Sasa tulitegemea Serikali sasa ingejitokeza kwamba jamani eneo lile tulishaligawa la hawa. Hakuna mtu anayefika Mahakamani, hakuna anayeenda kuwatetea, wamehangaika wenyewe miaka miwili. Kwa bahati, Mungu sio Abdallah wala sio Athumani, wakashinda wale masikini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliposhinda, yule Hakimu aliyetoa hukumu hiyo akaonekana amekula rushwa, sijui rushwa gani kwa Wamasai akahamishwa kuja sijui Mkoa gani. Sasa yule tajiri amekata rufaa. Siwezi kuzungumzia zaidi kwa sababu kesi iko Mahakamani.

Kwa hiyo, la kwanza ninaloliona, hakuna mtu anayewalinda wafugaji wala hakuna mtu anayewalinda wakulima. Katibu Kata yupo, Katibu Tarafa yupo, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa. Sasa katika mazingira haya wananyanyasika! Hilo la kwanza. Kwa hiyo, nasema matatizo mengine yanayojitokeza, Serikali iko wapi? Mbona hatujitokezi tukakaa na hao watu wanaohangaika?

La pili, Njiapanda. Ukiangalia huu mgogoro wa Njiapanda, watu wamejenga kwenye makazi ya watu. Katika kitabu changu hiki, tumefafanua hatua Serikali ilizochukua, barua za Serikali za kuonyesha huyo mtu amejenga kwenye

makazi ya watu na tena huyu aliyefafanua hivyo ni Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi. Hizi barua ni za Serikali. Serikali inasema, huyo mtu amevunja sheria na wakataja sheria zilizovunjwa. Sheria zilizovunjwa nane, anasema Naibu Waziri wa Wizara. Sheria hizo zilizovunjwa na huyo mmilikaji wa hilo eneo zimetajwa hapa. Ujenzi wa kiwanda hicho umekiuka sheria ya nchi ikiwemo Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999, Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya Mwaka 2007, Sheria ya Mamlaka ya Mji Na. 6 ya Mwaka 1982, Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 na Sheria ya Uhifadhi ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.

Sasa watu wanavunja sheria, Waziri anaainisha hapa, tungetegemea basi hatua zingechukuliwa. Ndiyo sababu Rais alifanya mabadiliko ya Mawaziri kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nimefurahi sana! Nilimpongeza Rais! Sasa kuna baadhi ya Mawaziri tunashangaa utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mama Tibaijuka namlaumu sana, namlaani kwa kweli, ameondoka akaniachia kesi na wananchi wangu. Sasa kama Waziri anawekewa fedha kwenye akaunti yake Shilingi bilioni 1.6 anakubali, sasa Waziri wa aina hiyo hata ukimwita mla rushwa, atakuwa amesingiziwa? Kama ameweza kupewa hizo hela, kule Vunjo kwangu tunajua watu wazuri wanaotoa hizo hela. Je, hakupewa kitu? Kwa nini huo mgogoro wa Njiapanda haujatatuliwa? *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakupongeza na Naibu wako, ni watu makini, watu wazuri, nakata rufani kwako kuanzia leo, ndani ya siku saba unipe majibu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ya Meresini, ninayo majina ya wananchi, yako hapa tena wengi wa CCM 381, wanalalamikia lile eneo la Meresini, nyie Serikali mmegawa, hamkuangalia maslahi ya wananchi wa Himo, mmewapa matajiri. Kwa hiyo, mpaka leo wanasema hajatendewa haki, wanataka maeneo ya shule na viwanja vya michezo. Kwa

nini kunakuwa na kigugumizi? Mheshimiwa Lukuvi, nakukabidhi hao watu.

Kwa hiyo, ninachosema, nyie mnavyoacha kutumia wajibu wenu, lawama zinakuja kwetu. Mnataka tusichaguliwe tuonekane Wabunge wazembe! Kwa hiyo, nakwambia na wewe Mheshimiwa Lukuvi, mtu mzuri, ndani ya siku saba hebu nitatulie tatizo la wananchi wangu wa Meresini, nitafurahi sana. Nilikwisha kata tamaa kuja kwenye Ofisi ya Ardhi, sasa nitakuja kiguu na njia. Nitakupigia simu na nitakushukuru sana kama unaweza kuja Njiapanda Moshi, ukaja na huko Mawala ukaja na Meresini Himo. Mkishatekeleza hizi kazi, mmefanya vizuri, njoo mfanye mikutano na Mbunge na wananchi muwape majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukiuliza Njiapanda hatujui kinachoendelea! Meresini hatujui! Matokeo yake wale matajiri wame-*join together* kwamba huyo Mbunge lazima aondolewe, anatufuatafuata. Wamechanga hela na kweli nina kazi kubwa kule kwa sababu nyie hamjaja kule Moshi mkaeleza ni Mbunge ndio mbaya anawaonea wivu hao matajiri au mwenye haki ni nani?

Sasa mnaponyamaza, sisi tutajiteteaje? Utaonekana Mbunge ni mzushi, mwongo, anawaonea wivu matajiri; na wenyewe kwa kuwa wana hela, wanawahamasisha wananchi kwamba tunataka Mbunge wa aina nyingine, sio huyu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lukuvi nakuomba sana, njoo unisaidie yale matatizo kule Vunjo, watu wangu waishi kwa amani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Ni kengele ya kwanza ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Ya pili.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nawashukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Moshi Kakoso, kama hayupo namwita Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza roho ilikuwa inanidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu kusema kwamba akina mama tunaweza na Spika na Bunge limewapendekeza na tumewaidhinisha akina mama wawili. Sasa katika *gallery* ya Spika, mko akina mama watatu na akina baba wawili. Kwa hiyo, ile asilimia 50 tumeivuka, mwendo ni huo huo! Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naungana na Kamati, lakini nilikuwa najiuliza, ile hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee aliyesema tunataka tuorodheshe maeneo yote waliyomiliki mashamba kwenye mapori; mashamba makubwa, mashamba madogo, majina yao na nini, nimeyachungulia katika daftari, nimeona lakini hayakutosheleza. Sishangai kwa nini labda mmeshindwa, kwa sababu muda mliopewa labda ni mdogo na nyie mmefanya kama *sample*. Lakini matatizo yaliyokuwepo ni makubwa kuliko haya tuliyoyaona humu katika hiki kitabu. Wao wameenda tu katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hata Mkoa wa Morogoro walikofika, hawakufika kote, wamefika tu baadhi, lakini kuna hatari. Hata juzi watu wameuawa katika vita ya mkulima na mfugaji. Hapo Kilosa ni sehemu tu, wamesema Rose; sasa huyo Rose hata wananchi hawamjui ni nani anayemiliki *Rose Estate* na anamiliki kwa mpango gani? Shamba haliendelezwi, wananchi hawana mahali pa kulima, mafuriko yameingia kwenye mkondoa, watu wameondolewa, wamewekwa pale pale Magomeni kwenye

mabanda, mpaka agizo la Mheshimiwa Rais Kikwete limetoka kwamba wale watu wapewe maeneo, mpaka leo hawajapewa maeneo, wala fidia yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanateseka nchi hii! Akina mama wanateseka, vijana wanateseka, watoto hawajui hatma yao na wazee wanateseka. Hata kwenye Katiba inapendekezwa, wanasema akina mama sasa tutamiliki ardhi, iko wapi? Wao wakubwa wanaume waliokuwepo hawana ardhi; hata Katiba ikisema sasa mtapewa ardhi, iko wapi? Ardhi haipo! Ipo mikononi kwa watu wachache.

Sasa mimi ninachoomba, pamoja na ripoti hii, naomba kusemea Mkoa wa Morogoro, wameenda baadhi tu ya maeneo, lakini hali ni tete yaani kuliko tunavyoiona katika hii ripoti. Ninachoomba, Serikali sasa kwa kutumia ripoti hii, kwa hizo *sample* walizoleta, waende sasa kwa kina ili waende huko chini; Ofisi ya TAMISEMI, Mawaziri wa TAMISEMI, Mawaziri wa Ardhi, Mawaziri wa Maliasili, waungane kwa pamoja na Mawaziri wa Kilimo waende huko chini wakafanye kazi chini, wasikae Maofisini kwa sababu hali ni mbaya. Kwa hiyo, mambo ya kubaki Ofisini yamepitwa na wakati. Sasa hivi waende chini, kwa sababu matatizo yako chini kwa wananchi.

Hebu fikiria Wilaya ya Kilombero, kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji vitatu havijafanya uchaguzi. Kisa nini? Chiwachiwa, hapo Namawala wanasema eti kuna mwekezaji. Mimi nauliza, mahali penye mwekezaji na wananchi wapo kaya karibu 1000 hawafanyi uchaguzi? Huyo mwekezaji anaenda kuwekeza wapi? Mbinguni! Kwa hiyo, wananchi wana hasira, hawajui hatma yao. Hivi palipo na mwekezaji wananchi hawafanyi uchaguzi? Kwa hiyo, haya ni matatizo makubwa; na hii yote ni kwa sababu gani? Ardhi yetu haijulikani ni nani anamiliki.

Kwa hiyo, tunaomba na tunapendekeza kwa Serikali, TAMISEMI mipaka haijulikani, shule zinalalamika, wananchi wanalalamika mipaka ya shule na mipaka ya wananchi

haionekani. Shule zinashindwa kuwekewa uzio. Wananchi wanaingia mpaka kwenye maeneo ya shule. Kwa hiyo, bado kuna kazi kubwa. Hospitali zinaingiliwa lakini hakuna mipaka. Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hivi, kuwepo na kitengo maalum kinachoshughulikia masuala ya upimaji. Leo mimi niko kwenye Kamati ya Ardhi na Maliasili lakini watu wa ardhi bajeti yao ni kiduchu. Sasa kama bajeti kiduchu, watapimaje hiyo ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye Masjala ya Ardhi pale Kilombero ukiangalia vumbi lake siyo la kawaida, hawana hata kompyuta moja. Mafaili ya kizamani, wafanyakazi wanakula vumbi, lakini matatizo yako kwenye ardhi. Kwa hiyo, Serikali kama kwenye *BRN* hamwezi mkafanya maendeleo ya kilimo ya uwekezaji bila kuipima ardhi. Kwa hiyo, naona kipaumbele ardhi ingepimwa kwanza ili watu wajulikane; ardhi ya kilimo, ardhi ya makazi, ardhi ya ufugaji halafu hata mkipeleka miradi ya maendeleo, inaweza ikafanya kazi vizuri na wananchi tukapata maendeleo.

Leo Wilaya Kilombero na Ulanga; Wilaya ya Kilombero vijiji 22 vyote vimeingiliwa mkuruzo wanaita *ramsar,* wananchi hawana mahali pa kulima, wananchi wanateseka, wakiingia huko wanapigwa, wananyang'anywa matrekta na hawana mahali pa kulima, upande huu kuna hifadhi ambayo wanaita Udzungwa, upande wa pili kuna *Selous,* wananchi wako katikati; hivi wananchi wa Kilombero waende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwuliza Afisa Wanyamapori kwa sababu yeye anaripoti kwenye Kamati yetu, nikasema kwa nini mnawaacha wananchi wa Kilombero wanateseka? Kwa nini hamwendi kuurekebisha ule mkuruzo? Mnaita *ramsar,* yaani eneo oevu! Hivi eneo oevu mkulima anahusiana nini akienda kulima kule maeneo mita 60 ya Mto Kilombero mnamzuia? Lakini leo ukipita Ruvu Darajani watu wamelima mpaka mita *Zero*. Leo kwenye mto Kilombero wanatuambia mita 60, zaidi ya mita 60 karibuni mita 2,000, wananchi wanafukuzwa. Tumewakosea nini?

Kwani kuna ubaya gani kuzaliwa Kilombero? Mnatuonea wivu kwa sababu ardhi ni chepe chepe, ni nzuri, ukipanda kila kitu kinaota! Kila anayekuja Kilombero, anataka kuchukua mashamba. Wafugaji wameingia, Watendaji wanakula rushwa. Mimi nakwambia ni rushwa, ni rushwa ni rushwa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Kamati ya Uchumi na Maliasili pale Halmashauri, wameleta taarifa, eti kuanzia tarehe 1 mpaka 30, *DED, DARDO*, Mkuu wa Wilaya, sijui Polisi, eti walikuwa *field* wakalipana posho, wamewapiga faini wafugaji Shilingi milioni 71, wametumia Shilingi milioni 58 eti kwa kulipana posho. Nikawaambia malambo yako wapi? Hivi kwenda kupiga faini huyo mfugaji na ng'ombe wake ndiyo kuondoa matatizo? Kwa nini hizo hela hamkujenga malambo? Yaani ni wizi, wizi, wizi mkubwa!

Naomba nendeni haraka Kilombero na Ulanga, mkawaokoe wananchi. Tumechoka kuteseka! Sisi ni wakulima, mmetuletea wafugaji, tunakula nyama na maziwa, ni marafiki zetu. Nendeni mkaweke mipango bora ya ardhi. Ninyi mnaruhusu vipi Mkoa wa Morogoro kwamba ingizeni wafugaji bila kwenda kuwawekea mipango mizuri ya ardhi? Haiwezekani! Ni Serikali gani? CCM mnajichimbia shimo wenyewe! Ndiyo maana Wilaya ya Kilombero tumebeba vijiji 57 kati ya vijiji 107.

Kwa hiyo, sisi UKAWA tuko juu, ninyi CCM mko chini na tunaenda kubeba Halmashauri. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Jikite kwenye hoja Mheshimiwa Susan. Muda umekwisha!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa taarifa tu. Mnajichimbia shimo! Tunachukua Jimbo na Halmshauri, tunaongoza, tuna...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Kakoso kama anaweza kutumia muda uliobaki.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nipate kuchangia. Kwanza nawashukuru sana walioongoza hii Kamati kwa uhalisia waliouleta na kujenga hisia ambayo itakuwa ni nzuri kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ni eneo muhimu sana. Tukitaka kuwasaidia jamii ya wakulima na wafugaji kwanza ni lazima tupime ardhi. Ardhi ni muhimu, ikipimwa itatoa malalamiko ambayo kwa kiwango kikubwa wakulima na wafugaji wanakuwa na migogoro. Lakini eneo ambalo tunahitaji tulifanyie kazi kwa kiwango kikubwa sana ni kupunguza maeneo ambayo yanashikiliwa na Serikali. Maeneo mengi bado Serikali imechukua maeneo kama hifadhi, WMA ambayo kwa kiwango kikubwa yanamnyima mkulima aweze kupata ardhi ambayo inaweza ikamsaidia kwa shughuli zake za kilimo, lakini inamfanya mfugaji akose sehemu za kupeleka malisho yake.

Naiomba sana Serikali na ninatolea mfano kwenye maeneo ya Mkoa wa Katavi ambapo kuna maeneo makubwa sana ambayo yamezungukwa na misitu minene na mikubwa sana. Lakini katika maeneo haya ndiko ambako kuna matatizo makubwa sana kati ya wafugaji ambao hawana maeneo ya malisho.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itenge baadhi ya maeneo, iwasaidie wakulima na wafugaji na itenganishe shughuli za wakulima na shughuli za wafugaji ili tuweze kutoa migogoro ambayo ina uwezekano wa kuweza kuepukika. Lakini maeneo mengine ambayo tunahitaji Serikali iweze kuyashughulikia ni yale ya WMA.

Mkoani kwangu kuna matatizo makubwa sana ya vijiji vya Kabage, Sibwesa, Kasekese na baadhi ya maeneo mengine ambayo yapo katika Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu, yale tunahitaji tuwasaidie wananchi waweze kupewa

maeneo yale wayamiliki wao na waweze kutumia shughuli zao za kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, WMA hakuna kitu chochote ambacho kimefanyika katika maeneo hayo. Hatujaona mrejesho wake ambao unawasaidia wananchi katika maeneo hayo. Tunaiomba sana Serikali iangalie upya ile mipaka ambayo walipewa WMA ukilinganisha na hali halisi ilivyo kwa sasa kwamba wakulima ni wengi na ukizingatia kwamba Mkoa wa Katavi umewahamasisha wananchi wengi waje kuwekeza na wawekezaji wengi wamekuja ambao ni wakulima na wafugaji na ambao kimsingi sasa hawana maeneo ya kufanyia kazi.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie upya, yale maeneo ambayo yana migogoro yaweze kutolewa kwa wananchi ili waweze kuyafanyia kazi na kupisha mlolongo mzima usiokuwa na maana ambao tunawaletea migogoro isiyokuwa na ulazima kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni maeneo ambayo wakulima na wafugaji wameweza kupeleka ng'ombe wao katika maeneo ambayo yanamilikiwa na Serikali. Katika eneo hili, tunaiomba Serikali iangalie upya. Wafugaji wa Mkoa wa Katavi wamekula hasara sana; ng'ombe wameuawa kwenye Hifadhi, siyo vizuri kuua mifugo. Pale ambapo mkulima amekosea au mfugaji kakosea, ni vyema sasa wakachukua hatua kwa kushika wale mifugo na watozwe faini kuliko kuua mifugo. Ni jambo ambalo linasikitisha sana kwa wafugaji wetu na wakulima kwa ujumla. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie upya eneo hili ili liweze kuwasaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migogoro kati ya wakulima na wafugaji, suluhu yake itapatikana pale tu tutakapokuwa tumetenga maeneo tengefu ambayo yatawasaidia sana wakulima na wafugaji. Lakini kubwa zaidi kwa Serikali ni kuwapa elimu hasa jamii ya wafugaji ambao wana mifugo mingi na haijatumika ipasavyo na wao wameweza kuwa na mifugo mingi kwasababu ile mifugo

haina masoko. Kwa hiyo, tukiwatafutia masoko hawa wafugaji, watakuwa na nafasi ya kufuga kwa kutumia elimu na wanaweza kuwa na mahitaji ambayo yatawasaidia sasa na wakawekeza kwenye elimu na pia wakawekeza kwenye nyumba bora.

Kwa hiyo, ni elimu pekee ambayo itawasaidia jamii hii ya wafugaji ili waweze kuepukana na ufugaji wa kuhamahama. Kwa maeneo ya kwetu yalivyo hasa katika Mkoa wa Katavi, ni vyema sasa Serikali ikatenga maeneo ambayo yatasaidia kuwapa eneo muhimu litakalokuwa linatumiwa na wafugaji ili kuepusha migogoro isiyokuwa na ulazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima nao hawana eneo la kufanyia shughuli za kilimo na mfano halisi ni Kitongoji cha Mnyamasi ambacho kimsingi kina mgogoro mkubwa sana na eneo hili la Luhafwe – Mnyamasi.

Naomba Serikali ifikirie kuangalia umuhimu wa kuachia wananchi ili waweze kufanya shughuli zao za kilimo na ufugaji. Tukiwapa eneo hili, litawasaidia sana kufanya shughuli zao za kila siku na litatoa mgogoro ambao hautakuwa na ulazima. Lakini kipo Kijiji cha Kapanga ambacho nacho kimeingia kwenye mgogoro kati ya Serikali na wananchi. Wakulima walitenga maeneo yao, lakini Mtendaji wa Kijiji akayagawa kwa wakulima badala ya kuwapa wafugaji. Kwa hiyo, eneo hili lina mgogoro mkubwa, Serikali iangalie kulifuatilia ili mgogoro huu nao uweze kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la Inyonga Kijiji cha Mapili kuna mgogoro wa ardhi ambao kimsingi tukiwasaidia, tukawapa eneo kati ya Mapili na Kijiji cha Ilunde tunaweza tukawasaidia sana wakulima ambao wako kwenye maeneo yale ili waweze kutumia fursa iliyopo wakaweka kama eneo la mifugo ili kuondoa migogoro ambayo siyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchango wangu uishie hapo. Nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo. Wote tuelewe kwamba hoja hii inaendelea kuchagiwa mpaka kesho. Kwa hiyo, wale ambao hawakupata nafasi leo, wasiwe na hofu, inawezekana kesho wakaweza kupata nafasi hiyo. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Kanuni ya 28 Kanuni ndogo ya (8) naongeza muda wa nusu saa ili kumpa nafasi Mheshimiwa James Mbatia atoe maelezo binafsi na ninampa dakika 15 kutoa maelezo hayo. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kutoa maelezo binafsi ndani ya Bunge hili. Maelezo haya nayatoa kwa mujibu wa Kanuni ya 50 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya nayatoa kukanusha kwa moyo wangu wote matamshi yaliyotolewa ndani ya Bunge hili na Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya tarehe 5 Februari, 2015, wakati wa kuahirisha Bunge, Mheshimiwa Augutine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, alitoa maelezo ambayo siyo sahihi alipoeleza kuwa mimi James Francis Mbatia, niliwahi kusema kuwa yeye ni mgonjwa anayeugua maradhi ya Ukosefu wa Kinga Mwilini, yaani UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yote aliyoyatoa siyo sahihi na sijawahi na sitawahi kutamka maneno hayo ndani ya Tanzania na hata nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kumnyanyapaa Dkt. Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema na wala mtu yeyote aliyeathirika na maradhi ya aina yoyote ikiwemo maradhi ya Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ugonjwa wa aina yoyote ni masuala binafsi na hivyo siyo busara kwa mtu ambaye hana idhini ya mhusika kuzungumzia magonjwa yake. Maradhi ni kitu kinachoweza kumpata binadamu yeyote, hivyo siyo uungwana kuyazungumzia kwa namna ya kumkashifu mtu mwenye tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nimekuwa mstari wa mbele katika kushughulikia matatizo ya watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali na waathirika wa UKIMWI, binafsi nimekuwa karibu na watoto ambao wamepoteza wazazi wao kutokana na maradhi aliyoyanzungumzia Mheshimiwa Mbunge.

Hivyo, nafahamu uchungu unaotokana na maradhi hayo. Nimesomesha kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2000 na ninaendelea kusomesha watoto kuanzia ngazi za Shule ya Msingi hadi Vyuo Vikuu wapatao 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Sophia Simba (Mbunge), Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kwa msaada alionipatia na anajua fika jitihada zangu binafsi za kusaidia kutatua matatizo na changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto hapa nchini wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi, 2012 niliweza kumleta *Miss African Scandinavian Countries* Mitchell Gin kusaidia vifaa vya aina mbalimbali na akatoa ufadhili wa aina mbalimbali kwa Kituo cha Walemavu wa Ngozi, *Under The Same Sun,* Shirika ambalo siyo la Kiserikali na Mheshimiwa Al-Shymaa yuko pale analijua fika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilishirikiana na Mheshimiwa William Lukuvi yuko pale (Mbunge) Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati akiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Jimbo Kuu Katoliki Mkoa wa Dar es Salaam, kuhamasisha na kupambana na unyanyasi wa watu wenye ulemavu wa ngozi. Mheshimiwa Lukuvi tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kipindi hiki ninavyozungumza hapa, namsomesha kijana mmoja anaitwa Ali Bane na nimemnunulia viungo vya mkono na mguu na katika Hospitali ya Muhimbili *(MOI),* na ninamsomesha Jeshi la Wokovu Jijini Dar es Salaam kwa miaka minne mfululizo, ambaye aligongwa na treni huko Kibaha Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limenigusa sana, niwe mkweli, kwani ndani ya familia yangu limetupa uchungu mkubwa kwasababu ninaye mtoto ambaye kutokana na athari za ugonjwa wa UKIMWI alipoteza wazazi wake wote jambo lililonifanya nichukue hatua za kumuasili *(adoption)* ili niweze kumpatia upendo na malezi kama mwanangu.

Hivyo suala la kutukana, kudharau, kukashifu mtu wa maradhi hayo, siyo jambo ambalo ningeweza kuthubutu kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanihuzunisha kwamba suala hili linawatia uchungu sana familia yangu, kwani leo asubuhi mwanangu Andrew ameniuliza, "ni kweli baba umesema maneno hayo?" Wakati anam-*protect* dada yake ambaye anajua fika kwamba wazazi wake hawako duniani na ni mtoto wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina uadui wowote na mtu yeyote, akiwemo Mheshimiwa Mrema, hata sasa hivi amekaa kwenye kiti change, sina ugomvi wowote naye. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mzee Mrema kama Mzee wangu, hivyo kimaadili nisingeweza kumkosea nidhamu kwa kiwango hicho alichokieleza hapa Bungeni. Nimezaliwa na kukuzwa katika familia ya Wacha Mungu, siwezi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muumini wa siasa safi na sina utaalamu wa aina yoyote wa propaganda zilizozungumzwa jana na Mheshimiwa Mrema. Binafsi ninaamini kwenye ukweli na ukweli utatuweka huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi fulani ninaamini na ninaomba niendelee kuamini kwamba kuzeeka siyo kukua. *To grow old is mandatory, but to be wise is optional.* Ninaamini katika kumcha Bwana inakuwa ni chanzo cha maarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatamka neno lolote, namwomba Mungu awe ni mlinzi kinywani pangu na mngojezi mlangoni pa mdomo wangu. *Lord place a guard at my mouth, a sentry at the door of my lips.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaongea neno lolote, natafakari naongea nini na nani na mahali gani, wakati gani halafu kitatokea nini? Hii ni *tautology* kwenye *mathematics*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu, ni rai yangu kwa Watanzania wote wachague Viongozi wenye uwezo, Wacha Mungu, wakweli na wenye kuchukia propaganda, ubaguzi, chuki, ubinafsi na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Chama, nafanya kazi nchi nzima ya Tanzania na ninafanya kazi za Kisiasa kwenye maeneo mbalimbali. Huko kote sijawahi kutuhumiwa kwa ubaguzi wa aina yoyote, iweje nituhumiwe kwa ubaguzi katika Jimbo moja la Tanzania, Jimbo la Vunjo? Kulikoni? Kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Viongozi walioko madarakani sasa, wanadai kuwa wana hatimiliki ya maeneo wanayoongoza. Dhana hii siyo sahihi, bali nataka kuwakikishia Watanzania kwamba wenye hatimiliki na nchi yao ni Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshimia kubwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hiyo hoja haijadiliwi, wote tunafahamu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaelewa kuwa kesho hakuna kipindi cha maswali asubuhi, kwa hiyo, naomba nianze kutaja Waheshimiwa Wabunge watakaoanza kuchangia kesho asubuhi. Tutaanza na Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdul Marombwa na Mheshimiwa Sara Msafiri na wengine watafuata.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.54 usiku, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 7 Februari, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*